**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# MAPITIO YA HALI YA UCHUMI 2023 NA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO 2023/2024

## KITABU CHA KWANZA

**TUME YA MIPANGO ZANZIBAR**

**JUNI, 2024**

## YALIYOMO

**YALIYOMO ........................................ i**
**ORODHA YA VIFUPISHO ........................................ vii**
**UTANGULIZI ........................................ ix**
**SURA YA KWANZA ........................................ 1**
**1.0 HALI YA UCHUMI ........................................ 1**
1.1 Uchumi wa Dunia ........................................ 1
1.2 Uchumi wa Nchi Zilizoendelea ........................................ 2
1.3 Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi ........................................ 2
1.4 Hali ya Uchumi wa Bara la Afrika ........................................ 4
1.4.1 Uchumi wa Afrika ........................................ 4
1.4.2 Uchumi wa Nchi za Visiwa Vilivyo Barani Afrika ........................................ 6
1.4.3 Uchumi wa Baadhi ya Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara .. 7
1.4.4 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ........................................ 9
1.4.5 Nchi zenye uhusiano wa kibiashara na Zanzibar (Zanzibar Trading Partners) ........................................ 11
1.5 Hali ya Mfumko wa Bei ........................................ 11
1.5.1 Mfumko wa Bei wa Dunia ........................................ 11
1.5.2 Mfumko wa Bei kwa Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara .. 12
1.5.3 Mfumko wa bei wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ........................................ 13
1.5.4 Mfumko wa bei kwa Nchi zenye uhusiano wa kibiashara na Zanzibar (Zanzibar Trading Partners) ........................................ 15
1.5.5 Mwenendo wa Bei kwa baadhi ya bidhaa katika Soko la Dunia .... 16
**SURA YA PILI ........................................ 18**
**2.0 HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR ........................................ 18**
2.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi ........................................ 18
2.2 Pato la Mwananchi ........................................ 19
2.3 Mwenendo wa Mfumko wa Bei Zanzibar ........................................ 20
2.4 Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani ........................................ 21
2.5 Mwenendo wa Uingiaji wa Watalii Zanzibar ........................................ 22
2.6 Ukuaji wa Sekta katika Pato la Taifa ........................................ 24
2.6.1 Sekta ya Huduma ........................................ 24
2.6.2 Sekta ya Viwanda ........................................ 25
2.6.3 Sekta ya Kilimo ........................................ 26
2.7 Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa ........................................ 27
2.7.1 Sekta ya huduma ........................................ 27
2.7.2 Sekta ya Viwanda ........................................ 28

2.7.3 Sekta ya Kilimo.......................................................................... 28
2.8 Ukuzaji Rasilimali ........................................................................ 37
2.8.1 Sekta Binafsi Kupitia Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA)........ 40
2.8.2 Mgawanyo wa Miradi iliyosajiliwa na ZIPA kwa Sekta na Umiliki 2022/2023. ................................................................... 41
2.8.3 Mgawanyo wa Miradi iliyosajiliwa na ZIPA kwa Mabara mwaka 2023......................................................................................... 41
2.8.4 Faida za Kiuchumi na Kijamii kutoka katika Miradi ya Uwekezaji... 42
2.8.5 Hali ya Upatikanaji wa Ajira.......................................................... 42
**SURA YA TATU ............................................................................ 44**
**3.0 SEKTA YA NJE........................................................................ 44**
3.1 Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi.............................................. 44
3.1.1 Usafirishaji wa Mazao ya Biashara (Karafuu na Mwani).................. 44
3.2 Uagiziaji wa Bidhaa kutoka Nje ya Nchi......................................... 46
3.3 Urari wa Biashara ......................................................................... 47
3.4 Uhaulishaji wa Bidhaa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara................ 48
**SURA YA NNE ............................................................................. 50**
**4.0 SEKTA YA FEDHA................................................................... 50**
4.1 Sekta Ndogo ya Benki ................................................................... 50
4.1.1 Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ...................................................... 50
4.1.2 Huduma za Kibenki ..................................................................... 53
4.1.3 Amana ........................................................................................ 54
4.1.4 Mikopo........................................................................................ 55
4.1.5 Mwenendo wa riba za benki ......................................................... 56
4.1.6 Wakala wa Huduma za Kibenki..................................................... 57
4.1.7 Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji wa Fedha za Kigeni (Exchange Rate Movement) ..................................................... 58
4.2 Benki ya Watu wa Zanzibar............................................................ 58
4.2.1 Utekelezaji wa kibajeti Julai 2023 hadi Machi 2024....................... 58
4.2.2 Malengo ya PBZ kwa mwaka 2024................................................. 60
4.2.3 Miradi ya PBZ kwa mwaka 2024 ................................................... 60
4.3 Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ............................ 63
4.3.1 Usajili wa watoa huduma za Bima.................................................. 63
4.3.2 Mfumo wa Kusimamia na Kudhibiti Soko ...................................... 64
4.3.3 Msuluhishi wa migogoro ya bima (Ombudsman) ........................... 64
4.3.4 Hali ya soko la huduma za Bima Zanzibar ...................................... 64
4.3.5 Mafanikio.................................................................................... 65
4.3.6 Matarajio .................................................................................... 66

4.4 Shirika la Bima la Zanzibar ................................................................ 73
4.4.1 Majukumu Makuu ya Shirika la Bima Zanzibar........................... 73
4.4.2 Ofisi Za Shirika ............................................................................ 73
4.4.3 Huduma Zinazotolewa na Shirika................................................ 73
4.4.4 Utekelezaji Halisi wa Kazi za Shirika kwa Kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 ................................................................ 74
4.4.5 Mafanikio Yaliyopatikana kwa Shirika katika Sekta ya Fedha..... 74
4.5 Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar ............................................. 76
4.5.1 Utekelezaji kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 ............ 76
4.5.2 Mafanikio ..................................................................................... 82
4.5.3 Changamoto ................................................................................. 86
4.6 Idara ya Maendeleo ya Ushirika ..................................................... 86
4.6.1 Maendeleo ya Ushirika Zanzibar .................................................. 87
4.6.2 Mafanikio ..................................................................................... 89
4.6.3 Changamoto ................................................................................. 89
4.6.4 Matarajio na Muelekeo kwa Sekta ya fedha Machi 2025............. 90
4.7 Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ........................ 92
4.7.1 Majukumu makuu ya Mamlaka (CMSA) ..................................... 92
4.7.2 Maendeleo ya Masoko ya Mitaji kwa Kipindi cha Julai 2023 Hadi Machi 2024.............................................................................. 92
4.7.3 Biashara Katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ........................... 96
4.7.4 Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja ................................................. 98
4.7.5 Jitihada za Mamlaka Katika Kukuza Masoko ya Mitaji............. 101
4.7.6 Changamoto Zinazokabili Masoko ya Mitaji Nchini................. 103
4.7.7 Mapendekezo ya Namna ya Kupata Ufumbuzi wa Changamoto.... 103
**SURA YA TANO.................................................................................. 105**
**5.0 SEKTA YA MIUNDOMBINU......................................................... 105**
5.1 Wakala wa Barabara........................................................................ 105
5.2 Kitengo cha Mfuko wa Barabara ..................................................... 108
5.2.1 Mapato ya Mfuko wa Barabara.................................................... 108
5.2.2 Hatua Zinazochukuliwa .............................................................. 109
5.3 Nishati ya Umeme............................................................................. 109
5.4 Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ..............................................113
5.4.1 Usimamizi na Uendelezaji Rasilimali Maji na utatuzi wa changamoto za maji. ..................................................................114
5.4.2 Huduma ya Maji Vijijini ..............................................................114
5.4.3 Huduma za Maji Mijini mwaka 2023 ..........................................115

**SURA YA SITA ..................................................................... 118**
**6.0 SEKTA YA ELIMU ............................................................. 118**
6.1 Elimu na Mafunzo ya Amali ................................................ 118
6.1.1 Idadi ya Wanafunzi: Maandalizi, Msingi, Kati na Sekondari kwa Skuli za Serikali ........................................................ 118
6.1.2 Idadi ya Wanafunzi: Maandalizi, Msingi, Kati na Sekondari kwa Skuli za Binafsi ........................................................ 120
6.1.3 Idadi ya Wanafunzi wa Skuli za Sekondari kwa Jinsia kwa skuli za Serikali na Binafsi. ........................................................ 122
6.2 Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ................................... 124
6.2.1 Idadi ya Mikopo Iliyopangwa kutolewa ................................ 124
6.2.2 Mwenendo wa utoaji wa mikopo na Utaratibu wa kurejesha mikopo ........................................................ 125
6.2.3 Ukusanyaji wa marejesho ya mikopo ................................ 126
6.2.4 Changamoto za Urejeshaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu ............ 126
6.2.5 Mapendekezo ya Kutatua Changamoto za Urejeshaji Mkopo wa Elimu ya Juu; ........................................................ 127
6.2.6 Mikakati ya Bodi Juu ya Urejeshajiwa Mikopo kwa Wanufaika. 128
**SURA YA SABA ..................................................................... 129**
**7.0 SEKTA YA AFYA ............................................................... 129**
7.1 Wataalamu wa afya ........................................................ 129
7.2 Idadi ya Vituo vya Afya na Wagonjwa ................................ 129
7.3 Vizazi hai na wagonjwa walio tibiwa na kurudi majumbani ............. 130
7.4 Huduma kwa Kinamama Wajawazito ................................... 132
7.5 Idadi ya Kinamama Wajawazito Waliojifungua kwa Njia ya Upasuaji na Mimba Zilizoharibika ........................................ 132
7.6 Mpango wa Kumaliza Malaria Nchini. ................................ 133
7.6.1 Vituo vinavyotumia MRDT ............................................ 134
7.6.2 Dawa Zinazotumika Kutibu Malaria Nchini. ............................ 134
7.6.3 Madaraja ya Dawa za Kutibia Malaria Nchini ........................ 134
7.6.4 Mikakati ya Kupambana na malaria Zanzibar 2019-2023 ........... 135
7.6.4.1 Kazi kuu zilizofanywa na Programu katika kupambana na malaria Zanzibar mwaka 2019-2023 ................................ 135
7.6.4.2 Idadi ya Nyumba Zilizopuliziwa Dawa ................................ 136
7.7 Huduma za Upasuaji Mkubwa ........................................... 136
7.8 Mpango wa Damu Salama ............................................... 137
7.9 Lishe ya Mama na Mtoto ................................................ 137
7.10 Maradhi ya Kuambukiza ................................................ 138

7.11 Idadi ya nyumba na wakaazi walioathirika kwa madawa ya kulevya (sober houses) ....139
7.12 Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ....140
7.13 Ustawi wa Jamii ....140
7.13.1 Watoto Yatima ....141
7.13.2 Ukatili dhidi ya Wanawake, Wanaume na Watoto ....141
7.13.3 Ubakaji na Shambulio la Aibu ....141
7.13.4 Matukio ya Uhalifu ....142
**SURA YA NANE ....144**
**8.0 MAENDELEO YA KIUCHUMI NA KIJAMII ZANZIBAR MWAKA 2023 ....144**
**SURA YA TISA ....145**
**9.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2023/2024 ....145**
9.1 Mapato ya Serikali ....145
9.1.1 Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ....145
9.1.2 Ukusanyaji wa Mapato Kitaasisi ....145
9.1.3 Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ....146
9.2 Matumizi ya Serikali 2023/2024 ....146
9.2.1 Matumizi ya Kazi za Kawaida ....146
9.2.2 Mishahara ....146
9.2.3 Matumizi Mengineyo ....146
9.2.4 Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali ....147
9.2.5 Matumizi ya Kazi za Maendeleo ....147
9.2.6 Deni la Taifa ....147
**SURA YA KUMI ....148**
**10.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MIRADI YA KIMKAKATI KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 ....148**
**10.1 UTANGULIZI ....148**
**10.2 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA KIMKAKATI KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 - MACHI 2024 ....148**
**SURA YA KUMI NA MOJA ....161**
**11.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 ....161**
**11.1 UTANGULIZI ....161**

**11.2 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 KWA KILA WIZARA.....................................................................................162**
11.2.1 Ofisi ya Rais Ikulu.....................................................................163
11.2.2 Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji ...............................166
11.2.3 Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango .............................................167
11.2.3.1 Tume ya Mipango Zanzibar ................................................173
11.2.3.2 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ..................................175
11.2.4 Ofisi ya Rais Katiba,Sheria,Utumishi na Utawala Bora ............178
11.2.4.1 Mahakama Kuu ....................................................................179
11.2.5 Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ......................................181
11.2.5.1 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya ..........................................................................................188
11.2.6 Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais - Sera,Uratibu na Baraza la Wawakilishi..........................................................................................190
11.2.7 Wizara ya Afya .........................................................................192
11.2.8 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ........................201
11.2.9 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Mali ......................................204
11.2.10 Wizara ya Habari,Vijana, Utamaduni na Michezo ...................209
11.2.11 Wizara ya Kilimo,Umwagiliaji,Maliasili na Mifugo ...............210
11.2.12 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto.........218
11.2.13 Wizara ya Maji, Nishati na Madini ........................................222
11.2.14 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ..................................230
11.2.15 Wizara ya Ujenzi,Mawasiliano na Uchukuzi ..........................233
11.2.16 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale .......................................243

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ACTs | Artemisinin-based Combination Therapy |
| ADB | Asia Development Bank |
| ALU | Artemether+ Lumefantrine |
| ASAQ | Artesunate +Amodiaqune |
| BADEA | Arab Bank For Economic Development in Africa |
| BIG-Z | Boosting Inclusive Economic Growth for Zanzibar |
| BOT | Bank of Tanzania |
| BMEJZ | Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar |
| CHVs | Community Health Volunteers |
| CHVs | Wahudumu wa Afya wa Kujitolea |
| DHAP | Dihydroartemisin+Piperaquine |
| DPP | Director Of Public Prosecutions (Mkurugenzi Wa Mshtaka) |
| ECOWAS | Economic Cooperation of West Africa State |
| GPE | Global Partnership for Education |
| HIV | Human Immunodeficiency Virus (Upungufu Wa Kinga Mwilini) |
| HESLB | Higher Education Students Loan Board. |
| IFAD | International Fund For Agricultural Development |
| IITA | Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropikali |
| JICA | Japan International Cooperation Agency |
| KOICA | Korea International Cooperation Agency |
| KM | Kilomita |
| LNG | Liquefied Natural Gas |
| MRDT | Malaria Rapid Diagnostic Test (Kipimo Cha Kuchunguza Malaria) |
| PHCU+ | Primary Health Care Unity Plus (Vituo Vya Huduma Za Afya Kwa Ngazi Ya Msingi) |
| TASAF | Tanzania Social Action Fund |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| UUB | Ujenzi na Utunzaji wa Barabara |
| UNEP | United Nations Evironment Program |
| UNICEF | United Nations International Children's Emergency Fund |
| UN-WOMEN | United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women |
| WHO | World Health Organization (Shirika La Afya Duniani) |
| ZADEP | Zanzibar Development Plan |
| ZBA | Zanzibar Building Agency |
| ZBS | Zanzibar Bureau of Standard |

| | |
|---|---|
| ZAFICO | Zanzibar Fisheries Company |
| ZARI | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar |
| ZAWA | Zanzibar Water Authority |
| ZECO | Zanzibar Electricity Cooperation |
| ZRA | Zanzibar Revenue Authority |
| ZIPA | Zanzibar Investment Promotion Authority |
| ZOLAS | Zanzibar Online Loan Application Sustem |
| ZSSF | Zanzibar Social Security Fund. |

## UTANGULIZI

Katika juhudi za kuinua uchumi na kuleta maendeleo kwa mwaka 2022/23, Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya Maendeleo kwa lengo la kuimarisha ustawi wa nchi na wananchi pamoja kuwa na utawala bora kama ilvyoelezwa na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (ZDV 2050) iliyotafsiriwa na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP 2021-2026 ) na Mipango mengine ya Kitaifa ikiwemo Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025 na Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi wakati akizindua Baraza la kumi mwezi wa Novemba 2020. Mpango huu umezingatia pia Sera na Mikakati ya Kisekta; Kikanda na Kimataifa zikiwemo Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ya mwaka 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ya mwaka 2050; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2063; na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya mwaka 2030.

Kwa mwaka 2023 uchumi wa Dunia umekuwa kwa kasi ndogo ya wastani wa asilimia 3.2 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2022. Uchumi wa nchi Zilizoendelea umefikia ukuaji wa wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 2.7 kwa mwaka 2022. Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi umefikia ukuaji wa wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2023, ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2022.

Aidha, Uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika kwa kukuwa kwa kasi ya asilimia 7.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2022. Ukuaji huu umetokana na juhudi za Serikali za kuimarisha sekta za kiuchumi na kijamii na kuendelea kuwa na hali ya Amani na utulivu. Pato halisi la Taifa (GDP at constant price) limeongezeka na kufikia thamani ya TZS 3,758.8 bilioni mwaka 2023 kutoka thamani ya TZS 3,499.0 bilioni mwaka 2022. Aidha, Pato la Taifa kwa bei ya soko (GDP at current price) limeongezeka na kufikia thamani ya TZS 6,041.3 bilioni mwaka 2023 kutoka thamani ya TZS 5,400.3 bilioni mwaka 2022.

Kwa upande wa mwenendo wa mfumko wa bei kwa mwaka 2023 , Kasi ya mfumuko wa bei imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 6.9 kutoka wastani wa asilimia 5.1 Mwaka 2022. Kuongezeka kwa kasi ya mfumko wa bei kumetokana na ongezeko la bei za bidhaa za chakula na zisizo za chakula katika soko la dunia. Kwa mwaka 2023, bidhaa za chakula zimeongezeka na kufikia

wastani wa asilimia 11.1 kutoka wastani wa asilimia 6.0 mwaka 2022, na bidhaa zisizo za chakula zimefikia wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2022.

Hata hivyo, Kasi ya mfumuko wa bei ingeweza kuwa ya juu zaidi kama Serikali isingechukua juhudi za kupunguza na kusamehe ushuru kwa baadhi ya bidhaa muhimu ili wananchi waweze kumudu kununua bidhaa hizo muhimu.

Kwa upande wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/2024, Serikali ilitekeleza na inaendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo miradi ya kimkakati pamoja na maeneo saidizi kwa lengo la kukuza uchumi na kuimarisha hali za wananchi.

## SURA YA KWANZA

## 1.0 HALI YA UCHUMI

### 1.1 Uchumi wa Dunia

Kwa nchi Zilizoendelea, Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi zikiwemo na nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo hujumuishwa kwenye uchumi wa Dunia kwa kawaida mwenendo wa kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi hizo unatafautiana kulingana na maeneo husika. Kwa mujibu wa Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi **Duniani** (World Economic Outlook) ya mwezi wa April mwaka 2024 inaonesha kwamba kwa mwaka 2023 kasi ya ukuaji wa uchumi wa Dunia imefikia wastani wa asilimia 3.2 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2022. Kasi ndogo ya ukuaji huo imetokana na kupungua kwa uzalishaji kwa baadhi ya nchi zilizoendelea, mabadiliko ya sera za kifedha kwa nchi zilizoendelea ili kupunguza athari za kupanda kwa bei na kuongezeka kwa gharama za mikopo.

Ukuaji wa uchumi kwa **Nchi Zilizoendelea** umefikia wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 2.7 kwa mwaka 2022. Ukuaji huo umetokana na mabadiliko ya sera za kifedha ambayo yameanza kuleta athari kwa nchi hizo.

Uchumi wa **Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi** umefikia wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2023, ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2022. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa uwekezaji viwandani, kuimarika kwa miundombinu ya umma na biashara ya silaha za kijeshi kwa nchi ya Urusi. Kwa **Nchi za Afrika** kasi ya ukuaji imefikia wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022. Hii ni kutokana na kupungua kwa usafirishaji wa mazao ya kilimo, Biashara na kupungua kwa uzalishaji na uuzaji wa mafuta ghafi na madini kwa baadhi ya nchi za Afrika.

Kwa **Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara** kasi ya ukuaji uchumi kwa mwaka 2023 imefikia wastani wa asilimia 3.4 kutoka wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2022 ukuaji huo umechangiwa na kupungua kwa misaada ya Washirika wa Maendeleo kwa nchi nyingi za ukanda huo na kupelekea Serikali za nchi hizo kuendelea kukabiliana na uhaba wa fedha, gharama kubwa za ukopaji na ulipaji mdogo wa madeni. Kwa **Nchi za Afrika Mashariki** kasi ya ukuaji uchumi imefikia wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2022. Hii imetokana na kuongezeka kwa uwekezaji wa miundombinu

kupitia sekta binafsi pamoja na kuimarika kwa shughuli za kitalii kwa baadhi ya nchi hizi ikiwemo Kenya na Tanzania.

### 1.2 Uchumi wa Nchi Zilizoendelea

Nchi Zilizoendelea ni pamoja na Marekani, Japani, Uingereza pamoja na baadhi ya nchi za Jumuia ya Ulaya. Mwaka 2023, uchumi wa nchi zilizoendelea umefikia wastani wa asilimia 1.6 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2022. Kupungua kwa kasi ya Ukuaji kwa nchi hizi kumetokana na mabadiliko ya sera za kifedha ambayo yameanza kuleta athari kwa nchi hizo.

Mwenendo wa Uchumi kwa nchi zenye uchumi mkubwa kama vile Marekani, kasi ya ukuaji uchumi imefikia wastani wa asilimia 2.5 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.9 mwaka 2022. Nchi ya Japani, kasi ya ukuaji ilifikia wastani wa asilimia 1.9 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.0 mwaka 2022. Jumuia ya Ulaya, kasi ya ukuaji uchumi ilifikia wastani wa asilimia 0.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2022. Uingereza, kasi ya ukuaji uchumi ilifikia wastani wa asilimia 0.1 kutoka wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2022.

### 1.3 Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi


Miongoni mwa nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi ni Brazil, Urusi, India, China na Afrika ya Kusini. Ukuaji wa uchumi kwa nchi hizi ni kichocheo cha maendeleo ya ukuaji wa uchumi wa nchi nyingi duniani, kutokana na mgawanyiko wa uzalishaji wa malighafi, uwekezaji na rasilimali watu. Kwa mwaka 2023, ukuaji wa uchumi kwa nchi hizi umefikia wastani wa asilimia 4.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2022.

Kwa upande wa nchi ya **India**, kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 7.8 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 7.2 mwaka 2022. Ukuaji huo umetokana na kuongezeka kwa viwango vya mtaji ya uwekezaji wa umma. Nchi ya **China,** mwaka 2023 kasi ya ukuaji uchumi ilifikia wastani wa asilimia 5.2 kutoka wastani wa asilimia 3.0 mwaka 2022. Hii imetokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na kupelekea kuongezeka kwa uwekezaji viwandani na kuimarika kwa miundombinu.

Kwa upande wa nchi ya **Urusi,** kasi ya ukuaji wa uchumi imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia hasi ya

1.2 mwaka 2022. Ukuaji huo unatokana na kuimarika kwa biashara ya ununuzi wa silaha za kijeshi. Nchi ya **Brazil** kasi ya ukuaji wa uchumi imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 2.9 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 3.0 mwaka 2022. Ukuaji huo umechochewa na kuongezeka kwa mahitaji ya ndani yaliyopelekea kuongezeka kwa upatikanaji wa ajira na uwekezaji, *(Mchoro Namba 1)*

**Mchoro Nam 1: Ukuaji wa Uchumi wa Dunia, nchi Zilizoendelea na Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi 2022-2023**




***Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia, 2024***

### 1.4 Hali ya Uchumi wa Bara la Afrika

#### 1.4.1 Uchumi wa Afrika

Uchumi wa Bara la Afrika umekuwa kwa kasi ya wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022. Kwa Kanda ya Kaskazini mwa Bara la Afrika, uchumi umefikia wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2022; Kanda ya Kusini imefikia wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2022; Kanda ya Afrika Mashariki umefikia wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2022. Kanda ya Afrika ya Kati imefikia wastani wa asilimia 3.8 kutoka wastani wa asilimia 5.0 na kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ukuaji wa uchumi umefikia wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2023 kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2022. Kwa nchi za Afrika ya Kati kasi ya ukuaji imefikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2022. Kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi katika bara hili, imetokana na kuongezeka kwa gharama za uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi na kuyumba kwa sekta za kifedha pamoja na kupunguwa kwa usafirishaji wa mazao ya kilimo, Biashara na uzalishaji na uuzaji wa mafuta ghafi na madini, *(Jadweli namba 1)*.

**Jadweli Nam 1: Ukuaji Halisi wa Uchumi kwa Kanda za Afrika**

| KANDA ZA AFRIKA | UKUAJI HALISI (ASILIMIA) | |
|---|---|---|
| | **2022** | **2023** |
| Afrika | 3.8 | 3.5 |
| Kanda ya Kaskazini | 4.6 | 3.9 |
| Kanda ya Kusini | 2.8 | 1.6 |
| Kanda ya Magharibi | 3.9 | 3.2 |
| Kanda ya Mashariki | 5.0 | 5.1 |
| Kanda ya Kati | 5.2 | 3.8 |

***Chanzo: Hali Halisi na Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika, (AfDB) 2024***

**Kwa mwaka 2023, miongoni mwa nchi za Afrika ambazo uchumi wake ulikuwa kwa Kasi Kubwa ni;**

**(a) Mozambique**

Kwa mwaka 2023, kasi ya ukuaji uchumi wa nchi hii umekua kwa wastani wa asilimia 7.0 kutoka wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2022. Hali hii imetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa gesi asilia (Liquefied natural gas (LNG)) katika mradi wa Coral South pamoja na kuboreshwa kwa usalama katika maeneo ya Kaskazini mwa nchi hiyo.

**(b) Djibouti**

Mwaka 2023, kasi ya ukuaji uchumi wa nchi hii, imefikia wastani wa asilimia 5.0 kutoka wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2022. Hii imetokana na kukua kwa biashara kupitia Bandari ya kisasa iliyojengwa nchini humo.

**(c) Guinea**

Ukuaji wa uchumi wa nchi hii ulifikia wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2022. Kasi hii ya ukuaji imetokana na kuchochewa na uzalishaji wa madini, upatikanaji wa nishati, na uwekezaji wa miundombinu.

**Kwa mwaka 2023, miongoni mwa nchi za Afrika zilizokuwa na Kasi Ndogo ya Ukuaji wa Uchumi ni:**

**(a) Niger**

Kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi hii imepungua na kufikia wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 11.9 mwaka 2022. Kutokana na athari za migogoro ya kisiasa, pamoja na vikwanzo vya kibiashara vya ECOWAS na kufungwa kwa mipaka iliyopelekea kupungua kwa mauzo ya nje na kuchelewesha usafirishaji wa mafuta kupitia bomba jipya.

**(b) Sudani**


Uchumi wa nchi ya Sudani umekua kwa kasi ndogo ya wastani wa asilimia hasi ya 0.1 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia hasi ya 5.2 mwaka 2022. Hali hii

imetokana na kukosekana kwa utulivu wa kisiasa ambao umepelekea mdororo wa kiuchumi (economic recession) na ukosefu wa akiba za fedha za kigeni.

**(c) Namibia**

Uchumi wa nchi hii umefikia wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2022. Hii imetokana na kupungua kwa shughuli za usindikaji na mauzo ya almasi, na kupungua kwa biashara ya jumla na rejareja na shughuli za utalii, (Mchoro namba 2)

**Mchoro Nam 2: Wastani wa Kasi ya Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za Afrika mwaka (2019-2023)**




***Chanzo: Uchumi wa Afrika, (AfDB) 2024***

### 1.4.2 Uchumi wa Nchi za Visiwa Vilivyo Barani Afrika

Uchumi wa nchi za Visiwa Barani Afrika umefikia wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 6.0 mwaka 2022. Hii inatokana na kuyumba kwa sekta za huduma, kuongezeka kwa gharama za maisha, na kuzorota kwa sekta ya utalii na kupunguwa kwa mauzo ya nje. Miongoni mwa visiwa hivyo ni:

**a. Visiwa vya Seychelles**

Kwa mwaka 2023, kasi ya ukuaji uchumi wa visiwa vya Seychelles imepungua kufikia wastani wa asilimia 4.2 kutoka wastani wa asilimia 8.9 mwaka 2022. Upungufu huu umetokana na kuyumba kwa sekta za huduma ikiwemo uingiaji wa watalii, sekta ya uchumi wa Buluu na kupelekea kupungua kwa upatikanaji wa fedha za kigeni.

**b. Visiwa vya Mauritius**

Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi ya Mauritius imepungua kufikia wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 8.7 mwaka 2022. Kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kumesababisha kuongezeka kwa gharama za maisha katika visiwa hivi.

**c. Visiwa vya Comoro**

Mwaka 2023, uchumi wa visiwa vya Comoro umekua na kufikia wastani wa asilimia 3.0 kutoka wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2022. Hii imetokana na kuimarika kwa shughuli za huduma na kilimo na kuongezeka kwa usambazaji wa mahitaji ya matumizi ya Kaya.

**d. Madagascar**

Kasi ya ukuaji uchumi kwa nchi ya Madagascar imekua kwa kasi ndogo ya wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2022. Hii imechangiwa na kudorora kwa uchimbaji madini, mawe na kupungua sekta ya utalii pamoja na usafirishaji.

### 1.4.3 Uchumi wa baadhi ya Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara

Mwaka 2023, kasi ya ukuaji uchumi katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara imepungua kufikia wastani wa asilimia 3.4 kutoka wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2022. Upungufu huu umetokana na uhaba wa fedha za kigeni na kuongezeka kwa gharama za kukopa pamoja na kupungua kwa uwezo wa kulipa madeni.

**(a) Nchi ya Zimbambwe**

Kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi kwa nchi ya Zimbabwe imefikia wastani wa asilimia 5.3 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2022. Hii ni kutokana na kupungua kwa uzalishaji katika sekta ya kilimo na usafirishaji wa madini.

**b) Nchi ya Burkina Faso**

Kwa nchi ya Burkina Faso, kasi ya ukuaji wa uchumi imekua na kufikia wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 1.5 mwaka 2022. Kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji na kuimarika kwa hali ya usalama.

**(c) Nchi ya Sierra Leone**

Kwa mwaka 2023, ukuaji wa uchumi wa Sierra Leone umefikia wastani wa asilimia 3.4 kutoka wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2022. Kutokana na kupungua uzalishaji kwa sekta ya madini, kilimo, viwanda, ujenzi na utalii, *(Jadweli Namba 2)*.

**Jadweli Nam 2: Mwenendo wa Uchumi kwa Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa kipindi cha miaka miwili (2022 na 2023), (asilimia)**

| Nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara | 2022 | 2023 |
|---|---|---|
| **Nchi zinazozalisha Mafuta** | | |
| Angola | 3.0 | 0.5 |
| Cameroon | 3.6 | 4.0 |
| Chad | 3.1 | 4.4 |
| Gabon | 3.0 | 2.3 |
| **Nchi zenye kipato cha kati** | | |
| Jamhuri ya watu wa kongo | | |
| Kenya | 4.8 | 5.0 |
| Nigeria | 3.3 | 2.9 |
| Tanzania | 4.7 | 5.2 |
| Namibia | 4.6 | 3.2 |
| Rwanda | 8.2 | 6.9 |
| **Nchi zenye kipato cha chini** | | |
| Ethiopia | 6.4 | 7.2 |
| Zambia | 5.2 | 4.3 |
| Burundi | 1.8 | 2.7 |
| Malawi | 0.8 | 1.6 |
| Uganda | 6.3 | 4.8 |
| Bukina Faso | 1.8 | 3.6 |

***Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia, 2024***

### 1.4.4 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 5.3 mwaka 2023, kutoka wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2022. Ukuaji huo umetokana na kuongezeka kwa uwekezaji wa miundombinu kupitia sekta binafsi pamoja na kuimarika kwa shughuli za kitalii kwa baadhi ya nchi za ukanda huo zikiwemo Kenya na Tanzania.

**(a) Tanzania**

Uchumi wa Tanzania umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2022. Ukuaji huo umetokana na hatua zinazochukuliwa na Serikali ikiwemo utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na athari za vita; utoaji wa ruzuku ya mbolea na mafuta ya petrol pamoja na uwekezaji wa kimkakati wa Serikali katika miundombinu ya nishati, huduma za kijamii na usafirishaji. Vile vile, kuongezeka kwa uzalishaji wa madini na kuimarika kwa sekta ya utalii.

**(b) Kenya**

Ukuaji wa uchumi wa nchi hii umefikia wastani wa asilimia 5.5 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 4.8 mwaka 2022. Ukuaji huo umetokana na kuimarika kwa sekta ya Kilimo na sekta ya Huduma, kuimarika kwa sekta ya Utalii pamoja na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi na kuimarika kwa shughuli za uzalishaji na usindikaji wa mazao ya Kilimo.

**(c) Uganda**

Kasi ya ukuaji uchumi kwa nchi ya Uganda imepungua na kufikia wastani wa asilimia 4.8 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 6.4 mwaka 2022. Kutokana na kupungua kwa uzalishaji na usafirishaji wa mazao ya biashara kwa baadhi ya Mikoa na kupungua kwa misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**(d) Rwanda**

Kwa mwaka 2023, uchumi wa Rwanda umefikia wastani wa asilimia 6.9 kutoka wastani wa asilimia 8.2 mwaka 2022. Kasi hii ndogo ya uchumi imetokana na changamoto ya mafuriko yaliyoharibu mazao ya kilimo na miundombinu.

**(e) Burundi**

Uchumi wa Burundi umefikia wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 1.8 mwaka 2022. Ukuaji huo umechangiwa na hali ya hewa nzuri na kuimarika kwa uwekezaji umma na binafsi.


**(f) Sudani ya Kusini**

Uchumi wa nchi ya Sudani ya Kusini umeendelea kukuwa kwa asilimia hasi ya 0.1 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia hasi ya 0.5 mwaka 2022. Hali hii imetokana na kuongezeka kwa sekta ya uzalishaji wa mafuta ghafi na kupunguwa kwa migogoro ya ndani ya kisiasa kwa nchi hii.

**(g) Jamhuri ya Demokrasia ya Congo**

Kwa mwaka 2023, uchumi wa nchi hii umekuwa kufikia wastani wa asilimia 6.1 kutoka wastani wa asilimia 8.8 mwaka 2022. Ukuaji huo umetokana na kupunguwa kwa uzalishaji kupitia sekta ya kilimo na kupungua kwa uwekezaji binafsi na mauzo ya nje, ***(Mchoro Namba 3).***

**Mchoro Nam 3: Kasi ya Ukuaji wa Uchumi kwa nchi za Afrika Mashariki 2022 na 2023, (asilimia)**




***Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia, 2024.***

### 1.4.5 Nchi zenye uhusiano wa kibiashara na Zanzibar (Zanzibar Trading Partners)

Zanzibar ina mahusiano ya karibu zaidi ya kibiashara na nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), India na China. Hii ni kutokana na historia ya uhusiano wa muda mrefu na eneo la Zanzibar kijiografia. Kukua na kupungua kwa uchumi wa nchi hizo kunapelekea athari kwa maendeleo ya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar. Kwa mwaka 2023 kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi hizi imepanda na kufikia wastani wa asilimia 5.2 kutoka ukuaji wasilimia 4.5 mwaka 2022.

**a) India,**

Kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 7.8 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2022. Ukuaji huo umetokana na kuendelea kuongezeka kwa Mauzo ya huduma pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji wa umma.

**b) China**

Kwa mwaka 2023 kasi ya ukuaji wa uchumi ilifikia wastani wa asilimia 5.2 kutoka wastani wa asilimia 3.0 mwaka 2022. Hii imetokana na kuimarika kwa uwekezaji viwandani na kuimarika kwa miundombinu.

**c) Jumuiya ya Nchi za Falme za Kiarabu (U.A.E)**

Kwa upande wa nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu kasi ya ukuaji uchumi imefikia wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 7.9 mwaka 2022. Kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi imetokana na kupungua kwa uzalishaji wa mafuta kwa wanachama wa OPEC na kushuka kwa bei ya mafuta ghafi katika soko la dunia.

## 1.5 Hali ya Mfumko wa Bei


### 1.5.1 Mfumko wa Bei wa Dunia

Kasi ya mfumko wa bei duniani kwa mwaka 2023 imefikia wastani wa asilimia 6.8 kutoka wastani wa asilimia 8.7 mwaka 2022. Upungufu huo umetokana na kuimarishwa kwa sera za kifedha na kupungua kwa bei za bidhaa na huduma katika soko la Dunia.

Kasi ya mfumko wa bei kwa Nchi Zilizoendelea imepunguwa kwa wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 7.3 mwaka 2022. Nchi **Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi** imefikia wastani wa asilimia 8.3

mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 9.8 mwaka 2022. Kupungua kwa mfumuko wa bei kumetokana na kupunguwa kwa bei za chakula na bidhaa za viwandani hasa kwa nchi ya China. *(Mchoro namba 4)*

**Mchoro Nam 4: Mfumko wa Bei wa Dunia mwaka (2019-2023), (Asilimia)**





***Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia, 2024***

### 1.5.2 Mfumko wa Bei kwa Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara

Kasi ya mfumko wa bei katika ukanda wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 16.2 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 13.8 mwaka 2022. Ongezeko hili limesababishwa na kupanda kwa bei za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje na kuongezeka kwa mikopo yenye riba kubwa. *(mchoro namba 5).*

**Mchoro Nam 5: Kasi ya mfumko wa bei katika Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa kipindi cha miaka mitano (2019-2023)**




***Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia, 2024.***

### 1.5.3 Mfumko wa bei wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Kasi ya mfumko wa bei kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 11.6 mwaka 2023, kutoka wastani wa asilimia 10.4 mwaka 2022. Hii imesababishwa na kupanda kwa bei za bidhaa za chakula na zisizo za chakula, vipindi vidogo vya mvua na ukame kwa baadhi ya maeneo ya nchi za Afrika Mashariki. *(Mchoro namba 6).*

#### (a) Tanzania

Kasi ya mfumko wa bei kwa nchi ya Tanzania mwaka 2023 umefikia wastani wa asilimia 4.0 ukilinganishwa na wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2022. Kupunguwa kwa mfumko wa bei kumesababishwa na kupunguwa kwa bei kwa baadhi ya bidhaa za vyakula kama vile mchele, samaki, Dagaa na matunda.

#### (b) Kenya

Mwaka 2023, mfumko wa bei kwa nchi ya Kenya umefikia wastani wa asilimia 7.7 kutoka wastani wa asilimia 7.6 mwaka 2022. Kupanda kwa mfumko wa bei kumetokana na athari ya migogoro ya kisiasa kulikopelekea upungufu wa bidhaa kutokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji.

**(c) Uganda**

Mfumko wa bei umefikia wastani wa asilimia 5.4 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 7.2 mwaka 2022. Upungufu huo umetokana na kupunguwa kwa bei za huduma za usafirishaji wa abiria kwa asilimia hasi 7.0, pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya ndizi ambazo ndio chakula kikuu nchini humo.

**(d) Rwanda**

Mwaka 2023, mfumko wa bei wa nchi hii umeongezeka kidogo kufikia wastani wa asilimia 14.0 kutoka wastani wa asilimia 13.9 mwaka 2022. Mfumko huo umechangiwa na kuongezeka kwa bei za vyakula kutokana na uzalishaji mdogo wa ndani uliosababishwa na hali mbaya ya hewa, pamoja na kuongezeka kwa bei ya nishati ya mafuta na mbolea.

**(e) Burundi**

Kwa nchi ya ya Burundi kasi ya mfumko wa bei imeongezeka kwa wastani wa asilimia 27.0 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 18.9 mwaka 2022. Hii ni kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa za vyakula ikiwemo mafuta ya kula.


**(e) Sudani ya Kusini**

Mfumko wa bei umefikia wastani wa asilimia 40.2 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia -3.2 mwaka 2022. Hii imetokana na kushuka kwa thamani ya Pauni ya Sudani na kuongezeka kwa gharama za bidhaa kutoka nje.

**(f) Jamhuri ya Demokrasia ya Congo**

Mwaka 2023, mfumko wa bei wa Jamhuri ya Demokrasia ya Congo umeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 19.9 kutoka wastani wa asilimia 9.3 mwaka 2022. Hali hii imetokana na kupunguwa kwa uzalishaji katika sekta ya kilimo, kuongezeka kwa bei za bidhaa zinazoagizwa nje ya nchi na kushuka kwa viwango vya ubadilishaji wa fedha. *(Mchoro namba 6)*

**Mchoro Nam 6: Kasi ya Mfumko wa Bei kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (2022-2023) , (%)**




*Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia, 2024*

### 1.5.4 Mfumko wa bei kwa Nchi zenye uhusiano wa kibiashara na Zanzibar (Zanzibar Trading Partners)

Zanzibar ina mashirikiano zaidi ya kibiashara na nchi za India, China na Umoja wa Falme za Kiarabu (U.A.E), ambapo bidhaa zinazotumika Zanzibar zinapatikana katika masoko ya nchi hizi. Kupanda na kushuka kwa kasi ya mfumko wa bei una athari ya moja kwa moja na mfumko wa bei wa Zanzibar. Kwa mwaka 2023 hali ya mfumko wa bei imekuwa kama ifuatavyo:

#### (a) India

Kwa mwaka 2023, kasi ya mfumko wa bei wa India imepungua na kufikia wastani wa asilimia 5.4 kutoka wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2022. Upungufu huo umetokana na kupungua kwa viwango vya riba katika sekta za uzalishaji na kupelekea kushuka kwa mfumko wa bei.


#### (b) Jumuiya ya Nchi za Falme za Kiarabu (U.A.E)

Kasi ya mfumko wa bei kwa nchi za UAE imeshuka na kufikia wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia hasi 4.8 mwaka 2022. Hii imetokana na kupunguwa kwa bei za bidhaa za chakula na zisizo za chakula zinazoagizwa kutoka nje ya Jumuia hii.

**(c) China**

Kasi ya mfumko wa bei imeshuka na kufikia wastani wa asilimia 0.2 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 2.0 mwaka 2022. Hii ni kutokana na kushuka kwa usafirishaji kwa bidhaa nje na kupunguwa kwa bei za bidhaa katika maeneo ya utalii na burudani. *(Mchoro namba 7)*

**Mchoro Nam 7: Mfumko wa Bei kwa Nchi zenye Uhusiano wa karibu wa Kibiashara na Zanzibar (Trading Partners) 2022-2023, (asilimia)**




***Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia, 2024***

### 1.5.5 Mwenendo wa Bei kwa baadhi ya bidhaa katika Soko la Dunia

Changamoto mbalimbali zinazojitokeza Duniani zikiwemo Migogoro ya kisiasa na vita vinavyooendelea baina ya Urusi na Ukraine na Israel na Palesitina vinapelekea kuathiri usambazaji wa bidhaa za vyakula na visizo za vyakula katika soko la duniani na kupelekea kupanda kwa bei za bidhaa muhimu. Kwa mwaka 2023 bei za bidhaa zenye matumizi makubwa na zinazouzwa zaidi katika soko la dunia ni kama ifuatavyo:

**i. Nishati ya Mafuta**

Bei ya nishati za mafuta kwa mwaka 2023 ilifikia wastani wa Dola za Kimarekani 97.1 kwa pipa kutoka Dola za Kimarekani 80.8 kwa pipa mwaka 2022. Sawa na ongezeko la asilimia 17.6. Kutokana na kuongezeka kwa gharama za usafishaji na usambazaji wa mali ghafi na mafuta.

**ii. Mchele**

Bei ya mchele kwa mwaka 2023 imepanda na kufikia Dola za Kimarekani 553.7 kwa tani ikilinganishwa na Dola za Kimarekani 436.8 kwa tani mwaka 2022. Sawa na ongezeko la asilimia 26.7. Hii ni kutokana kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa hiyo pamoja na athari za El Niño zilizotokea nchini india.

**iii. Unga wa Ngano**

Katika mwaka 2023, bei ya unga wa ngano katika soko la dunia ilishuka na kufikia wastani wa Dola za Kimarekani 257.7 kwa tani ikilinganishwa na wastani wa Dola za Kimarekani 381.9 kwa tani mwaka 2022. Sawa na upungufu wa asilimia 32.5. Hii ni kutokana kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usambazaji wa ngano kutokana na kupungua kwa mapigano kwa nchi za Urusi na Ukraine.

**iv. Sukari**

Katika mwaka 2023, bei ya sukari katika soko la dunia imeongezeka na kufikia wastani wa Dola za kimarekani 520.0 kwa tani ikilinganishwa na wastani wa Dola za Kimarekani 410.0 kwa tani mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 26.8. Ongezeko hilo limetokana na mabadiliko ya hali ya hewa na motokeo ya El Nino yalitokea barani Asia yaliyopelekea uharibifu wa zao la miwa. Vile vile, wazalishaji wengine kama vile India walitumia bidhaa ya miwa katika kuzalisha "biofuel"gesi mbadala wa nishati ya mafuta baada ya uhitaji wa gesi kuongezeka. (*Jadweli namba 3)*.

**Jadweli Nam 3: Mwenendo wa Bei kwa baadhi ya Bidhaa katika Soko la Dunia**

| BIDHAA | KIPIMO | 2022 (usd) | 2023 (usd) | Tofauti (usd) |
|---|---|---|---|---|
| Mchele | Tani | 436.8 | 553.7 | 26.7 |
| Unga wa ngano | Tani | 381.9 | 257.7 | 32.5 |
| Sukari | Tani | 410.0 | 520.0 | 26.8 |
| Nishati ya Mafuta | Pipa | 80.8 | 97.1 | 17.6 |

***Chanzo: Takwimu za Bidhaa za Dunia 2024***


# SURA YA PILI

## 2.0 HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR

### 2.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi

Kuimarika kwa shughuli za kiuchumi kumepelekea kuongezeka kwa Pato halisi la Taifa (GDP at constant price) kufikia thamani ya TZS 3,758.8 bilioni mwaka 2023 kutoka thamani ya TZS 3,499.0 bilioni mwaka 2022. Aidha, Pato la Taifa kwa bei ya soko (GDP at current price) imeongezeka na kufikia thamani ya TZS 6,041.3 bilioni mwaka 2023 kutoka thamani ya TZS 5,400.3 bilioni mwaka 2022. Kwa mujibu wa takwimu hizo uchumi wa Zanzibar umeendelea kuwa imarika na kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 7.4 mwaka 2023 ukilinganisha na wastani wa asilimia 6.8 mwaka 2022, (Mchoro namba 8)

**Mchoro Nam 8: Kasi ya Ukuaji wa Uchumi mwaka (2019-2023)**




***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na kijamii Zanzibar, 2024.***

Kuongezeka kwa Pato la Taifa na kasi ya ukuaji wa uchumi kumetokana na mambo yafuatayo:-

i. Kuimarika kwa Sekta ya Huduma, kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 9.9 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 7.7 mwaka 2022. Ukuaji huu umetokana na ukuaji wa Sekta ndogo ya Biashara kwa asilimia

12.6, shughuli za Fedha na Bima kufikia asilimia 54.6, Huduma za Utawala na usaidizi kufikia asilimia 17.0, Sanaa, Burudani na Ubunifu kufikia asilimia 33.8 na Usafiri na uhifadhi kwa asilimia 9.2;

ii. Kuongezeka kwa watalii waliotembelea Zanzibar kufikia watalii 638,498 mwaka 2023 kutoka watalii 548,503 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 16.4. Kati ya mwezi wa Julai 2022 mpaka Juni 2023, Mapato yatokanayo na utalii yaliyorikodiwa katika mifumo ya Serikali yamefikia TZS 59.74 bilioni ukilinganisha na TZS 51.32 bilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2021/2022;

iii. Kuongezeka kwa thamani ya mazao ya biashara yaliyosafirishwa nje ya nchi. Mwani wenye thamani ya TZS 19,233.2 milioni mwaka 2023 kutoka TZS 16,010.2 milioni mwaka 2022 ulisafirishwa na Mauzo ya Karafuu zenye thamani TZS 47,081.1 milioni mwaka 2023;

iv. Kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji kufikia miradi 114 yenye thamani ya TZS 4,646 milioni mwaka 2023 kutoka miradi 93 yenye thamani ya TZS 4,550 milioni mwaka 2022;


v. Kuimarika kwa miundombinu ya barabara, kiasi cha kilomita 946.85 za barabara zimejengwa kwa kiwango cha lami nchini;

vi. Kuongezeka kwa mapato ya ndani kufikia TZS 1,075.9 bilioni mwaka 2023/2024 sawa na asilimia 98 ya makadirio ukilinganisha na jumla ya TZS 801.4 bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023.

## 2.2 Pato la Mwananchi

Kufikia mwaka 2023 Zanzibar inakadiriwa kuwa na watu wapatao 1.94 milioni. Pato la mwananchi ni kiwango kinachokadiriwa kukipata mwananchi kwa mwaka. Kiwango hicho hukisiwa kwa kugawanywa Pato la Taifa na idadi ya watu. Kuongezeka kwa Pato la Taifa Zanzibar kumepelekea kuongezeka kwa kipato cha Mwananchi. Kwa mwaka 2023 Pato la Mwananchi limeongezeka kufikia TZS 3.1 milioni sawa na Dola za Kimarekani 1,241 kutoka TZS 2.8 milioni sawa na Dola za Kimarekani 1,235 mwaka 2022. *(Mchoro namba 9).*

**Mchoro Nam 9: Idadi ya Watu Pamoja na Pato la Mwananchi kwa Thamani ya (TZS) na (USD) (2019 - 2023)**





| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Pato la mwananchi ('000 TZS) | 2,551 | 2,526 | 2,704 | 2,859 | 3,111 |
| Pato la mwananchi (USD) | 1,115 | 1,099 | 1,171 | 1,235 | 1,241 |
| Idadi ya watu(Milioni) | 1,621 | 1,666 | 1,713 | 1,889 | 1,941 |

**Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na kijamii Zanzibar, 2024.**

## 2.3 Mwenendo wa Mfumko wa Bei Zanzibar

Kasi ya mfumko wa bei kwa mwaka 2023 imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 6.9 kutoka wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2022. Kuongezeka kwa kasi ya mfumko wa bei kumetokana na ongezeko la bei za bidhaa za chakula zikiwemo mchele, sukari na unga wa ngano kufikia wastani wa asilimia 11.1 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 6.0 mwaka 2022, na bidhaa zisizo za chakula zikiwemo bidhaa za nishati ya mafuta kufikia wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2022. *(Mchoro namba 10)*.

**Mchoro Nam 10: Kasi ya mfumko wa Bei wa Zanzibar (2019-2023)**




***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024***

Serikali imechukua na inaendelea kuchukua hatua za kupunguza na kudhibiti kasi ya mfumko wa bei na kuhakikisha upatikanaji wa huduma na bidhaa muhimu kwa wananchi. Hatua zilizochukuliwa ni kama ifuatavyo:-


i. Kuendelea kutoa bei elekezi na kusimamia bidhaa zinazoingia nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi;
ii. Kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inaendelea kufuatilia na kuchukua hatua za kudhibiti, kushuka kwa thamani kwa sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine duniani;
iii. Kuimarisha ufanisi wa Bandari ya Malindi kwa ununuzi wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya kupunguza muda wa kutoa mizigo bandarini; na
iv. Serikali kuimarisha maghala na mifumo ya uhifadhi wa chakula ili kuwa na uhakika wa chakula nchini sambamba na kuendelea kutoa na kusimamia utoaji wa ruzuku.

### 2.4 Mwendendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani

Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani imepunguwa thamani kwa wastani wa asilimia 8.2 kufikia wastani wa TZS 2,506.0 kwa dola moja mwaka 2023 ikilinganishwa na TZS 2,315 kwa dola moja mwaka 2022. Hii ni kutokana na kuendelea kupanda kwa uhitaji wa dola na kupunguwa

kwa mzunguko wa fedha za kigeni ndani na nje ya nchi.  Hata hivyo, hali ya upatikanaji wa fedha za kigeni nchini imeendelea kuwa himilivu. Uhimilivu huo unatokana na kuendelea kuwepo kwa akiba ya fedha za kigeni, ambapo hadi kufikia mwezi Disemba 2023, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani TZS 5.5 bilioni, ambayo inatosheleza miezi minne na nusu ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje.

**Mchoro Nam 11: Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola moja ya Kimarekani 2019-2023**




*Chanzo: Bank Kuu ya Tanzania, 2024*

## 2. 5 Mwenendo wa Uingiaji wa Watalii Zanzibar


Utalii ni sekta kiongozi kwa uchumi wa Zanzibar ambayo inasababisha ukuaji wa sekta nyengine na kuongeza fedha za kigeni. Inakadiriwa kuchangia asilimia zaidi ya 29.4 ya Pato la Taifa. Kwa mwaka 2022, idadi ya watalii waliongia kupitia kiwanja cha ndege na bandari ya Zanzibar imeongezeka kwa asilimia 16.4 wamefikia watalii 638,489 kutoka watalii 548,503 mwaka 2022. (Mchoro namba 12).

**Ongezeko hilo limesababishwa na:**

i. Juhudi zinazochukuliwa na Serikali za kuitangaza Zanzibar Kimataifa;
ii. Kuongezeka kwa mawakala wa usafirishaji watalii pamoja na kuitangaza Zanzibar kiutalii kupitia maonesho ya nje na ndani ya nchi;

iii. Kushiriki katika makongamano ya kibiashara na uwekezaji katika Mataifa mbali mbali duniani;
iv. Mabalozi wa Tanzania nje ya nchi kuendelea kuutangaza utalii;
v. Kufunguliwa kwa hoteli za nyota tano zenye uwezo wa kutoa huduma kwa watalii wa kipato cha juu;
vi. Kuendelea kuwa na Mashirika ya ndege yanayofanya safari za moja kwa moja Zanzibar yakiwemo Polish Airline, Azur Airline, Inter Airline, Eurowings Discover Airline, Airfrance Airline na Edelweiss Airline;
vii. Kuendelea kuimarika kwa hali ya amani na utulivu nchini.

**Mchoro Nam 12: Mwenendo wa Uingiaji wa Watalii Zanzibar (2019-2023)**




***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na kijamii Zanzibar, 2024.***

Nchi ambazo zimeongoza kwa kuleta watalii wengi mwaka 2023 ni **Ulaya** watalii 87,419 sawa na ongezeko la asilimia 13.7 ikifuatiwa na **Ufaransa** watalii 68,079 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 10.7; **Itali** watalii 67,584 sawa na ongezeko la asilimia 10.6; **Ujerumani** watalii 57,178 sawa na ongezeko la asilimia 8.9; Poland watalii 46,289 sawa na ongezeko la asilimia 7.2; **Uingereza** watalii 38,628 sawa na ongezeko la asilimia 6.0 na **Afrika** watalii 38,039 sawa na ongezeko la asilimia 5.9.

## 2.6 Ukuaji wa Sekta katika Pato la Taifa

### 2.6.1 Sekta ya Huduma

Sekta ya huduma inajumuisha sekta ndogo za Elimu, Chakula na Vinywaji, Afya, Mawasiliano, Malazi, Sanaa, Burudani na Ubunifu, na nyenginezo. Sekta hii ni sekta mhimili katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar. Sekta ya huduma imekua na kufikia wastani wa asilimia 9.9 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 7.7 mwaka 2022. Ukuaji huo umesababishwa na kukuwa kwa:

i. Sekta ndogo ya Fedha na Bima kufikia wastani wa asilimia 54.6 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2022 hali hii imesababishwa na kuboreshwa kwa sera ya fedha, mifumo ya kisheria na udhibiti na kuimarisha huduma za kifedha.

ii. Sekta ndogo ya Sanaa, Burudani na Ubunifu imekua na kufikia wastani wa asilimia 33.8 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 1.9 mwaka 2022 ukuaji huo umesababishwa na kuwepo kwa programu ya elimu kwa wasanii na wadau wa Sanaa kuhusiana na nafasi ya Sanaa katika jamii, kuwahamasisha na kuwashajihisha wasanii kupitia mikutano ya wadau wa Sanaa juu ya namana bora ya kuwatumia wasanii, kufanya kaguzi za mara kwa mara kwa ajili ya kushajihisha jamii juu ya utekelezaji mzuri wa Sheria na Kanuni za Sanaa, kuimarisha mahusiano kati ya baraza na wamiliki wa maeneo yanayofanya shughuli za Sanaa ili kuendeleza na kukuza Sanaa zetu pamoja na ushiriki wa baraza la Sanaa katika warsha, matamasha na mikutano ya kimataifa kumesaidia kuongeza wigo katika namna bora ya kusimamia na kuendesha shughuli za Sanaa nchini.


iii. Sekta ndogo ya Huduma za Utawala imekua kwa wastani wa asilimia 17.0 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia hasi 1.5 mwaka 2022. Sekta ndogo ya Ustawi wa afya ya jamii imekuwa na kufikia wastani wa asilimia 15.8 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 8.9 mwaka 2022 ,ukuaji huo umesababishwa na jitihada za makusudi za Serikali katika kuboresha miundo mbinu ya afya na vifaa tiba .

iv. Sekta ndogo ya Biashara na Ukarabati imekua na kufikia wastani wa asilimia 12.6 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2022 hali hii imetokana na juhudi za Serikali kuimarisha fursa za biashara nchini na uwekezaji kupitia sekta zake kama vile: Wizara ya Biashara,

ZIPA kwa kupitia kupitia programu ya kituo cha pamoja cha utoaji wa huduma.(One stop centre) .

vi. Sekta ndogo ya huduma ya chakula na vinywaji kwa mwaka 2023 imekua na kufikia wastani waasilimia 9.8 kutoka wastani wa asilimia 9.0 mwaka 2022 ukuaji huo umesababishwa na kuimarika kwa shughuli za kitalii na biashara nchini . sekta ndogo ya Usafirishaji na Uhifadhi imekua na kufikia wastani wa asilimia 9.2 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022, sekta ndogo ya Taaluma ya Sayansi na Ufundi kwa mwaka 2023 imekua na kufikia wastani wa asilimia 3.5 kutoka wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2022, *(Mchoro Namba 13)*

**Mchoro Nam 13: Ukuaji wa Sekta ya Huduma katika Pato la Taifa (%) (2019 -2023)**




| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Fedha na Bima | 2.8 | 2.2 | 9.9 | 3.7 | 54.6 |
| Sanaa ,burudani na Ubunifu | 3.3 | -4.9 | 1.1 | 1.9 | 33.8 |
| Huduma za Utawala | 6.9 | -4.6 | 6.6 | -1.5 | 17 |
| Ustawi wa afya ya jamii | 2.5 | 1.4 | 2.4 | 8.9 | 15.8 |
| Biashara na Ukarabati | 9.2 | 7.4 | 14.9 | 4.2 | 12.6 |

Fedha na Bima   Sanaa ,burudani na Ubunifu   Huduma za Utawala
Ustawi wa afya ya jamii   Biashara na Ukarabati


***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na kijamii Zanzibar, 2024.***

## 2.6.2 Sekta ya Viwanda

Sekta ya Viwanda imejumuisha sekta ndogo ya Uzalishaji Viwandani, Ujenzi, Uchimbaji Mawe na Mchanga, Umeme na Gesi, na nyenginezo. Mwaka 2023, sekta ya viwanda imekua kwa kasi ndogo na kufikia wastani wa asilimia 6.6 kutoka wastani wa asilimia 9.3 mwaka 2022. Upungufu huu umesababishwa na kupunguwa kwa sekta ndogo ya umeme na gesi kwa mwaka 2023 kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 12.4 kutoka wastani wa asilimia 22.3 mwaka

2022. Sekta ndogo ya Ujenzi imepungua kasi ya ukuaji na kufikia wastani wa asilimia 5.5 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 10.2 mwaka 2022. Hali hii imetokana na kukamilika kwa baadhi ya miradi ikiwemo, skuli, hospitali, masoko na barabara. Sekta ndogo ya Uzalishaji Viwandani kwa mwaka 2023 imefikia ukuaji wa wastani wa asilimia 6.9 kutoka wastani wa asilimia 8.1 mwaka 2022, hali hii imesababishwa kwa kupungua kwa uzalishaji kutokana na kufungwa kwa baadhi ya viwanda ikiwemo viwanda vya maji. Sekta ndogo ya Usambazaji maji safi na maji taka kasi ya ukuaji imepungua kufikia wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2022. Hata hivyo, sekta ndogo ya Uchimbaji mawe na Mchanga kwa mwaka 2023 imekua na kufikia wastani wa asilimia 10.4 kutoka wastani wa asilimia 9.1 mwaka 2022 kutokana na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi na uwekezaji.*(Mchoro Namba 14)*.

***Mchoro Nam 14: Ukuaji wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa (2019-2023)***




| | Umeme na gesi | Ujenzi | Uchimbaji mawe na mchanga | Uzalishaji viwandani | Usambazaji maji safi na maji taka |
|---|---|---|---|---|---|
| 2019 | 5.2 | 3.1 | -1.7 | 20.5 | 12.6 |
| 2020 | -2.8 | 6.5 | -6 | 6.5 | 1.9 |
| 2021 | 8 | 8.9 | 9.9 | 1.1 | 6.9 |
| 2022 | 22.3 | 10.2 | 9.1 | 8.1 | 7 |
| 2023 | 12.4 | 5.5 | 10.4 | 6.9 | 4.6 |

2019 2020 2021 2022 2023

***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, 2024.***

### 2.6.3 Sekta ya Kilimo

Sekta ya Kilimo inajumuisha sekta ndogo za Misitu, Ufugaji, Uvuvi na Mazao. Sekta hii ni muhimu ikiwa ni chanzo cha upatikanaji wa chakula nchini. Kwa mwaka 2023, sekta ya kilimo imekua kwa kasi ndogo na kufikia wastani wa asilimia 2.3 kutoka wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2022. Hali hii imetokana na kupungua kwa ukuaji wa sekta ndogo ya Ufugaji na sekta ndogo ya Mazao, ambapo kwa mwaka 2023 sekta ndogo ya Ufugaji imekua kwa wastani wa asilimia hasi 4.3 kutoka wastani wa asilimia 2.3 mwaka 2022. Upungufu huo umesababishwa na kuzorota kwa shuguli za uzalishaji wa ndani ikiwemo kuku, mayai na maziwa kulikochangiwa na kukosekana kwa malighafi ikiwemo

vifaranga na chakula cha kuku. Aidha, sekta ndogo imefikia ukuaji wa wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2022, upungufu huo umesababishwa na kupungua kwa uzalishaji wa zao la karafuu kutoka tani 4,734.1 za mwaka 2022 hadi kufikia tani 2,654.7 mwaka 2023 ikiwa ni sawa na upungufu wa asilimia 44. Zao la Karafuu ni la msimu, hali hii imetokana na kuwepo kwa msimu mdogo wa uzalishaji na kuzeeka kwa mikarafuu.

Sekta ndogo ya Uvuvi kwa mwaka 2023 imekua na kufikia wastani wa asilimia 8.1 kutoka wastani wa asilimia 3.0 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilima 170, kutokana na wananchi hususan vijana kushajihika katika kujishughulisha na shughuli za uvuvi, ukulima wa mwani, na ufugaji wa mazao mengine ya baharini katika kujipatia ajira na kipato. Sekta ndogo ya Misitu kwa mwaka 2023 imekua na kufikia wastani wa asilimia 6.4 kutoka wastani wa asilimia 2.9 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 120. Hali hii imesababishwa na kuongezeka kwa uvunaji wa bidhaa za misitu kutokana na kukatwa kwa miti kwa ujenzi na kuni pamoja na kupisha miundombinu ya barabara.

## 2.7 Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa


### 2.7.1 Sekta ya huduma

Sekta ya huduma ina mchango mkubwa zaidi katika kukuza Uchumi wa Zanzibar. Mchango wa sekta ya huduma katika Pato la Taifa umeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 46.6 mwaka 2023 kutoka asilimia 46.3 mwaka 2022. Kwa mwaka 2023 sekta ndogo ya Bima na Fedha imechangia kwa wastani wa asilimia 6.2 kutoka wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2022, na sekta ndogo ya Ustawi wa Afya ya jamii kwa mwaka 2023 imechangia wastani wa asilimia 0.9 kutoka 0.7 mwaka 2022. Sekta ambazo mchango wake umepungua kidogo ni ni sekta ndogo ya huduma ya chakula na malazi kwa mwaka 2023 imechangia wastani wa asilimia 15.3 kutoka wastani wa asilimia 15.9 mwaka 2022, sekta ndogo ya Malazi imechangia wastani wa asilimia 12.8 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 13.3 mwaka 2022, sekta ndogo ya Ukodishwaji wa Majengo kwa mwaka 2023 imechangia wastani wa asilimia 7.2 kutoka wastani wa asilimia 7.5 mwaka 2022, sekta ndogo ya biashara na ukarabati imechangia na kufikia wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2022, sekta ndogo ya Utawala kwa mwaka 2023 imechangia wastani wa asilimia 4.5 kutoka wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2022, sekta ndogo ya Usafirishaji na Uhifadhi nayo imechangia wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2022, sekta ndogo ya Elimu imechangia wastani wa asilimia 2.2 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 2.4 mwaka 2022.

### 2.7.2 Sekta ya Viwanda

Kwa mwaka 2023 mchango wa sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa umefikia wastani wa asilimia 20.8 kutoka wastani wa asilimia 19.4 mwaka 2022. Ongezeko hilo limechangiwa zaidi na mchango wa sekta ndogo ya Ujenzi ,ambapo kwa mwaka 2023 sekta hiyo imechangia kwa wastani wa asilimia 10.4 kutoka wastani wa asilimia 8.8 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 1.6, hali hii imetokana na ujenzi wa kazi za maendeleo. Kwa sekta ndogo ya uzalishaji viwandani, mwaka 2023 imechangia kwa wastani wa asilimia 8.0 kutoka wastani wa asilimia 8.1 mwaka 2022, sawa na upungufu wa wastani wa asilimia 0.1. *(Mchoro nambari 15)*

**Mchoro Nam 15: Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa (2019-2023)**




***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024.***

### 2.7.3 Sekta ya Kilimo

Kwa mwaka 2023 mchango wa sekta ya kilimo umepungua na kufikia wastani wa asilimia 24.9 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 25.9 mwaka 2022. Mchango sekta ya kilimo umepungua kidogo kutokana na kupungua kwa sekta ndogo ya Ufugaji ambayo ilichangia wastani wa asilimia 12.8 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 12.9 mwaka 2022. Sekta ndogo ya mazao imechangia wastani wa asilimia 6.9 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.3 mwaka 2022, sekta ndogo ya Uvuvi imechangia wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2022 na sekta ndogo ya Misitu imechangia wastani wa asilimia 1.0 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.1 mwaka 2022.

#### 2.7.4.1 Sekta ndogo ya Mazao

Sekta hii imejumuisha Uzalishaji wa mazao ya Chakula na mazao ya Biashara. Kwa upande wa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2023 ni kama ifuatavyo:-

**a) Zao la Mpunga.**

Zanzibar inalima na kuvuna mpunga wa umwagiliaji maji na mpunga wa kutegemea maji ya mvua. Kwa mwaka 2023 kilimo cha mpunga kwa njia ya kutegemea mvua uzalishaji wake umeongezeka na kufikia tani 29,992.5 zenye thamani ya TZS 32,707.0 milioni kutoka tani 23,683.0 zenye thamani ya TZS 24,069.4 milioni mwaka 2022. Hata hivyo, eneo la uzalishaji wa mpunga wa kutegemea mvua limepungua na kufikia ekari 25,591.3 mwaka 2023 kutoka ekari 26,243.0 mwaka 2022. Hali hii imetokana na baadhi ya maeneo kuendelezwa miundombinu ya umwagiliaji na baadhi ya maeneo ya kutegemea mvua kuwa ya umwagiliaji kwa njia mbadala za uvunaji maji ya mvua.

Kwa upande wa zao la mpunga kwa njia ya umwagiliaji maji, uzalishaji umeongezeka na kufikia tani 7,279.4 zenye thamani ya TZS 9,793.4 milioni mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 4,264.5 zenye thamani ya TZS5,347.1 milioni mwaka 2022. Aidha, eneo la uzalishaji limeongezeka na kufikia ekari 3,928.2 mwaka 2023 kutoka ekari 2,843 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asimilia 38.17. Kwa ujumla, mavuno ya mpunga yameongezeka kutoaka na kuimarika kwa shughuli za umwagiliaji, utoaji wa mbegu himilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuimarika kwa taaluma ya ugani.

**(b) Zao la Muhogo**

Kwa mwaka 2023 uzalishaji wa zao la muhogo umeongezeka na kufikia tani 220,411.8 zenye thamani ya TZS 167,920.0 milioni ikilinganishwa na tani 202,519.5 zenye thamani ya TZS TZS 143,792 milioni kwa mwaka 2022. Hii imetokana na kuongezeka kwa eneo la uzalishaji na kufikia ekari 37,548.9 mwaka 2023 kutoka ekari 34,500.8 mwaka 2022. Ongezeko hili limetokana na kushajihika kwa wakulima kutumia mbegu himilivu zinazostahamili mabadiliko ya tabianchi zilizo fanyiwa utafiti na Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI) kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Tropical (IITA).

**(C) Zao la Ndizi**

Kwa mwaka 2023 uzalishaji wa ndizi umeongezeka na kufikia tani 96,975.8 zenye thamani ya TZS 139,509 milioni kutoka tani 52,337.3 zenye thamani ya TZS 70,169.8 milioni mwaka 2022, hii ni kulikotokana na kuongezeka kwa muamko kwa wakulima juu ya namna bora ya kuongeza maeneo ya uzalishaji wa zao hili kwa kuchanganya na vipando vyengine bila kuathiri mazao hayo. Vile vile, eneo la uzalishaji wa zao la ndizi limeongezeka na kufikia ekari 8,664.4 mwaka 2022 kutoka ekari 6,085.7 mwaka 2022.

**(d) Zao la Viazi Vikuu**

Kwa mwaka 2023 mavuno ya zao la viazi vikuu yameongezeka na kufikia tani 9,241.3 zenye thamani ya TZS 11,003.3 milioni kutoka tani 6,692 zenye kufikia ekari 1,848.3 mwaka 2023 kutoka ekari 1,338.4 mwaka 2022. Hali hii imesababishwa na kuongezeka kwa uhitaji wa zao hilo katika masoko ya ndani na ya Utalii pamoja na kuimarika kwa taaluma ya kilimobiashara kwa wakulima.

**(e) Zao la Njugu Nyasa**

Kwa mwaka 2023 uzalishaji wa zao la njugu nyasa umeongezeka na kufikia tani 698 zenye thamani ya TZS 1,500.2 milioni kutoka tani 624.2 zenye thamani ya TZS 1,250.2 milioni mwaka 2022. Eneo la uzalishaji limeongezeka na kufikia ekari 1,454.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na ekari 1,300.5 mwaka 2022. Ongezeko hilo limetokana na kuwepo kwa fursa za kimasoko kwa zao hilo na kukua kwa taaluma ya lishe bora nchini.

**(e) Mboga mboga za Majani**

Mboga za Majani hujumuisha kilimo cha mazao ya mboga mboga na matunda kama vile matikiti, tungule, matango, mabilingani, bamia, pili pili na nyenginezo za aina hiyo. Mwaka 2023, uzalishaji wa mazao hayo umeongezeka na kufikia tani 87,970.69 kutoka tani 66,303.8 mwaka 2022. Jumla ya ekari 21,379.6 zimetumika katika ulimaji wa mazao hayo mwaka 2023, ikilinganishwa na ekari 17,691.6 mwaka 2022. Ongezeko hilo limetokana na juhudi za Wizara za kuimarisha mbinu za uzalishaji wenye tija zaidi kama vile TANSHEP, zinazo muwezesha mkulima kutumia matokeo ya tafiti katika uzalishaji na kuongezeka kwa masoko ya matunda na mboga mboga. *(Jadweli Namba 4.)*

**Jadweli Nam 4: Eneo la Uzalishaji kwa ekari kwa mazao ya chakula (2019-2023)**

| Zao | Ekari | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** |
| Mpunga | 27,375.0 | 30,412.6 | 25,383.6 | 26,243.0 | 25,591.3 |
| Muhogo | 30,204.3 | 26,995.7 | 30,948.6 | 34,500.8 | 37,548.9 |
| Ndizi | 7,595.5 | 7,772.1 | 7,104.0 | 6,085.7 | 8,664.4 |
| Njugu nyasa | 902.3 | 642.3 | 775.0 | 1,300.5 | 1,454.3 |
| Viazi vikuu | 613.0 | 582.4 | 1,549.3 | 1,338.4 | 1,848.3 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na kijamii Zanzibar, 2024.***

**Jadweli Nam 5: Kiwango na Thamani ya Bidhaa za Chakula Zilizozalishwa (2019-2023) (TZS milioni)**

| Zao | 2019 | | 2020 | | 2021 | | 2022 | | 2023 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamani |
| **Mpunga** | 41,062.4 | 39,288.4 | 35,886.8 | 35,229.0 | 25,511.0 | 25,369.1 | 23,683.0 | 24,069.4 | 29,992.5 | 32,707.0 |
| **Muhogo** | 177,299.2 | 118,513.3 | 158,464.9 | 108,678.0 | 181,668.0 | 126,210.5 | 202,519.5 | 143,792.0 | 220,411.8 | 167,920.0 |
| **Ndizi** | 65,321.2 | 82,448.9 | 66,839.6 | 86,559.0 | 61,094.4 | 80,147.4 | 52,337.3 | 70,169.8 | 96,975.8 | 139,509.0 |
| **Viazi vikuu** | 3,065.0 | 3,202.0 | 2,911.8 | 3,121.0 | 7,746.3 | 8,410.8 | 6,692.0 | 7,425.9 | 9,241.3 | 11,003.3 |
| **Njugu nyasa** | 433.1 | 816.7 | 308.3 | 596.0 | 372.0 | 729.0 | 624.2 | 1,250.2 | 698.0 | 1,500.2 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024.***

### 2.7.5.2 Hatua Zinazoendelea Kuendeleza Kilimo

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imechukua hatua za kuendeleza na kukuza kilimo ili kuongeza uzalishaji na kuongeza upatikanaji wa chakula, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na:-

a) **Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji:** Ujenzi wa misingi ya kumwagilia maji kwa kiwango cha saruji (lining of tertiary canals) yenye jumla ya urefu wa kilomita 35.3 katika mabonde yafuatayo: Chaani, Kibokwa, Cheju A, Kilombero na Mlemele; ujenzi wa eneo la Cheju B sambamba na kazi za uchimbaji wa misingi mikubwa na midogo ya kutolea maji ya ziada (Primary and Tertiary Drainage Canals); Ujenzi wa uzio (fence) katika bwawa la Kinyasini (mita 400) na Chaani (mita 1300). Kufanya tathmini na ukarabati wa vibanda vya pampu katika visima vya Cheju na Kibokwa zimefanyika; na Kufanya mikutano na majadiliano mara 136 (mikutano 71 na wakulima viongozi, mikutano 65 na kulima wa kawaida) kupanga na kujadili maendeleo ya kilimo cha mpunga katika mabonde yote ya Umwagiliaji maji. Aidha kazi ya kutoa mafunzo kwa wakulima 500 (wanaume 218 na wanawake 282) kati ya hao wakiwemo vijana 78 na watu wazima 422 imefanyika. Aidha, malipo ya fidia kwa wananchi 31 katika bonde la Chaani, Kilombero na Mlemele walioathirika wakati wa utekelezaji wa kazi za ujenzi wa miundombinu yamefanyika.

b) **Mfuko wa Pembejeo na Utafiti wa Mbegu kuimarishwa :** Jumla ya mbegu kumi (10) za muhogo zimechaguliwa kati ya hizo mbegu nane (8) mpya, moja iliyoboreshwa (improved) na moja ya kienyeji. Mbegu hizi zilichaguliwa kwa kigezo cha uwezo wa kustahamili mradhi ya michirizi kahawia (Cassava Brown Streak Desease) na Bato Bato, pia mbegu hizo zimetoa mavuno mazuri. Jumla ya aina 66 za mbegu za mpunga kutoka IRRI zilipandwa katika bonde la Kinyasini kwa ajili ya kuzitafiti ubora wake katika ukuaji na uzazi. Jaribio hili limevunwa na kuanza kufanyiwa uchambuzi wa kitaalamu kwa kutumia takwimu zilizokusanywa ili kugundua aina bora za mbegu kati ya hizo 66. Aina 15 za mbegu za kienyeji za mpunga zilipandwa ili kuendeleza kizazi cha mbegu hizo kisipotee kwa ajili ya matumizi ya baadae. Mbegu hizo tayari zimeshavunwa na kuhifadhiwa. Jaribio la njugu nyasa limekamilika na aina 10 kati ya 35 zimechaguliwa kuendelea na uchunguzi mashambani badala ya kituoni; pamoja na Utafiti wa afya ya udongo na kuimarisha

mnyororo wa thamani; ambapo wakulima 198 (Unguja 94, Pemba 104) walipata mafunzo ya uzalishaji wa mbegu bora za mboga mboga (Quality Declared Seeds). Sampuli za udongo 150 zilikusanywa kwa kufanyiwa uchunguzi nje ya nchi kwa lengo la kutengeneza ramani ya udongo ya Zanzibar na sampuli 500 za udongo kutoka kwa mkulima mmoja mmoja ndani ya Wilaya kumi (10) zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi wa virutubisho.

c) **Kuendelezwa Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula:** Kupanda mbegu ya mpunga katika eneo lenye ukubwa wa ekari mbili (2) katika bonde la Mwera na Kibonde mzungu. Jumla ya kilogramu 840 za mbegu mama zimezalishwa. Kwa kushirikiana na ofisi ya e-government mahitaji ya msingi Wizara inaandaa Mfumo wa Kidijitali wa kutambua mahitaji ya pembejeo kwa wakulima wa mpunga na Kufanya tathmini ya uzalishaji wa mpunga ekari 33,800 Unguja na Pemba. Kazi zinazoendelea ni kuotesha miche 49,050 ya minazi (Pemba 10,050 na Unguja 39,300) na miche 353,540 ya miti ya matunda na viungo (Unguja 244,233 na Pemba 109,307)

d) **Kilimo cha Mazao ya Biashara kuendelezwa:** Mazao makuu ya biashara kwa uchumi wa Zanzibar ni karafuu na mwani. Kwa mwaka 2023, mavuno ya zao la karafuu yamepungua na kufikia tani 2,654.7 zenye thamani ya TZS 37,980.7 milioni ikilinganishwa na tani 4,734.1 zenye thamani ya TZS 63,145.8 milioni mwaka 2022. Wizara imefanya jitihada ya kuotesha miche 134,777 ya mikarafuu (Pemba 97,777 na Unguja 37,000) na kuisambaza kwa wakulima ili kuimarisha uwepo wa zao hilo nchini, kutoa elimu na kufanya utafiti wa kuweza kuimarisha zao la karafuu. Kwa upande wa mavuno ya zao la mwani mwaka 2023 uzalishaji umeongezeka na kufikia tani 16,652.8 zenye thamani ya TZS 16,514.8 milioni kutoka tani 11,048.8 zenye thamani ya TZS 8,563.9 milioni mwaka 2022. Hali hii imesababishwa na Wizara kuweza kuwapatia wakulima 350 vifaa vya kilimo cha mwani ikiwemo kamba, taitai na boti kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mwani pamoja na kushajihisha wanaume katika ukulima wa zao la mwani.

**Jadweli Nam 6: Uzalishaji wa mazao ya Karafuu na Mwani (2019-2023) (TZS milioni)**

| Zao | 2019 | | 2020 | | 2021 | | 2022 | | 2023 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamani |
| Karafuu | 1,691.0 | 23,647.2 | 3,072.1 | 42,954.2 | 7,840.8 | 102,030.9 | 4,734.1 | 63,145.8 | 2,654.6 | 37,980.6 |
| Mwani | 9,663.2 | 5,667.7 | 8,784.6 | 5,387.1 | 10,530.8 | 6,402.8 | 11,048.8 | 8,563.9 | 16,652.8 | 16,514.8 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024.***

### 2.7.6.3 Sekta Ndogo ya Mifugo

Kwa mwaka 2023 idadi ya ng'ombe waliochinjwa imeongezeka na kufikia 29,851 ikilinganishwa na ng'ombe 27,326 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 9.2. Kwa mwaka 2023, idadi ya kuku waliochinjwa wamefikia jumla ya kuku 1,161,238 ikilinganisha na idadi ya kuku 1,130,891 waliochinjwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 2.7. Kwa mwaka 2023 idadi ya mbuzi waliochinjwa imeongezeka na kufikia mbuzi 13,704 ikilinganishwa na mbuzi 4,416 waliochinjwa mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 210. Idadi ya kondoo waliochinjwa mwaka 2023 imeongezeka na kufikia 273 Ongezeko hilo ni kutokanana , kuimarika kwa vyanzo vya ukusanyaji wa takwimu.

### 2.7.7.4 Sekta Ndogo ya Uvuvi.

Mwaka 2023 upatikaji wa samaki umeongezeka na kufikia tani 80,085 zenye thamani ya TZS 569,080 milioni kutoka tani 61,794 zenye thamani ya TZS 391,370 milioni mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 29.5. Hali hii imesababishwa na kuimarisha usimamizi wa maeneo ya hifadhi ya bahari kwa kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira ya bahari kwa jamii na kuzijengea uwezo Kamati za uvuvi 102 Unguja na Pemba ili kuongeza ufanisi katika shughuli za uvuvi na kuanzisha maeneo mapya ya ufugaji wa pweza na samaki wa miambani, pia kuimarika kwa sekta ya uvuvi kwa kuwapatia wavuvi nyenzo za kisasa za uvuvi ambapo kwa mwaka 2023 jumla ya boti 449 zimetolewa kwa wananchi Unguja na Pemba .

### 2.7.8.5 Sekta ndogo ya Misitu

Misitu ni rasilimali muhimu kwa utunzaji wa mazingira. Serikali inaendelea na mikakati ya kutunza na kuhifadhi misitu ya asili ili kupunguza athari za tabianchi. Bidhaa za misitu zilizouzwa kwa mwaka 2023 ni kama ifuatavyo:-
Boriti 2,053.5 zenye thamani ya TZS 225.9 milioni zimeuzwa mwaka 2023 ikilinganishwa na boriti 1,741.1 zenye thamani ya TZS 195.6 milioni mwaka 2022; Nguzo 1,091.7 zenye thamani ya TZS 54.6 milioni zimeuzwa mwaka 2023 ikilinganishwa na nguzo 2,947.9 zenye thamani ya TZS 98.3 milioni zilizouzwa mwaka 2022; Mapau 2,084.8 yenye thamani ya TZS 225.9 milioni yameuzwa mwaka 2023 ikilinganishwa na mapau 2,970.0 yenye thamani ya TZS 237.6 milioni mwaka 2022; Mizigo ya kuni 25,909.7 yenye thamani ya TZS 113.2 milioni yameuzwa mwaka 2023 ikilinganishwa na mizigo ya kuni 26,236.6 yenye thamani ya TZS 1836.6 milioni yaliyouzwa mwaka 2022; Fito 1,091.7 zenye thamani ya TZS 5.5 milioni zimeuzwa kwa mwaka 2023 ikilinganishwa na fito 1.878.0 zenye thamani ya TZS 939.0 milioni zilizouzwa mwaka 2022

na kwa upande wa makaa tani 2,128.2 zenye thamani ya TZS 1,702.6 milioni zimeuzwa mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 1,943.6 zenye thamani ya TZS 1,360.6 milioni mwaka 2022.

### 2.8 Ukuzaji Rasilimali

Ukuzaji rasilimali ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii kupitia upatikanaji wa ajira, fedha za kigeni, uimarishaji wa sekta za kiuchumi na kijamii zinazochangia katika ukuaji wa Pato la Taifa. Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) inaendelea kutoa huduma bora na kuhamasisha wawekezaji wa Mataifa mbali mbali kwa kuhamasika kuja kuwekeza Zanzibar. Kwa mwaka 2023, ZIPA imeidhinisha jumla ya miradi 114 yenye thamani ya TZS 4.6 trilioni kutoka miradi 93 yenye thamani ya TZS 4.5 trilioni mwaka 2022, sawa na ongezeko la thamani ya asilimia 2.1. Miradi ya hoteli na migahawa imechukua nafasi kubwa ya miradi ya uwekezaji na kufikia idadi ya miradi 44 sawa na wastani wa asilimia 39 ya miradi yote 114 kwa mwaka 2023, miradi ya uwekezaji wa nyumba za biashara (real estate) imefikia idadi ya miradi 33 sawa na wastani wa asilimia 29 na miradi mengine iliyobakia imefikia idadi ya miradi 37 sawa na wastani wa asilimia 32 ya miradi yote 114 mwaka 2023, *(Jadweli namba 7 na 8).*

**Jadweli Nam 7: Idadi na Mgawanyo wa Miradi iliyosajiliwa na ZIPA (2019-2023)**

**Jadweli Nam 7: Idadi na Mgawanyo wa Miradi iliyosajiliwa na ZIPA (2019-2023)**

| MIRADI | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | 5 | 2 | 8 | 7 | 3 |
| Uzalishaji Viwandani | 9 | 3 | 19 | 8 | 7 |
| Umeme na Gesi | 0 | 1 | 1 | 3 | 5 |
| Shughuli za Usimamizi wa Taka Taka | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Shughuli za Ujenzi | 0 | 0 | 2 | 7 | 1 |
| Biashara za (jumla na reja reja), pamoja na Vyombo vya Moto | 3 | 2 | 2 | 3 | 4 |
| Usafirishaji na Uhifadhi | 1 | 1 | 2 | 1 | 1 |
| Huduma za Malazi na Migahawa | 17 | 19 | 40 | 27 | 44 |
| Huduma za Fedha na Bima | 0 | 0 | 0 | 3 | 1 |
| Taarifa na Mawasiliano | 0 | 1 | 2 | 1 | 0 |
| Huduma za Ukodishaji wa Nyumba za Biashara | 3 | 1 | 7 | 25 | 33 |
| Shughuli za Kiutawala | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Elimu | 0 | 2 | 3 | 1 | 0 |
| Huduma za Afya na Kazi za Kijamii | 1 | 0 | 3 | 2 | 2 |
| Sanaa na Michezo | 2 | 2 | 5 | 3 | 11 |
| Huduma Nyenginezo | 0 | 0 | 1 | 2 | 2 |
| **Jumla** | **41** | **34** | **97** | **93** | **114** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024***

**Jadweli Nam 8: Mwenendo wa Mitaji ya Uwekezaji iliyoidhinishwa na ZIPA 2019-2023 (TZS Milioni)**

| MIRADI | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo , Misitu na Uvuvi | 9,962 | 35,175 | 42,575 | 44,021 | 139,512 |
| Uzalishaji Viwandani | 134,731 | 5,986 | 115,474 | 34,907 | 1,030,080 |
| Umeme na Gesi | 0 | 2,758 | 237,121 | 1,827,227 | 1,495,920 |
| Usimamizi wa Taka Taka | 0 | 0 | 165,985 | 0 | 0 |
| Shughuli za Ujenzi | 6,180 | 0 | 88,920 | 91,644 | 24,480 |
| Biashara na Vyombo vya Moto | 1,145 | 138,225 | 3,912 | 8,774 | 13,968 |
| Usafirishaji na Uhifadhi | 45,780 | 5,478 | 27,269 | 17,087 | 9,600 |
| Huduma za Malazi na Migahawa | 803,634 | 252,522 | 1,704,153 | 525,482 | 1,248,666 |
| Huduma za Fedha na Bima | 0 | 0 | 0 | 1,738,677 | 4,800 |
| Taarifa na Mawasiliano | 0 | 45,960 | 1,423 | 46,180 | 0 |
| Huduma za Ukodishaji wa Nyumba za Biashara | 25,408 | 20,470 | 77,064 | 193,363 | 286,909 |
| Shughuli za Kiutawala | 0 | 0 | 4,742 | 0 | 0 |
| Elimu | 0 | 4,826 | 12,662 | 693 | 0 |
| Huduma za Afya na Kazi za Kijamii | 1,602 | 0 | 121,083 | 12,700 | 6,840 |
| Sanaa na Michezo | 1,860 | 1,953 | 9,722 | 5,195 | 380,475 |
| Huduma Nyenginezo | 0 | 0 | 1,541 | 4,119 | 4,800 |
| **Jumla** | **1,030,302** | **513,353** | **2,613,646** | **4,550,069** | **4,646,050** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024***

### 2.8.1 Sekta Binafsi Kupitia Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA)

Sekta binafsi ina mchango mkubwa katika kuimarisha uzalishaji wa ndani, upatikanaji wa ajira na kukuza hali ya uchumi nchini. Kwa mwaka 2023, jumla ya ajira mpya 6,146 kutoka ajira 3,970 zilizopatikana mwaka 2022 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 55, ambapo miradi ya mahoteli na migahawa imechangia jumla ya ajira mpya 4,442 sawa na wastani wa asilimia 72, ikifuatiwa na miradi ya uwekezaji wa nyumba za biashara (real estate) imetoa ajira mpya 1,019 sawa na asilimia 17 na miradi mengineyo imechangia jumla ya ajira mpya 685 sawa na wastani wa asilimia 11 mwaka 2023, (Jadweli namba 9).

**Jadweli Nam 9: Idadi ya Ajira Zilizopatikana Kupitia Miradi ya Sekta Binafsi, iliyoidhinishwa na ZIPA Mwaka 2019-2023**

| MIRADI | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo , Misitu na Uvuvi | 117 | 24 | 496 | 446 | 65 |
| Uzalishaji Viwandani | 3,199 | 179 | 2,779 | 206 | 100 |
| Umeme na Gesi | 0 | 12 | 0 | 100 | 120 |
| Usimamizi wa Taka Taka | 0 | 0 | 30 | 0 | 0 |
| Shughuli za Ujenzi | 0 | 0 | 520 | 383 | 70 |
| Biashara na Vyombo vya Moto | 39 | 23 | 40 | 127 | 39 |
| Usafirishaji na Uhifadhi | 36 | 35 | 266 | 400 | 15 |
| Huduma za Malazi na Migahawa | 1,337 | 809 | 2,043 | 1,240 | 4,442 |
| Huduma za Fedha na Bima | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 |
| Taarifa na Mawasiliano | 0 | 20 | 19 | 30 | 0 |
| Huduma za Ukodishaji wa Nyumba za Biashara | 80 | 50 | 234 | 903 | 1,019 |
| Shughuli za Kiutawala | 0 | 0 | 20 | 0 | 0 |
| Elimu | 0 | 80 | 215 | 20 | 0 |
| Huduma za Afya na Kazi za Kijamii | 47 | 0 | 900 | 20 | 25 |
| Sanaa na Michezo | 29 | 24 | 190 | 95 | 204 |
| Huduma Nyenginezo | 0 | 0 | 39 | 0 | 27 |
| **Jumla** | **4,884** | **1,256** | **7,791** | **3,970** | **6,146** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024***

### 2.8.2 Mgawanyo wa Miradi iliyosajiliwa na ZIPA kwa Sekta na Umiliki 2022/2023.

Mgawanyo wa miradi iliyosajiliwa na kuidhinishwa na ZIPA kwa Wageni na Wazawa mwaka 2023 ni miradi 114 yenye thamani ya TZS 4.6 trilioni, kati ya hiyo miradi 86 sawa na wastani wa asilimia 75 ya miradi yote yenye thamani ya TZS 4.4 trilioni inamilikiwa na Wageni, na miradi 28 sawa na wastani wa asilimia 25 ya miradi yote yenye thamani ya TZS 226.0 bilioni inamilikiwa na Wazawa, *(Jadweli namba 10 na 11).*

**Jadweli Nam 10: Mgawanyo wa Miradi iliyosajiliwa na ZIPA kwa Wazawa na Wageni (2019-2023)**

| Umiliki/Mwaka | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Wazawa | 16 | 15 | 28 | 35 | 28 |
| Wageni | 25 | 19 | 69 | 58 | 86 |
| **Jumla** | **41** | **34** | **97** | **93** | **114** |

***Chanzo:Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024***

**Jadweli Nam 11: Mgawanyo wa Thamani ya Miradi iliyoidhinishwa na ZIPA kwa Wazawa na Wageni (2019-2023) (TZS Milioni)**

| Umiliki/ Mwaka | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Wazawa | 86,547 | 229,223 | 200,584 | 216,512 | 226,075 |
| Wageni | 943,754 | 284,131 | 2,413,064 | 4,333,557 | 4,419,975 |
| **Jumla** | **1,030,301** | **513,354** | **2,613,648** | **4,550,069** | **4,646,050** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024***

### 2.8.3 Mgawanyo wa Miradi iliyosajiliwa na ZIPA kwa Mabara mwaka 2023

Kwa mwaka 2023, kati ya miradi 114 iliyoidhinishwa na ZIPA, miradi 44 ni kutoka Bara la Ulaya, miradi 38 kutoka Bara la Afrika, miradi 25 kutoka Bara la Asia na miradi 7 kutoka Bara la Amerika. Mamlaka ya Ukuzaji Uwekezaji Zanzibar inaendelea na kukuza, kuimarisha huduma na kuitangaza Zanzibar Kitaifa na Kimataifa kuwekeza nchini. *(Jadweli namba 12).*

**Jadweli Nam 12: Mgawanyo wa Miradi iliyosajiliwa kwa Mujibu wa Mabara (2019-2023)**

| Orodha ya Mabara | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Europe | 11 | 11 | 36 | 33 | 44 |
| Afrika | 20 | 13 | 38 | 37 | 38 |
| Asia | 7 | 3 | 13 | 17 | 25 |
| Amerika | 3 | 3 | 9 | 4 | 7 |
| Australia | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 |
| **Jumla** | **41** | **30** | **97** | **93** | **114** |

*Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024*

### 2.8.4 Faida za Kiuchumi na Kijamii kutoka katika Miradi ya Uwekezaji

Miongoni mwa faida zinazopatikana kutoka katika Miradi ya Uwekezaji ni pamoja na:-

i Kuongeza fursa za upatikanaji wa ajira nchini hali inayosaidia kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana na utegemezi wa ajira kutoka Serikalini;

ii Kuongeza mapato ya Serikali yanayosaidia katika ufanikishaji wa miradi ya maendeleo;

iii Kuimarisha huduma za kijamii ikiwemo huduma za elimu, afya, huduma za makaazi na miundombinu;

iv Kuendeleza uhusiano mwema wa kiurafiki baina ya Zanzibar na Mataifa mengine yanayokuja kuwekeza Zanzibar;

v Kuimarisha taaluma ya uongozi na masoko katika sekta za mbali mbali za miradi inayoekezwa ndani ya nchi;

vi Upatikanaji wa teknolojia za kisasa pamoja na ujuzi kutoka kwa wawekezaji wageni.

### 2.8.5 Hali ya Upatikanaji wa Ajira

Upatikanaji wa Ajira una mchango mkubwa katika kuongeza uzalishaji wa ndani pamoja na kuimarisha uchumi wa Zanzibar. Kwa Mwaka 2022/2023, ajira mpya zilizosajiliwa zimefikia 82,225 ikilinganishwa na ajira 68,632 mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 20, kati ya hizo ajira kutoka Serikalini zimefikia jumla ya 37,867 (wanaume ni 15,603 na wanawake ni 22,264) mwaka

2022/2023. Ajira kutoka Mashirika ya Serikali zimefikia 6,853 (wanaume ni 4,442 na wanawake ni 2,411) mwaka 2022/2023, na ajira Binafsi zimefikia 37,505 (wanaume ni 23,598 na wanawake ni 13,907) mwaka 2022/2023.

Kuongezeka kwa ajira mpya kumechangiwa zaidi na kuongezeka kwa uhitaji wa wafanyakazi katika Sekta ya Elimu imeajiri wafanyakazi wapya 22,060, ikifuatiwa na ajira katika Huduma za Malazi na Chakula kufikia ajira 15,786 na ajira za Utawala wa Umma kufikia ajira 15,501 mwaka 2022/2023, *(Jadweli namba 13)*.

**Jadweli Nam 13: Mchanganuo wa Ajira Mpya kwa Sekta na Jinsia kwa mwaka (2018/19 – 2022/23).**

| Sekta | Jinsia | 2018/2019 | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | 2022/2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Serikali** | Wanaume | 14,562 | 15,545 | 16,190 | 15,541 | 15,603 |
| | Wanawake | 17,753 | 19,888 | 22,556 | 21,648 | 22,264 |
| | **Jumla ndogo** | **32,315** | **35,433** | **38,746** | **37,189** | **37,867** |
| **Mashirika ya Serikali** | Wanaume | 4,395 | 4,306 | 4,526 | 4,522 | 4,442 |
| | Wanawake | 2,085 | 2,153 | 2,476 | 2,365 | 2,411 |
| | **Jumla ndogo** | **6,480** | **6,459** | **7,002** | **6,887** | **6,853** |
| **Binafsi** | Wanaume | 16,031 | 17,102 | 14,141 | 15,947 | 23,598 |
| | Wanawake | 7,978 | 8,101 | 6,767 | 8,609 | 13,907 |
| | **Jumla ndogo** | **24,009** | **25,203** | **20,908** | **24,556** | **37,505** |
| **Serikali, Mashirika ya Serikali na Binafsi** | Wanaume | 34,988 | 36,953 | 34,857 | 36,010 | 43,643 |
| | Wanawake | 27,816 | 30,142 | 31,799 | 32,622 | 38,582 |
| | **Jumla Kuu** | **62,804** | **67,095** | **66,656** | **68,632** | **82,225** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024***

# SURA YA TATU

## 3.0 SEKTA YA NJE

Sekta ya nje ni sekta ya uagiziaji, usafirishaji na uhaulishaji wa bidhaa za ndani ya nchi na nje ya nchi. Sekta hii ni muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi kupitia fursa mbali mbali za ajira, upatikanaji wa fedha za kigeni na kuongezeka kwa mapato ya Serikali. Zanzibar ni miongoni mwa nchi za visiwa yenye fursa nzuri ya ushindani wa kibiashara katika upande wa usafirishaji na uagiziaji wa bidhaa. Aidha, historia ya Zanzibar inaonesha kuwa, Zanzibar ilikuwa ni kitovu cha biashara kwa ukanda wa Afrika Mashariki. Hivyo ni dhahiri kwamba iwapo fursa zilizopo zitatumika vizuri, sekta hii itachangia ukuaji wa uchumi wa Zanzibar.

### 3.1 Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi

Kwa mwaka 2023, usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi umefikia thamani ya TZS 109.2 bilioni kutoka thamani ya TZS 180.3 bilioni mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 39. Kupungua kwa thamani ya usafirishaji mwaka 2023 kumechangiwa na kupungua kwa thamani ya usafirishaji wa zao kuu la Karafuu kufikia thamani ya TZS 47.0 bilioni mwaka 2023 ikilinganishwa na thamani ya TZS 118.2 bilioni mwaka 2022, hali hii imesababishwa na mabadiliko ya msimu wa zao hilo nchini. Miongoni mwa nchi zilizopokea mazao ya biashara yaliyosafirishwa kutoka Zanzibar mwaka 2023 ni nchi ya Singapore kwa thamani ya TZS 27.7 bilioni, nchi ya India kwa thamani ya TZS 20.4 bilioni na nchi ya Denmark kwa thamani ya TZS 8.4 bilioni. Mazao ya biashara yaliyosafirishwa ni pamoja na karafuu na mwani.


#### 3.1.1 Usafirishaji wa Mazao ya Biashara (Karafuu na Mwani)

Mazao makuu ya biashara kwa Zanzibar ni zao la Karafuu na Mwani. Mazao haya yana historia kubwa ya kulimwa nchini na ni kichocheo kikubwa cha kukuza uchumi wa Zanzibar kupitia upatikanaji wa ajira, kuongeza thamani ya usafirishaji ambayo itasaidia kupunguza nakisi ya biashara nchini pamoja na kukuza upatikanaji wa fedha za kigeni. Aidha, mazao haya yanauzwa katika nchi mbali mbali ikiwa ni pamoja na Singapore, Indonesia, U.A.E, India na Denmark.

Usafirishaji wa zao la Karafuu kwenda nje ya nchi mwaka 2023, umefikia jumla ya tani 3,197.3 zenye thamani ya TZS 47.0 bilioni kutoka tani 6,452.8 zenye thamani ya TZS 118.2 bilioni zilizosafirishwa mwaka 2022, sawa na upungufu

wa thamani kwa asilimia 60 mwaka 2023. Hali hii imesababishwa na mabadiliko ya msimu wa zao hili na mvua nyingi zilizoathiri mavuno ya karafuu kwa mwaka 2023, *(Mchoro namba 16).*

**Mchoro Nam 16: Tani na Thamani ya Usafirishaji wa Zao la Karafuu 2019-2023, TZS Milioni**





| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Thamani TZS Mil | 19,844.60 | 38,370.90 | 115,358.70 | 118,287.30 | 47,081.10 |
| Tani | 1,744.90 | 3,506.80 | 6,775.50 | 6,452.80 | 3,197.30 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024***

Kwa mwaka 2023, usafirishaji wa zao la Mwani, umefikia tani 11,737.3 zenye thamani ya TZS 19.2 bilioni kutoka tani 13,972.5 zenye thamani ya TZS 16.0 bilioni zilizosafirishwa nje ya nchi mwaka 2022, sawa na ongezeko la thamani ya wastani wa asilimia 20.1 mwaka 2023. Kuongezeka kwa thamani ya usafirishaji wa zao la Mwani mwaka 2023 kumetokana na kuongezeka kwa bei ya uuzaji wa Mwani mwaka 2023 kutoka thamani ya TZS 600 kwa kilo moja ya mwani (wa Spinosum) hadi kufikia bei ya TZS 1,000 kwa kilo moja ya mwani mwaka 2023. Aidha, sababu iliyopelekea kuongezwa kwa bei hiyo ni kuzingatiwa kwa maslahi bora ya wakulima wa mwani nchini. Hii imechochea uzalishaji wa mwani. *(Mchoro namba 17).*

**Mchoro Nam 17: Tani na Thamani ya Usafirishaji wa Zao la Mwani 2019-2023 TZS Milioni**




| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Thamani TZS Mil | 10,382.50 | 11,700.10 | 11,960.70 | 16,010.20 | 19,233.20 |
| Tani | 11,203.70 | 11,382.60 | 12,611.10 | 13,972.50 | 11,737.30 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024***

## 3.2 Uagiziaji wa Bidhaa kutoka Nje ya Nchi

Kwa mwaka 2023, thamani ya Uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi imeongezeka na kufikia TZS 1.5 trilioni mwaka 2023 kutoka thamani ya TZS 1.2 trilioni mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 19.2. Aidha, Uagiziaji mkubwa wa bidhaa mwaka 2023 umefanyika kutoka nchi za Falme za Kiarabu (U.A.E) kwa thamani ya uagiziaji wa TZS 704.6 bilioni ikifuatiwa na China kwa thamani ya TZS 161.9 bilioni, India kwa thamani ya TZS 157.8 bilioni. Kwa upande wa bidhaa zilizoingizwa nchini, asilimia 23 ni bidhaa za mashine, asilimia 51 ni bidhaa za nishati ya mafuta pamoja na malighafi za viwandani, na asilimia 26 ni bidhaa za vyakula.

Uagiziaji wa bidhaa za chakula kama vile Mchele na Sukari umeongezeka kwa mwaka 2023 ikilinganishwa na mwaka 2022. Bidhaa ya mchele imefikia tani 133,727 mwaka 2023 kutoka tani 81,460 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 64; na kwa upande wa bidhaa ya sukari imeongezeka kufikia tani 36,910 mwaka 2023 kutoka tani 32,122 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 15. Ongezeko hili limetokana na kuwepo kwa uhitaji mkubwa wa bidhaa hizo nchini. Aidha, uagiziaji wa bidhaa ya unga wa ngano umepungua kufikia tani 4,070 mwaka 2023 kutoka tani 38,885 mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 90, hali hii imetokana na kuwepo kwa uzalishaji mkubwa wa bidhaa ya unga wa ngano hapa nchini ambao unatosheleza kwa wananchi wake. Kwa sasa kampuni ya Azam inauwezo wa kuzalisha unga wa ngano kilo 5,000 kwa kila mwezi hapa nchini ambapo wananchi wanatumia si zaidi ya kilo 3,000 kwa mwezi mzima, hali hii imepelekea kwa wafanyabiashara kutokuagizia unga wa ngano kutoka nje ya nchi na kupelekea kupungua uagiziaji wa bidhaa hiyo mwaka 2023.

Uagiziaji wa bidhaa za nishati ya mafuta ya Petroli na Dizeli umeongezeka kwa mwaka 2023 ikilinganishwa na uagiziaji wa mwaka 2022; mafuta ya petroli yamefikia lita 110,852,126 mwaka 2023 kutoka lita 97,391,360 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 13.8 na mafuta ya dizeli yamefikia lita 71,759,929 mwaka 2023 kutoka lita 62,079,332 sawa na ongezeko la asilimia 15.6 mwaka 2022. Uagiziaji huu umechangiwa na uwepo wa uhitaji mkubwa wa bidhaa hizo nchini. Aidha, uagiziaji wa nishati ya mafuta ya taa umeendelea kupungua nchini kwa asilimia 91, kufikia lita 2,876,641 mwaka 2023 kutoka lita 31,568,615 mwaka 2022 kutokana na uhamasishaji mkubwa wa matumizi ya nishati ya gesi na umeme, badala ya utumiaji wa majiko ya mkaa na kuni yanayohitaji mafuta ya taa, hali inayopelekea uharibifu wa mazingira kutokana na moshi pamoja na ukataji wa miti. *(Jadweli namba 14)*.

**Jadweli Nam 14: Uagiziaji wa Bidhaa Kuu za Chakula na Nishati ya Mafuta Nchini Mwaka 2019 – 2023**


| Tani | | | | Lita | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka** | **Mchele** | **Sukari** | **Unga wa Ngano** | **Petroli** | **Diseli** | **Mafuta ya Taa** |
| **2019** | 106,518 | 24,462 | 12,812 | 77,733,376 | 54,028,523 | 5,940,403 |
| **2020** | 104,804 | 34,299 | 7,967 | 75,112,831 | 48,449,368 | 5,883,706 |
| **2021** | 36,161 | 26,630 | 5,424.4 | 92,326,260 | 47,817,251 | 5,990,116 |
| **2022** | 81,460 | 32,122 | 38,884.7 | 97,391,360 | 62,079,332 | 31,568,615 |
| **2023** | 133,727 | 36,910 | 4,069.6 | 110,852,126 | 71,759,929 | 2,876,641 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024***

## 3.3 Urari wa Biashara

Nakisi ya biashara mwaka 2023 imefikia thamani ya TZS 1.39 trilioni kutoka thamani ya TZS 1.07 trilioni mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 29 kutokana na kuongezeka kwa uagiziaji mkubwa wa bidhaa zikiwemo za nishati ya mafuta na malighafi za viwandani, bidhaa za mashine na bidhaa za chakula. Licha ya kuongezeka kwa nakisi ya biashara mwaka 2023, usafirishaji wa mazao makuu ya biashara yamesaidia kupunguza nakisi hii ambayo ingeweza kuwa kubwa zaidi endapo hakukuwa na usafirishaji wa mazao hayo kwenda nje ya nchi, *(Mchoro namba 18)*.

**Mchoro Nam 18: Thamani ya Usafirishaji na Uagiziaji wa Bidhaa Nje ya Nchi (2019-2023)**





***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024***

### 3.4 Uhaulishaji wa Bidhaa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara

Historia inaonyesha kuwa Zanzibar na Tanzania Bara zimekuwa na desturi ya uhaulishaji wa bidhaa zao kwa muda mrefu hali iliyopelekea kuimarisha umoja na udugu wao ulioasisiwa na Raisi wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyarere pamoja na Raisi wa kwanza wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Sheikh Abeid Amani Karume mwaka 1964. Uhaulishaji huu umejenga uhusiano wa karibu wa kibiashara, kuleta ushindani wa kibiashara na hivyo kuimarisha soko la bidhaa zinazopatikana pande zote mbili.

Uhaulishaji huu wa bidhaa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara umekuwa na tabia ya kupanda na kushuka kulingana na uhitaji wa bidhaa katika soko na msimu wa bidhaa husika. Kwa mwaka 2023, uhaulishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara umeongezeka na kufikia thamani ya TZS 159.7 bilioni kutoka thamani ya TZS 37.6 bilioni mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 324.2 kwa mwaka 2023. Bidhaa zilizohaulishwa zaidi ni chuma chakavu na mafuta ya kula. Kwa upande wa uhaulishaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar umeongezeka na kufikia thamani ya TZS 431.5 bilioni mwaka 2023 kutoka thamani ya TZS 375.8 bilioni mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 15 mwaka 2023. Bidhaa zilizohaulishwa zaidi ni mchele wa mbeya na unga wa ngano (Azania), *(Mchoro namba 19)*.

**Mchoro Nam 19: Mchanganuo wa Uhaulishaji wa bidhaa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara (2019-2023) TZS Milioni**




*Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2024*

## SURA YA NNE

## 4.0 SEKTA YA FEDHA

Sekta ya Fedha inajumuisha huduma za Mabenki, Bima, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Soko la Mitaji na Dhamana, Mifumo ya malipo na huduma ndogo ndogo za fedha (Microfinance). Sekta hii ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi na kupunguza umaskini. Ofisi ya Rais - Fedha na Mipang kupitia Idara ya Sera za Kodi na Fedha ina jukumu la kusimamia maendeleo ya Sekta ya Fedha Zanzibar na kuhakikisha Sekta hii inakuwa imara, endelevu na yenye kusaidia katika kukuza uchumi wa nchi na kupunguza umasikini wa kipato kwa wananchi. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2023/2024 Utekelezaji wa Sekta ya Fedha ulikuwa kama ifuatavyo:

### 4.1 Sekta Ndogo ya Benki

Sekta ndogo ya benki ni moja kati ya sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Sekta inajumusha Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ikiwa ndiyo msimamizi mkuu wa shughuli za fedha nchini; benki za biashara; mawakala wa huduma za kibenki na mitandao ya simu. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, Julai 2023 - Machi 2024, sekta hii iliendelea kuimarika na hivyo kuchangia katika ukuaji wa Pato la Taifa la Zanzibar kwa wastani wa asilimia 2.3.

#### 4.1.1 Benki Kuu ya Tanzania (BoT)

Jukumu la msingi la Benki Kuu ni kuandaa, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kudhibiti mfumko wa bei na kujenga mfumo imara wa sekta ya fedha unaozingatia ukuaji endelevu wa uchumi. Benki pia, husimamia mabenki na taasisi za fedha, kutoa ushauri kwa Serikali zote mbili, Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika masuala ya uchumi na fedha, kusimamia na kudhibiti mifumo ya malipo nchini, kutengeneza na kusambaza noti na sarafu, kuhifadhi akiba ya fedha za kigeni na kutoa huduma za kibenki kwa Serikali na benki za biashara. Katika kipindi cha Julai 2023 - Machi 2024 Benki Kuu imeendelea kutekeleza majukumu yaliyoanishwa hapo juu kama ifuatavyo:-

**1. Kuandaa na Kutekeleza Sera ya Fedha**

Utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwaka 2023/24 umekuwa wa mafanikio makubwa kwani katika nusu ya pili ya mwaka wa fedha Benki Kuu ilianza Akutekeleza Sera ya Fedha kwa kutumia Mfumo wa Riba. Mabadiliko ya utekelezaji wa Sera ya Fedha kwa kutumia mfumo wa riba badala ya ujazi wa fedha


unalenga kuimarisha sekta ya fedha na uchumi. Mafanikio katika utekelezaji wa sera ya fedha yanajidhihirisha katika ukuaji wa uchumi wa Zanzibar unaoendelea kukua na kufikia asilimia 7.4 kwa mwaka 2023 kutoka ukuaji wa asilimia 6.8 kwa mwaka 2022. Mafanikio haya yanatarajiwa kuongezeka zaidi katika kipindi cha mwaka 2024 kwa kadiri ya uchumi wa Zanzibar unavyotarajia kuimarika. Pamoja na changamato za migogoro inayoendelea mashariki ya kati, utekelezaji wa sera ya fedha katika kipindi cha mwaka 2023/24, ulikuwa wa mafanikio. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 5.5 mwaka 2023/2024 kutoka wastani wa asilimia 8.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023 . Kupungua huku kwa mfumuko wa bei kulitokana na kupungua kwa mfumuko wa bei za vyakula na zisizo za vyakula.

Mfumuko wa bei za vyakula ulipungua hadi kufikia asilimia 8.4 kutoka asilimia 12.7 katika kipindi cha mwaka 2022/23. Bidhaa za vyakula zilizochangia kupungua ni pamoja na mafuta ya kula, unga wa mahindi, ndizi za kupika za kijani na njano na mchele wa mbeya. Mfumuko wa bei kwa bidhaa zisizo za vyakula zilipungua kufikia asilimia 3.2 kutoka asilimia 4.9 mwaka 2022/23. Mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu kwani umekuwa ndani ya viwango vya ukuaji wa jumuia ya Afrika Mashariki ambayo ni asilimia 8 na ndani ya viwango vya SADC ambavyo ni kati ya asilimia 3-7.

Ili kudhibiti kasi ya ongezeko la mfumuko wa bei nchini, Benki Kuu ilipunguza kiwango cha ongezeko la ukwasi kwenye uchumi, hali ambayo iliendelea kuimarisha ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Sera hii ilitekelezwa kwa kutumia nyenzo mbalimbali kama vile Riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate) dhamana za Serikali na kwa kuuza dhamana maalum za Serikali kwa lengo la kupunguza ukwasi kwenye uchumi (liquidity papers). Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo katika miezi ijayo kutokana na kuimarika kwa hali ya ugavi wa chakula na kupungua kwa bei za bidhaa duniani.

**Mchoro Nam 20: Mwenendo wa Mfumuko wa bei, Zanzibar**

*Asilimia*




**Chanzo**: *Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali - Zanzibar.*

Kufuatia utekelezaji wa sera ya fedha, riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mabenki iliongezeka hadi wastani wa asilimia 4.4 katika kipindi cha mwaka 2023/24, kutoka asilimia 3.6 katika mwaka 2022/23. Wastani wa ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana ulikua kwa asilimia 13.8 ukilinginisha na asilimia 13.1 kwa mwezi uliopita na ukipungua ukilinginisha na asilimia 15.9 kwa mwezi kama huo kwa mwaka wa fedha uliopita 2022/2023. Ukuaji wa fedha taslimu (reserve money) na mikopo kwa sekta binafsi kwa Zanzibar iliongezeka kwa wastani wa asilimia 13.1 na asilimia 16.6, mtawalia. Kiwango cha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kilikuwa juu ya lengo lililowekwa la asilimia 10.7 kwa mwaka 2022/23. Ukuaji huo ulitokana na kuimarika kwa uhitaji wa mikopo kwa sekta binafsi, kufuatia uwekezaji unaotekelezwa na Serikali kwenye miundombinu, uboreshwaji wa mazingira ya kufanya biashara, na sera wezeshi za kibajeti zinazoendelea kuchochea kuongezeka kwa shughuli binafsi za kiuchumi nchini.

## 2 .Kusambaza Noti na Sarafu

Benki Kuu imeendelea kutimiza jukumu lake la kusambaza fedha (noti na sarafu) ili kutosheleza mahitaji ya uchumi bila kusababisha mabadiliko ya kasi ya upandaji wa bei ya bidhaa na huduma (yaani mfumko wa bei). Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Benki Kuu ilisambaza jumla ya TZS 1,590.36 bilioni, kati ya hizo TZS 1.545.48 bilioni zilisambazwa kupitia Ofisi ya Unguja na TZS 44.88 bilioni kupitia Kituo cha Pemba, *(Jadweli namba 15)*.

**Jadweli 15: Fedha (Shilingi) Zilizosambazwa Zanzibar: Julai 2023 - Machi 2024 ,** ***TZS***

| | Kituo cha Unguja | Kituo cha Pemba | Jumla |
|---|---|---|---|
| Noti | 1,545,477,500,000 | 44,877,000,000 | 1,590,354,500,000 |
| Sarafu | 5,221,300 | 9,800,000 | 15,021,300 |
| **Jumla** | **1,545,482,721,300** | **44,886,800,000** | **1,590,369,521,300** |

*Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania*

### 3. Kuhifadhi Akiba ya Nchi

### Fedha za Kigeni za Nchi

Benki Kuu ni mtunzaji wa hazina ya fedha za kigeni kwa kuzingatia malengo ya usalama, ukwasi, faida na usimamizi wa madeni ya nje. Hadi kufikia Machi 2024, akiba ya fedha za kigeni iliongezeka hadi kufikia dola milioni 5,327.1, ikilinganishwa na dola milioni 5,012.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Hifadhi hii itatosheleza kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.4 ikilinganishwa na makadirio ya miezi 4.0 kwa nchi ya Tanzania na makadirio ya miezi 4.5 kwa nchi za Afrika Mashariki.

### 4. Utoaji wa Huduma za Kibenki kwa Serikali na Mabenki

Miongoni mwa huduma za kibenki zinazotolewa ni kutunza fedha za Serikali na taasisi zake pamoja na kufanya malipo kwa Serikali, na kutoa mikopo ya muda mfupi kwa Serikali kwa kutumia huduma yake ya overdraft. Velevile BOT, hutunza amana za benki za biashara hapa nchini zikiwemo amana za kisheria (statutory minimum reserve requirement) zinazotakiwa kuwekwa Benki Kuu pamoja na kiasi cha amana kinachohitajika kwa ajili ya malipo au matumizi ya kila siku (Clearing balances). Benki Kuu inaendelea kuwa mhifadhi na mlipaji mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Taasisi za Jamhuri ya Muungano zilizopo Zanzibar pamoja na kutoa huduma za kibenki kwa Benki za Biashara zilizopo Zanzibar.

### 4.1.2 Huduma za Kibenki

Huduma za kibenki hapa Zanzibar zinaendelea kuimarika kila siku zikichagizwa zaidi na kukua kwa teknolojia, utumiaji wa njia mbadala wa kufikisha huduma kwa wateja ikiwa ni pamoja na mawakala wa benki (agent banking). Hadi kufikia Machi 2024, idadi ya benki zilizokuwa zikitoa huduma zilikuwa 14, huku idadi ya matawi ya benki yakiwa 36, ambapo Pemba ilikuwa na matawi 9 na Unguja

ikiwa na matawi 27 (Kiambatanisho A). Idadi ya ATM zikiwa 94. Idadi ya mawakala wa benki wakiwa 1,555 wakijumuisha mawakala 290 waliokuwa Pemba na mawakala 1,265 waliopo Unguja. Maduka ya kubadili fedha za kigeni (Bureau de Change) yalikuwa 4, hata hivyo benki zote za biashara pia zilitoa huduma ya kubadili fedha.

### 4.1.3 Amana

Hadi kufikia Machi, 2024 katika mwaka wa fedha 2023/24, amana katika benki zilizopo ziliongezeka hadi kufikia shilingi 2,859.7 bilioni kutoka shilingi 1,738.4 bilioni zilizokuwepo kipindi kama hicho kwa mwaka uliotangulia 2022/2023. PBZ ilikuwa na asilimia 55.8 ya amana zote; ikifuatiwa na benki za NMB, NBC, CRDB na Amana Bank ambazo kwa pamoja zilizochangia asilimia 30.2 ya amana zote.

**Jadweli Nam 16: Amana katika benki**

*TZS Bilioni*

| Muda | Amana Zinazohitajika Muda wowote (Demand Deposits) | Amana za Muda Maalum (Time Deposit) | Amana za Akiba (Savings) | Amana Nyinginezo (Others) | Jumla ya Amana zote |
|---|---|---|---|---|---|
| 21-Jun | 547.52 | 216.88 | 306.03 | 28.25 | **1,098.68** |
| 21-Sep | 501.14 | 220.53 | 330.83 | 38.79 | **1,091.28** |
| 21-Dec | 652.29 | 174.48 | 334.24 | 47.42 | **1,208.44** |
| 22-Mar | 836.55 | 248.13 | 428.7 | 51.42 | **1,564.80** |
| 22-Jun | 756.16 | 268.85 | 354.36 | 53.27 | **1,432.65** |
| 22-Sep | 267.61 | 337.89 | 338 | 85.47 | **1,028.97** |
| 22-Dec | 306.17 | 270.41 | 375.58 | 643.8 | **1,595.96** |
| 23-Mar | 973.36 | 327.52 | 396 | 41.53 | **1,738.41** |
| 23-Jun | 491.2 | 265.32 | 380.74 | 842.79 | **1,980.06** |
| 23-Sep | 1,233.39 | 484.59 | 390.48 | 75.52 | **2,183.98** |
| 23-Dec | 765.57 | 597.13 | 534.69 | 1,099.70 | **2,997.10** |
| 24-Mar | 1,256.17 | 780.76 | 652.01 | 170.77 | **2,859.72** |

***Chanzo: Benki za Biashara***

### 4.1.4 Mikopo

Mikopo ni sehemu kubwa ya rasilimali za benki na chanzo chake kikubwa ni amana za wateja. Uchambuzi wa mikopo unaonyesha kuwa kwa kipindi cha Julai 2023- Machi 2024 thamani ya mikopo iliyotolewa ilifikia shilingi 2,393.35 bilioni, ambayo ni ongezeko la asilimia 55 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia 2022/2023.

Mikopo binafsi (ambayo zaidi inalenga wafanyakazi wa muda mrefu au wenye mikataba) ilichukua asilimia 37.9 ya mikopo yote iliyotolewa katika kipindi cha mwaka 2023/24. Hii ilifuatiwa na sekta za kilimo, biashara na utalii ambazo kwa pamoja zilipata asilimi 29.6. Mikopo iliyoelekezwa kwenye sekta ya utalii iliongezeka kwa asilimia 28 hadi kufikia Shillingi 147.4 billioni ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

*TZS (Milioni)*

| **Sekta** | **2022/2023** | **2023/2024** | **% Mgawanyo 2023/2024** |
|---|---|---|---|
| | **Shilingi Milioni** | | |
| Kilimo | 519,812.38 | 333,894.98 | 13.95 |
| Biashara | 510,979.63 | 227,657.75 | 9.51 |
| Utalii | 400,801.66 | 147,387.15 | 6.16 |
| Mawasiliano | 48,214.69 | 63,338.17 | 2.65 |
| Ujenzi | 202,382.80 | 31,656.59 | 1.32 |
| Uzalishaji Viwandani | 133,587.76 | 47,268.24 | 1.97 |
| Mikopo Binafsi | 2,528,237.78 | 887,579.80 | 37.09 |
| Taasisi za Fedha | 1,937.07 | 525.15 | 0.02 |
| Nyinginezo | 330,317.65 | 654,043.73 | 27.33 |
| **Jumla** | **4,676,271.42** | **2,393,351.56** | |

***Chanzo: Benki za Biashara***

### 4.1.5 Mwenendo wa riba za benki

Viwango vya riba za mikopo inayotolewa na benki havikuwa na mabadiliko makubwa katika mwaka 2023/24. Wastani wa riba za jumla za mikopo ulikuwa asilimia 15.50, ukilinganishwa na asilimia 16.07 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, wastani wa riba za amana uliongezeka na kufikia asilimia 2.12 kutoka asilimia 1.77 kipindi kama hicho mwaka 2022/23.


**Jedweli Nam 18: Mwenendo wa Riba za Benki kwa mwezi, July 2023 – Machi 2024**

Asilimia

| | 23-Jul | 23-Aug | 23-Sep | 23-Oct | 23-Nov | 23-Dec | 24-Jan | 24-Feb | 24-Mar |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Riba ya Amana( Savings deposit rate) | 1.68 | 1.68 | 1.69 | 2.45 | 2.56 | 2.6 | 2.69 | 2.54 | 2.7 |
| Riba ya Jumla ya amana ya Muda Maalum( Overall time deposit) | 6.85 | 6.91 | 6.85 | 7.05 | 7.64 | 7.45 | 7.4 | 7.39 | 7.55 |
| Riba ya amana ya mwaka (I Year deposit rate) | 8.7 | 8.93 | 8.98 | 9 | 9.16 | 8.92 | 9.15 | 9.06 | 8.94 |
| Riba ya amana ya maelewano( Negotiated deposit rate) | 9.08 | 9.04 | 9.29 | 9.24 | 9.15 | 9.19 | 9.56 | 9.52 | 9.59 |
| Riba ya Jumla ya Mikopo(Overall lending rate) | 15.56 | 15.73 | 15.53 | 15.49 | 15.38 | 15.44 | 15.39 | 15.44 | 15.51 |
| Riba ya mikopo ya muda mfupi hadi mwaka 1 (Short term lending rate up to 1 year) | 16.3 | 17.01 | 16.07 | 15.93 | 15.63 | 15.94 | 15.82 | 16.1 | 16.17 |
| Riba ya miko[o ya maelewano (Negotiated lendig rate) | 13.19 | 13.31 | 13.37 | 13.26 | 13.29 | 13.38 | 13.44 | 13.4 | 13.46 |
| Riba ya dhamana za serikali za siku 364 (364 T Bills yield) | 7.02 | 7.03 | 7.72 | 8.73 | 9.49 | 10.51 | 11.81 | 12.25 | 11.82 |
| Riba za dhamana za serikali kwa ujumla(Overall treasure bills) | 6.56 | 6.92 | 7.44 | 8.43 | 9.34 | 10.48 | 11.76 | 12.21 | 11.65 |
| Riba ya siku moja baina ya mabenki (Overnight interbank rates) | 3.94 | 4.35 | 4.64 | 5.36 | 5.7 | 6.56 | 6.75 | 6.35 | 6.2 |

***Chanzo: Benki za Biashara***

**Mchoro Nam 21: Wastani wa riba za Benki kwa mwezi, Julai 2023 - Machi 2024**




*Chanzo: Benki za Biashara*

### 4.1.6 Wakala wa Huduma za Kibenki

Hadi kufikia mwezi Machi 2024, idadi ya mawakala wa benki (agent banking) ilikuwa 2,376 ambao ni asilimia 2.8 ya mawakala wote nchini Tanzania. Pemba kulikwa na mawakala 418 na Unguja mawakala 1,958. Thamani ya miamala pia iliongezeka maradufu kwenye kuweka na kutoa. Kwa upande wa kuweka thamani ya miamala iliongezeka hadi kufikia TZS1,872,798 milioni ukilinganisha na TZS 1,628,522.3 million mwaka 2022/23. Na kwa upande wa kutoa thamani ya miamala iliongezeka hadi kufikia TZS 699,780milioni kutoka TZS 608,504.9 milioni mwaka 2022/23. (Jadweli namba 19).

**Jadweli Nam 19: Wakala wa benki, Zanzibar**

| KUWEKA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/2023 | | 2023/2024 | |
| | Idadi ya Miamala | Thamani ya Miamala (Milion TZS) | Idadi ya Miamala^p | Thamani ya Miamala (Milion TZS) |
| Pemba | 927,602 | 671,608 | 1,066,742 | 772,349 |
| Unguja | 1,358,388 | 956,913 | 1,562,146 | 1,100,449 |
| Jumla | **2,285,990** | **1,628,521** | 2,628,888 | 1,872,798 |
| **KUTOA** | | | | |
| | 2022/2023 | | 2023/2024 | |
| | Idadi ya Miamala | Thamani ya Miamala (Milion TZS) | Idadi ya Miamala^p | Thamani ya Miamala (Milion TZS) |
| Pemba | 666,807.00 | 202,260.90 | 766,828 | 232,600 |
| Unguja | 1,339,241.00 | 406,244.00 | 1,540,127 | 467,180 |
| Jumla | **2,006,048.00** | **608,504.90** | 2,306,955 | 699,780 |

*Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania*

#### 4.1.7 Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji wa Fedha za Kigeni (Exchange Rate Movement)

Katika kipindi cha mwaka 2023/24, hadi kufikia Machi, 2024 shilingi ya Tanzania iliendelea kuwa tulivu dhidi ya dola ya Marekani, ikibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,546.1 kwa dola ya Marekani, ikilinganishwa na shilingi 2,527.5 kwa dola ya Marekani kwa mwezi uliopita na Shilingi 2,310.65 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Hii ilikuwa ni sawa na kupungua kwa thamani kwa asilimia 10.2 kwa shilingi ya Tanzania ikilinginishwa na dola ya Marekani. Aidha Shilingi inaendelea kuimarika hali iliyochangiwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, mfumuko mdogo wa bei nchini ukilinganishwa na nchi washirika wa kibiashara, na nakisi ndogo ya urari wa bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nchi za nje. Hali hii pia ilichangiwa na hatua zilizochukuliwa katika kuongeza utulivu katika soko la fedha za kigeni nchini.

### 4.2 Benki ya Watu wa Zanzibar

#### 4.2.1 Utekelezaji wa kibajeti Julai 2023 hadi Machi 2024

Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 PBZ imeendelea kukuza mapato yake halisi na kufikiaTZS. 131,615 milioni ikiwa ni ongezeko la asilimia 6 ukilinganisha na mapato yaliokadiriwa ya TZS. 124,011 milioni. Halikadhalika mapato hayo yaliongezeka kwa asilimiaishirini na nne (24) ukilinganisha na mapato ya TZS 105,753 milioni katika kipindi kama hicho cha Julai 2022- hadi Machi 2023. Ongezeko la Mapato kwa kiwango kikubwa kumesababishwa na kuongezeka kwa utoaji wa mikopo ambayo iliongeza mapato kwa kipindi hicho. Katika kipindi kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 benki imeweza kufanya matumizi ya TZS. 53,947-milioni ukilinganisha na makadirio ya bajeti ya TZS 78,633 milioni ikiwa ni pungufu kwa asilimia 31, wakati katika kipindi kama hicho cha Julai 2022 hadi Machi 2023 matumizi yalikuwa ni TZS.61,031 milioni ikiwa ni pungufu kwa asilimia 12. Matumizi pungufu ya PBZ kwa kiasi kikubwa ilisababishwa na umakini katika usimamizi wa matumizi yasio ya msingi na kutoongezeka kwa mishahara kama ilivyokadiriwa. Benki imeweza kuvuka lengo la kupata faida kwa asilimia 71 katika kipindi cha Julai 2023 mpaka Machi 2024 kutoka kiwango kilichokadiriwa cha TZS. 45,377 milioni na kufikia TZS 77,667 milioni. Kiwango hiki cha faida ni sawa na ongezeko la asilimia 74 ukilinganisha na faida iliyopatikana katika kipindi cha Julai 2022 mpaka Machi 2023 ya TZS 44,722 milioni. Hadi kufikia Machi 2024 benki ilikuwa na jumla ya rasilimali zenye thamani ya za TZS. 2,210,281 Milioni ikiwa ni ongezeko

la asilimia tano (5) kutoka katika makisio ya bajeti ya TZS.2,098,702 milion. sawa na ongezeko la asilimia 43 ukilinganisha na raslimali zilizokuweko hadi Machi 2023 za TZS. 1,546, 77 milioni. Ukuwaji huo wa rasilimali kumeifanya PBZ kuwa katika kundi la mabenki makubwa Tanzania. Amana za wateja zilikadiriwa kufika TZS.1,767,643 milioni hadi Machi 2024, kiwango hicho kihalisia kiliongezeka kwa asilimia tatu (3) na kufikia TZS.1,827,877 milioni, wakati raslimali hizo ziliongezeka kwa asilimia 65 ukilinganisha na kiwango cha amana kilichokuweko hadi Machi 2023 cha TZS 1,111,053 milioni.

Hadi Machi 2024, mikopo kutoka katika sekta tofauti imekuwa kwa asilimia 24 na kufikia TZS. 964,255 ukilinganisha na Machi 2023, kwa TZS 780,670 milioni. Mtaji wa benki uliongezeka kwa asilimia 14 hadi Machi 2024 na kufikia TZS. 181,394 milioni ukilinganisha na mtaji uliokuweko hadi Machi 2023 wa TZS 159,320 millioni. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 PBZ imefanikiwa kufungua tawi la Amani, vituo vya kutolea huduma vya Uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume Zanzibar (Terminal 3) ambacho kinachotoa huduma kwa masaa 24, Paje, Tunguu na Nungwi, hivyo kurahisisha utoaji wa huduma kwa kuwafikia wateja wake katika maeneo muhimu na katika makazi yao. Pia PBZ imefanikiwa kufanya ukarabati mkubwa katika majengo ya matawi ya Malindi na Mlandege na kuleta haiba nzuri na mazingira rafiki kwa wateja.

Matawi haya tayari yanaendelea kutoa huduma. Hadi Machi 2024 mawakala wa PBZ wamefikia 1,237 ukilinganisha na mawakala 807 waliokuwepo hadi Machi 2023 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 53. Hadi kufikia Machi 2024 PBZ ilikuwa na mashine za kutolea fedha (ATM) 45 ukilinganisha na ATM 42 zilizokuweko hadi Machi 2023. PBZ ni miongoni mwa walipakodi wakubwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Katika kipindi cha miezi tisa Julai 2023 mpaka Machi 2024, PBZ imelipa jumla ya kodi ya TZS 30,317 millioni ikiwa ongezeko la ulipaji wa asilimia 16 ukilinganisha na kiwango cha TZS 26,212 millioni iliyolipwa katika kipindi cha Julai 2022 mpaka Machi 2023.

#### 4.2.2 Malengo ya PBZ kwa mwaka 2024

Katika kutekeleza bajeti yake ya mwaka 2024, PBZ inakadiria kufikia viwango vifuatavyo:

a) Mapato ya benki kuongezeka kwa asilimia 38 kutoka TZS. 154,784 milioni na kufikia TZS. 214,079 milioni.

b) Matumizi yanakadiriwa kuongezeka kutoka TZS. 80,721 milioni na kufikia TZS. 118,141 milioni, ikiwa ni ongezeko la asilimia 46.

c) PBZ imekadiriakupata faida ya TZS 95,938 milioni, ikiwa ni ongezeko asilimia 30 ukilinganisha na faida halisi ilioipata ya TZS 74,063 milioni katika mwaka 2023.

d) Raslimali za benki zinakadiriwa kuongezeka kwa aslimia 27 na kufikia TZS. 2,605,242 milioni ukilinganisha na rasilimali za TZS 2,051,804 milioni zilizorekodiwa mwaka 2023.

e) Amana za wateja zinatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 35 na kufikia TZS 2,162,724 milioni ukilinganisha na amana za TZS 1,607,253 milioni zilizopatikana mwishoni mwa bajeti ya mwaka 2023.

f) Jumla ya mikopo ya kawaida na inayofuata sharia ya kiislam imekadiriwa kukuwa kwa asilimia 27 kutoka TZS 1,038,921 milioni iliyofikiwa mwaka 2023 na kufikia TZS 1,318,735 milioni kwa mwaka 2024.

g) Mtaji wa benki umekadiriwa kufikia TZS 226,805 milioni kwa mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko la asilimia 28 ukilinganisha na mtaji uliofikiwa mwaka 2023 wa TZS 176,855 milioni .

#### 4.2.3 Miradi ya PBZ kwa mwaka 2024

i. Ufunguzi wa matawi mapya katika mikoa ya Mbeya na Morogoro.

ii. Kuanza ujenzi wa matawi katika mikoa ya Mwanza, Arusha na Tanga.

iii. Ujenzi wa vituo vya kutolea huduma (service centres) katika maeneo ya Pemba (ZSTC Madungu na Konde), Unguja (Kiwengwa na Kinyasini), na Dar-es-salaam (Ubungo, Bandarini Dar es salaam (TPA) na Mbagala)

iv. PBZ kwa mwaka 2024 imepanga kuweka mashine za kutolea fedha ATM katika maeneo ya Machomane, Jumbi, Mwera, Fumba, Kombeni, Kwa nyanya kituo cha mabasi na Mkokotoni

v. PBZ inatarajia kuboresha miundombinu ya tehama kwa kununua switchi yake (Financial Switch) ambayo itarahisisha na kuiongezea mapato benki kwenye huduma za mashine za kutolea fedha (ATM), vile vile inategemea kuzindua mfumo wa kisasa wa benki kiganjani (mobile application).

### 4.2.4 Changamoto na Utatuzi

**Jadweli namba (20).**

| S/N | CHANGAMOTO | UTATUZI |
|---|---|---|
| 1. | Kuwa na mtaji mdogo unaozuia benki kuingia katika ushindani wa kutoa mikopo mikubwa zaidi na kujitanua kibiashara (kufungua matawi) kwa haraka. | Serikali tayari ishatoa kibali kwa PBZ kutafuta mwekezaji wa kimkakati, ambae ataongeza mtaji pamoja na ujuzi utakaosaidia benki kujiendesha kisasa na kuboresha huduma zake. |
| 2. | Sheria ya manunuzi na uajiri inazotumia PBZ ambazo bado haziendani na uharaka kama sekta yenyewe ilivyo | Sheria za manunuzi na uajiri kwa taasisi za serikali zinazofanya biashara bado hazijabadilika ila taasisi hizi huwasilisha maombi ya kufanya manunuzi au ajira kwa mamlaka husika kutegemeana na uharaka wa mahitajio yake. |
| **3.** | Maslahi ya wafanyakazi yapo chini na hayaendani na sekta ya kibenki. | PBZ imeshapeleka mapendekezo ya viwango vya mishahara Utumishi Serikalini kama ilivyopendekezwa na washauri elekezi kampuni ya Delloitte. |
| **4.** | Upungufu mkubwa wa fedha za kimarekani US Dollar (US $), hali iliopelekea kuwaathiri sana wateja (waagizaji wa bidhaa kutoka nje) na kuwafanya kutoa fedha zao za TZS. mara kwa mara na nyingi kwa wakati mmoja kwenda kutafuta fedha hizo za kigeni katika benki nyengine | PBZ inaendelea na juhudi mbali mbali ikiwemo kufungua matawi Tanzania Bara ili kuweza kuvifikia vianzio mbalimbali vya fedha za kigeni na sio kutegemea na vianzio vinavyotokana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Sekta ya Utalii pekee, lakini pia benki kuu wanachukua juhudi mbali mbali kuhakikisha inaimarisha upatikanaji wa fedha za kigeni kwa uhakika. |

| | | |
|---|---|---|
| **5.** | Kutokuwepo kwa (kanuni) regulations zinazosimamia uendeshaji wa benki zinazofwata misingi ya kiislamu. Hali hii inapelekea Benki ya Kiislam kukosa miongozo ya kiuendeshaji wake. | Benki kuu ya Tanzania ipo kwenye mchakato wa kuhakikisha kanuni za kuiongoza benki zinazofwata misingi ya kiislamu zinapatikana, japo jambo hili limekua linachukua muda mrefu kukamilika ambapo unazidi kudhoofisha benki za kiislam. |

## 4.3 Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Sura 394, shughuli za Mamlaka hufanyika Tanzania Bara na Visiwani. TIRA inaongozwa na Kamishna wa Bima ambaye ndie Mtendaji Mkuu wa Mamlaka chini ya uongozi wa Bodi ya Bima ya Taifa (National Insurance Board). Kamishna wa Bima anasaidiwa na Naibu Kamishna wa Bima ambaye anaongoza shughuli za Mamlaka kwa upande wa Zanzibar. Majukumu mahsusi ya Mamlaka ni; kusajili na kutoa leseni kwa watoa huduma za bima; kusimamia mwenendo,ustahimilivu, uendelevu na ukwasi kwa watoa huduma za Bima; kulinda maslahi ya wateja na wanufaika wa huduma na bidhaa za bima; kuendeleza soko la bima; kutoa elimu kwa umma na kuishauri Serikali kuhusu masuala ya Bima.

### 4.3.1 Usajili wa watoa huduma za Bima

Mamlaka imekuwa ikifanya usajili kwa watoa huduma za bima mbalimbali nchini ikiwemo kampuni za bima mtawanyo za ndani na nje, Wataalamu wa Ushauri wa Bima Mtawanyo (Re Insurance Brokers) wa ndani na nje, wauza Bima Kidijitali (Insurance Digital Platform),Watathmini Bima (Insurance Actuaries firms), Wachunguzi Binafsi na Maafisa wauza Bima. Watoa huduma za bima hawa hawana matawi/ofisi hapa Zanzibar.

Kati ya kampuni za bima 38 zilizosajiliwa, kampuni 16 ndio zina matawi/ofisi zao hapa Zanzibar sawa na 42% ya kampuni zote za bima nchini. Aidha kampuni ya kwanza yenye kutoa huduma za bima kwa misingi ya sharia imesajiliwa Zanzibar (ZIC Takaful) ambayo makao makuu yapo Zanzibar. ***(Jedwali namba 21.)***

**Jedwali Nam 21:Ulingano wa watoa huduma za bima Tanzania**.

| Nam | Watoa huduma za Bima | Idadi | | % ya Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Tanzania | Zanzibar | |
| 1 | Kampuni za Bima | 38 | 17 | 42% |
| 2 | Washauri wa bima | 116 | 5 | 4% |
| 3 | Mawakala wa bima | 1,096 | 80 | 7% |
| 4 | Benkiwakala | 30 | 7 | 23% |
| 5 | Wakadiria hasara | 56 | 1 | 2% |
| 6 | Kampuni ya TAKAFUL | 2 | 1 | 50% |
| 7 | Watoa huduma za Afya (Health services providers) | 8 | 2 | 25% |
| **Jumla** | | **1,346** | **112** | **8%** |

### 4.3.2 Mfumo wa Kusimamia na Kudhibiti Soko la Bima

Katika kuhakikisha soko la bima linakua imara, thabiti na kutoa huduma kwa mujibu wa Sheria, Mamlaka ina mfumo unaojulikana kama TIRA RBS unatumika kusajili watendaji wote wa bima zikiwemo kampuni na madalali wa bima, kuwasilisha hesabu, kuchambua na kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu utendaji wa soko la bima nchini. Pia ipo mifumo mengine ya TEHAMA inayotumika na Mamlaka kama; TIRA-ORS, TIRA-MIS, mifumo ambayo inasomana na baadhi ya mifumo mengine ya Serikali kama; NIDA, TRA, BRELA, ZRA, BPRA, Polisi n.k. Mifumo hii pia imeunganishwa na mifumo ya kampuni zote za bima nchini. Lengo na madhumuni ya mifumo hii ni; kupokea na kuchakata taarifa za mwenendo na bishara ya bima ikiwemo; usajili wa watoa huduma za bima, uwasilishaji wa taarifa za biashara ya bima, upokeaji wa malalamiko kuhusu bima, uhakiki na uhalali wa bidhaa za bima na uchakataji wa taarifa za bima.

### 4.3.3 Msuluhishi wa migogoro ya bima (Ombudsman)

Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima ni Taasisi inayojitegemea iliyoanzishwa chini ya sheria ya Bima ya Mwaka 2009 Sura ya 394. Lengo la kuanzisha ofisi hii ni kutatua migogoro baina ya wateja wa Bima na kampuni za Bima kupitia njia za usuluhishi nje ya utaratibu wa kawaida wa kimahakama. Shughuli za usuluhishi kwa upande wa Zanzibar hufanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa bima ofisi ya Zanzibar. Maafisa kutoka ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima wanafika Zanzibar iwapo kuna haja ya kufanya hivyo ili kushirikiana na watendaji wa Mamlaka waliopo Zanzibar. Malalamiko yote yatakayofikia kuwa migogoro hupelekwa kwenye Kamati ya Utekelezaji wa Sheria(LEC) na itakaposhindikana hupelekwa katika ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya bima.

### 4.3.4 Hali ya soko la huduma za Bima Zanzibar.

Hali ya soko la Bima kwa upande wa Zanzibar kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 imeimarika. Biashara ya bima imekua na kufikia asilimia 3 na kuwepo na ongezeko la watoa huduma ya bima kufikia kampuni kumi na saba (17) hapa Zanzibar, hivyo kuandikisha bima zenye thamani ya TZS 20.4 bilioni kwa mikataba ya bima 38,266 ambapo Jumla ya TZS 5.8 bilioni zililipwa kama fidia kwa wahanga 3,364 .

### 4.3.5 Mafanikio

1. Tasnia ya Bima kushiriki katika uchumi wa Gesi na Mafuta kwa Kuanzishwa kwa Muungano wa Kampuni za Bima za Utoaji wa Bima za Mafuta na Gesi (Oil and Gas Consortium);

2. Kuanzishwa kwa muungano wa kampuni za utoaji wa bima za Kilimo (Agriculture Insurance consortium);

3. Taasisi kuendelea kufanya marekebisho katika Sheria ya Bima Sura Na. 394 na Kanuni zake, pamoja na kuandaa Kanuni Mpya za Bima kwa lengo la kuboresha mfumo wa usimamizi na uendelezaji wa bima nchini;

4. Kulinda haki ya mteja wa bima kwa kuwepo na mkakati kabambe wa kushughulikia kero na malalamiko kwa wananchi, kwa kuandaa semina kwa ofisi za kanda na Zanzibar katika ulipaji wa madai;

5. Kuanzishwa kwa aina mpya za bidhaa za bima ambapo jumla ya bidhaa 17 zimeanzishwa kwenye soko la bima kukidhi mahitaji ya wananchi hususan wa kipato cha chini. Bidhaa hizi ni pamoja na huduma za bima kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo na wa kati na bidhaa za kilimo na uvuvi;

6. Uunganishwaji wa mifumo ya TEHAMA ya usimamizi wa bima kati ya TIRA na Mamlaka zingine za Serikali Mfumo wa TEHAMA wa bima ulioundwa na TIRA - TIRAMIS umeunganishwa na mifumo ya Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA), Jeshi la Polisi Tanzania (TPF), na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA);

7. Kuongezeka kwa wigo wa Bima za lazima ili kujumuisha masoko ya umma, majengo ya biashara, vyombo vya kusafiria majini na uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi;

8. Jumla ya miongozo mitatu (3) katika kuimarisha soko la bima la Tanzania imeandaliwa ikiwa ni pamoja na: Miongozo ya usimamizi na ubakizaji wa bima na bima mtawanyo (Guidelines on Rentation and Reinsurance Management); Miongozo ya bima ya afya na usajili wa watoa huduma za afya (Guidelines for Medical Insurance and Registration of health service providers (HSPs)) na Miongozo ya utoaji ithibati kwa warekebishaji na watengenezaji wa vyombo vya moto (Guidelines on Accreditation of Automobile repairs and Maintainers (ARMs)) na

9. Kufunguliwa kwa ofisi mbili za Kanda ambazo ni Kanda ya Unguja Kusini itahudumia mikoa mitatu Unguja kati, Mjini Magharibi na Kaskazini, kwa upande wa Pemba itahudumia Mkoa wa Kaskazini na Kusini.

### 4.3.6 Matarajio

1. Kukamilishwa kwa Sera ya Bima ya Taifa (National Insurance Policy - NIP);
2. Kuendelea na uunganishwaji wa mifumo ya TEHAMA ya usimamizi wa bima kati ya TIRA na Taasisi zingine za Serikali (kama vile TASAC, TPA, NIDA, ZRA, Idara ya Usafirishaji na Mawasiliano Zanzibar, NSSF, ZSSF, NHIF, CHF, na WCF) ili kuongeza tija na ufanisi ndani ya sekta ndogo ya bima na pia kupunguza gharama za usimamizi;
3. Kuanzishwa kwa Bodi ya Wataalam kwenye Tasnia za Bima, bodi hiyo itaitwa Insurance, Social Protection, and Actuarial Board – ISPAB. Lengo la bodi ni kuongeza fursa za kutambulika na tija kwa wanataaluma husika.
4. Kukamilisha kwa Kanuni za Bima za Lazima. TIRA kama msimamizi wa Bima inaendelea kukamilisha kanuni za Bima za lazima katika maeneo ya; Majengo ya Biashara, Masoko ya Umma, Bidhaa zinazotoka nje, Vyombo vya Usafiri wa Majini kama vile Meli, Boti na Feri au Vivuko.

Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea na utekelezaji wa matakwa ya Mpango Mkuu wa Serikali wa Kuendeleza Sekta ya Fedha (FSDMP) ikiwemo, kutekeleza mkakati wa kitaifa wa elimu ya Bima; kutekeleza mkakati wa kitaifa wa Bima jumuishi na kuweka na kutekeleza mfumo madhubuti wa kushughulikia madai, malipo na malalamiko ya wateja.

**Jadweli Nam 22: Hali ya soko la huduma za Bima Zanzibar kwa bidhaa za Bima Julai 2023 – Machi 2024**

| Na m. | Bidhaa | Jumla ya ada za Bima | | Ziada/ Pungufu |
|---|---|---|---|---|
| | | **2024** | **2023** | |
| 1 | Moto | 7,386,350,736 | 8,156,385,526.38 | -9% |
| 2 | Ufundi | 1,550,245,214 | 533,591,398.45 | 191% |
| 3 | Majini | 2,320,611,686 | 1,232,375,952.87 | 88% |
| 4 | Vyombo vya Moto | 4,482,731,375 | 5,501,933,079.80 | -19% |
| 5 | Mchanganyiko | 1,972,629,851 | 1,116,309,827.65 | 77% |
| 6 | Anga | 804,041,867 | 120,159,652.55 | 569% |
| 7 | Afya | 3,400,000 | - | 0% |
| 8 | Nyenginezo | 1,777,503,743 | 3,116,766,964.53 | -43% |
| 9 | Maisha | 155,531,446 | 54,229,332.00 | 187% |
| | **Jumla** | **20,453,045,918** | **19,831,751,734.24** | **3%** |

**Jedwali Nam 23: Hali ya soko la huduma za Bima Zanzibar kwa kampuni Julai 2023 – Machi 2024**

| Nam | Makampuni ya Bima | Thamani ya Bima za kawaida | Idadi ya mikataba ya Bima za kawaida | Thamani ya Bima za maisha | Idadi ya mikataba ya Bima za maisha | Jumla ya thamani ya Bima | Jumla ya mikataba ya Bima |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | BUMACO | 696,796,921 | 4,659 | - | - | 696,796,921 | 4,659 |
| 2 | HERITAGE | 2,112,804,304 | 3,714 | - | - | 2,112,804,304 | 3,714 |
| 3 | JUBILEE Allianz | 8,493,162,579 | 2,918 | - | - | 8,493,162,579 | 2,918 |
| 4 | MAYFAIR | 623,605,920 | 488 | - | - | 623,605,920 | 488 |
| 5 | NIC | 271,210,054 | 130 | 32,689,728 | 225 | 303,899,782 | 355 |
| 6 | RELIANCE | 121,778,899 | 514 | - | - | 121,778,899 | 514 |
| 7 | SANLAM LIFE | - | - | 122,841,718 | 674 | 122,841,718 | 674 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 8 | STRATEGIES | 394,422,345 | 1,492 | - | - | 394,422,345 | 1,492 |
| 9 | UAP | 171,737,785 | 426 | - | - | 171,737,785 | 426 |
| 10 | ZIC | 2,923,303,893 | 5,109 | - | - | 2,923,303,893 | 5,109 |
| 11 | ICEA LION | 807,864,403 | 9,996 | - | - | 807,864,403 | 9,996 |
| 12 | MILEMBE | 19,340,000 | 116 | - | - | 19,340,000 | 116 |
| 13 | FIRST ASSURANCE | 816,059,247 | 1,714 | - | - | 816,059,247 | 1,714 |
| 14 | GA INSURANCE | 304,797,550 | 3,942 | - | - | 304,797,550 | 3,942 |
| 15 | MO ASSURANCE | 408,548,767 | 1,333 | - | - | 408,548,767 | 1,333 |
| 16 | TANZINDIA | 673,625,692 | 31 | - | - | 673,625,692 | 31 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 17 | ZIC TAKAFUL | 1,458,456,113 | 785 | - | - | 1,458,456,113 | 785 |
| | **JUMLA** | **20,297,514,472** | **37,367** | **155,531,446** | **899** | **20,453,045,918** | **38,266** |

*Chanzo: Makampuni ya Bima yalipo Zanzibar*

**Jedwali 24: <u>Hali ya malipo ya fidia ya Majanga ya Bima Zanzibar Kuanzia Julai 2023 hadi Disemba, 2023</u>**

| Na m. | Makampuni ya Bima | Thamani ya fidia za majanga ya Bima za kawaida | Idadi ya fidia za Bima za kawaida | Thamani ya fidia za majanga ya Bima za maisha | Idadi ya fidia za Bima za maisha | Jumla ya thamani ya fidia za majanga ya Bima | Jumla ya idadi ya fidia za Bima |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | BUMACO | 34,515,650 | 13 | - | - | 34,515,650 | 13 |
| 2 | HERITAGE | 687,675,820 | 1,313 | - | - | 687,675,820 | 1,313 |
| 3 | JUBILEE Allianz | 2,036,440,986 | 372 | - | - | 2,036,440,986 | 372 |
| 4 | MAYFAIR | 205,948,051 | 73 | - | - | 205,948,051 | 73 |
| 5 | NIC | - | - | 39,084,259 | 49 | 39,084,259 | 49 |
| 6 | RELIANCE | 54,661,522 | 9 | - | - | 54,661,522 | 9 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 7 | SANLAM LIFE | - | - | 268,483,974 | 1,282 | 268,483,974 | 1,282 |
| 8 | STRATEGIES | 1,452,129,741 | 7 | - | - | 1,452,129,741 | 7 |
| 9 | UAP | 2,690,000 | 2 | - | - | 2,690,000 | 2 |
| 10 | ZIC | 699,127,834 | 197 | - | - | 699,127,834 | 197 |
| 11 | ICEA LION | 165,510,454 | 33 | - | - | 165,510,454 | 33 |
| 12 | MILEMBE | - | - | - | - | - | - |
| 13 | FIRST ASSURANCE | 3 | 4 | - | - | 3 | 4 |
| 14 | GA INSURANCE | 1 | | - | - | 1 | - |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 15 | MO ASSURANCE | 141,621,262 | 8 | - | - | 141,621,262 | 8 |
| 16 | TANZINDIA | 4,781,700 | 1 | - | - | 4,781,700 | 1 |
| 17 | ZIC TAKAFUL | 100,000 | 1 | - | - | 100,000 | 1 |
| | **JUMLA** | **5,485,203,024** | **2,033** | **307,568,233** | **1,331** | **5,792,771,257** | **3,364** |

*Chanzo: Makampuni ya Bima yalipo Zanzibar*

### 4.4 Shirika la Bima la Zanzibar

Shirika la Bima la Zanzibar katika kufanikisha Maendeleo ya Sekta ya Bima na Sekta ya Fedha Zanzibar na Tanzania kwa ujumla linaendelea kutoa huduma zake kwa Wananchi kupitia ofisi zake mbili ziliopo Zanzibar (Unguja na Pemba) na ofisi za matawi yake zilizopo Tanzania Bara Pamoja na maeneo mbalimbali kupitia kwa ofisi za mawakala na madalali.

Shirika linazidi kuonyesha muelekeo mzuri wa mabadiliko kwa kuongeza mapato yake, kupunguza gharama za uwendeshaji na kufanya uwekezaji wenye tija.

#### 4.4.1 Majukumu Makuu ya Shirika la Bima Zanzibar

Majukumu makuu ya Shirika la Bima la Zanzibar ni kama ifuatavyo: -

a) Kusimamia mapato ya Shirika kutokana na vyanzo mbalimbali. Mapato hayo yanajumuisha mapato ya bima za magari, bima za moto, bima za meli, pamoja na mapato yatokanayo na uwekezaji;
b) Kusimamia Mali za Shirika kupitia usimamizi wa ununuzi, utunzaji na uondoaji wa mali za Shirika kwa mujibu wa Sheria za Ununuzi;
c) Kusimamia fedha za Shirika. Katika jukumu hili Shirika linasimamia utekelezaji wa Bajeti yake kwa kila mwaka wa fedha, huduma za Uhasibu na ukaguzi wa ndani na ukaguzi wa nje;
d) Shirika linasimamia maendeleo ya Sekta ya Bima Tanzania kwa kushirikiana na wadau wote, na
e) Kusimamia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kupitia mifumo inayohusisha kudhibiti mapato na matumizi ya Shirika.

#### 4.4.2 Ofisi Za Shirika

Shirika lina jumla ya wafanyakazi 118 , Mawakala na Madalali 151 na linafanya kazi zake kwa kupitia ofisi ya Makao Makuu Mpirani Zanzibar, ofisi ya Tawi Amani Unguja, Kanda Pwani Dar es salaam, Kanda ya Ziwa Mwanza, Kanda ya kati Dodoma, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya, Kanda ya Kaskazini Arusha, Kanda ya Kusini Mtwara, Ofisi ya Pemba, Ofisi ya mauzo Tanga, Ofisi ya mauzo Kahama na Ofisi ya mauzo Posta Dar es salaam.

#### 4.4.3 Huduma Zinazotolewa na Shirika la Bima Zanzibar

Lengo kubwa la taasisi hii ni kutoa huduma bora za Bima kwa Wananchi na Idara za Kiserikali ili kuboresha maisha yao na kuwakinga dhidi ya majanga yasiyotabirika. Shirika la Bima la Zanzibar linasimamiwa na Sheria ya Bima

namba 10 ya mwaka 2009 katika utekelezaji wa utoaji wa huduma zake chini ya usimamizi wa Kamishna wa Bima Tanzania (TIRA). Vilevile Shirika linafanya kazi zake chini ya Sheria ya Msajili wa Hazina namba 6 ya mwaka 2021.

### 4.4.4 Utekelezaji Halisi wa Kazi za Shirika kwa Kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024

**a. Mapato**

Mapato ya Shirika yanatokana na vianzio vyake vya mauzo ya Bima pamoja na faida zinazotokana na Uwekezaji, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Shirika limefanikiwa kukusanya jumla ya TZS 35.1bilioni ya mauzo ya Bima ambayo ni sawa na asilimia 87% ya makadirio ya kukusanya TZS 40.5 bilioni katika kipindi cha tathmini.Vile vile Shirika limefanikiwa kupata jumla ya TZS 620 milioni ya mapato yanayotokana na Uwekezaji.

**b. Matumizi**

Matumizi ya Shirika katika kipindi cha Julai hadi Machi 2023/2024, , yamegawika kama ifuatavyo: -

i. TZS 6.9 bilioni zilitumika kwa ajili ya gharama za uwendeshaji wa ofisi (Management Expenses) sawa na asilimia 71% ya makadirio ya matumizi katika kipindi cha tathmini ambayo ni TZS 9.7bilioni;
ii. TZS 9.6 bilioni zimetumika kakulipa madai mbalimbali ya wateja wake waliopata ajali na kutimiza matakwa ya Sheria za bima Nchini, na
iii. TZS 3.1bilioni zimetumika kulipa ujira kwa Mawakala na Madalali wanaofanya biashara ya bima kwa niaba ya Shirika Nchini.

### 4.4.5 Mafanikio Yaliyopatikana kwa Shirika katika Sekta ya Fedha

Chini ya usimamizi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Shirika limeendelea kufanya kazi zake kwa kutoa huduma bora kwa Wananchi Tanzania nzima na limepata mafanikio mbali mbali kama ifuatavyo: -

i. Uwezo wa Shirika katika maeneneo mbalimbali umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka kwa kutoa huduma bora kwa Wananchi kwa lengo la kujiongezea mapato;
ii. Shirika limeweza kufikia malengo yake kwa asilimia kubwa yaliyopangwa katika Bajeti;
iii. Shirika kwa kupitia ofisi zake linandelea kupunguza gharama za uendeshaji, kuongeza wigo wa biashara pamoja na Uwekezaji wenye tija kwa Serikali.

iv. Shirika limeweza kulipa madai ya aina mbalimbali ya halali na yaliyohakikiwa kwa wateja wake kwa wakati;
v. Wafanyakazi wameendelea kupatiwa mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo na kuboresha utendaji kazi wao;
vi. Shirika kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Zanzibar na Tanzania Bara limeweza kutoa taaluma kuhusiana na masuala ya usalama barabarani kwa kuandaa makongamano mbalimbali lengo likiwa ni kupunguza majanga mbalimbali ya ajali;
vii. Shirika limefanikiwa kuongeza wigo wa Biashara ya Bima kwa mashirikiano ya kimkakati na Makampuni na Mabenki mbalimbali katika mfumo wa (Banc assurance) kama vile (VodaBima, Tigo Zantel Bima, Shirika la Posta Tanzania, NMB Bank, CRDB Bank, EXIM Bank, TCB Bank, DCB Bank, NBC Bank, BOA Bank, Mwalimu Commercial Bank, MUKOBA Bankna PBZ Bank). Lengo ni kuongeza mapato ya Shirika;
viii. Shirika linaendelea kutoa huduma bora na za kisasa kwa haraka na ufanisi kwa Wananchi kwa kupitia mifumo ya TEHAMA, na
ix. Shirika limefanikiwa kuzindua huduma mpya za kinga ya bima kwa Wananchi kama ifuatavyo: -

- ‘’Queen Motor Insurance” Aina ya kinga ya bima mpya na maalumu kwa Wanawake ambao wanakatia bima kubwa “Comprehensive” magari yao;
- ‘’ZIC Bima Mobile App” vilevile ni aina mpya ya bidhaa ya huduma katika soko la bima Tanzania ambapo Shirika limeweza kushirikiana na makampuni ya Simu katika kufanikisha utoaji wa huduma bora za bima kwa Wananchi kwa haraka, usahihi na wakati. Kwa sasa Shirika linatoa huduma hiyo kwa kushirikiana na Kampuni za Tigo Zantel Bima na Voda Bima ambapo wateja wa makampuni hayo ya simu wanaweza kupata huduma za bima za Shirika kwa kupitia simu zao;
- ‘’Inbound Travel Insurance”. Aina mpya ya huduma ya bima inayotolewa na Shirika kwa wageni hususani watali wanaofika Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kwa kupatiwa kinga hiyo kwa ajili ya mali na afya zao, na
- “Tour Operator Liability Insurance” ni aina mpya ya kinga ya huduma ya bima iliyobuniwa na inayotolewa na Shirika kwa watembeza wageni kwa kuwakinga na majanga yoyote ambayo yanaweza kuwatokea pindi wanapokuwa katika kazi zao za kuwatembeza watalii Nchini

## 4.5 Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), umeanzishwa chini ya sheria nambari 2 ya mwaka 1998 ambayo ilifanyiwa mapitio makubwa na kuundwa upya na sheria nambari 2 ya mwaka 2005 na kufanyiwa tena marekebisho kwa sheria nambari 10 ya mwaka 2016. Lengo kuu ni kutoa hifadhi ya jamii kwa njia ya kulipa mafao kwa wanachama wachangiaji katika sekta za Serikali na Binafsi.

Malengo mengine madogo ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni haya yafuatayo:

1. Kusajili wanachama waajiri, waajiriwa na wanaojiajiri;
2. Kukusanya michango ya wanachama;
3. Kuweka taarifa za wanachama kwa usahihi, na
4. Kuwekeza fedha zinazokusanywa ili kuwezesha kuwalipa wanachama mafao yao.

Utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar na Maendeleo yake kwa kipindi cha Januari 2023 hadi Machi 2024 ni kama ifuatavyo:

### 4.5.1 Utekelezaji kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024

Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko umeendelea na utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Mpango Kazi wa Mwaka wa fedha 2023/2024 kama ifuatavyo: -

**1. Usajili**

**Idadi ya waajiri wa Mfuko**

Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko umesajili waajir**i 237** sawa na asilimi**a 98** ya makisio ya kuwasajili waajiri **243**. Hadi Machi 2024 Mfuko umewasajili Waajiri **3,029**, ukilinganisha na mwaka uliopita kipindi cha Julai 2022 - Machi **2023** Mfuko ulitarajia kusajili waaj**iri 230,** ambapo waajiri 269 walisajiliwa, sawa na asilimia **117**. Idadi ya waajiri waliosajiliwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii hadi kufikia mwezi Machi 2023 ni 2,731.

**Idadi ya wanachama kwa Mfuko wa lazima**

Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko umesajili waajiriwa **8,827** sawa na asilimia **63** ya makisio ya kuwasajili waajiriwa **13,988**, hadi Machi 2024 waajiriwa waliosajiliwa katika Mfuko wamefikia **128,995**, ukilinganisha na mwaka uliopita katika kipindi cha Julai **2022** - Machi **2023** Mfuko ulitarajia kusajili waajiriwa **10,411** na kufanikiwa kusajili waajiriwa **8,557**, sawa na

asilimi**a 82** na idadi ya wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii hadi kufikia mwezi Machi **2023** ni **119,277** kwa Mfuko wa lazima.

**Idadi ya wanachama kwa Mfuko wa kujichangia kwa hiari**

Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko wa Hiari umesajili wanachama **326** sawa na asilimi**a 23** ya makisio ya kuwasajili wanachama 1,400. Hadi Machi 2024 idadi ya wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii waliosajiliwa wamefikia **12,618** kwa Mfuko wa kujichangia kwa Hiari. ukilinganisha na kipindi cha Julai 2022 - Machi 2023 Mfuko wa Hiari ulitarajia kusajili wanachama **1,125**, ambapo Mfuko uliweza kusajili Wanachama 459 ikiwa ni sawa na asilimia **41**. Idadi ya wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii hadi kufikia mwezi Machi 2023 ni **11,986** kwa Mfuko wa kujichangia kwa Hiari.

Kwa kulinganisha utekelezaji wa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 na Julai 2022 hadi Machi 2023, Mfuko wa lazima ulifanya jitihada za kuendelea kwa kufanikiwa kuwasajili waajiri wapya ambao walifuatiliwa kwa karibu pamoja na mashirikiano makubwa yaliyopatikana katika ofisi zetu za Mikoa na Ofisi ya Pemba, malengo ya kusajili wafanyakazi wa Serikali yamefikiwa kiasi kikubwa kutokana na ajira mpya za wafanyakazi hao ambao wamesajiliwa kwa kipindi hiki. Ofisi ya Pemba imefanikiwa kusajili waajiriwa wengi kutokana na ongezeko la ajira za Serikali na pia waajiri binafsi wamepatikana na kwa jumla kufikia asilimia 98 ya lengo lililopangwa kwa kipindi cha Julai 2023 – Marchi 2024. Sababu ya kutofikia malengo ya usajili kwa upande wa Mfuko wa Hiari, ni mwamko mdogo wa jamii katika kujiwekea akiba ya baadae .

**2 .Mapato ya Mfuko**

Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko ulikadiria kupata mapato ya TZS 174.34 bilioni. Mapato hayo yalitegemewa kutoka katika vyanzo vikuu viwili, ambapo jumla ya TZS 110.25 bilioni ni michango ya wanachama na TZS 64.09 bilioni mapato ya uwekezaji.

**Mchanganuo wa mapato kama ufuatavyo: -**

**Michango ya mwanachama**

Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko ulipanga kukusanya TZS 110.25 bilioni kutoka kwa michango ya wanachama na zilikusanywa TZS 111.45 bilioni sawa na asilimia 101 ya ufanisi. Na ukilinganisha na mwaka uliopita kuanzia Julai 2022 hadi Machi 2023 Mfuko ulikusanya TZS 97.28 bilioni sawa

na ongezeko la asilimia 14.57. Mchanganuo wa michango ya wanachama kama ufuatavyo: -

i. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko ulikusanya michango kutokana na Mfuko wa lazima ulikusanya jumla ya TZS 106.0 bilioni sawa na asilimia 101ya makadirio ya TZS 105.2 bilioni na ukilinganisha na mwaka uliopitakuanzia Julai 2022 - Machi 2023 Mfuko ulikusanya TZS 97.28 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 8.9;

ii. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko ulikusanya michango kutokana na Adhabu, ya jumla ya TZS 34.8 milioni sawa na asilimia 72.8 ya makadirio ya TZS 47.8 milioni na ukilinganisha na mwaka uliopitakuanzia Julai 2022 hadi Machi 2023 Mfuko ulikusanya TZS 100 milioni kutokana na Adhabu ya michango sawa na anguko la asilimia 65;

iii. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko ulikusanya michango kutokana na Mfuko wa Hiari TZS 192.1 milioni sawa na asilimia 48.5 ya makadirio ya TZS 396 milioni ya kipindi cha tathmini. Na ukilinganisha na mwaka uliopita Julai 2022 hadi Machi 2023, Mfuko ulikusanya TZS 62 milioni kutokana na Mfuko wa Hiari sawa na ongezeko la asilimia 209, na

iv. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko ulikusanya michango kutokana na Skimu ya Fidia TZS 5.1 bilioni sawa na asilimia 110 ya makadirio ya TZS 4.63 bilioni. Na ukilinganisha na mwaka uliopita Julai 2022 hadi Machi 2023 michango ya skimu ya Fidia haikuanza kukusanywa.

**Mapato ya uwekezaji**

Kwa kipindi cha Julai 20203 hadi Machi 2024 Mfuko umepata mapato ya uwekezaji TZS 66.15 bilioni dhidi ya lengo la kupata TZS 64.09 bilioni sawa na asilimia 103 na ukilinganisha na kipindi kama hiki mwaka uliopita tulipata TZS 46.19 bilioni ikiwa ni ongezeko la asilimia 43.3.

**Thamani ya uwekezaji hadi kufikia Machi 2024**

Uwekezaji wa Mfuko unajumuisha uwekezaji wa mabenki, hati fungani za Serikali na makampuni, hisa, uwekezaji wa majengo na mikopo. Hadi kufikia March 2024, thamani ya uwekezaji wa Mfuko iliongezeka kwa asilimia 22.6

na kufikia TZS 958.8 bilioni ulikinganisha na uwekezaji kipindi kama hicho mwaka 2022/23 kwa kiasi cha TZS 782.2 bilioni. Ongezeko hilo linachangiwa na uwekezaji wa ziada uliofanywa katika kipindi hicho kutokana na ongezeko la michango na mapato ya uwekezaji.

**3. Matumizi Ya Mfuko**

Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko ulipanga kutumia jumla ya TZS 267.5 bilioni ambapo, TZS 59.2 bilioni kwa ajili ya kulipia mafao, TZS 197.5 bilioni kwa ajili ya uwekezaji, TZS 1.04 bilioni kwa ajili ya kusimamia miradi na TZS 9.8 bilioni kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji. Jumla ya TZS 246 bilioni zilitumika sawa na asilimia 92, ikiwa TZS 56.72 bilioni kwa ajili ya kulipia mafao, TZS 180.95 bilioni kwa ajili ya uwekezaji, TZS 1.15 bilioni kwa ajili ya kusimamia miradi na TZS 7.17 bilioni kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji.
Mchanganuo wa matumizi kama ufuatavyo: -

**Gharama za uendeshaji**

Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko ulipanga kutumia TZS 9.8 bilioni gharama za uendeshaji lakini umetumia TZS 7.17 bilioni sawa na asilimia 73 ya makadirio, ukilinganisha na kipindi kama hiki cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Mfuko ulitumia TZS 4.9 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 47 ambapo ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji.

**Malipo ya Mafao kwa wanachama**

Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko ulipanga kutumia TZS 59.2 bilioni kulipia mafao ya wanachama lakini umelipa TZS 56.72 bilioni sawa na asilimia 95.8 ya makadirio. Ukilinganisha na kipindi cha kama hicho cha Julai 2022 – Machi 2023 Mfuko ulitumia TZS 42.8 bilioni kwa ajili ya kulipa mafao sawa na ongezeka la asilimia 32.52. Hii inatokana na kuongezeka kwa kima cha chini cha pencheni ambapo kinaathiri utekelezaji wa bajeti pamoja ongezeko la idadi ya wastaafu waliostaafu pamoja na marejesho kwa wageni wanaoondoka katika kipindi hicho.

**Mchanganuo wa mafao kwa wanachama kama ufuatavyo: -**

i. Katika kipindi cha Julai 2023 - Machi 2024 Mfuko ulitarajia kulipa mafao ya uzeeni (kiinua mgongo) kwa wanachama 1,589 kwa TZS 20.35 bilioni Jumla ya wanachama 986 wamelipwa mafao na jumla ya TZS. 20.900 bilioni zimetumika. Ukilinganisha na kipindi kama hiki cha Julai 2022

- Machi 2023 Mfuko ulilenga kulipa mafao ya uzeeni (kiinua mgongo) kwa wanachama 1,440 kwa TZS 19,59 bilioni na jumla ya wanachama 866 walilipwa na jumla ya TZS 17,75 bilioni zimetumika;

ii. Katika kipindi cha Julai 2023 - Machi 2024 Mfuko ulitarajia kulipa mafao ya uzazi kwa wanachama 922 kwa TZS 210 milioni. Jumla ya wanachama 1,266 wamelipwa mafao ambapo jumla ya TZS 254 milioni zimetumika. Ukilinganisha na kipindi kama hiki cha Julai 2022 - Machi 2023 kulikuwa na lengo la kulipa mafao ya uzazi kwa wanachama 1,159 kwa TZS 215 milioni waliolipwa ni wanachama 984 na jumla ya TZS 211 milioni zilitumika;

iii. Katika kipindi cha Julai 2023 - Machi 2024 Penchenia 12,450 walitarajiwa kulipwa pencheni zao kwa TZS 31.08 bilioni. Wastaafu 18,507 wamelipwa pencheni zao na jumla TZS 27.93 bilioni zilitumika. Ukilinganisha na kipindi kama hiki cha Julai 2022 - Machi 2023 kulikuwa na lengo la kulipa Penchenia 10,790 kwa TZS 13.72 bilioni na Wastaafu 11,620 wamelipwa pencheni zao na jumla TZS 17.16 bilioni zilitumika;

iv. Kwa kipindi cha Julai 2023 - Machi 2024 Mfuko ulitaraji kulipa marejesho ya TZS 1.89 bilioni kwa wanachama 304. Wanachama 549 walifanyiwa marejesho hayo na jumla ya TZS 3.38 bilioni zilitumika. Ukilinganisha na kipindi kama hiki cha Julai 2022 - Machi 2023 kulikuwa na lengo la kulipa marejesho kwa wanachama 241 kwa TZS 2 bilioni. Wanachama 161 walifanyiwa marejesho hayo na Jumla ya TZS 3.57 bilioni zilitumika, na

v. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko umewalipa wanachama 44 mafao ya kuumia kazini (Fidia) jumla ya TZS 93 milioni kwa makisio ya kuwalipa wanachama 92 kwa jumla ya TZS 810 milioni. Na ukilinganisha na mwaka jana kipindi cha Julai 2023hadi Machi 2023 Mfuko haukufanya malipo kwa mafao ya kuumia kazini (Fidia).

**Gharama za uwekezaji na usimamizi wa miradi**

Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko ulipanga kuwekeza TZS 197.5 bilioni na Mfuko ulitumia TZS 180.95 bilioni sawa na asilimia 91.6 ya makadirio, ukilinganisha na kipindi kama hiki cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Mfuko ulitumia TZS 159 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 14 ambapo ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa uwekezaji.

Aidha, kwa upande wa gharama za usimamizi wa miradi na uwekezaji Mfuko ulipanga kutumia TZS 1 bilioni na umetumia TZS 1.15 bilioni sawa na asilimia 110 ya makadirio. Ukilinganisha na kipindi kama hiki kwa mwaka 2022/2023 Mfuko umetumia TZS 1.14 bilioni kutokana na gharama za usimamizi wa miradi sawa na ongezeko la asilimia 1. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa gharama za usimamizi wa miradi.

Kwa kulinganisha utekelezaji wa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 na Julai 2022 hadi Machi 2023, Wastaafu wengi walilipwa ndani ya robo ya kwanza na robo ya pili na kupelekea kupungua kwa malipo katika robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2023/2024. Kwa upande wa mafao ya uzazi ni kwamba malipo yamelipwa kwa mujibu wa maombi yaliyopokelewa na kina mama waliojifungua au kutarajiwa kujifungua. Kiwango cha malipo ya Pencheni kimeongezeka kutokana na kuongezeka kwa muda wa uchangiaji na viwango vya mshahara kwa wanaostaafu. Kwa upande wa marejesho ukubwa wa mishahara kwa wastaafu wengi wa Sekta Binafsi ambao hawajatimiza sifa za kupata mafao kumeongeza idadi ya malipo yaliyowekwa ukilinganisha na idadi ya waliorejeshewa. Kwa upande wa mafao ya kuumia kazini (Fidia) limeanza kutekelezwa rasmi kuanzia mwaka wa fedha wa 2023/2024.

**4 .Ukaguzi**

Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Waajiri 1,388 walitarajiwa kufanyiwa ukaguzi. Waajiri 1,767 wamekaguliwa, kati ya hao waajiri 946 walikaguliwa kwa ufuatiliaji (Follow-up), waajiri 508 walikaguliwa kwa ukaguzi wa kawaida (Routine) na waajiri 313 walikaguliwa katika zoezi la ukaguzi la waajiri wapya (Survey Inspection). Na ukilinganisha na mwaka uliopita kipindi cha Julai 2022 - Machi 2023 waajiri 1,853 walitarajiwa kufanyiwa ukaguzi. Waajiri 2,183 walikaguliwa, kati ya hao waajiri 1,102 walikaguliwa kwa ufuatiliaji (Follow-up), waajiri 739 walikaguliwa kwa ukaguzi wa kawaida (Routine) na waajiri 342 walikaguliwa katika zoezi la ukaguzi la waajiri wapya (Survey Inspection).

Kwa kulinganisha utekelezaji wa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 na Julai 2022 hadi Machi 2023, kutokana na kuwepo kwa masuala mengi yaliyohitaji kufuatiliwa Mfuko ulifanya maamuzi na jitihada za ziada na waajiri wengi walifuatiliwa. Hasa katika suala la uwasilishaji wa michango kwa kutumia “Employers Portal” pamoja na kuwafuatilia waajiri wapya. Aidha kuanzishwa kwa Ofisi za mikoa zimendelea kuongeza Ufanisi wa Utendaji wa Ukaguzi ingawa mafanikio makubwa yanaonekana kwa kipindi cha robo tatu kwa mwaka

fedha 2022/2023 ukilinganisha na kipindi cha robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mfuko uliweza kufuatilia taasisi mpya nyingi za biashara na utajitahidi kuendelea kuengeza juhudi ili kuweza kufikia malengo yake.

### 4.5.2 Mafanikio

#### 4.5.2.1 Utekelezaji wa Ilani 2020 - 2025

Katika ibara ya 220 ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020 – 2025 Mfuko umeweza kutekeleza Ilani kwa asilimia 95. Mfuko umetekeleza maeneo yafuatayo: -

i. Kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Hifadhi ya Jamii kwa manufaa ya wananchi wote na taifa kwa ujumla.Mfuko wa Hifadhi ya jamii Zanzibar unaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ambapo mnamo mwaka 2022 Mfuko uliendelea kusimamia Sera na Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014 ambayo ilipelekea kufanyika marekebisho ya Sheria ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kuongeza Mafao mawili (Fao la upotevu wa ajira na Fao la kuumia kazini). Sambamba na hayo, Mfuko unaendelea kutoa elimu kwa wananchi wote kupitia vyombo mbali mbali vya habari juu ya utekelezaji wa Sera na Sheria za Mfuko;

ii. Kujenga Majengo ya Makaazi na Biashara katika eneo la Mombasa Unguja. SMfuko unaendelea na ujenzi wa Mradi wa Majengo ya makazi na Biashara katika eneo la Mombasa Unguja, Mradi huo utakua na nyumba 276 za gharama nafuu na Maduka ya biashara 42 na utekelezaji umefikia asilimia 85;

iii. Kuongeza kiwango cha usajili wanachama hadi kufikia asilimia 50 ya wanachama wanaoweza kufanya kazi.Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko ulitarajia kusajili waajiriwa 13,988 na kufanikiwa kusajili waajiriwa 8,827 ikiwa ni sawa na asilimia 63 ya malengo ya kusajili wafanyakazi wote wenye uwezo wa kufanya kazi. Hadi kufikia Machi 2024 Idadi ya wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar kwa Mfuko wa lazima ni 128,995. Kwa kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko umesajili waajiri 237 sawa na asilimia 98 ya makisio ya kuwasajili waajiri 243. Hadi sasa Mfuko umekuwa na Waajiri waliosajiliwa kufikia 3,029 na idadi ya wanachama wa Mfuko wa Hiari imefikia wanachama 12,618;

iv. Kufungua Ofisi za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii katika Mikoa ya Zanzibar Mfuko tayari umeshafungua Ofisi za Mikoa, ambapo kwa Mkoa wa Kusini Ofisi ipo katika Jengo la Halmashauri Wilaya ya Kusini (Kitogani) na kwa upande wa kaskazini Ofisi ipo Kinduni katika Jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mfuko unakamilisha taratibu za kufungua Ofisi Mkoa wa Kaskazini Pemba-Wete, na

v. Kuanzisha Mafao mapya kama vile Mafao ya Matibabu na kupunguza muda wa kulipa Mafao kufikia wiki mbili Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umefanikiwa kuongeza mafao mawili mapya kama ilivyoelekezwa kwenye ilani ikiwemo Fao la kuumia kazini na Fao la upotevu wa ajira. Kwa upande wa Fao la Matibabu tayari Serikali imeandaa utaratibu maalum wa kutoa Fao hilo.

Kwa kushirikiana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali Zanzibar (CAG), Mfuko umetengeneza Mfumo maalum wa kielektroniki wa mchakato wa upitiaji wa Mafaili ya wastaafu. Mafaniko ya Mfumo huo umepelekea upunguzwaji wa taratibu za ulipaji wa Mafao kutoka muda wa awali ambao ni zaidi ya siku 30 hadi ndani ya siku 14, ambapo kwa sasa mafao yote yanalipwa ndani ya siku 14 za kazi.

**Mafanikio kwa ujumla**

i. **Utekelezaji wa ahadi ya Mh. Rais ya Ongezeko la kima cha chini cha Pencheni**
Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umefanya malipo kwa ongezeko la pensheni kutoka TZS 90,000 hadi kufikia TZS 180,000 kuanzia mwezi Julai 2023. Hii ikiwa ni kutekeleza ahadi ya Mh. Rais aliyoitoa katika Sherehe za Mei Mosi 2023 huko Nungwi.

**ii. Uimarishaji Utendaji kazi**
Mfuko umeweza kuboresha, kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi kwa watendaji kwa kuwapatia mafunzo ya kazi na pia kubadilisha na kurekebisha baadhi ya miongozo na kanuni zinazoongoza utendaji kazi za kila siku za mfuko ili ziendane na hali halisi ya sasa. Miongozo hiyo imesaidia na kuupatia mfuko mafanikio makubwa kwenye utekelezaji wa majukumu yake.

**iii. Uwekezaji**

Kutokana na Uwekezaji unaoendelea kufanyika na pia kuongezeka kwa Mapato ya uwekezaji na Ukusanyaji wa Michango, Mfuko umeendelea kuimarika uhimilivu wake na kuongezeka uwezo wa kulipa Mafao kwa miaka 25 ijayo bila ya kutetereka.

**iv. Mifumo ya Tehama**

Kuanzishwa kwa mifumo mipya ya mawasiliano na TEHAMA kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na kurahisisha huduma kwa wanachama wetu, mifumo imesaidia wafanyakazi kujipima utendaji kazi na ufanisi wa huduma wanazozitoa. Pia mifumo imesaidia wanachama wetu kupata taarifa fupi kupitia simu zao za mkononi ikiwemo kujua mienendo ya michango yao na kupata taarifa mbali mbali zinazohusiana na Mfuko.

**v. Mafao Mapya**

Mfuko umeweza kutoa mafao mapya kwa wanachama wake mafao ambayo yalianzishwa mwaka 2023 ikiwemo Fao la kuumia kazini (Workers Compensation Benefit) na Fao la upotevu wa ajira (Unemployment Benefit), Mafao ambayo yameongeza imani kwa wanachama dhidi ya Serikali na Mfuko.

**vi. Ushirikiano kwa Taasisi za Kikanda na Kimataifa**

Mfuko umeweza kuimarisha ushirikiano na Taasisi za fedha na Taasisi zinazojishughulisha na masuala ya hifadhi ya jamii za kikanda na za nje ya nchi. Pia Mfuko unatarajia kusaini Mkataba wa mafahamiano (MoU) na Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi Tanzania (WCF) na Mfuko wa Pensheni kwa watumishi wa Umma Tanzania (PSSSF).

**vii. Kuogezeka Ukwasi wa Mfuko.**

Kutokana na utofauti baina ya dhima, mapato ya uwekezaji na rasilimali unazozimiliki, Mfuko umeendelea kuongeza ukwasi wake na unaweza kumudu kulipa mafao kwa wanachama wake bila ya wasiwasi wowote. Aidha Mfuko unalipa pencheni kwa wastaafu kila ifikapo tarehe 15 ya kila mwezi ili kuwapunguzia wazee msongamano katika Mabenki.

**Miradi inayotekelezwa**

Pamoja na kuwekeza kwenye masoko ya fedha na maeneo mengine yenye fursa nzuri za uwekezaji, mfuko tayari ulishapanga na kuanza kutekeleza miradi mbali mbali ya kijamii yenye tija na maslahi kwa Taifa kama ifuatavyo:

i. Kwa upande wa mradi wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu Majengo 14 yanaendelea kujengwa na utekelezaji umefikia asilimia 85 na mradi huo tayari umeshawekewa jiwe la msingi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi tarehe 24, Oktoba 2023 na unategemewa kukamilika ifikapo Julai 2024;

ii. Kwa upande wa mradi wa ujenzi wa maegesho ya gari Malindi, kwa sasa mradi huo unaendelea na ujenzi na utekelezaji umefikia asilimia 75. Mradi huo tayari umeshawekewa jiwe la msingi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi tarehe 21, Disemba 2023 na unategemewa kukamilika ifikapo Juni 2024;

iii. Kwa upande wa mradi wa kituo cha mabasi Kijangwani, Mfuko ulitumia Utaratibu wa Usanifu na ujenzi na kwa sasa Mkandarasi wa mradi huo anaendelea na ujenzi na utekelezaji umefikia asilimia 60. Mradi huo tayari umeshawekewa jiwe la msingi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi tarehe 31, Disemba 2023 na unategemewa kukamilika ifikapo Juni 2024;

iv. Ujenzi wa mradi wa Michezo na Biashara Mbweni, mradi unaendelea na hatua iliyofikia uwekaji "interlock" katika eneo la kuegeshea gari, sehemu ya "swimming pool" inaendelea na baadhi ya sehemu zimekamilika zikiwemo maduka, msikiti na uzio wa eneo;

v. Ujenzi wa Kituo cha kisasa cha Mabasi Malindi, Mfuko umeshapatiwa ruhusa kutoka Serikalini kwa sasa hatua za kusaini mkataba na Mshauri elekezi zimekamilika na unatarajiwa kuanza ndani ya robo ya nne ya mwaka 2023/24, na

vi. Kuendelea na ujenzi wa Soko la Mombasa ambapo mjenzi tayari ameshaanza kazi ya ujenzi wa soko kwa hatua za awali ambazo ni uchimbaji wa msingi na hatua ndogo ndogo ndani ya kipindi cha maandalizi ya ujenzi.

### 4.5.3 Changamoto

Mfuko unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

1. Uelewa mdogo wa umuhimu wa hifadhi ya jamii kwa baadhi ya waajiri na waajiriwa hali inayopelekea kutokuwajibika ipasavyo katika uchangiaji na usajili wa michago ya waajiriwa wao.

2. Kushuka kwa viwango vya faida katika uwekezaji wa Soko la fedha duniani hivyo wakati mwengine kuathiri malengo tunayojiwekea.

3. Kutokusomana kwa Mifumo ya utendaji kazi baina ya ZSSF, TRA, ZRA, Idara ya vitambulisho, ZIPA, Idara ya Uhamiaji na Kamisheni ya Utalii kunapelekea kukosekana kwa taarifa sahihi za waajiri, waajiriwa na wageni wanaoingia kufanya kazi na kuondoka.

**Hatua zanazochukuliwa kuondoa changamoto hizo ni pamoja na:**

1. Mfuko unaendelea kutoa elimu kwa ajili ya kuelewesha waajiri, waajiriwa pamoja na wachangiaji kwa hiari umuhimu wa kujisajili na kuchangia katika Mfuko.

2. Kuongeza juhudi katika utafutaji wa fursa za uwekezaji wenye tija ndani na nje ya nchi kwa mustakabali mpana wa uhimilivu wa Mfuko.

3. Kuanzishwa mahusiano ya karibu na taasisi za TRA, ZRA, Idara ya vitambulisho, BPRA, ZIPA, Idara ya Uhamiaji na Kamisheni ya Utalii kwa aajili kupata taarifa sahihi za waajiri, waajiriwa na wageni wanaoingia kufanya kazi na kuondoka.

### 4.6 Idara ya Maendeleo ya Ushirika

Idara ya Maendeleo ya Ushirika Zanzibar ipo chini ya Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji - Zanzibar. Idara hii ina dhamana ya kusimamia maendeleo na shughuli za Vyama vya Ushirika Zanzibar.

Idara imeanzishwa rasmi mwaka 1980, kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar Nambari 3 ya mwaka 1979. Hivi sasa Idara ya Maendeleo ya Ushirika inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Nambari 15 ya mwaka 2018, Sera ya Maendeleo ya Ushirika 2014 na kanuni mbili (Kanuni ya SACCOS na kanuni ya Vyama vya Uzalishaji) za mwaka 2019.

### 4.6.1 Maendeleo ya Ushirika Zanzibar

Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Idara ya Maendeleo ya Ushirika, pamoja na mambo mengine imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: -

- Imesajili vyama vya ushirika 1,645 (Unguja 791; Pemba 854), kati ya hivyo SACCOS 3 na vyama vya uzalishaji na utoaji huduma 1,642. Vyama vya uzalishaji vinajumuisha kilimo mchanganyiko, huduma za maduka na Biashara ndogo ndogo, Ufugaji, uvuvi na kazi za mikono kama vile kupamba, uchoraji, uchongaji, kudarizi, fundi gereji nk. Zoezi hili limeongeza idadi ya vyama vilivyosajiliwa kufikia jumla ya 5,713 Zanzibar (Unguja 2,805; Pemba 2,926);
- Imekagua hesabu za Vyama vya Ushirika 354 (Unguja 116 na Pemba 238). Matokeo yameonesha kwamba, kuna uhaba wa elimu juu ya uendeshaji na usimamizi wa vyama. Baadhi ya vyama vinaendeshwa bila ya bajeti, mpango kazi na utunzaji usioridhisha wa kumbukumbu za hesabu na vikao. Idara inaendelea kutoa elimu, mafunzo na ushauri juu ya mapungufu yanayojichomoza. Aidha jumla ya SACCOS 4 zimekata leseni ambazo ni BoT SACCOS, Bandari Taxi SACCOS, Mamlaka SACCOS na Amani SACCOS;
- Imefanya ukaguzi wa kawaida na ufuatiliaji kwa vyama 376 (Pemba 285; Unguja 91). Lengo ni kujiridhisha juu ya uendeshaji wa shughuli za vyama kwa ujumla, ikiwemo utunzaji wa vitabu vya hesabu, kumbukumbu na uendeshaji vikao kama zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria Nam 15 ya mwaka 2018, kanuni na sheria ndogondogo, pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa changamoto zinazoonekana;
- Imetoa mafunzo mbali mbali ikiwemo ya Dhana ya Ushirika, misingi na kanuni zake, Majukumu ya Viongozi, Uhamasishaji wa mitaji kupitia SACCOS na ujazaji wa fomu za maombi ya mikopo. Jumla ya washiriki 9,706 (wanawake 6,566; wanaume 3,140) kutoka vyama 1,387 (Unguja 483 na Pemba 904) walipatiwa mafunzo hayo;
- Kwa kushirikiana na wadau, imeadhimisha siku ya ushirika Duniani ambapo kilele cha maadhimisho hayo kilifanyika tarehe 8/7/2023 Ukumbi wa Polisi Ziwani na kuhudhuriwa na washiriki 414 (wanawake 224; wanaume 190). Maadhimisho hayo yaliambatana na shughuli za kufanya usafi, uchangiaji damu salama pamoja na Kongamano lililowashirikisha wataalamu waliobobea kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi,

Shirikisho la SACCOS Afrika (ACOSCCA) na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC). Kauli mbiu ilikua "Ushirika ni Wadau wa Kuharakisha Maendeleo Endelevu";

- Imeviunganisha vyama vya ushirika 269 (Unguja 252 na Pemba 17) kwenye taasisi za fedha ambazo ni CRDB 165, PBZ 60, Azania 29 na Equity 15 na kuwawezesha kufungua Hesabu zao katika Benki hizo. Lengo ni kurahisisha upatikanaji wa mikopo pia kuwa na usalama wa kuhifadhi fedha za wanachama;
- Idara imesimamia Mikutano Mikuu ya vyama vikubwa 27 vilifanya Mikutano ambayo iliyoambatana na chaguzi za viongozi. Lengo la mikutano hiyo ni kutoa Haki kwa wanachama kujadili shughuli za vyama vyao ikiwemo mafanikio na changamoto. Pia kuidhinisha Mipango kazi na Bajeti, kujadili utekelezaji wa shughuli za ushirika, kuthibitisha wanachama wapya na kuwatoa wanachama waliokosa sifa za kuwa wanachama na kuchagua Viongozi wapya wa vyama ya ushirika. Jumla ya washiriki katika mikutano hiyo ni 1,574 wakiwemo (wanawake 907: wanaume 667);
- Imeshiriki kutatua migogoro 6 kutoka vyama 6 vya ushirika, iliyojitokeza kwa kipindi hicho, vyama vyenyewe ni Bandari Taxi SACCOS, Twitange Cooperative, Jiti jeupe coop, Jitihada Njema, Fadhila Cooperative na Vinamba Cooperative;
- Imeshiriki kufanikisha maonesho ya Wajasiriamali katika Sherehe za Kizimkazi Day. Jumla ya vyama 12 vilishiriki Maonesho hayo wakiwa na bidhaa mbali mbali zikiwemo, Usarifu wa Tungule, Usarifu wa mwani, bidhaa za usumba, mikoba na vipochi, mkaa wa makaratasi, sabuni za maji, majani ya chai na ushoni. lengo ni kutafuta masoko kwa bidhaa za wajasiriamali hao;
- Imeshiriki zoezi la ukusanyaji wa Takwimu za ajira lililoanza tarehe 2/11/2023 hadi 22/12/2023. Jumla ya vyama 254 vilifikiwa na kufanya mahojiano na viongozi wao. Matokeo ya takwimu hizi yatatolewa na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Zanzibar (OCGS), na
- Kwa upande wa SACCOS hadi kufikia mwezi Disemba 2023 Vyama vilivyokuwepo ni 217 vyenye jumla ya michango TZS 24,031,135,057(Hisa, Akiba, Amana), aidha Mikopo iliyotolewa imefikia TZS 35,763,298,847 kwa Jumla ya wanachama 27,486 ( wanawake 14,332, wanaume12,607 na vikundi 547) *Jedwali na. 25* .

### 4.6.2 Mafanikio

**Mafanikio yaliyopatikana kwa SACCOS ni pamoja na: -**

- Kukua kwa Demokrasia katika SACCOS; kwa sasa SACCOS zinaendesha Mikutano yao na wanachama wanapata fursa ya kuhoji na kupata maelezo ya kutosha juu ya shughuli zinazoandaliwa na SACCOS zao kupitia Mikutano Mikuu. Hii ni kutokana na kufuatwa kwa sheria na kanuni za ushirika na pia taaluma za Ushirika kwa wanachama na viongozi wa SACCOS;
- Kuajiri: Baadhi ya SACCOS zimepata fursa ya kuajiri ili kuziimarisha katika utendaji, nafasi za uajiri ni Meneja, Afisa Mikopo, Madereva, Mshika fedha na Walinzi ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji katika SACCOS na vyama vya ushirika, na
- Kuwekeza: Baadhi ya SACCOS zimepata kuwekeza katika vitega uchumi mbali mbali kwa lengo la kutanua fursa za maendeleo na kujiongezea kipato, aidha baadhi ya maeneo ambayo SACCOS zimewekeza ni Maduka, Mashamba, Gari, Nyumba, kumbi za mikutano ).

### 6.6.3 Changamoto

Changamoto zinazo zikabili SACCOS za Zanzibar ni kama zifuatazo: -

- Baadhi ya SACCOAS hawatekelezi sheria hivyo kupelekea migogoro kwenye vyama vyao na ukiukwaji wa utkelezaji wa majukumu yao. Katika kulitatua hili Idara inaendelea kutoa taaluma ya Sheria na kanuni za ushirika ili kupunguza migogoro kwenye vyama vyetu;
- Ujuzi wa utumiaji wa vitabu vya Hesabu; SACCOS nyingi za Vijijini hazina ujuzi wa kutosha katika kutumia vitabu vya hesabu, hali hii inapelekea vyama hivyo kukosa kumbukumbu za hesabu. Katika kulitatua hili Idara tayari imeanzisha programu za mafunzo ambazo zimejumuisha somo la uwekaji wa kumbukumbu na namna ya kurikodi taarifa za fedha kwenye vyama vya ushirika;

- Kuibua mbinu za uwekezaji (taaluma ya Ujasiriamali); baadhi ya vyama vya ushirika havina taaluma ya ujasiriamali hali hii inapelekea kukosa kuwa na vyanzo ambavyo vitawasaidia wanachama na ushirika kwa ujumla. Katika kulitatua hili Idara tayari imeanzisha programu za mafunzo ambazo zimejumuisha somo la Wajasiriamali katika vyama vya ushirika;
- Ucheleweshaji wa taarifa za SACCOS; Baadhi ya SACCOS zinachelewesha taarifa za mwenendo wa Ushirika wao hii hupelekea kutokupatikana kwa taarifa za Portfolio ndani ya wakati, na
- Matumizi ya mfumo; SACCOS nyingi zilizopo nchini hazitumii Mifumo, ambayo ingaliweza kuwasaidia kurahisisha shughuli zao mbali mbali na kupatikana kwa urahisi ripoti mbali mbali.

**4.6.4 Matarajio na Muelekeo kwa Sekta ya fedha Machi 2025.**

- Vyama vya SACCOS kupata usimamizi wa karibu kutoka BoT kupitia Sheria ya Microfinance ya mwaka 2024;
- Kuwa na SACCOS zilizo imara kupitia Uhakiki maalum kwa Vyama vya SACCOS Zanzibar, na
- Kutoa Mafunzo kwa Wanachama, Viongozi na Watendaji wa SACCOS.

.

**Jadweli Nam. 25 : Zanzibar Saccos Portfolio as at December, 2023**

| | | NUMBER OF | | LOAN | LOAN | INDIVI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Nam | S/No. | SACCOS | TOTAL CAPITAL | DISBURSEMENT | OUTSTANDING | FEMAI |
| 1 | Urban District | 40 | 8,027,029,208 | 6,859,763,106 | 11,087,014,478 | 4,171 |
| 2 | West "A" | 13 | 719,744,625 | 1,267,122,656 | 625,448,250 | 726 |
| 3 | West "B" | 17 | 10,101,340,291 | 17,604,670,563 | 3,099,393,277 | 2,864 |
| 4 | North "A" | 15 | 251,909,000 | 844,617,000 | 158,885,000 | 1,110 |
| 5 | North "B" | 11 | 304,709,747 | 716,829,000 | 117,340,336 | 429 |
| 6 | Central | 19 | 392,975,920 | 597,585,100 | 205,004,748 | 641 |
| 7 | South | 8 | 196,997,276 | 344,259,800 | 77,511,200 | 276 |
| 8 | Wete | 26 | 818,207,500 | 990,688,222 | 353,619,250 | 1,496 |
| 9 | Micheweni | 12 | 203,381,600 | 384,385,000 | 128,331,000 | 532 |
| 10 | Mkoani | 20 | 853,600,000 | 1,726,750,000 | 372,830,000 | 610 |
| 11 | Chakechake | 36 | 2,225,223,890 | 4,426,628,400 | 2,571,805,461 | 1,477 |
| | TOTAL | 217 | 24,031,135,057 | 35,763,298,847 | 18,797,183,000 | 14,332 |

## 4.7 Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)

Masoko ya mitaji ni sehemu ya mfumo wa sekta ya fedha inayowezesha upatikanaji wa fedha za muda mrefu, yaani zaidi ya mwaka mmoja, kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo. Fedha za kugharamia shughuli za maendeleo huweza kupatikana kwa kuuza hisa za kampuni (shares), hatifungani za kampuni (corporate bonds), hatifungani za Serikali (Government bonds) au vipande katika uwekezaji wa pamoja (collective investment schemes). Fedha hupatikana kutoka kwa watu binafsi, taasisi na kampuni na hatimaye huwekezwa katika sekta ya uzalishaji na hivyo kuchochea maendeleo ya uchumi.

Hapa nchini, masoko ya mitaji yanaendelezwa na kusimamiwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ambayo imeanzishwa chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania. Pamoja na Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kuna kanuni na taratibu 19 zinazoongoza masuala mahsusi kuhusu masoko ya mitaji.

### 4.7.1 Majukumu makuu ya Mamlaka (CMSA)

Fungu la 10 la Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana linabainisha malengo na majukumu ya Mamlaka kama ifuatavyo:

a) Kuendeleza na kusimamia biashara katika masoko ya mitaji ili kuhakikisha kwamba biashara inafanyika kwa kufuata sheria, taratibu na miongozo ili kuleta usawa na haki kwa washiriki;
b) Kusajili na kutoa leseni kwa masoko ya dhamana, watendaji na washauri wa uwekezaji;
c) Kuandaa kanuni na miongozo katika sekta hii ili kulinda maslahi ya wawekezaji, kusimamia uadilifu na usalama wa masoko dhidi ya vitendo viovu; na
d) Kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu masuala yanayohusu biashara ya masoko ya mitaji.

### 4.7.2 Maendeleo Ya Masoko Ya Mitaji Kwa Kipindi Cha Julai 2023 Hadi Machi 2024

Katika kipindi cha miezi tisa, kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ilipanga kufanya yafuatayo:

i. Kuongeza idadi ya bidhaa na huduma katika masoko ya mitaji;
ii. Kusimamia Soko la Hisa ili kulinda maslahi ya wawekezaji;
iii. Kuongeza idadi ya wataalamu wa masoko ya mitaji wanaokidhi viwango vya kimataifa; na
iv. Kutoa elimu kwa umma.

Katika kipindi cha miezi tisa, Julai 2023 hadi Machi 2024, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imefanya yafuatayo:

i. Imewezesha kuongezeka kwa bidhaa na huduma katika masoko ya mitaji;
ii. Imesimamia Soko la Hisa na kuhakikisha kuwa shughuli katika soko zinafanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu;
iii. Imeendesha mafunzo yaliyowezesha kuongezeka kwa idadi ya wataalamu wa masoko ya mitaji wanaokidhi viwango vya kimataifa; na
iv. Imetoa elimu kwa umma ambayo imeongeza uelewa na ushiriki wa wananchi katika masoko ya mitaji.

Masoko ya mitaji yamegawanyika katika ngazi mbili ambazo ni masoko ya awali na masoko ya upili. Katika masoko ya awali, dhamana hutolewa kwa umma kwa mara ya kwanza ambapo kampuni au Serikali huweza kupata fedha kwa ajili ya miradi ya uwekezaji wa muda mrefu. Kwa upande mwingine, masoko ya upili yanawezesha wawekezaji kuuza na kununua dhamana ambazo zilizotolewa katika masoko ya awali.

#### 4.7.2.1 Masoko ya Awali

Shughuli zilizotekelezwa katika masoko ya awali zilikuwa ni pamoja na kuongeza idadi ya bidhaa na huduma katika masoko ya mitaji.

**Kuongeza idadi ya bidhaa katika masoko ya mitaji**

Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Mamlaka ilichambua na kuidhinisha bidhaa mpya sita (6), ikilinganishwa na bidhaa tatu (3) zilizopangwa kuidhinishwa, sawa na mafanikio ya asilimia 200. Bidhaa zilizoidhinishwa ni kama ifuatavyo: -

1) Hatifungani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kuhifadhi mazingira na yenye mguso na matokeo chanya kwa jamii yaani NMBMulticurrency Green, Social and Sustainability Bond yenye thamani ya TZS 1 trilioni , ambapo Benki ya NMB imepata idhini kutoa hatifungani hii katika awamu 10. Mauzo ya awamu ya kwanza iliyoitwa NMB Jamii Bond yamefanyika, ambapo kiasi cha TZS 212.94 bilioni kimepatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 284. CMSA pia, ilitoa idhini kwa benki ya NMB kuuza hatifungani hii katika fedha za kigeni, ambapo kiasi cha Dola za Marekani 73 milion zimepatikana, ikilinganishwa na Dola za Marekani 10 milioni zilizotarajiwa kupatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 730;

2) Hatifungani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kutunza na kuhifadhi mazingira na yenye mguso na matokeo chanya kwa jamii yaani CRDBMulticurrency Green, Social and Sustainability Bond yenye thamani ya TZS 780 bilioni, sawa na dola za Marekani milioni 300, ambapo benki ya CRDB imepata idhini ya kutoa hatifungani hii katika awamu tano. Mauzo ya awamu ya kwanza iliyoitwa CRDB Kijani Bond yamefanyika, ambapo kiasi cha TZS 171.83 bilioni kimepatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 430;
3) Hatifungani ya Miaka 10 ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Jiji la Tanga (Tanga-UWASA) yenye thamani ya TZS 53.1 bilioni. Hatifungani hii ina ubunifu unaojumuisha vipengele vinavyogusa taasisi ya umma, ujenzi wa miundombinu ya huduma endelevu za maji, utunzaji wa mazingira na miradi yenye uwezo wa kujiendesha kibiashara. Hatifungani hii imeweka historia ya kuwa hatifungani ya kwanza ya kijani kutolewa na taasisi ya umma katika Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara inayowezesha kupata fedha za kutekeleza shughuli za kuboresha miundombinu ya maji na utunzaji wa mazingira. Mauzo ya hatifungani hii yalizinduliwa rasmi tarehe 22 Februari 2024 na Mh. Dkt Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufungwa tarehe 4 Aprili 2024, ambapo kiasi cha TZS 54.72 bilioni zimepatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 103.
4) Hatifungani aina ya Sukuk iliyotolewa na Taasisi ya Fedha iTrust, ambapo kiasi cha TZS 11.32 bilioni zimepatikana sawa na mafanikio ya asilimia 226.4. Fedha zilizopatikana zinatumika kuwekeza katika biashara ndogo na za kati zinazokidhi misingi ya Shariah.
5) Hatifungani aina ya Sukuk iliyotolewa na shule ya Sekondari ya Wasichana Premier (Premier Girls Secondary School), ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kimepatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 100. Hatifungani hii imeweka historia ya kuwa hatifungani ya kwanza katika Sekta ya Elimu iliyotolewa na Shule ya Sekondari na ambayo inakidhi misingi ya Shariah. Fedha zilizopatikana zinatumika kutekeleza shughuli za kuboresha miundombinu ya Kituo cha Afya cha Shule ya Sekondari Premier, ambacho kinatoa huduma kwa wanafunzi wa shule, walimu, wafanyakazi na wananchi wanaoishi karibu na eneo la shule.
6) Mauzo ya hisa stahiki 72,957,660 za kampuni ya TCCIA Investment Plc kwa wanahisa wake kwa bei ya Shilingi 145 kwa kila hisa katika uwiano wa hisa moja mpya kwa kila hisa moja aliyokuwanayo mwekezaji,

ambapo kiasi cha TZS 10.58 bilioni kimepatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 100. Fedha zilizopatikana kupitia mauzo haya zimeiwezesha TCCIA Investment Plc kukuza uwekezaji wake katika dhamana mbalimbali za masoko ya mitaji, ikiwa ni pamoja na kuwekeza katika hisa za kampuni, hatifungani na vipande katika mifuko ya uwekezaji wa pamoja hapa nchini na katika ukanda wa Afrika Mashariki (EAC) na Kusini mwa Jangwa la Sahara.

#### 4.7.2.2 Soko la Upili

Shughuli zilizotekelezwa katika soko la upili zilikuwa ni pamoja na utoaji leseni kwa watendaji wa Soko na usimamizi wa biashara katika soko.

**Utoaji Leseni**

Mamlaka ilipanga kutoa leseni 170 za utendaji katika masoko ya mitaji.
Katika kipindi kilichoishia Machi 2024, jumla ya leseni 184 zilitolewa ikilinganishwa na leseni 170 zilizopangwa kutolewa, sawa na mafanikio ya asilimia 108.2. Leseni hutolewa baada ya Mamlaka kuchambua na kujiridhisha kuwa waombaji wanakidhi matakwa ya sheria. Leseni zilizotolewa zilikuwa katika makundi yafuatayo: Soko la Hisa (1); Soko la Bidhaa (1); Hifadhi Kuu ya Dhamana (1); kampuni za utendaji katika Soko la Hisa (18); Watendaji katika Soko la Bidhaa (5);Watendaji katika Soko la Hatifungani (8);Washauri Wateule (6); Washauri wa Uwekezaji (23); Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (10); Mameneja wa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (12); Watunza Dhamana (7); na Wawakilishi wa Taasisi zinazotoa huduma katika masoko ya mitaji (92).

**Usimamizi wa Soko**

Mamlaka ilipanga kusimamia masoko ya mitaji kwa kutumia mfumo wa vihatarishi (Risk Based Supervision) na kuhakikisha kuwa shughuli katika masoko zinafanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

a) Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Mamlaka ilisimamia masoko ya mitaji kwa kutumia mfumo unaozingatia vihatarishi yaani Risk Based Supervision (RBS) ambapo mfumo huu umewezesha kuchambua na kubaini mapema vihatarishi ambavyo vinaweza kuathiri utendaji wa Soko la Hisa, kampuni za watendaji wa Soko la Hisa, washauri wa uwekezaji, mifuko ya uwekezaji wa pamoja, kampuni zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa, na watendaji wengine katika masoko ya mitaji. Uchambuzi uliofanywa umewezesha kubaini vihatarishi na kuchukua

hatua stahiki, hivyo kuwezesha masoko ya mitaji kuwa salama, himilivu na imara. Mfumo wa RBS unatumika kimataifa na umesaidia watendaji wa soko kubaini viashiria hatarishi na kudhibiti mapema athari ambazo zingeweza kujitokeza. Kwa ujumla, utendaji katika masoko ya mitaji ulikuwa salama na uliendeshwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu husika.

b) Hadi kufikia Machi 2024, Mamlaka ilisimamia kampuni za watendaji wa soko la hisa, washauri wa uwekezaji, mifuko ya uwekezaji wa pamoja, kampuni zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa, na watendaji wengine katika masoko ya mitaji kwa kufanya yafuatayo: -

   i. Kukagua kampuni za watendaji wa soko la hisa (on-site inspections) na kuchambua taarifa za mahesabu (Off-site surveillance);
   ii. Kuchambua taarifa kuhusu mipango ya uwekezaji wa pamoja na uzingatiaji wa sharia na taratibu;
   iii. Kuchambua taarifa za hesabu za kampuni zilizoorodhesha hisa zao sokoni (DSE) ili kuhakikisha kuwa zinatoa taarifa kwa wanahisa na umma kwa ujumla kulingana na kanuni za kimataifa za utoaji taarifa za fedha (IFRS) na Sheria ya Kampuni ya mwaka 2002; na
   iv. Kufuatilia kwa wakati shughuli za kibiashara kupitia mfumo wa kufanyia biashara wa kielektroniki (ATS) wa DSE pamoja na Mfumo Mkuu wa Hifadhi (Central Securities Depository and Registry - CSDR).

Kwa ujumla utendaji katika masoko ya mitaji uliendeshwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu husika.

### 4.7.3 Biashara Katika Soko La Hisa La Dar Es Salaam

Mwenendo wa biashara katika soko la hisa hupimwa kwa kuangalia viashiria ambavyo huonyesha mwelekeo wa ufanisi wa soko. Viashiria hivyo ni pamoja na:

i. Mauzo katika Soko la Hisa;
ii. Mtaji wa Soko (Market Capitalisation);
iii. Fahirisi za Soko (Share Index); na
iv. Idadi ya wawekezaji.

#### 4.7.3.1 Mtaji wa Soko

Mtaji wa Soko la Hisa kwa kampuni za ndani yaani Domestic Market Capitalisation katika kipindi kilichoishia Machi 2024 uliongezeka kwa asilimia 9.2 na kufikia TZS 11.82 trilioni ikilinganishwa na TZS 10.82 trilioni katika kipindi kilichoishia Machi 2023. Kuongezeka kwa mtaji wa Soko la Hisa kwa kampuni za ndani kulitokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa. Kampuni hizo ni pamoja na CRDB Bank Plc, NMB Bank Plc, DSE Plc, National Investment Company Limited (NICO), Swissport Tanzania Plc, Twiga Cement Plc, Tanga Cement Plc, Tanzania Breweries Plc na Tanzania Cigarette Plc.

Mtaji wa Jumla wa Soko la Hisa yaani Total Market Capitalisation katika kipindi kilichoishia Machi 2024 ulipungua kwa asilimia 5.08 na kufikia TZS 14.94 trilioni ikilinganishwa na TZS 15.74 trilioni katika kipindi kilichoishia Machi 2023. Kupungua kwa Mtaji wa Jumla wa Soko la Hisa kumetokana na kupungua kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa DSE kutoka Soko la Hisa la Nairobi (Cross Listed Companies). Kampuni hizo ni pamoja na National Media Group, Jubilee Holding Limited, Kenya Airways na KCB Group Plc.

#### 4.7.3.2 Fahirisi ya Soko (Market Index)

Fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni za ndani yaani Tanzania Share Index (TSI) katika kipindi kilichoishia Machi 2024, iliongezeka kwa asilimia 9.1 na kufikia alama 4,462.29 ikilinganishwa na alama 4,091.56 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Machi 2023. Kuongezeka kwa Tanzania Share Index kunaashiria ufanisi wa soko la hisa kwa kampuni za ndani hususan kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa DSE, ambazo zinatoa huduma katika sekta za viwanda na fedha.

Fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni zote yaani All Share Index katika kipindi kilichoishia Machi 2024, ilipungua kwa asilimia 5.2 na kufikia alama 1,790.24 ikilinganishwa na alama 1,888.79 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Machi 2023. Kupungua kwa All Share Index kumetokana na kupungua kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa DSE kutoka Soko la Hisa la Nairobi

#### 4.7.3.3 Mauzo ya Hatifungani za Serikali

Mauzo ya hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam katika kipindi kilichoishia Machi 2024 yaliongezeka kwa asilimia 35 na kufikia TZS 3.95 trilioni, ikilinganishwa na TZS 2.93 trilioni zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Machi 2023. Kuongezeka kwa mauzo ya hatifungani

za Serikali kumetokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine.

#### 4.7.3.4 Mauzo ya Hatifungani za kampuni (Corporate Bonds)

Mauzo ya hatifungani za kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam katika kipindi kilichoishia Machi 2024 yaliongezeka kwa asilimia 278.7 na kufikia TZS 3.54 bilioni, ikilinganishwa na TZS 850.25 milioni zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Machi 2023. Kuongezeka kwa mauzo ya hatifungani za Kampuni kumetokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine.

#### 4.7.3.5 Mauzo ya Hisa (Equity Market Turnover)

Mauzo ya hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam katika kipindi kilichoishia Machi 2024 yaliongezeka kwa asilimia 106.31 na kufikia TZS 245.98 bilioni, ikilinganishwa na TZS 119.23 bilioni zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Machi 2023. Kuongezeka kwa mauzo ya hisa kumetokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine.

### 4.7.4 Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja

Mwenendo wa uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja ulikuwa mzuri. Thamani ya uwekezaji katika mifuko ya uwekezaji wa pamoja iliongezeka kwa asilimia 40.63 na kufikia TZS 2.0 trilioni katika kipindi kilichoishia Machi 2024, ikilinganishwa na TZS 1.4 trilioni katika kipindi kilichoishia Machi 2023. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine, pamoja na matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma kwa wawekezaji. *Jadweli namba 26.*

**Jedwali Namba 26: linaonesha mwenendo wa uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja.**

| | | 31 Machi 2024 | | 31 Machi 2023 | | Ongezeko la thamani | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Meneja wa Mifuko** | **Jina la Mfuko** | **Thamani ya Mfuko (TSH)** | **Bei ya Kipande (TSH)** | **Thamani ya Mfuko (TSH)** | **Bei ya Kipande (TSH)** | **Ongezeko la Thamani ya Mfuko** | **Ongezeko la Bei ya Kipande (%)** |
| UTT AMIS Plc | Mfuko wa Umoja | 347,871,026,357.21 | 1006.8175 | 311,546,992,055.25 | 903.7726 | 11.66 % | 11.40 % |
| | Mfuko wa Wekeza Maisha | 13,556,133,317.68 | 884.5232 | 8,200,947,926.48 | 772.1019 | 65.30 % | 14.56 % |
| | Mfuko wa Watoto | 16,968,294,965.39 | 648.95 | 9,568,813,873.36 | 569.5515 | 77.33 % | 13.94 % |
| | Mfuko wa Jikimu | 24,786,286,063.92 | 172.2141 | 19,448,126,708.07 | 162.7009 | 27.45 % | 5.85% |
| | Mfuko | 998,074,598,520.4 | 393.2 | 695,715,800,912 | 352.511 | 43.46 | 11.55 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | wa Ukwasi | 4 | 13 | .18 | 6 | % | % |
| | Mfuko wa Hatifungani | 605,135,269,207.04 | 116.7778 | 382,593,090,196.94 | 115.4184 | 58.17% | 1.18% |
| Watumishi Housing Investments | Mfuko wa Faida | 21,118,751,721.94 | 112.9776 | 14,634,005,454.77 | 102.5569 | 44.31% | 10.16% |
| Thamani ya Jumla | | **2,027,510,360,153.62** | | **1,441,707,777,127.05** | | 40.63% | |

### 4.7.5 Jitihada Za Mamlaka Katika Kukuza Masoko Ya Mitaji

Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Mamlaka ilifanya jitihada mbalimbali zilizolenga kukuza masoko ya mitaji hapa nchini. Jitihada hizo ni pamoja na kutoa elimu ya masoko ya mitaji kwa umma; kuongeza idadi ya wataalamu wanaokidhi viwango vya kimataifa; kuboresha na kuimarisha huduma za masoko ya mitaji.

#### 4.7.5.1 Utoaji Elimu kwa Umma

Katika jitihada za kuongeza idadi ya wawekezaji katika masoko ya mitaji, Mamlaka imeendelea kubuni, kuboresha na kutekeleza mikakati mbalimbali ya utoaji wa elimu kwa umma ili kuongeza uelewa juu ya masoko ya mitaji na dhamana. Mikakati hiyo ni pamoja na:

a) Kutoa mada mbalimbali kuhusu fursa zinazopatikana kwenye masoko ya mitaji kwa njia ya machapisho magazeti na mahojiano kwenye vipindi vya redio na runinga;

b) Kutengeneza na kusambaza shajara na vipeperushi vyenye elimu ya masoko ya mitaji na dhamana;

c) Kuchapisha na kusambaza kwa wadau mbalimbali Ripoti ya Mwaka ya Mamlaka ili kutoa elimu na taarifa ya utendaji kazi wa sekta ya masoko ya mitaji;

d) Kutoa mada na semina zinazohusu masoko ya mitaji kwa makundi maalumu kama vile wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Taasisi za elimu ya juu zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, Chuo cha Taifa cha Jeshi la Ulinzi; na wananfunzi wa vyuo na shule za sekondari; na

e) Kushiriki katika maonyesho ya kitaifa na kimataifa yenye lengo la kutoa elimu kuhusu fursa na faida za kutumia masoko ya mitaji, ikiwa ni pamoja na Wiki ya Wawekezaji Duniani (world Investor Week); Wiki ya Huduma za Fedha (Financial Services Week); na maonyesho ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba).

Utoji wa elimu kwa umma umewezesha kuongezeka ushiriki wa wawekezaji katika masoko ya mitaji, ambapo thamani ya uwekezaji katika masoko ya mitaji imeongezeka kwa asilimia 10.8 na kufikia TZS 38.36 trilioni katika kipindi kilichoishia Machi 2024, ikilinganishwa na TZS 34.61 trilioni katika kipindi kilichoishia Machi 2023.

#### 4.7.5.2 Kuongeza idadi ya wataalamu wanaokidhi viwango vya kimataifa

Katika jitihada za kuongeza wataalamu wenye weledi na ujuzi kwa ngazi ya kimataifa kwenye masoko ya mitaji, Mamlaka kwa kushirikiana na Taasisi ya Uwekezaji na Dhamana ya nchini Uingereza yaani Chartered Institute for Securities and Investment iliendesha mafunzo yanayotambulika kimataifa kwa watendaji wa masoko ya mitaji hapa nchini. Mafunzo haya yamewezesha kujenga uwezo na ufanisi kwa watendaji wa masoko ya mitaji hapa nchini, ambapo idadi ya washiriki imeongezeka kutoka 737 katika kipindi kilichoishia Machi 2023 na kufikia 798 katika kipindi kilichoishia Machi 2024, ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.3. Aidha, mafunzo haya yamewapatia wataalamu wa masoko ya mitaji fursa ya kupata leseni za kutoa huduma katika masoko ya Kitaifa, Afrika Mashariki na kimataifa.

#### 4.7.5.3 Kampuni Zinazotoa Huduma Katika Masoko ya Mitaji

Mamlaka iliendelea na usimamizi wa sekta ya masoko ya mitaji ikiwa ni pamoja na utoaji leseni na usimamizi wa kampuni zinazotoa huduma katika sekta hiyo. Katika kipindi kilichoishia Machi 2024, Kampuni ya Zan Securities Limited ni miogoni mwa kampuni zilizopewa leseni ya kutoa huduma ya ushauri katika uwekezaji katika masoko ya mitaji. Kampuni hii makao yake makuu yako Zanzibar, ambapo imeongeza wigo wa upatikanaji wa bidhaa na huduma za masoko ya mitaji kwa wananchi wengi zaidi. Aidha, Mamlaka iliiwezesha Kampuni ya Usimamizi katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (UTT-AMIS) inayosimamia mifuko sita (6) ya Uwekezaji wa Pamoja, ambayo ni Mfuko wa Umoja (Umoja Fund), Mfuko wa Wekeza Maisha (Invest Life Fund), Mfuko wa Jikimu (Jikimu Fund), Mfuko wa Watoto (Watoto Fund), Mfuko wa Ukwasi (Liquid Fund) na Mfuko wa Hatifungani (Bond Fund) kuendesha shughuli zake katika ofisi yake mpya mjini Unguja, Zanzibar kwa mujibu wa sheria. Hii inatoa fursa kwa wananchi walioko Zanzibar kuwekeza katika mifuko ya uwekezaji wa pamoja yaani collective investment schemes.

#### 4.7.5.4 Kuanzisha Mpango wa Mafunzo Endelevu kwa Wataalamu wa Masoko ya Mitaji

Mamlaka imezindua mpango wa mafunzo endelevu kwa wataalamu wa masoko ya mitaji yaani Continuous Professional Development Program (CPD) wenye lengo la kuhuisha uelewa na kujenga uwezo wa watalamu hawa kuhusu mabadiliko, changamoto za maendeleo na masuala yanayoibuka siku hadi siku katika nyanja za masoko ya mitaji nchini na ulimwenguni kote. Mafunzo endelevu kwa wataalamu wa masoko ya mitaji ni muhimu katika kuimarisha udhibiti na

kulinda maslahi ya wawekezaji katika masoko ya mitaji kwani yanawajengea watendaji ujuzi wa kudhibiti viashiria vya hatari vinavyoweza kujitokeza katika masoko ya mitaji. Hatua hii ni muhimu katika kutekeleza Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wenye lengo la kujenga uwezo wa rasilimali watu katika Sekta ya Fedha.

### 4.7.6 Changamoto Zinazokabili Masoko ya Mitaji Nchini

Masoko ya mitaji na dhamana yanakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(a) Ushiriki wa mifuko ya hifadhi ya jamii: Kumekuwa na upungufu wa ushiriki wa wanunuzi wakuu ambao ni mifuko ya hifadhi ya jamii ambao umetokana na maboresho yaliyofanywa katika sekta ya hifadhi ya jamii kwa kuunganisha mifuko ya jamii iliyokuwa ikihudumia sekta ya umma kutoka minne (LAPF, GEPF, PPF, PSPF) kuwa mmoja (PSSSF). Ushiriki wa mifuko ya hifadhi ya jamii baada ya kuundwa kwa PSSSF, haujawa mkamilifu kama ilivyokuwa hapo awali na hivyo kupunguza ukwasi kwenye soko la hisa.

(b) Elimu ya Masoko ya Mitaji kwa Umma: Elimu juu ya fursa na faida za kutumia masoko ya mitaji bado haijawafikia wadau wote.

(c) Utandawazi na matumizi ya teknolojia: Uwekezaji katika masoko ya hisa unahusisha utumiaji wa teknolojia ya mawasiliano na mitandao ambayo ina uwezekano wa kudukuliwa na kuhusishwa na vitendo vya jinai ambavyo vinaweza kuathiri mfumo wa sekta ya fedha.

### 4.7.7 Mapendekezo ya Namna ya Kupata Ufumbuzi wa Changamoto

Katika kukabiliana na changamoto zilizoainishwa hapo juu Mamlaka inafanya yafuatayo:

(a) Kujadiliana na mifuko ya hifadhi ya jamii ili kuongeza ushiriki wao kwenye masoko ya mitaji kwa lengo la kuongeza idadi ya wanunuzi wa ndani wa hisa na hivyo kuleta uwiano kati ya ugavi na mahitaji ya dhamana na kuogeza ukwasi katika Soko la Hisa;

(b) Kutoa elimu kwa umma juu ya fursa na faida za kutumia masoko ya mitaji kwa kutumia njia za kisasa, ikiwa ni pamoja na teknolojia ya habari na mawasiliano;

(c) Kufuatilia kwa karibu maendeleo katika masoko ya kimataifa kwa lengo la kujenga utayari wa kuchukua hatua stahiki pindi kunapotokea viashiria vya hatari kwenye masoko ya mitaji hapa nchini kwa kushirikiana na taasisi zinazosimamia sekta ya fedha na mawasiliano hapa nchini kwa kupitia 'Tanzania Financial Stability Forum' ambayo inahusisha Wizara ya Fedha na Mipango Tanzania; Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ya Zanzibar; Benki Kuu ya Tanzania; Mamlaka ya Usimamizi wa Bima; na Tume ya Maendeleo ya Vyama Ushirika Tanzania. Aidha, Mamlaka inashirikiana na mamlaka za usimamizi wa masoko ya mitaji katika ukanda wa Afrika Mashariki (EAC); Ukanda wa Kusini mwa Afrika (SADC) na Taasisi ya Kimataifa ya Usimamizi wa Masoko ya Mitaji (IOSCO) katika kubadilishana taarifa za kiusimamizi na kiudhibiti kwa lengo la kuchukua hatua stahiki kunapotokea viashiria vya hatari.

## SURA YA TANO

## 5.0 SEKTA YA MIUNDOMBINU

Sekta ya miundombinu nikiunganishi muhimu ambacho kinachochea maendeleo endelevu nchini na kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa Taifa. Sekta hii inasaidia kukuza na kuimarisha sekta nyenginezo kama vile biashara, utalii na viwanda. Serikali kupitia Sekta ya miundombinu inachukua jitihada mbalimbali kuhakikisha huduma za miundombinu zinapatikana kikamilifu nchini.

### 5.1 Wakala wa Barabara

Wakala wa barabara ni taasisi ya Serikali inayojitegemea ambayo imeundwa kwa Sheria Namba 11 kifungu Namba 3 (1) ya mwaka 2019. Taasisi hii imetokana na mageuzi yaliyofanywa ya muundo wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara (UUB) kwa lengo la kuimarisha huduma zinazotolewa na taasisi hiyo. Aidha, Serikali ilinunua vifaa vipya kwa kuiwezesha kuingia katika soko la ushindani na mapato yanayopatikana katika biashara na shughuli zinazofanywa na wakala ziwezekuendesha kazi zao za kila siku.

Hadi kufikia mwaka 2023, Zanzibar ina barabara zenye urefu wa kilomita 1,530.27 ukilinganisha na urefu wa kilomita 1,334.74 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 14.6, kati ya hizo zenye lami ni kilomita 946.85 mwaka 2023 ukilinganisha kilomita 865.50 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 9.3 na zisizo na lami ni kilomita 583.42 mwaka 2023 ukilinganisha na kilomita 469.23 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 24.3, Barabara kuu ni kilomita 358.31 mwaka 2023 sawa na kilomita 358.31 kwa mwaka 2022, barabara za vijijini kilomita 544.79 kwa mwaka 2023 ukilinganisha na kilomita 537.88 sawa na ongezeko la asilimia 1.2, barabara za mijini ni kilomita 125.33 kwa mwaka 2023 ukilinganisha na kilomita 69.2 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 81.1 na barabara za ndani ni kilomita 501.84 mwaka 2023 ukilinganisha na kilomita 379.34 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 32.2. *(Jadweli namba 27)*

**Jadweli Nam 27: Mchanganuo wa Barabara za Zanzibar mwaka 2023**

| Aina za Barabara | Urefu (km) | Zenye Hali Nzuri | | Zilizo Afadhali | | Zenye Hali Mbaya | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | km | Asilimia (%) | km | Asilimia (%) | km | Asilimia (%) |
| Barabara Kuu za Lami | 358.31 | 234.44 | 65.43 | 27.51 | 7.68 | 96.36 | 26.89 |
| Barabara Kuu zisizokua na lami | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Barabara za Vijijini zenye lami | 365.47 | 252.80 | 69.17 | 17.40 | 4.76 | 95.27 | 26.07 |
| Barabara za Vijijini zisizokua na lami | 179.32 | 0.00 | 0.00 | 62.70 | 34.97 | 116.62 | 65.03 |
| Barabara za Mjini zenye lami | 82.96 | 43.27 | 52.16 | 21.30 | 25.68 | 18.39 | 22.16 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Barabara za Mjini zisizokua na lami | 42.37 | 0.00 | 0.00 | 15.61 | 36.84 | 26.76 | 63.16 |
| Barabara za ndani zenye lami | 140.11 | 75.26 | 53.71 | 12.40 | 8.85 | 52.45 | 37.43 |
| Barabara za Ndani zisizokua na lami | 361.73 | 0.00 | 0.00 | 127.56 | 35.26 | 234.17 | 64.74 |
| **Jumla (km)** | **1,530.27** | **605.77** | **39.59** | **239.57** | **15.66** | **640.02** | **44.75** |

***Chanzo: Wakala wa Barabara, 2024***

### 5.2 Kitengo cha Mfuko wa Barabara

Mfuko wa Barabara ni mfuko ulioundwa kwa Sheria Namba 2 ya mwaka 2001 iitwayo *"Zanzibar Roads Fund Act, 2001"* pia kwasasa ni kitengo cha Serikali chenye kujitegemea. Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho Disemba 2008. Majukumu ya msingi ya Mfuko wa Barabara ni kuhakikisha kuwa fedha za matengenezo ya barabara zinakusanywa na vyombo vilivyowekwa na kuwasilishwa katika mfuko huo. Aidha, mfuko wa barabara una jukumu la kuhakikisha matumizi mazuri ya fedha hizo kwa kuwepo usimamiaji, ufuatiliaji na ukaguzi wa mara kwa mara kwa kuweka mpango maalum kila mwaka. Aidha, Mfuko hautengenezi barabara bali hutunza fedha na kufanya malipo kwa lengo la kukarabati barabara. na kuweka udhibiti sahihi wa fedha ili kusimamia ujenzi kwa kupita wakala wa utekelezaji na kuhakikisha malengo ya mwaka yanafikiwa kulingana na vipaumbele na viwango vya utendaji.

#### 5.2.1 Mapato ya Mfuko wa Barabara

Kwa kipindi cha Julai 2023 mpaka Machi 2024 Mfuko wa Barabara umekusanya jumla ya TZS 14.98 Bilioni ikilinganishwa na makusanyo ya TZS 10.57 Bilioni kwa kipindi kama hicho 2023 sawa na ongezeko la asilimia 29.43. Kwa mujibu wa sheria ya Mfuko wa Barabara kifungu Namba 4, mapato ya mfuko wa barabara yanapatikana kutokana na tozo ya nishati ya mafuta ( Fuel levy) na ada ya magari yanayoingia nchini (motor vehicle levy). Kwa kipindi cha Julai 2023 mpaka Machi 2024, Mfuko wa Barabara umewapatia Wakala wa barabara jumla ya TZS 8.0 Bilioni sawa na asilimia 46.6 ya makusanyo ya Julai, 2023 hadi machi 2024 kwa ajili ya kufanya ukarabati katika maeneo mbali mbali kwa Matengenezo ya Muda Maalum kama vile Kipapo- Mgelema (4km), Kuyuni – Kilani (2.5km), Mauani - Kisimani –Kajirambeni ( 1.3km), Minazini – Shikazako (0.5km), Mshelishelini – Bandamaji (1.2 km), (Jadweli namba 28).

**Jadweli Nam 28: Mchanganuo wa Barabara, Zilizofanyiwa Ukarabati kwa kiwango cha Lami Unguja na Pemba, (2022 – 2023)**

| AINA YA KAZI | Km | FEDHA (milioni) |
|---|---|---|
| **Matengenezo ya Muda Maalum:** Kipapo- Mgelema (4km), Kuyuni – Kilani (2.5km), Mauani - Kisimani –Kajirambeni ( 1.3km), Minazini – Shikazalo (0.5km), Mshelishelini – Bandamaji (1.2km) | 9.5 | 1,255.8 |
| Ujenzi wa mitaro na Kalvati | 4.5 | 2,155.6 |
| Matengenezo ya dharura: | 5.57 | 80.0 |
| Matengenezo ya kawaida ya usafi wa barabara ( Routine maintenance) | 546.75 | 812.71 |
| Matengenezo ya kawaida Uzibaji wa viraka (patchwork) | 6,109 $m^2$ | 160.0 |

***Chanzo: Mfuko wa Barabara, 2024***

### 5.2.2 Hatua Zinazochukuliwa

Kitengo cha Mfuko wa Barabara kimechukua hatua ya kushauri na kuainisha vyanzo vyengine vya mapato ikiwemo:-

i. Uwekaji wa mezani za kupimia uzito wa magari (overloading fine).
ii. Kupatiwa tozo kutoka katika upasishwaji wa vyombo vya moto
iii. Aidha kufanya ufuatiliaji wa kina (Monitoring) kwa collecting agent (TRA na ZRA) juu ya vyanzo viliopo sasa.

## 5.3 Nishati ya Umeme

Umeme ni nyenzo muhimu katika kufikia maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Nishati ya umeme hutumika kwa shughuli mbali mbali zikiwemo miradi ya uwekezaji, viwandani, majumbani na kuendeshea biashara. Sekta hio inaubora mkubwa katika maisha ya mwanadamu na kukuza maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi. Kawaida shughuli za usambazaji na uunganishaji wa nishati ya umeme kwa Zanzibar inatekelezwa na shirika la Umeme (ZECO) ambalo linamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100.

Kwa mwaka 2023 idadi ya wateja waliounganishwa na huduma ya umeme katika Gridi ya Taifa imeongezeka na kufikia wateja 32,099 ikilinganishwa na wateja 28,020 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 15 . Ongezeko hilo kwa kiasi kikubwa limetokana na agizo la Mh. Raisi wa Zanzibar la kushusha bei ya uungaji wa umeme kwa wateja wapya kwa asilimia 50 kutoka thamani ya TZS 400,000 hadi TZS 200,000 na kuongezeka kwa mahitaji ya umeme majumbani, shughuli za kiuchumi pamoja na uwekezaji. *(Jadweli namba 29)*

**Jadweli Nam 29: Idadi ya Wateja Wapya Waliounganishwa na Gridi ya Taifa Zanzibar (2019 – 2023)**

| **Eneo** | **2019** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **Asilimia (%) ya ukuaji kwa mwaka 2023** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 4,945 | 4,479 | 8,110 | 7,605 | 11,838 | 55 |
| Kusini Unguja | 3,532 | 3,199 | 7,604 | 7,144 | 6,124 | -14 |
| Mjini Unguja | 5,652 | 5,118 | 9,632 | 8,297 | 9,591 | 15 |
| Kaskazini Pemba | 1,321 | 1,105 | 3,235 | 1,989 | 2,264 | 13 |
| Kusini Pemba | 1,825 | 1,525 | 4,468 | 2,985 | 2,282 | -23 |
| **Jumla** | **17,275** | **15,426** | **33,049** | **28,020** | **32,099** | **15** |

***Chanzo: Shirika la Umeme Zanzibar, 2024***

Kiwango cha umeme kilichosambazwa kimeongezeka kwa asilimia 0.45 kufikia 505,736 kWh mwaka 2023 kutoka 503,460 kWh mwaka 2022. Thamani ya mauzo ya umeme katika kipindi hicho imepungua na kufikia TZS 139,703 bilioni mwaka 2023 kutoka TZS 141,835 bilioni mwaka 2022 *(Jadweli namba 30 na 31)*

**Jadweli Nam 30: Kiwango cha Umeme kilichosambazwa (2019-2023) (KWH "000")**

| MAELEZO | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Majumbani (Z 0) | 1,484 | 205 | 13 | 25 | 502 |
| Majumbani na Biashara (Z1) | 18,090 | 4,763 | 2,494 | 1,710 | 1,782 |
| ViwandaVidogovidogo (Z 2) | 8,206 | 9,713 | 8,914 | 14,163 | 20,098 |
| Viwanda vya Kati na Vikubwa (Z3) | 150,982 | 109,447 | 142,154 | 163,800 | 170,484 |
| Taa za Barabarani (Z4) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| TUKUZA | 243,338 | 269,384 | 286,136 | 323,762 | 313,371 |
| **Jumla** | **422,100** | **393,512** | **439,711** | **503,460** | **505,736** |

***Chanzo: Shirika la Umeme Zanzibar, 2024***

.

**Jadweli Nam 31: Thamani ya Umeme Uliosambazwa (2019 – 2023) (TZS Milioni)**

| MAELEZO | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Majumbani (Z 0) | 324 | 43 | 2.9 | 7.7 | 0.042 |
| Majumbani na Biashara (Z1) | 5,745 | 2,124 | 698.1 | 479 | 499 |
| ViwandaVidogo vidogo (Z 2) | 2,056 | 2,198 | 2,037.80 | 2,773 | 4,140 |
| Viwanda vya Kati na Vikubwa (Z3) | 29,095 | 20,348 | 24,263 | 28,284 | 28,811 |
| Taa za Barabarani (Z4) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| TUKUZA | 83,633 | 95,182 | 97,997 | 110,291 | 106,251 |
| **Jumla** | **120,852** | **119,895** | **124,999** | **141,835** | **139,703** |

***Chanzo: Shirika la Umeme Zanzibar, 2024***

## 5.4 Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)

Nishati ya maji ni muhimu kwa maisha ya mwanadamu na bila ya maji hakuna maisha. Serikali imekuwa ikihakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa Zanzibar na kuendelea kuvitunza na kuhifadhi vyanzo vya asili vya maji. Hili ni moja ya lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuwaondolea wananchi usumbufu wa upatikanaji wa huduma muhimu ya maji safi na salama. Kwa mwaka 2023 visima vinavyozalisha mji vimeongezeka kwa asilimia 2.66 kufikia jumla ya visima 309 kutoka visima 301 mwaka 2022. Hii imetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya maji safi na salama inayotokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na matumizi ya maji ikiwemo umwagiliajimaji katika shughuli za kilimo na viwandani, *(Jadweli namba 32)*

**Jadweli Nam 32: Visima Vinavyozalisha Maji na Kutoa Huduma (2019 – 2023)**

| Mkoa | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 50 | 49 | 46 | 46 | 47 |
| KusiniUnguja | 46 | 53 | 48 | 44 | 44 |
| MjiniMaghribi | 83 | 85 | 81 | 81 | 82 |
| Kaskazini Pemba | 47 | 48 | 48 | 49 | 53 |
| Kusini Pemba | 74 | 81 | 70 | 81 | 83 |
| **Total** | **300** | **316** | **293** | **301** | **309** |

***Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2024***

### 5.4.1 Usimamizi na Uendelezaji Rasilimali Maji na utatuzi wa changamoto za maji.

Wananchi wanazidi kupata uelewa juu ya umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji na kushirikiana na Serikali kuunga mkono hatua za Mamlaka ya Maji ya kuvitunza vyanzo hivyo. Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) inaendelea na kukabiliana na tatizo la kuondosha wavamizi katika maeneo ya vianzio vya maji kwa kufanya shughuli zisizostahiki katika maeneo hayo kama vile shughuli za kilimo na ujenzi wa nyumba za makaazi. Kwa mwaka 2023, ZAWA imeshuhulikia migogoro (122) inayohusiana na maeneo ya uzalishaji wa maji, kati yake migogoro (120) imetatuliwa na miwili (2) bado inaendelea. Chanzo cha migogoro hiyo nikuhusiana na maeneo yaliyochimbwa visimakupitia miradi mbalimbali kama vile mradi wa Bank ya Exim India, mradi wa fedha wa IMF Covid -19. Aidha Mamlaka ya Maji Zanzibar inaendelea kuchukua juhudi za kutatua migogoro iliyobakia , *(Jadweli namba 33)*.

**Jadweli Nam 33: Migogoro ya Watumiaji Maji Iliyopatiwa Ufumbuzi (2019-2023)**

| Hali ya migogoro | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Migogoro iliyomalizika | 0 | 0 | 3 | 5 | 120 |
| Migogoro inayoendelea | 1 | 0 | 6 | 2 | 2 |
| Jumla | 1 | 0 | 9 | 7 | 122 |

***Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2024***

### 5.4.2 Huduma ya Maji Vijijini

Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa mwaka 2023, imeweza kusimamia na kuendeleza kusambaza huduma ya maji safi na salama ilikurahisisha shughuli za maendeleo Unguja na Pemba. Hata hivyo miradi mitano (5) ya usambazaji maji imetekelezwa katika kipindi cha mwaka 2023 ikilinganishwa na miradi miwili (2) iliyotekelezwa mwaka 2022. Katika miradi hiyo, mradi mmoja (1) umetekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na miradi minne (4) imetekelezwa chini ya ufadhili wa Washirika wa Maendeleo. Huu ni mwendelezo wa azma njema ya

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuhakikisha kila mwananchi anapata maji safi na salama, *(Jadweli namba 34).*

**Jadweli Nam 34: Idadi ya miradi ya maji na wafadhili (2019-2023)**

| Aina ya Ufadhili | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 |
| Washirika wa Maendeleo | 4 | 2 | 1 | 1 | 4 |
| **Jumla** | **5** | **3** | **2** | **2** | **5** |

***Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2024***

### 5.4.3 Huduma za Maji Mijini mwaka 2023

Uzalishaji Maji.

**Jadweli Nam 35: Uzalishaji Maji.**

| WILAYA | UZALISHAJI 2019-2023 (Cubic Meter) | MAHITAJI KWA SENSA 2022 | UZALISHAJI (%) | MAPUNGUFU YA MAHITAJI KWA SENSA 2022 | MAPUNGUFU (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| MJINI MAGHARIBI | 55,614,880 | 125,043,660 | 44% | 69,428,780 | 56% |

***Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2024***

**Miundombinu na uchimbaji wa visima mwaka 2019-2023.**

Kwa mwaka 2019-2023, mikakati ya usambazaji maji safi na salama kwa Mkoa wa Mjini Magharibi bado inaendelea kuimarika kwa ulazaji wa miundo mbinu ya maji kiasi cha 11,732m, uchimbaji wa visima pamoja na usafishaji wa visima 81 kwa miaka hiyo, na ulazaji wa miundombinu ya maji unaendelea kupitia miradi ya JICA, Japan, UNICEF, Exim Bank, India. *(Jadweli namba 36).*

**Jadweli Nam 36: Mchanganuo wa Usambazaji Maji Mijini, 2019-2023.**

| **Kazi** | **Mwaka 2019/2023** | |
|---|---|---|
| Ulazaji wa miundo mbinu ya maji (m) | 11,732 | Kazi ya ulazaji wa miundombinu na uchimbaji wa visima vya maji unaendelea kwa miradi kama vilee JICA, Japan, UNICEF, Exim Bank India. |
| Uchimbaji na Usafishaji visima | 81 | Kama vile mradi wa ukarabati na uboreshaji wa huduma za maji (Ahueni ya Uviko 19), mfumo wa usambazaji maji Zanzibar (Mradiwa Exim Bank India.) |
| | | |

***Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2024***

**Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2024**

Kwa uwazi kabisa Serikali inaendelea na mikakati ya kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa Zanzibar kwa lengo la kuwaondolea usumbufu wanachi wake kupata huduma hiyo kwa wakati na uhakika. Serikali na washirika wa Maendeleo JICA, Japan, UNICEF, Exim Bank, India. wanaendelea kusimamia lengo la kutoa huduma za maji safi na salama katika maeneo yote ya mijini na vijijini na kuwawezesha wananchi wote kunufaika na huduma hiyo muhimu.

Jumla ya Visima 81 vimechimbwa na kuanza kutoa huduma kwa wananchi wa maeneo husika kama vile Bint Amrani – 2, Sebleni Kwa Wazee, Sebleni-Semuso, Chumbuni M'bunge, Chumbuni TASAF Chumbuni – 1, Chumbuni -1. *(Jadweli namba 37).*

**Jadweli Nam 37: Idadi ya Miradi Mipya ya Maji Vijijini (2019-2023)**

| Miradi | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Maendeleo ya miundo mbinu ya maji | 1 | 3 | 9 | 1 | 2 |
| Uchimbaji wa visima | 2 | 1 | 0 | 28 | 0 |
| Usafishaji maji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jumla | 3 | 4 | 9 | 29 | 2 |

**Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2024**

Vile vile kwa mwaka 2023, Mamlaka ya Maji Zanzibar imeweza kuzalisha na kusambaza maji jumla ya (Cubic Meter )191.9 milioni na kukusanya TZS 2.1 bilioni kwa mikoa yote ya Unguja na Pemba. Sawa na asilimia 6.3 ya mahitaji yote ya maji ya Cubic Meter 275.9 milioni.

**Jadweli Namba 38: Ukusanyaji Mapato, Uzalishaji na Usambazaji Maji (2022)**

| Mwaka | Jumla ya uzalishaji wa maji (Cubic meter) | Makadirio ya mahitaji ya maji (Cubic meter) | Upungufu katika mahitaji ya maji (percent) | Ukusanyaji wa mapato |
|---|---|---|---|---|
| **2019** | 56,447,478 | 83,295,998 | 32.20 | 4,412 |
| **2020** | 42,263,672 | 60,744,856 | 30.40 | 2,407 |
| **2021** | 131,812,147 | 240,465,120 | 45.20 | 2,613 |
| **2022** | 108,540,710 | 188,556,661 | 42.44 | 2,271 |
| **2023** | 191,959,675 | 275,980,481 | 30.0 | 2,127 |

***Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2024***

## SURA YA SITA

## 6.0 SEKTA YA ELIMU

### 6.1 Elimu na Mafunzo ya Amali

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuwekeza katika sekta ya elimu kwa ujenzi wa skuli mpya zenye vifaa vya kisasa vya maabara na kushajihisha wanafunzi kwa kuendelea kuwapa hamasa pale wanapofaulu kwa madaraja ya juu na kuondoa michango ya wanafunzi. Kuwekeza katika sekta ya elimu kunalihakikishia taifa kuwa na wataalamu na kuweza kutatua changamoto za maendeleo za sasa na baadae.

Kwa mwaka 2023 jumla ya skuli za Maandalizi zimeongezeka na kufikia 599 ikilinganishwa na skuli 498 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 20, kati ya Skuli hizo, Skuli za Serikali kwa mwaka 2023 zimefikia 56 kutoka skuli 42 mwaka 2022 na skuli Binafsi ni 543 mwaka 2023 kutoka skuli 456 kwa mwaka 2022. Hii inatokana na baadhi ya skuli binafsi kutokidhi vigezo na wakati mwengine kukosa wanafunzi kwa baadhi ya skuli. Skuli za Msingi mwaka 2023 zimefikia 576 kutoka skuli 488 kwa mwaka 2022, ambapo skuli za Serikali zimefikia 326 mwaka 2023 kutoka skuli 310 mwaka 2022 na skuli Binafsi, zimefikia 250 mwaka 2023 kutoka skuli 178 mwaka 2022. Aidha, Skuli za Sekondari mwaka 2023 zimeongezeka kufikia skuli 245 kutoka skuli 229 mwaka 2022, skuli za Serikali ni 216 mwaka 2023 kutoka skuli 217 mwaka 2022 na skuli Binafsi ni 29 mwaka 2023 kutoka skuli 12 mwaka 2022.

#### 6.1.1 Idadi ya Wanafunzi: Maandalizi, Msingi, Kati na Sekondari kwa Skuli za Serikali

Jumla ya wanafunzi 109,046 wameandikishwa katika skuli za Maandalizi na Msingi kwa mwaka 2023 kutoka wanafunzi 88,162 walioandikishwa kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 24. Kwa upande wa skuli za Maandalizi za Serikali, kwa mwaka 2023, idadi imeongezeka na kufikia wanafunzi 63,732 kutoka wanafunzi 61,765 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Kati ya hao, wanafunzi wa kiume ni 31,596 mwaka 2023, kutoka wanafunzi 30,859 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 2.3 na wanafunzi wa kike ni 32,136 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 30,906 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 4.

Idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika skuli za Msingi za Serikali imepungua kufikia wanafunzi 45,314 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 46,769 mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 3.1, kati ya hao wanafunzi wa kiume ni 23,436 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 24,364 mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 4 na wanafunzi wa kike ni 21,878 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 22,405 mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 2.3. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa skuli binafsi pamoja na ukaribu wa skuli hizo kwa jamii.

Jumla ya wanafunzi katika skuli za Msingi za Serikali kwa mwaka 2023 imefikia 324,457 kutoka wanafunzi 311,413 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 4.1. Aidha, wanafunzi wa kiume wamefikia 164,088 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 158,932 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 3.2, wanafunzi wa kike wamefikia 160,369 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 152,481 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 5.1. Hata hivyo, idadi ya wanafunzi katika skuli za Msingi za Serikali na Binafsi kwa mwaka 2023 imefika 380,638 kutoka wanafunzi 357,071 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 7.

Idadi ya wanafunzi waliofaulu Kidato cha Pili imepungua na kufikia 27,571 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 27,588 mwaka 2022 ambapo wanafunzi wa kiume ni 11,806 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 11,818 mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 0.1 na wanafunzi wa kike ni 15,765 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 15,770 mwaka 2022 , *(Jadweli namba 39).*

**Jadweli Nam 39: Idadi ya Wanafunzi wa Skuli za Sekondari za Serikali Kidato cha I-IV (2019-2023)**

| Mwaka | | Kidato | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jinsia | I | II | III | IV | |
| **2019** | Wanaume | 16,198 | 14,932 | 11,398 | 9,861 | 52,389 |
| | Wanawake | 17,903 | 17,181 | 14,831 | 16,198 | 66,113 |
| | **Jumla** | **34,301** | **32,113** | **26,229** | **26,059** | **118,502** |
| **2020** | Wanaume | 15,385 | 14,958 | 11,021 | 8,796 | 50,159 |
| | Wanawake | 16,636 | 16,965 | 15,039 | 12,817 | 61,457 |
| | **Jumla** | **32,021** | **31,923** | **26,059** | **21,613** | **111,616** |
| **2021** | Wanaume | 15,445 | 14,964 | 10,688 | 8,897 | 49,994 |
| | Wanawake | 16,710 | 16,260 | 15,051 | 12,693 | 60,714 |
| | **Jumla** | **32,155** | **31,224** | **25,739** | **21,590** | **110,708** |
| **2022** | Wanaume | 7,610 | 13,670 | 8,922 | 9,206 | 39,408 |
| | Wanawake | 11,075 | 14,960 | 12,261 | 12,902 | 51,198 |
| | **Jumla** | **18,685** | **28,630** | **21,183** | **22,108** | **90,606** |
| **2023** | Wanaume | 12,841 | 9,138 | 10,658 | 8,937 | 41,574 |
| | Wanawake | 11,547 | 12,068 | 14,292 | 13,029 | 50,936 |
| | **Jumla** | **24,388** | **21,206** | **24,950** | **21,966** | **92,510** |

**Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2024**

### 6.1.2 Idadi ya Wanafunzi: Maandalizi, Msingi, Kati na Sekondari kwa Skuli za Binafsi

Kwa mwaka 2023 idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika skuli za Maandalizi kwa skuli binafsi imeongezeka na kufikia 39,176 ukilinganisha na wanafunzi 33,511 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 17, ambapo wanafunzi wa kiume wamefikia 19,492 kwa mwaka 2023 ukinganisha na wanafunzi 16,649 kwa mwaka 2022, wanafunzi wa kike wamefikia 19,684 kwa mwaka 2023 ukilinganisha na wanafunzi 16,862 kwa mwaka 2022.

Kwa mwaka 2023 Idadi ya wanafunzi kwa skuli za Msingi imeongezeka na kufikia 56,181 kutoka wanafunzi 45,658 sawa na ongezeko la asilimia 23. Kati ya hao wanafunzi wa kiume wamefikia 27,886 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 22,844 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 22 na wanafunzi wa kike

wamefikia 28,295 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 22,814 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 24.

Idadi ya wanafunzi katika skuli za Sekondari (Kidato cha Kwanza hadi cha Nne) imeshuka na kufikia wanafunzi 11,023 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 12,683 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 13. Idadi ya wanafunzi wa kike imepungua na kufikia 5,811 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 6,758 mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 14 na idadi ya wanafunzi wa kiume pia imepungua na kufikia 5,212 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 5,925 mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 12. *(Jadweli namba 40).*

**Jadweli Nam 40: Idadi ya Wanafunzi wa Skuli za Sekondari za Binafsi Kidato I-IV (2019-2023)**

| **Mwaka** | **Kidato** | | | | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jinsia | I | II | III | IV | |
| **2019** | Wanaume | 1,485 | 1,247 | 1,508 | 1,328 | 5,568 |
| | Wanawake | 1,639 | 1,534 | 1,865 | 1,603 | 6,641 |
| | **Jumla** | **3,124** | **2,781** | **3,373** | **2,931** | **12,209** |
| **2020** | Wanaume | 1,609 | 1,402 | 1,553 | 1,359 | 5,923 |
| | Wanawake | 1,748 | 1,617 | 1,823 | 1,766 | 6,954 |
| | **Jumla** | **3,357** | **3,019** | **3,376** | **3,125** | **12,877** |
| **2021** | Wanaume | 1,608 | 1,501 | 1,403 | 1,282 | 5,794 |
| | Wanawake | 1,665 | 1,527 | 1,837 | 1,602 | 6,631 |
| | **Jumla** | **3,273** | **3,028** | **3,240** | **2,884** | **12,425** |
| **2022** | Wanaume | 1,590 | 1,522 | 1,586 | 1,227 | 5,925 |
| | Wanawake | 1,742 | 1,613 | 1,769 | 1,634 | 6,758 |
| | **Jumla** | **3,332** | **3,135** | **3,355** | **2,861** | **12,683** |
| **2023** | Wanaume | 605 | 1,517 | 1,672 | 1,418 | 5,212 |
| | Wanawake | 475 | 1,766 | 1,898 | 1,672 | 5,811 |
| | **Jumla** | **1,080** | **3,283** | **3,570** | **3,090** | **11,023** |

***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2024.***

### 6.1.3 Idadi ya Wanafunzi wa Skuli za Sekondari kwa Jinsia kwa skuli za Serikali na Binafsi.

Idadi ya wanafunzi wa Kidato cha Kwanza imeongezeka na kufikia wanafunzi 25,468 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 22,017 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 16, ambapo skuli za Serikali ni wanafunzi 24,388 na skuli Binafsi ni wanafunzi 1,080. Wanafunzi wa kidato cha Pili kwa mwaka 2023 wamepungua kufikia wanafunzi 24,489 kutoka wanafunzi 31,765 kwa mwaka 2022 kati ya hao wakiume ni 10,655 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 15,192 mwaka 2022 na wanafunzi wa kike ni 13,834 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 16,573 mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 16.5. Kwa upande wa kidato cha Tatu, kwa mwaka 2023 idadi imeongezeka na kufikia wanafunzi 28,520 kutoka wanafunzi 24,538 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 16.2, wanafunzi wa kiume ni 12,330 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 10,508 mwaka 2022 na wakike ni 16,190 mwaka 2023 kutika wanafunzi 14,030 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 15.3. Hii inatokana na baadhi ya wanafunzi kushindwa kuendelea na masomo na wengine kurejea mwaka.

Aidha, wanafunzi wa Kidato cha Nne kwa mwaka 2023 imeongezeka na kufikia 25,056 kutoka wanafunzi 24,969 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 0.1 ambapo kwa mwaka 2023 wanafunzi wakiume wamefikia 10,355 kutoka wanafunzi 10,433 mwaka 2022 kutoka na wakike ni 14,701 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 14,536 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 1.1.
Kwa upande wa Kidato cha nne, idadi ya wanafunzi waliofaulu imeongezeka na kufikia 20,800 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 18,774 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 10.8, jumla ya wanafunzi wa kiume ni 8,469 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 7,437 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 14, na wanafunzi wakike ni 12,331 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 11,337 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 9. Hii ni kutokana na mikakati na juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali pamoja na Wizara katika kuhakikisha elimu inakua nchini.

Kwa upande wa Kidato cha Tano kwa mwaka 2023, idadi imeongezeka na kufikia wanafunzi 3,831 kutoka wanafunzi 2,978 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 29, kati ya hao wanafunzi wakiume kwa mwaka 2023 ni 1,898 kutoka wanafunzi 1,511 mwaka 2022 na wakike kwa mwaka 2023 ni 1,933 kutoka wanafunzi 1,467 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 32. Hii inatokana na baadhi ya wanafunzi kujiunga moja kwa moja katika vyuo vya kati kwa ajili ya kuendelea na fani mbalimbali.

Kwa upande wa Kidato cha Sita idadi ya wanafunzi imeongezeka kwa mwaka 2023 na kufikia wanafunzi 6,512 kutoka wanafunzi 3,606 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 80.5, kati ya hao wanafunzi wa kiume ni 3,215 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 1,715 mwaka 2022 na wanafunzi wakike ni 3,297 mwaka 2023 kutoka wanafunzi 1,891 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 74.3, *(Jadweli namba 41).*

**Jadweli Nam 41: Idadi ya Wanafunzi wa Shule za Sekondari kwa Jinsia na Kiwango: Kidato I-VI (2019-2023)**

| Mwaka | Jinsia | Kidato | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | I | II | III | IV | V | VI | |
| **2019** | Wanaume | 17,683 | 16,179 | 12,906 | 11,189 | 1,405 | 1,036 | 60,398 |
| | Wanawake | 19,542 | 18,715 | 16,698 | 17,601 | 1,340 | 1,027 | 75,121 |
| | **Jumla** | **37,225** | **34,894** | **29,602** | **28,990** | **2,745** | **2,063** | **135,519** |
| **2020** | Wanaume | 16,994 | 16,358 | 12,573 | 10,155 | 1,557 | 1,267 | 58,904 |
| | Wanawake | 18,384 | 18,584 | 16,862 | 14,583 | 1,578 | 1,277 | 71,268 |
| | **Jumla** | **35,378** | **34,942** | **29,435** | **24,738** | **3,135** | **2,544** | **130,172** |
| **2021** | Wanaume | 17,053 | 16,465 | 12,091 | 10,179 | 1,953 | 1,250 | 58,991 |
| | Wanawake | 18,375 | 17,787 | 16,888 | 14,295 | 2,090 | 1,403 | 70,838 |
| | **Jumla** | **35,428** | **34,252** | **28,979** | **24,474** | **4,043** | **2,653** | **129,809** |
| **2022** | Wanaume | 9,200 | 15,192 | 10,508 | 10,433 | 1,511 | 1,715 | 38,051 |
| | Wanawake | 12,817 | 16,573 | 14,030 | 14,536 | 1,467 | 1,891 | 61,314 |
| | **Jumla** | **22,017** | **31,765** | **24,538** | **24,969** | **2,978** | **3,606** | **109,873** |
| **2023** | Wanaume | 13,446 | 10,655 | 12,330 | 10,355 | 1,898 | 3,215 | 39,797 |
| | Wanawake | 12,022 | 13,834 | 16,190 | 14,701 | 1,933 | 3,297 | 61,977 |
| | **Jumla** | **25,468** | **24,489** | **28,520** | **25,056** | **3,831** | **6,512** | **113,876** |

***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2024.***

### 6.2 Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Zanzibar ina jumla ya Vyuo Vikuu vitatu, kati ya hivyo kimoja ni cha Serikali na Vyuo Vikuu Viwili ni vya Binafsi. Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Vyuo Vikuu vya Serikali na Binafsi imepungua na kufikia wanafnzi 11,277 kwa mwaka wa masomo 2023/2024 kutoka wanafunzi 12,917 kwa mwaka wa masomo 2022/2023 sawa na upungufu wa asilimia 13 ambapo wanaume ni 4,545 kutoka 5,489 na wanawake ni 6,732 kutoka 7,428 upungufu huo unatokana na kuongezeka kwa idadi vyuo na programu mpya Tanzania bara ambazo hazipo katika vyuo vyetu hapa Zanzibar.. Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) imepungua na kufikia 6,807 kwa mwaka wa masomo 2023/2024 kutoka wanafunzi 7,279 mwaka 2022/2023 sawa na upungufu wa asilimia 6.4. Idadi ya wanafunzi wanawake imefikia 4,074 mwaka 2023/2024 kutoka wanafunzi 4,436 kwa mwaka 2022/2023 na wanaume imefikia 1,335 mwaka 2023/2024 kutoka wanafunzi 2,843 kwa mwaka 2022/2023.

Kwa upande wa Vyuo Vikuu Binafsi, idadi ya wanafunzi waliodahiliwa imepungua na kufikia wanafunzi 4,470 kwa mwaka 2023/2024 kutoka wanafunzi 5,638 kwa mwaka 2022/2023 sawa na upungufu wa asilimia 20.3. Kati ya hao wanawake ni 2,658 kwa mwaka 2023/2024 kutoka wanafunzi 2,992 kwa mwaka 2022/2023 sawa na upungufu wa asilimia 11.1 na wanaume ni 1,812 kwa mwaka 2023/2024 kutoka wanafunzi 2,646 kwa mwaka 2022/2023 sawa na upungufu wa asilimia 31.5

#### 6.2.1 Idadi ya Mikopo Iliyopangwa kutolewa

Kwa mwaka wa masomo 2023/24 jumla ya wanafunzi waliyo omba mkopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar ni 4,526 mwaka 2023/2024 kutoka wanafunzi 4,812 kwa mwaka wa masomo 2022/23 , kati ya hao, kwa mwaka 2023/24 wanaume ni 1,848 na wanawake ni 2,678 . Aidha, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar imefanikiwa kutoa mikopo kwa wanafunzi 2,502 kwa mwaka wa masomo 2023/24 kutoka wanafunzi 1,815 mwaka 2022/2023, sawa na ongezeko la asilimia 37.9 kwa mwaka wa masomo 2022/23, kati ya hao kwa mwaka wa masomo 2023/24 wanaume ni 1,127 na wanawake ni 1,375.Hii mimetokana na Serikali kuongezeka kiwango cha Bajeti ya mikopo ya Elimu ya juu kwa wanafunzi wa Zanzibar, *(Jadweli namba 42)*.

**Jadweli Nam 42: Idadi ya Wanafunzi wa Vyuo Vikuu Walioomba na Waliopata Mkopo Kutoka Bodi ya Mikopo Mwaka 2022/23 na 2023/24**

| **Walioomba Mkopo** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **2022/23** | | | **2023/24** | | |
| Wanaume | Wanawake | **Jumla** | Wanaume | Wanawake | **Jumla** |
| 2,358 | 2,454 | 4,812 | 1,848 | 2,678 | 4,526 |
| **Waliopata Mkopo** | | | | | |
| **2022/23** | | | **2023/24** | | |
| Wanaume | Wanawake | **Jumla** | Wanaume | Wanawake | **Jumla** |
| 889 | 926 | 1,815 | 1,127 | 1,375 | 2,502 |
| **Wanaoendelea na kunufaika naMkopo** | | | | | |
| **2022/23** | | | **2023/24** | | |
| Wanaume | Wanawake | **Jumla** | Wanaume | Wanawake | **Jumla** |
| 1,447 | 1,505 | 2,952 | 1,795 | 1,840 | 2,635 |

***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2024***

### 6.2.2 Mwenendo wa utoaji wa mikopo na Utaratibu wa kurejesha mikopo

Utoaji wa mikopo wa elimu ya juu Zanzibar ulianza mwaka wa fedha 2006/2007 na hadi kufikia mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya TZS 115,432,484,435 zimetumika kwa utoaji wa mikopo kwa wanufaika 18,454 ikilinganishwa na TZS 93,920,367,420 zilizotumika kwa utoaji wa mikopo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa wanufaika 15,952. Bajeti ya utoaji mikopo kwa mwaka wa fedha 2023/24 ni TZS 29,052,900,000 kwa wanafunzi 6,060 (wapya 2,425 na wanaoendelea ni 3,635) ikilinganishwa na TZS 17,660,151,300 zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2022/23. Hadi mwaka wa fedha 2022/2023 wanufaika 9,931 walikopeshwa kiasi cha TZS 69,815,844,724 ambazo ni mikopo iliyoiva kati ya TZS 93,920,367,420 zilizotumika kwa utoaji mikopo hadi mwaka 2023 na muda wa urejeshaji mikopo yao ulikuwa umefika kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za BMEJZ.

Aidha, katika utaratibu wa urejeshaji wa mikopo mnufaika hutakiwa kuanza kulipa mkopo wake miaka miwili tangu kumaliza masomo yake na kupata ajira. Mkopo huo hulipwa kwa kiwango maalum cha malipo kwa mwezi na mnufaika hulipa deni hilo bila ya nyongeza yoyote (Riba).

### 6.2.3 Ukusanyaji wa marejesho ya mikopo

Urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu Zanzibar ulianza mwaka wa fedha 2011/12 mwezi wa Februari takribani miaka sita (6) tangu kuanza utoaji wa mikopo na hadi kufikia mwezi Machi 2023 jumla ya wadaiwa 5,453 walikuwa wameanza kurejesha mikopo yao na jumla ya deni lao lilikuwa ni TZS 37,388,539,162. Aidha, hadi kufikia Machi mwaka 2023 jumla ya TZS 19,437,085,206.19 zimekusanywa kutoka kwa wanufaika hao (5,453) na kati ya hao wanufaika 1,813 wamemaliza kulipa mikopo yao.

Kwa kipindi cha miezi tisa ya mwanzo ya mwaka wa fedha 2022/2023 (Julai 2022- Machi 2023) jumla ya TZS 3,011,944,311.60 za marejesho ya mikopo zimekusanywa ikiwa ni wastani wa TZS 334,660,479 kwa mwezi.

Aidha, kwa kipindi Julai 2023-Machi 2024 jumla ya TZS 3,138,092,211 za marejesho ya mikopo zimekusanywa sawa na asilimia 84 ya lengo la mwaka.

### 6.2.4 Changamoto za Urejeshaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu

Kuna changamoto nyingi katika urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu, miongoni mwa hizo ni;

1. Kutokua tayari kwa wanafunzi walionufaika na mikopo kurejesha mikopo yao kwa hiari pale muda wa kurejesha mkopo unapofikia; baadhi ya wanufaika wa elimu ya juu wamekopa mikopo zaidi ya mmoja hivyo kutowezekana kulipa kiwango kinachotakiwa cha mkopo wa elimu ya juu kutokana kwa kuwepo kwa muongozo unaokataza zaidi ya thuluthi ya mshahara wa mfanyakazi. Kwa vile mnufaika hukopeshwa kiwango kikubwa kwa muda mfupi na kulipa deni lake kwa kipindi kirefu, kasi ya makusanyo ya marejesho hailingani na ongezeko la fedha zinazohitajika kukopeshwa kila mwaka. Kwa mfano muhitimu aliyekopeshwa TZS 8,000,000 kwa kipindi cha masomo ya miaka mitatu hulipa deni lake hilo kidogo kidogo baada ya kumaliza masomo kwa kipindi cha miaka mitano (5)..
2. Kuwepo kwa wadaiwa wanaostaafu kazi kabla ya kumaliza kulipa madeni yao ya mkopo wa elimu ya juu. Kwa sasa utaratibu hauruhusu kukata kiinua mgongo cha mstaafu aliyekopea mafao yake kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar kulipa deni la mkopo wa elimu ya juu;

3. Kuwepo wanufaika wanaochukuwa likizo bila malipo kabla ya kumaliza kulipa madeni yao na kupelekea marejesho ya mikopo yao ya kila mwezi kusita;
4. Ugumu wa kuwatambua na kupata marejesho ya mkopo kutoka kwa wanufaika wanaofanya kazi katika baadhi ya Taasisi za SMT; Ugumu wa kupata orodha za waajiriwa wapya wa Taasisi za Serikali ya Muungano yaTanzania kwa ajili ya kuhakiki majina ya wanufaika wa mikopo; na
5. Ugumu wa kupata marejesho ya mikopo kutoka kwa wafanyakazi wa Sekta Binafsi. Mara nyingi waajiri wao huwa hawako tayari kutoa mashirikiano.

### 6.2.5 Mapendekezo ya Kutatua Changamoto za Urejeshaji Mkopo wa Elimu ya Juu;

a. Elimu iendelee kutolewa kwa jamii juu ya umuhimu na wajibu wa kurejesha mikopo ya Elimu ya Juu;
b. Waajiri wote (Serikalini na Taasisi Binafsi) waendelee kupewa elimu juu ya wajibu wa kutekeleza Sheria Namba 3, 2011 ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (BMEJZ) na Sheria ya Utumishi wa Umma inayowataka kuwasilisha BMEJZ orodha za wafanyakazi wapya wanaowaajiri;
c. Kuwepo na ufuatiliaji wa kutosha wa makubaliano kati ya BMEJZ ya HESLB ya kubadilishana taarifa za waajiriwa katika Taasisi za Muungano na Taasisi za SMZ ili kuwatambua wanufaika wa mkopo wa BMEJZ wanaofanya kazi katika Taasisi za Muungano;
d. Makubaliano ya hiari ya kupokea mikato ya mikopo ya wafanyakazi wa Taasisi za SMT kupitia Hazina-SMT yafikiwe ili kuondoa changamoto ya kuchelewa kupokea mikato ya taasisi kwa wakati;
e. Ziwepo njia mbadala za kubadilishana taarifa na Taasisi nyengine ili kuwapata wanufaika wa mkopo kama vile uhakiki wa wanufaika wa mikopo wakati wa kutoa leseni za aina mbalimbali, kuomba mikopo katika Taasisi za Fedha na wakati wa kuomba hati ya kusafiria; na
f. Mkopo wa elimu ya juu uwe ni mkato wa lazima (compulsory deduction) kama ilivyo mikato ya kodi ya mapato na mifuko ya hifadhi ya jamii ili kusiwe na kikwazo cha thuluthi moja.

### 6.2.6 Mikakati ya Bodi Juu ya Urejeshajiwa Mikopo kwa Wanufaika

a. Kuunganisha mfumo wa (ZOLAS) na mifumo mengine ya Serikali ili kuwabaini walipo wanufaika ambao hawajaanza kulipa mikopo yao. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 BMWEJZ itakamilisha uunganishaji wa mfumo wa ZOLAS na Mfumo wa Rasilimali Watu na Mishahara wa SMZ unaosimamiwa na (OR)-Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha katika mwaka wa fedha 2024/2025, bajeti imetengwa kwa ajili ya kuunganisha mifumo ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Tanzania (HESLB);
b. Sheria Namba 2/2024 imeweka mazingira ya kuwafuatilia kwa karibu wanufaika wanaohitimu;
c. Sheria Namba 2/2024 imeweka mazingira ya kuwashajiisha wanufaika kulipa mikopo yao kwa kuweka punguzo maalum kwa watakaolipa vizuri mikopo yao;
d. Kupeleka barua za kuomba majina ya wahitimu wa elimu ya juu katika Taasisi mbalimbali za Serikali na Binafsi;
e. Kuendelea na ziara za uhakiki kwa kuwatafuta wafanyakazi waliokopa katika Taasisi mbalimbali kwa kushirikiana na waajiri;
f. Kuwatumia wadhamini wa wadaiwa katika kuwatafuta waliowadhamini na kuwataka waanze kurejesha mikopo yao;
g. Kuwashajiisha wahitimu kuwa Wazalendo kwa kurejesha mikopo yao kwa hiayari kupitia vyombo vya habari na makongamano;
h. Kufanya kazi kwa mashirikiano na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Tanzania (HESLB) kwa kubadilishana taarifa za wajiriwa katika Taasisi za Serikali na Binafsi na kufanya ziara za pamoja kwenye

## SURA YA SABA

## 7.0 SEKTA YA AFYA

Uchumi wa Zanzibar kama ilivyo kwa Mataifa yote Duniani unategemea nguvu kazi yenye afya na huo ndio umuhimu na msingi mkubwa wa sekta ya afya. Wananchi wenye afya njema ndio wazalishaji na watoa huduma katika sekta zote za kiuchumi na kijamii.

Huduma za afya zinaendelea kuimarika hapa Zanzibar, kupitia mageuzi yanayoendana na ujenzi wa miundombinu, uwekaji wa vifaa tiba vya kisasa, upatikanaji wa Madawa na rasilimali watu kwa lengo la kuimarisha na kusimamia utoaji wa huduma bora za afya nchini na kuendelea kutoa ushauri, elimu na matibabu kwa wananchi. Huduma za afya zinaendelea kutolewa bila malipo kwa matakwa ya Kikatiba na kisera na hutolewa katika Hospitali na vituo mbali mbali vya afya nchini.

### 7.1 Wataalamu wa afya

Mwaka 2023, idadi ya madaktari bingwa wamefikia 81 kutoka 71 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 14.0, ongezeko hilo limetokana na madaktari wengi wa kawaida kurejea masomoni na kupata shahada za juu hadi kufikia ngazi ya kuwa madaktari bingwa (specialist). Aidha madaktari bingwa kutoka nje ya nchi wamefikia Madaktari 12. Kwa Mwaka 2023 Madaktari wa kawaida wameongezeka na kufikia 478 kutoka 343 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 39.3. Wauguzi walioajiriwa Serikalini wameongezeka na kufikia 1,424 mwaka 2023 kutoka wauguzi 1,384 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 2.8. Mabwana na Mabibi afya wameongezeka hadi kufikia 227 mwaka 2023 ikilinganishwa na 171 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 32.7. Hii imetokana na watumishi wengi kubadilisha kada zao na kuongezeka kwa uwajiri wa Serikali kwa kipindi cha mwaka 2023.

### 7.2 Idadi ya Vituo vya Afya na Wagonjwa

Wizara ya Afya inajukumu la kuhakikisha Afya ya Wananchi ipo salama ili kujenga jamii yenye Afya njema kwa maendeleo endelevu ya jamii na Taifa kwa ujumla na kutoa huduma za afya kupitia ngazi mbali mbali za kitabibu kutokana na miongozo iliyopo ambayo inaenda sambamba na Shirika la Afya Ulimwenguni, huduma hizo hutolewa kupitia ngazi za vituo mbali mbali vya ya Afya msingi na sekondari (PHCUs na PHCU+) na hospitali za Wilaya na

Mkoa. Katika ngazi ya juu huduma za Afya Zanzibar zinapatikana katika hospitali za rufaa.

Zanzibar ina jumla ya vituo vya afya 339 mwaka 2023 kutoka 129 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 163. Idadi ya vituo vya (PHCUs na PHCU+) iliongezeka kwa asilimia 3.8 kutoka vituo 129 mnamo 2022 hadi vituo 134 mwaka 2023. Ongezeko hili limetokana na jitihada za makusudi za Serikali kuimarisha na kuboresha miundombinu ya Afya ili kutoa huduma stahiki kwa wananchi na kuimarisha maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Mwaka 2023 hospitali binafsi zimeongezeka kufikia 151 kutoka 137 mwaka 2022 sawa na asilimia 10.2.

## 7.3 Vizazi hai na wagonjwa walio tibiwa na kurudi majumbani

Jumla ya vizazi hai 57,162 vilirekodiwa katika vituo vyote vya afya mwaka 2023 ambapo Wilaya ya Mjini ina idadi kubwa ya watoto wanaozaliwa wakiwa hai ikilinganishwa na Wilaya nyengine. kwa kipindi cha miaka mitano idadi ya watoto wanaozaliwa wakiwa hai katika vituo vya afya imekuwa ikiongezeka kutoka mwaka 2019 hadi 2023 *(Jedwali 43*)

**Jadweli Nam. 43 Idadi ya Vizazi hai kwa Wilaya za Zanzibar, 2019-2023**

| Wilaya | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini A‘ | 3,657 | 4,432 | 4,590 | 5,112 | 5,600 |
| Kaskazini ‘B’ | 655 | 576 | 532 | 512 | 648 |
| Kati | 924 | 1,104 | 1,010 | 1,154 | 1,830 |
| Kusini | 1,148 | 1,349 | 1,578 | 1,619 | 1,849 |
| Magharibi ‘A’ | 754 | 928 | 1,580 | 1,819 | 2,805 |
| Magharibi ‘B’ | 2,136 | 2,633 | 2,490 | 2,484 | 3,939 |
| Mjini | 22,248 | 19,551 | 23,013 | 23,669 | 22,777 |
| Chake chake | 5,296 | 4,994 | 5,673 | 5,381 | 5,513 |
| Micheweni | 3,691 | 3,786 | 4,140 | 3,900 | 4,359 |
| Mkoani | 3,389 | 2,915 | 3,298 | 3,027 | 3,371 |
| Wete | 4,202 | 4,439 | 4,188 | 3,961 | 4,227 |
| **Jumla kuu** | **48,100** | **46,707** | **52,092** | **52,638** | **56,918** |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

Idadi ya wagonjwa waliotibiwa na kurudi majumbani kwa mwaka 2023 imeongezeka na kufikia wagonjwa 1,941,919 ikilingaishwa na idadi ya wagonjwa 1,923,0,16 mwaka 2022. Sawa na ongezeko la asilimia 1.0. Hii ni kutokana kuongezeka kwa idadi ya watu nchini.

## 7.4 Huduma kwa Kinamama Wajawazito

Mwaka 2023, idadi ya vizazi hai waliozaliwa imeongezeka kufikia watoto 56,918 ukilinganisha na watoto 52,638 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 8.5. Hali hii imetokana na kuimarika kwa huduma za afya na jitihada za mabibi na mabwana afya kuwapatia wajawazito elimu kwa muda sahihi, na kutoa muongozo wa upatikanaji huduma bora wakati wa ujauzito kumepekea muamko mkubwa kwa kina mam na kina baba kuhusika kwenye elimu ya uzazi salama na mifumo ya lishe sahihi kwa kinamama kipindi cha ujauzito. Hali hii imepelekea kuongezeka kwa vizazi hai ambavyo ni nguvu kazi ya baadae ya taifa.

## 7.5 Idadi ya Kinamama Wajawazito Waliojifungua kwa Njia ya Upasuaji na Mimba Zilizoharibika

Kwa mwaka 2023,Jumla ya kinamama waliojifungua hospital wamefikia 56,965 ambao 49,680 wamejifungua kwa njia ya kawaida na kinamama 7,285 wamejifungua kwa njia ya upasuaji ambapo hali hii imeongezeka kwa mwaka 2023 ukilinganisha na kinamama 6,684, mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 9.0 (Jadweli Nam 44). Wizara ya afya inaendelea na tafiti ili kuangalia sababu za kuongezeka kwa idadi ya kina mama wanaojifungua kwa njia ya upasuaji, pamoja na zile zilizozoeleka za kubeba mimba katika umri mdogo au umri mkubwa, watoto kuwa wakubwa tumboni, kuchelewa au kutokwenda kliniki mapema kwa kina mama wajawazito na wazazi kushindwa kujifungua kwa njia ya kawaida. Vile vile watoto kufia matumboni mwa mama zao kabla ya kuzaliwa.

Kwa upande mwengine, idadi ya kinamama walioharibu ujauzito imepungua kufikia mimba 3,942 mwaka 2023 kutoka mimba 5,214 mwaka 2022 sawa na upungufu asilimia 24.3. Hali hii imesababishwa na jitihada ya Wizara kutoa elimu ya uzazi kwa mama, mijini hadi vijijini juu ya ubebaji mimba kwenye muda na umri sahihi ili kuepuka, mimba kutunga nje ya mji wa uzazi, wajawazito kupata vifafa vya mimba, kushuka mafuko ya uzazi kwa kinamama wakati wa ubebaji mimba matumizi mabaya ya dawa Elimu hiyo imetolewa kupitia wataalamu wa Afya ya mama na mtoto.

**Jadweli Nam 44: Kinamama Wajawazito Waliojifungua kwa njia ya Upasuaji na Waliohuribu Mimba (2019 – 2023)**

| | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya kina mama waliojifungua kwa njia ya upasuaji | 4,409 | 4,482 | 6,028 | 6,684 | 7,285 |
| Idadi ya mimba zilizoharibika | 3,741 | 1,481 | 2,913 | 5,611 | 3,942 |

*Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24*

### 7.6 Mpango wa Kumaliza Malaria Nchini.

Zanzibar inaendelea na mikakati ya kukupambana kudhibiti ugonjwa wa Malaria na kwa kiasi kikubwa imefanikiwa kupunguza licha ya changamoto ambazo zinaibuka na kupelekea kuzorotesha jitihada za kuondosha maradhi haya chini ya program (Zero Malaria inaanza na mimi na wewe ), mikakati mbalimbali imeandaliwa ili kufikia azimio hilo. Kwa mwaka 2023 jumla ya wagonjwa 18,283 walichunguzwa vimelea na kugundulikana na malaria ikilinganisha na wagonjwa 4,557 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 301.0. Aidha matokeo ya vifo vitokanavyo na malaria nchini vimeongezeka kufikia 29 mwaka 2023 vikilinganishwa na vifo 4 kwa mwaka 2022. Kwa mujibu wa uchunguzi wa kitabibu umeonesha ongezeko la vifo hivyo limetokana na mripuko wa ghafla wa ugonjwa huo na wananchi wengi kuchelewa kuwahishwa hospitalini kwa wakati (Jadweli Nam 45).

**Jadweli Nam 45: Hali ya Malaria nchini na idadi ya vifo 2019-2023**

| | Hali ya Malaria nchini | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Idadi ya wagonjwa wa malaria | 6,963 | 14,188 | 6,616 | 4,557 | 18,283 |
| 2 | Vifo vya malaria | 13 | 20 | 9 | 4 | 29 |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

### 7.6.1 Vituo vinavyotumia MRDT

Kwa mwaka 2023, vituo vinavyotumia darubini (MRDT) vimefikia 169 ikilinganishwa na vituo 141  mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 19.8. Vipimo hivi vinatumika kwa ajili ya uchunguzi wa vimelea vya Malaria. Wizara kupitia Mpango wa kudhibiti Malaria inafuatilia kujua ni maeneo gani yanayoripotiwa kuwa na wagonjwa wengi wa malaria na kuchukua hatua za kutoa tiba na kinga kwa maeneo husika.

### 7.6.2 Dawa Zinazotumika Kutibu Malaria Nchini

Kwa sasa dawa zilizothibitishwa na kupewa nafasi ya kwanza kutumika kwa kutibu ugonjwa wa malaria ni dawa zile zile ambazo zinaendelea kutumika nchini ambazo ni mchanganyiko wa "Artemisinin Based Combination Therapy (ACTs)"kiwango cha 0.25mg/kg na *"Primaquinephosphate, Artemether Lumefantrine" na "primaquine"* inatumika kama njia ya pili ya tiba ya kutibu ugonjwa wa malaria sugu, dawa hizi ziko katika mfumo wa vidonge nchi nzima. Kwa upande wa watoto kuanzia miezi 0-5 wanapatiwa dawa yenye viwango vya kitoto "Pediatric formular" hii ni kwa mujibu wa ushauri wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kupitia Madaktari bingwa wa watoto waliopendekeza utumiaji wa dawa hiyo kwa watoto. Serikali imepiga hatua kubwa katika kupambana na malaria kwa lengo la kufikia kiwango cha chini ya asilimia zero. Wizara inaendeleza mikakati mbali mbali ya kudhibiti malaria ikiwemo programu ya Zanzibar bila malaria inawezekana kupitia utoaji wa vyandarua kwa kaya mbali mbali nchini.

### 7.6.3. Madaraja ya Dawa za Kutibia Malaria Nchini

Wizra ya Afya imeweka muongozo wa kutibu Malaria nchini ili kutoa tathmini halisi ya kitabibu juu ya matumizi sahihi ya utumiaji dawa kwa Hospitali za Serikali na Binafsi ili kuepuka kutumia madawa yasiyofaa kwa kutibia ugonjwa huo

i. Daraja la kwanza ni Artesunate +Amodiaqune (ASAQ)

ii. Daraja la pili ni Dihydroartemisin+Piperaquine (DHAP), Artemether+ Lumefantrine (ALU)

iii. Daraja la tatu ni Sindano ya Artesunate au Sindano ya Artemether7.6.4. Mikakati ya Kupambana na malaria Zanzibar 2019-2023

### 7.6.4 Mikakati ya Kupambana na Malaria Zanzibar 2019-2023

i. Utumiaji wa dawa mchanganyiko kwa homa ambayo sio kali (Artesunate +Amodiaqune (ASAQ), Dihydroartemisin+Piperaquine (DHAP), Artemether+ Lumefantrine (ALU) na kwa homa kali ni Sindano ya Artesunate au Sindano ya Artemether;

ii. Upulizaji wa dawa (viatilifu) ya kuuwa mbu wa malaria majumbani;

iii. Utumiaji wa vyandarua vyenye dawa ya Muda mrefu kwa ajili ya kuua na kufukuza mbu waenezao ugonjwa wa malaria;

iv. Ufuatiliaji wa wagonjwa majumbani waliogundulika kuwa na ugonjwa wa malaria kwa lengo la kukata maambukizi ya malaria;

v. Utiaji wa viatilifu (dawa) katika mazalio ya mbu, na

vi. Utoaji wa elimu ya afya kwa jamii juu ya kujikinga na ugonjwa wa malaria.

#### 7.6.4.1 Kazi kuu zilizofanywa na Programu katika kupambana na malaria Zanzibar mwaka 2019-2023

i. Kuhakikisha upatikanaji, ufikiaji na utumiaji sahihi wa dawa za Malaria katika vituo vya afya vya Serikali na binafsi kwa Unguja na Pemba;

ii. Upulizaji wa dawa (viatilifu) ya kuuwa mbu wa malaria majumbani;

iii. Kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya kutosha kwenye umuhimu wa utumiaji wa vyandarua vyenye dawa ya Muda mrefu kwa ajili ya kuua na kufukuza mbu waenezao ugonjwa wa malaria;

iv. Ufuatiliaji wa wagonjwa majumbani waliogundulika kuwa na ugonjwa wa malaria kwa lengo la kukata maambukizi ya malaria;

v. Utiaji wa viatilifu (dawa) katika mazalio ya mbu;

vi. Utoaji wa elimu ya afya kwa jamii juu ya kujikinga na ugonjwa wa malaria Pamoja na kushajihisha matumizi sahihi ya vyandarua;

vii. Uchunguzi wa vinasaba vya mbu waenezao Malaria, na

viii. Kuwepo kwa kikosi kazi cha kukamata na kuchunguza mbu wanaosambaza malaria,

### 7.6.4.2 Idadi ya Nyumba Zilizopuliziwa Dawa

Wizara inaendelea na mikakati maalum ya kupambana na kumaliza Malaria Zanzibar Wananchi wanapewa elimu na kupata muamko mkubwa ili wakubali kupigiwa dawa kwa hiari baada ya kuelewa athari za ugonjwa huo. Kwa mwaka 2023 jumla ya nyumba zilizopuliziwa dawa zimeongezeka na kufikia 47,963 ikilinganishwa na nyumba 18,697 zilizopuliziwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 156.5. (Jadweli Namba 46).

**Jadweli Nam 46: Idadi ya nyumba zilizopuliziwa dawa 2019-2023**

| Mwaka | Matarajio | Nyumba zilizotambulika | Nyumba zilizopigwa dawa | Asilimia ya nyumba zilizopigwa dawa | Wananchi waliokingwa na Malaria | Watoto chini ya miaka 5 | Wajawazito waliokingwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2019** | 88,355 | 99,126 | 94,339 | 95.2 | 477,243 | 82,717 | 12,892 |
| **2020** | 41,231 | 45,956 | 44,534 | 96.9 | 225,379 | 37,079 | 6,350 |
| **2021** | 62,982 | 65,288 | 61,856 | 94.7 | 322,489 | 52,128 | 8,224 |
| **2022** | 8,435 | 8,187 | 8,003 | 97.8 | 42,881 | 7,247 | 1,029 |
| **2023** | 51,505 | 50,750 | 47,963 | 94.5 | 250,239 | 41,454 | 7,385 |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24.***

## 7.7 Huduma za Upasuaji Mkubwa

Serikali inaendelea kuchukua Jitihada za makusudi kuhakikisha huduma ya upasuaji mkubwa inapatikana Nchini kwa lengo la kuboresha Afya za wananchi na kupunguza gharama kubwa ya upatikanaji wa huduma hii. Upasuaji wa uti wa mgongo na ubongo (Neurosurgery) kupitia kambi maalumu ya wataalamu wazawa na wakigeni kutoka nchini Hispania na Israel. Huduma hii imeanzishwa kwa msaada wa Taasisi ya 'NED Surgical Institute' ya nchini Hispania na imepelekea kupunguza wimbi kubwa la wagonjwa kwenda nje ya nchi, haya ni mapinduzi makubwa ya kitabibu nchini ambayo yanaamsha ari na kujenga uwezo wa madaktari wetu. Mwaka 2023, kitengo kimefanikiwa kuwapatia matibabu wagonjwa 256. kutoka wagonjwa 322 mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 20.4 . Serikali kupitia Wizara inaendelea na mikakati ya kuongeza

juhudi za kitaalamu na kuongeza idadi ya wataalamu wa fani husika ili kudhibiti magonjwa nchini.

### 7.8 Mpango wa Damu Salama

Damu ni uhai. Hivyo upatikanaji wa damu salama kwa wahitaji ni sehemu ya jitihada za kuokoa maisha ya binaadamu. Benki ya damu inaendelea kukusanya, kuchunguza, kuhifadhi na kusambaza damu salama katika hospitali nchini. Wananchi wengi wamehamasika kuchangia damu kwa hiari kwa ajili ya kuokoa maisha ya wananchi wenzao.

Kwa mwaka 2023, kupitia Mpango wa damu salama, Wizara ya Afya imekusanya jumla ya chupa za damu 15,313, kutoka chupa 14,552, zilizokusanywa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Hii imetokana na jitihada ya Benki kuimarisha uhamasishaji kwa wananchi juu ya kuchangia damu kwa hiyari ili kuokoa maisha ya watu kupitia mabonanza, mikutano ya kidini na mikusanyiko mikubwa ya watu kwa kipindi cha 2023.

Licha mafanikio hayo Benki ya damu salama imekuwa na changamoto ambazo zinarudisha nyuma shughuli za ukusanyaji kwa wakati kulingana na mahitaji halisi ya damu kwa muda sahihi na kuendana na mahitaji ya damu salama. (*Jadweli namba 47*).

**Jadweli Nam 47. Ukusanyaji wa damu kupitia Benki ya Damu**

| Mwaka | Idadi ya Chupa |
|---|---|
| 2019 | 15,206 |
| 2020 | 14,482 |
| 2021 | 16,386 |
| 2022 | 14,552 |
| 2023 | 15,313 |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

### 7.9 Lishe ya Mama na Mtoto

Kwa mwaka 2023, jumla ya watoto 218,468 wamepatiwa matone ya Vitamini A kwenye vituo vya Afya kutoka 108,288 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 101.7, na hutolewa mara mbili kwa mwaka. Mafanikio haya yamechangiwa na mashirikiano makubwa kutoka sekta za Serikali na jamii hususani Masheha na wahudumu wa afya wa kujitolea (CHVs) ambapo kampeni zao zimefanikiwa

kuwapa watoto 187,409 matone ya vitamain A Mikoa na Wilaya zote za Unguja na Pemba.

Wizara ya Afya inaendelea kusimamia miongozo yake pamoja na Shirika la Afya Duniani juu ya lishe ya mama na mtoto na kutoa maelekezo ya utekelezaji kwa kuupitia na kuukamilisha mkakati shirikishi wa lishe ambao unahusisha utekelezaji wa majukumu ya sekta zote zinazohusika kwa namna moja au nyengine katika kuimarisha afya na lishe ya mama na mtoto. Mkakati wa kuimarisha lishe kwa mama na watoto una shajihisha mambo yafuatayo:

a) Lishe kwa wajawazito na watoto wadogo kwa wakati;

b) Kutoa elimu shirikishi kwa vikundi ambavyo vitahusika moja kwa moja na lishe ya mama na mtoto pamoja na elimu ya uzazi;

c) Kupunguza tatizo la lishe kwa watoto wa skuli;

d) Kupambana na tatizo la utapiamlo kwa watoto walioathirika; na

e) Kutoa elimu ya kupunguza matatizo ya lishe yanayotokana na taratibu za ulaji usiofaa na mitindo ya maisha, uzito uliozidi na kiribatumbo (utapiamlo) kwa wanawake na wanaume.

### 7.10 Maradhi ya Kuambukiza

Wizara ya Afya inaendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya kutunza afya zao dhidi ya maradhi ya kuambukiza, ikiwemo kufanya uchunguzi wa afya mara kwa mara na kujenga tabia inayozingatia kanuni za afya. Wananchi wanaendelea kupata mwamko mkubwa wa kujua afya zao na kujikinga na maradhi yanayoambukiza ikiwemo UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma. Wananchi wengi hufika hospitali na kujua afya zao kwa kufanya vipimo, kupatiwa dawa na ushauri pale wanapogundulika wamepata maambukizi ya magojwa hayo.

Kwa Mwaka 2023, hali ya maambukizi mapya ya magonjwa ya virusi vya ukimwi imepungua kwa asilimia 40 kufikia 1,050 ikilinganishwa na maambukizi 1,759 mwaka 2022. Utoaji wa elimu ya kujitambua hasa kwa vijana wadogo kati ya umri wa miaka 18-35 umesaidia kupunguza maabukizi mapya ya UKIMWI.
Mwaka 2023 wagonjwa 1,135 wamegundulika na ugonjwa wa Kifua kikuu kutoka 1,090 mwaka 2022. Sawa na ongezeko la asilimia 4.1. Hii imetokana na muingiliano wa shughuli mbali mbali za kijamii. Juhudi za kuwaelimisha

wananchi zinaendelea na Wizara kupitia Maafisa wake wa Afya nchi nzima kuwapa wanajamii muamko juu ya kupunguza zaidi maambukizi ya magonjwa hayo nchini.

## 7.11 Idadi ya nyumba na wakaazi walioathirika kwa madawa ya kulevya (sober houses)

Janga la madawa ya kulevya ni adui mkubwa kwa maendeleo endelevu ya taifa lolote ulimwenguni ambalo linaathiri vijana wengi na kupoteza nguvu kazi ya taifa, tumaini kubwa la Serikali ni vijana kwa ujenzi wa taifa na maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.

Idadi ya nyumba za kurekebisha tabia zimepungua na kufikia nne (4) mwaka 2023 kutoka tano (5) mwaka 2022 ambazo zote ni za wanaume. Upungufu huo umetokana na nyumba moja kubadilishwa matumizi kutokana na idadi ndogo ya wakaazi wake. Jumla ya wakaazi waliorekodiwa kwenye nyumba za kurekebisha tabia ni 275 mwaka 2023 ukilinganish na 166 mwaka 2022. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 66. Hii imesababishwa na kuongezeka kwa magendo ya usafirishaji wa madawa ya kulevya kupitia bandari zisizokuwa rasmin (bandari bubu) na kupelekea kuongezeka kwa watumiaji wa madawa ya kulevya nchini. Idadi kubwa ya watumiaji wa madawa ya kulevya wako katika umri wa miaka 26-35 sawa na asilimia 36.0 huku kiwango cha chini zaidi ya watumiaji wa dawa za kulevya, iliyoripotiwa ni kundi la umri wa miaka 46 na kwenda juu ambao ni asilimia 15.6. Kwa ujumla kwa kipindi cha miaka mitatu 2019-2023 idadi ya watumiaji wa dawa za kulevya imekuwa ikipungua kutokana na jitihada kubwa zinazochukuliwa na Serikali ya awamu ya nane. (J*adweli Namba 48 na Jadweli Namba 48 Jadweli Namba 49* ).

**Jadweli Nam 48: Idadi ya Nyumba za Kurekebisha Tabia kwa Waathirika wa Madawa ya Kulevya Zanzibari (2019-2023)**

| Jinsia | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Wanaume** | 8 | 6 | 5 | 5 | 3 |
| **Wanawake** | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **8** | **6** | **6** | **5** | **4** |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

**Jadweli Nam 49: Idadi ya Wakaazi Katika Nyumba za Waathirika wa Madawa ya Kulevya Zanzibar (2019- 2023)**

| Mwaka | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 401 | 349 | 309 | 166 | 275 |
| Wanawake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Wakaazi** | **401** | **349** | **309** | **166** | **275** |

*Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24*

### 7.12 Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto,

Hii ni sekta inayo igusa jamii moja kwa moja, kijamii, na kiuchumi kwa lengo la kufikia jamii yenye usawa na kuondosha udhalilishaji wa aina zote dhidi ya wanawake, watoto na wazee nchini ili kuhakikisha nchi yetu ni sehemu salama ya kuishi.

Kwa mwaka 2023 Sekta hii imetekeleza mambo yafuatayo: -

- Kuweka mazingira bora ya Ustawi wa Jamii, Watoto, Wazee na kusimamia malipo ya Pencheni Jamii;
- Kuimarisha hifadhi ya wazee, utoaji wa misaada ya kiustawi kwa wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zaidi;
- Kuimarisha mfumo wa hifadhi ya mtoto na kusimamia haki na wajibu wao;
- Kuimarisha uratibu wa ufikiwaji wa usawa wa kijinsia na kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia;na
- Ajali za Barabarani.

### 7.13 Ustawi wa Jamii

Ustawi wa Jamii ni kitengo muhimu kwa ajili ya kushughulikia ustawi wa wananchi hasa wale walio katika makundi maalum. Takwimu zinaonyesha kuwa kwa mwaka 2023 Zanzibar ina jumla ya watu 8,100 wenye ulemavu, 4,262 ni wanaume na 3,838 ni wanawake.

### 7.13.1 Watoto Yatima

Idadi ya watoto yatima katika vituo vya kulelea watoto imepunguwa na kufikia 384 mwaka 2023 kutoka 437 mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 12.1. Idadi ya Wazee katika vituo vya Huduma iliongezeka kwa asilimia 13.6 kutoka Wazee 59 mwaka 2022 hadi 67 mwaka 2023, kuongezeka huko kumetokana na usajili wa wazee wapya kwenye vituo vya kutunzia wazee.

**Jadweli Namba 50: Watu wenye ulemavu na Mahitaji Maalumu**

| **Aina za ulemavu** | W/ume | W/Mke | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Ulemavu wa kimwili | 1,711 | 1,290 | **3,001** |
| Ulemavu wa macho | 539 | 451 | **990** |
| Ulemavu wa maskio | 617 | 745 | **1,362** |
| Ulemavu akili | 586 | 489 | **1,075** |
| Ulemavu Ngozi | 45 | 59 | **104** |
| Ulemavu jumuishi | 722 | 768 | **1,490** |
| Ulemavu Mwengineo | 42 | 36 | **78** |
| **Jumla kuu** | **4,262** | **3,838** | **8,100** |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

### 7.13.2 Ukatili dhidi ya Wanawake, Wanaume na Watoto

Ukatili dhidi ya wanawake, wanaume na watoto ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na janga kwa mustakabali wa taifa na jamii kwa ujumla.

Athari zake ni za muda mrefu kimwili na kiakili kwa wanawake, wanaume na watoto. Idadi ya matukio ya ukatili wa kijinsia yameongezeka kutoka matukio 1,360 yaliyoripotiwa mwaka 2022 hadi 1,954 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 43.7. Hii imesababishwa na jamii kuwa na muamko wa kutoa tarifa za makosa ya udhalilishaji kwenye vyombo vya sharia.

### 7.13.3 Ubakaji na Shambulio la Aibu

Kwa Mwaka 2023, matukio ya ubakaji na shambulio la aibu Zanzibar yameongezeka na kufikia 923 kutoka 859 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 7.4. Ongezeko hili limetokana na ukosefu wa elimu mtambuka juu ya masuali ya udhalilishaji wa kijinsia, na jamii kutowa taarifa yanapotokea makosa haya (Jadweli namba 51).

**Jadweli Nam 51: Makosa ya udhalilishaji wa kijinsia yaliyoripotiwa mwaka ; 2019-2023**

| Matukio/Mwaka | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Ubakaji | 651 | 571 | 621 | 651 | 923 |
| Ulawiti | 157 | 102 | 177 | 200 | 246 |
| Child Desertion | 8 | 46 | 83 | 88 | 90 |
| Wizi wa watoto | 180 | 150 | 95 | 84 | 109 |
| Utekaji watoto | 104 | 74 | 114 | 125 | 210 |
| Shambulio la Matusi | 269 | 420 | 132 | 212 | 376 |
| Jumla kuu | 1,369 | 1,363 | 1,222 | 1,360 | 1,954 |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

## 7.13.4 Matukio ya Uhalifu

Matukio ya uhalifu katika jamii yameongezeka na kupelekea jamii kukosa utulivu katika shughuli zao za kuleta maendeleo nchini, makosa hayo yamegawika katika kesi kubwa na ndogo. Njia zinazotumika kukusanya takwimu za uhalifu ni kutoka kwenye rekodi za kaya, hospitali, bima na Polisi ya Zanzibar.

Jumla ya kesi za uhalifu zilizoripotiwa Mwaka 2023 zimeongezeka kufikia 38,791 sawa na ongezeko la asilimia 72.0 ikilinganishwa na kesi 22,547 zilizoripotiwa mwaka 2022, (kesi ndogo zilikuwa 38,598 sawa na asilimia 99.5). Idadi ya wafungwa walioripotiwa mwaka 2023 imefikia 1,264, ambapo wanaume ni 1,241 sawa na asilimia 98.2 na wanawake 23 sawa na asilimia 1.8. wakiwa na umri kati ya miaka 18-30.

Makosa dhidi ya Mtu yamefikia 2,049 mwaka 2023 sawa na asilimia 44.2 ikilinganishwa na makosa 1,421 yaliyorekodiwa mwaka 2022. Makosa hayo yalihusishwa na kesi 824 za ubakaji sawa na asilimia 40.2 ikifuatiwa na shambulio la aibu na kujamiiana kinyume na maumbile sawa na asilimia 18.4.

### Makosa ya Jinai

Makosa ya Jinai mwaka 2023 yamefikia 1,016, kutoka 709 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 43.3.

### Jadweli Nam 52: Makosa ya Jinai yaliyoripotiwa mwaka 2019-2023

| Mwaka | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mauwaji ya Kukusudia | 34 | 33 | 41 | 34 | 44 |
| Waliojiuwa | 6 | 0 | 4 | 22 | 40 |
| Ubakaji kuanzia miaka 18 ... | 57 | 64 | 58 | 62 | 95 |
| Ubakaji kuanzia chini miaka 18 | 594 | 507 | 563 | 585 | 824 |
| Ubakaji wa vikundi | 1 | 0 | 0 | 4 | 4 |
| Jaribu la ubakaji | 10 | 0 | 4 | 2 | 9 |
| **Makosa kwa Jumla** | **702** | **604** | **670** | **709** | **1,016** |

***Chanzo:Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

### Matokeo ya Ajali za Barabarani

Jumla ya ajali za barabarani zilizorekodiwa mwaka 2023 zimeongeka kwa asilimia 12.2 kufikia ajali 193 ikilinganishwa na ajali 172, mwaka 2022. Idadi kubwa ya ajali za barabarani zilitokea mwezi wa Julai. Idadi ya waathirika walioripotiwa kutokana na ajali za barabarani ni 385 ambayo inaonyesha ongezeko la asilimia 19.2 ikilinganishwa na waathirika 323 walioripotiwa mwaka 2022. Kati ya waathirika hao, 153 walifariki na 232 wamejeruhiwa.

Makosa ya barabarani yaliyoripotiwa mwaka 2023 yalikuwa 38,598 ambayo yanaonyesha ongezeko la asilimia 72.5 ikilinganishwa na makosa 22,375 yaliyoripotiwa mwaka 2022. Wanaume wameripotiwa kufanya makosa mengi na kufika 38,518 yakilinganishwa na makosa 80 yaliyoripotiwa kwa wanawake. *(Jadweli namba 53*).

**Jadweli Nam 53: Ajali za Barabarani zilizo rikodiwa kwa mwaka 2019-2023**

| Sehemu | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| Zanzibar | 301 | 306 | 209 | 172 | 193 |
| Unguja | 256 | 256 | 165 | 137 | 143 |
| Pemba | 52 | 50 | 44 | 35 | 50 |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

## SURA YA NANE

## 8.0 MAENDELEO YA KIUCHUMI NA KIJAMII ZANZIBAR MWAKA 2023

Mwaka 2023 Uchumi wa Zanzibar umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 7.4 kutoka wastani wa asilimia 6.8 mwaka 2022, ukuwaji huo umetokana na sababu zifuatazo;

i. Kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji kufikia miradi 114 yenye thamani ya TZS 4,646 bilioni mwaka 2023 kutoka miradi 93 yenye thamani ya TZS 4,550 bilioni mwaka 2022.

ii. Kuongezeka kwa thamani ya mazao ya biashara yaliyosafirishwa nje ya nchi. Mwani wenye thamani ya TZS 19,233.2 milioni mwaka 2023 kutoka TZS 16,010.2 milioni mwaka 2022 ulisafirishwa na Karafuu zenye thamani TZS 47,081.1 milioni mwaka 2023 kutoka TZS 118,287.3 milioni mwaka 2022 zilisafirishwa;

iii. Kuimarika kwa Sekta ya Huduma, kwa kukua na kufikia wastani wa asilimia 9.9 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 7.7 mwaka 2022. Ukuaji huu umetokana na ukuaji wa Sekta ndogo ya Biashara na kwa asilimia 12.6, shughuli za Fedha na Bima kufikia asilimia 54.6, Huduma za Utawala na usaidizi kufikia asilimia 17.0, Sanaa, Burudani na Ubunifu kufikia asilimia 33.8 na Usafiri na uhifadhi kwa asilimia 9.2;

iv. Kuongezeka kwa watalii waliotembelea Zanzibar kufikia watalii 638,498 mwaka 2023 kutoka watalii 548,503 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 16.4;

v. Kuongezeka kwa ajira mpya zilizosajiliwa kufikia 82,225 mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na ajira 68,632 mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 20;

vi. Kuimarika kwa miundombinu ya barabara jumla ya kilomita 946.85 za barabara zimejengwa kwa kiwango cha lami nchini, na

vii. Kuongezeka kwa mapato ya ndani kufikia TZS 1,075.9 bilioni mwaka 2023/2024 sawa na asilimia 98 ya makadirio ukilinganisha na jumla ya TZS 801.4 bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023,

## SURA YA TISA

## 9.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2023/2024

### 9.1 Mapato ya Serikali

#### 9.1.1 Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali ilikadiriwa kukusanya mapato kutokana na vyanzo vya ndani jumla ya TZS 1,419.0 bilioni sawa na asilimia 24 ya Pato la Taifa. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 1,217.2 bilioni zilitarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya kodi na TZS 201.8 bilioni kutokana na vyanzo visivyo vya kodi. Kati ya TZS 1,217.2 bilioni zitokanazo na kodi, Mamlaka ya Mapato Zanzibar ilitarajiwa kukusanya kiasi cha TZS 675.6 bilioni, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikadiriwa kukusanya TZS 520.6 bilioni na TZS 21 bilioni zilipangwa kukusanywa na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kutokana na Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliopo Zanzibar.

Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 mapato ya ndani yalifikia TZS 1,075.9 bilioni sawa na asilimia 98 ya makadirio ya kipindi hicho ukilinganisha na jumla ya TZS 801.4 bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Aidha kumejitokeza ukuaji wa mapato wa TZS 274.5 bilioni sawa na asilimia 34.3 kati ya makusanyo hayo, mapato kutokana na kodi yalifikia TZS 948.3 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 101.1 ya makadirio. Mapato yasiyokuwa ya kodi yalifikia TZS 127.6 bilioni sawa na asilimia 79 ya makadirio.

#### 9.1.2 Ukusanyaji wa Mapato Kitaasisi

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilikusanya jumla ya TZS 373.2 bilioni katika kipindi cha Julai – Machi 2023/2024 ikilinganishwa na TZS 337.0 bilioni zilizokusanywa kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 11. Aidha, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) ilikusanya jumla ya TZS 559.3 bilioni sawa na asilimia 104.4 ya makadirio ya TZS 535.7 bilioni. Mapato ya ZRA kwa mwaka 2023/2024 yameongezeka kwa asilimia 24.6 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2021/2022 ambapo jumla ya TZS 448.7 bilioni zilikusanywa. Jumla ya TZS 127.6 bilioni sawa na asilimia 78.9. ya makadirio ya mapato ya ndani zimetokana na mapato ya mawizara.

### 9.1.3 Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Julai 2023 hadi Machi 2024 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepokea misaada ya kibajeti (GBS 4.5%) yenye thamaniya TZS 72.9 bilioni. Aidha, Ruzuku na Mikopo iliyopokelewa kwa ajili ya Miradi na Programu za Maendeleo imefikia TZS 483 bilioni sawa na asilimia 97 ya makadirio ya kipindi hicho ya TZS 498.1 bilioni.

## 9.2 Matumizi ya Serikali 2023/2024

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali ilikadiriwa kufanya matumizi ya jumla ya TZS 2,822.9 bilioni sawa na asilimia 47.7 ya Pato la Taifa. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 1,308.1 bilioni ni matumizi ya kazi za kawaida na jumla ya TZS 1,514.8 bilioni ni matumizi ya kazi za Maendeleo. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya TZS 1,678.1 bilioni zimekadiriwa kutumika. Kati ya matumizi hayo yaliyokadiriwa, TZS 957.8 bilioni ni kwa Kazi za Kawaida na TZS 720.3 bilioni ni kwa Kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2024 matumizi halisi yalifikia TZS 1,783.8 bilioni. Kati ya matumizi hayo TZS 915.4 bilioni sawa na asilimia 95.6 zilitumika kwa kazi za kawaida na TZS 868.4 bilioni sawa na asilimia 120.6 zilitumika kwa Kazi za Maendeleo.

### 9.2.1 Matumizi ya Kazi za Kawaida

Matumizi ya Kazi za Kawaida kwa kipindi cha (Julai 2023hadi Machi 2024) mwaka wa Fedha 2023/2024 yalifikia jumla ya TZS 915.4 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 25.2 ikilinganishwa na matumizi ya kawaida ya kipindi kama hicho mwaka 2022/2021, ambapo jumla ya TZS 731.2 bilioni zilitumika.

### 9.2.2 Mishahara

Kati ya matumizi ya kazi za kawaida, matumizi ya Mishahara yalifikia TZS 430.2 bilioni katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 mwaka wa fedha 2023/2024 sawa na asilimia 99.7 ya makadirio ya kipindi hicho. Matumizi hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 9.7 ikilinganishwa na kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, ambapo jumla ya TZS 392.1 bilioni zililipwa.

### 9.2.3 Matumizi Mengineyo

Matumizi mengineyo ukitoa Mfuko Mkuu wa Serikali yamefikia TZS 187.3 bilioni sawa na asilimia 78.1 ya makadirio ya kipindi hicho, matumizi hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 98.8 ikilinganishwa na matumizi mengineyo ya mwaka wa fedha 2022/2023 ya jumla ya TZS 94.2 bilioni.

### 9.2.4 Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali yalifikia TZS 214.9 bilioni sawa na asilimia 106.4 ya makadirio ya kipindi hicho. Matumizi hayo ni sawa na ongozeko la asilimia 68 ikilinganishwa na matumizi kama hayo katika mwaka wa fedha 2022/23, ambapo jumla ya TZS 127.9 bilioni zilitumika.

### 9.2.5 Matumizi ya Kazi za Maendeleo

Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya matumizi ya Maendeleo yalikuwa TZS 868.4 bilioni sawa na asilimia 120.6 ya lengo la TZS 720.3 bilioni. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani zilikuwa TZS 494.4 bilioni, sawa na asilimia 147.2 ya makadiriona fedha za washirika wa Maendeleo zilikuwa ni TZS 100.6 bilioni sawa na asilimia 37.6 ya makadirio ya TZS 267.3 bilioni na TZS 273.4 ni Mfuko wa kulipia Madeni.

### 9.2.6 Deni la Taifa

Hadi Machi 2024, deni la Taifa la Zanzibar limefikia TZS 934 bilioni ikilinganishwa na TZS 330.4 bilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2023, ikiwa ni ongezeko la asilimia 182.7. Mikopo hii ilitumika kugharamia miradi mbali mbali ya Maendeleo nchini . Aidha, hadi kufikia Machi 2024, Mikopo iliyokopwa kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miradi iliyotekelezwa Zanzibar imefikia TZS 2,550.9 bilioni ikilinganishwa na TZS 2,381.7 bilioni kwa kipindi kama hicho mwaka 2023.

**SURA YA KUMI**

# 10.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MIRADI YA KIMKAKATI KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024

## 10.1. UTANGULIZI

Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/24 ni Mpango wa tatu wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026 pamoja na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050. Mpango una kaulimbiu isemayo 'Uchumi wa Buluu kwa Ukuaji Jumuishi na Maendeleo Endelevu'. Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/2024 ulilenga kutekeleza programu na miradi 16 ya kimkakati ambapo jumla ya TZS 1,521.99 bilioni zimepangwa kutumika kwa kutekeleza shughuli za miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 915.87 bilioni sawa na asilimia 60.46 zimepangwa kutumika kwa Programu na Miradi ya Kimkakati.

Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 – Machi 2024), Serikali imepanga kutumia jumla ya TZS 1,244.09 bilioni kwa kutekeleza Programu na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Serikali ilipanga kutumia TZS 772.5 sawa na asilimia 62.09 ya bajeti ya Maendeleo kutoka fedha za ndani na TZS 471.59 sawa na asilimia 41.5 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo (TZS 1,244.09 bilioni), Serikali imepanga kutumia jumla ya TZS 686.90 bilioni sawa na asilimia 60.46 kwa Programu na Miradi ya Maendeleo ya Kimkakati.

Katika kuhakikisha Maendeleo makubwa yanafikiwa kwa mwaka 2023/24, Serikali imepanga kutekeleza miradi maalum ya kimkakati katika maeneo mahsusi yenye lengo la kuimarisha Utumiaji wa fursa za Uchumi wa buluu; Mazingira Wezeshi na Uimarishaji wa Miundombinu; Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii; pamona na Utawala Bora na uhimilivu.

## 10.2 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA KIMKAKATI KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 - MACHI 2024

Katika kuhakikisha Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/24, Serikali ilisimamia utekelezaji wa miradi maalum ya kimkakati katika maeneo mahsusi kwa kuimarisha Uchumi wa buluu, Uimarishaji wa Miundombinu, Huduma za Kijamii, pamoja na Utawala Bora na Uhimilivu. Maeneo haya ni yale ambayo yalitarajiwa kuleta matokeo makubwa na kwa haraka ikiwemo

upatikanaji wa ajira nyingi kwa wananchi, kuongeza uwekezaji, kuimarisha hali za wananchi pamoja na kuongeza mapato ya Serikali. Kwa kuzingatia maeneo hayo, programu na miradi ya kimkakati kumi na nne (14) ilipewa kipaumbele na kutekelezwa kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024. Katika kipindi hicho, jumla ya TZS 711.08 bilioni sawa na asilimia 104 ya bajeti iliyopangwa ya TZS 686.90 zilipatikana na kutumika katika utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo (TZS 317.83 bilioni sawa na asilimia 91.26 ya lengo la TZS 348.25 zilipatikana kutoka Serikalini na TZS 393.24 bilioni sawa na asilimia 116 ya lengo la TZS 338.64 bilioni zilipatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Utekelezaji wa Programu na Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

### i. Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu

Kwa mwaka 2023/2024 eneo hili lilipangiwa kiasi cha TZS 43.50 bilioni ambapo kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 32.62 bilioni zilipangwa kutumika kwa programu na miradi mitatu (3). Hadi kufikia Machi 2024, TZS 29.12 bilioni sawa na asilimia 89 ya lengo zimepatikana. Utekelezaji wa miradi ya eneo hili ni kama ifuatavyo:-

#### a) Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani

Mradi huu una lengo la kujenga bandari kubwa na ya kisasa ambayo itahusisha gati ikiwemo ya mizigo, eneo la ushushaji na upakiaji wa mafuta, bandari ya uvuvi, pamoja na chelezo cha kukarabati meli, kukamilika kwa ujenzi wa bandari hii kutasaidia kuimarika kwa sekta nyengine za kiuchumi ikiwemo sekta ya uvuvi, biashara na viwanda. Mradi huu ulianza utekelezaji wake mwaka wa fedha 2022/2023. Mradi unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali na wawekezaji kutoka katika sekta binafsi. Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 20.0 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa, jumla ya TZS 15.0 bilioni zimepangiwa utekelezaji wa mradi huu. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya TZS 29.12 bilioni sawa na asilimia 194 ya lengo zimetumika. Kazi ya tathmini ya fidia ya Barabara ya Mashariki na Kusini ambayo imehusisha maeneo ya Mangapwani, Kidanzini, Misufini na Makoba imekamilika na fidia kwa maeneo ya Kidanzini kwa Mbara, Bumbwini imeshalipwa kwa Wananchi walioathirika na ujenzi na maombi ya fedha za fidia kwa maneo yaliobakia tayari yameshapelekwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa kufanyiwa uhakiki ili malipo yafanyike. Aidha, ujenzi wa nyumba 370 za kuwalipa fidia wananchi unaendelea kwa nyumba 110 katika hatua mbalimbali na Kazi ya upelekaji

wa huduma za maji na umeme zimekamilika na ujenzi wa barabara za ndani katika eneo la bandari unaendelea, kwa upande wa eneo la Magharibi ujenzi upo asilimia 35 na hatua iliyofikiwa ni uwekaji wa lami.

### ii. Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu

Kwa mwaka 2023/2024 lilipangiwa kutekeleza miradi mitano ya maendeleo ambayo inagharimu jumla ya TZS 549.62 bilioni ambapo kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023- Machi 2024) jumla ya TZS 412.16 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2024, TZS 479.18 sawa na asilimia 116.26 ya lengo la TZS 412.16 bilioni zimepatikana. Utekelezaji wa program na miradi ya eneo hili ni kama ifuatavyo:-

#### *a) Programu ya Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege- Pemba.*

Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya anga ili iweze kuwa katika viwango vya kimataifa. Kwa mwaka 2023/2024 programu inahusisha ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba kwa hatua za awali za ujenzi, ujenzi wa maegesho, njia za kupitia ndege pamoja na sehemu za kukaa abiria. Programu ilipangiwa kugharimu jumla ya TZS 120.0 bilioni kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) (TZS 7.5 bilioni kutoka Serikalini na TZS 112.5 billioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya TZS 146.6 bilioni zimetolewa sawa na asilimia 122 ya lengo la TZS 120 bilioni kwa kipindi hicho. Kati ya fedha hizo TZS 12.65 bilioni sawa na asilimia 169 ya lengo kutoka Serikalini zimetumika kwa ajili ya malipo ya fidia na TZS 133.87 bilioni sawa na asilimia 119 ya lengo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (United Kingdom Export Finance -UKEF) ambao ni mkopo ikiwa ni malipo ya awali (advance payment) kumlipa Mkandarasi ili aanze kazi (Mobilization works). Aidha, wananchi 649 kati ya 719 sawa na asilimia 90.26 tayari wamelipwa fidia katika eneo la mradi na kazi ya kufanya uhakiki wa fidia hizo unaendelea ili kukamilisha ulipaji wa fidia na wananchi kuondoka katika eneo la mradi na mradi kuanza kutekelezwa. Programu hii ikikamilika itasaidia kukua kwa uchumi, kuongezeka kwa ajira, kuja kwa mashirika ya ndege ya Kimataifa , kuongezeka kwa uingiaji wa watalii na kuifungua Pemba katika Nyanja za kibiashara na kiuchumi.

#### *b) Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu*

Programu ya ujenzi wa barabara kuu imeanza mwaka 2022/23 na inahusisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 407.6. Kwa mwaka 2023/2024 programu

imehusisha ujenzi wa barabara kuu ikiwemo barabara mpya na zinazoendelea na inatarajiwa kutekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali, Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo. Programu ina lengo la kujenga kwa kiwango cha lami, ujenzi wa mitaro pamoja na uwekaji wa taa na alama za barabarani Unguja na Pemba. Programu imejumuisha ujenzi wa barabara ya Tunguu-Makunduchi km 53; ujenzi kwa barabara ya Chake Chake-Mkoani km 43.5; ujenzi wa barabara ya Fumba - Kisauni kilomita 12. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya 249 billioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) programu imepangiwa jumla ya TZS 187.04 bilioni (TZS 56.54 bilioni kutoka Serikalini na TZS 130.5 bilioni kutoka kwa United Kingdom Export Finance -UKEF). Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya TZS 245.8 bilioni sawa na asilimia 131 ya lengo la TZS 187.04 bilioni zimetolewa kwa kipindi hicho. Kati ya fedha hizo TZS 64.66 bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 114 ya lengo la TZS 56.54 bilioni na TZS 181.99 bilioni sawa 139 ya lengo la TZS 130.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (United Kingdom Export Finance –UKEF).

Ujenzi wa barabara ya Wete -Chake Chake, hadi Machi 2024, jumla ya TZS 94.67 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (BADEA) zimeingizwa. Kazi zinazoendelea katika ujenzi wa barabara hii yenye urefu wa km 22 ni usafishaji wa barabara ambayo imekamilika kwa asilimia 100; Uwekaji wa tabaka la chini la mwanzo la kifusi (G7) asilimia 80; Uwekaji wa tabaka la juu la mwanzo la kifusi (G15) asilimia 25; Uwekaji wa tabaka la pili la kifusi (G45) asilimia 32; Ujenzi wa kalvati 2; Ujenzi wa Madaraja asilimia 30 na Ujenzi wa mabomba ya kupitishia miundombinu (Service duct) asilimia 80 kwa urefu wa km 10. Kwa ujumla kazi ipo asilimia 25.

Programu hii itasaidia kuunganisha miji mikubwa ya Zanzibar na kushajihisha uchumi na uwekezaji. Barabara hizi ni kiunganishi cha miji na maeneo ya usafirishaji ikiwemo viwanja vya ndege na bandari pamoja na maeneo mengine ya kibiashara na kiuchumi. Vilevile, Barabara hizi zitapunguza ajali za barabarani, misongamano ya magari, uharibikaji wa vyombo vya usafiri na mituwamo ya maji.

### *c) Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani*

Programu hii imeanza mwaka 2022/2023 ambayo itahusisha ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 katika maeneo ya mijini na vijijini Unguja na Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 44.0 billioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi

2024), zimepangwa jumla ya TZS 33.0 bilioni. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 16.46 bilioni sawa na asilimia 50 zimetumika. Kazi zilizofanyika ni uwekaji wa lami km 32.25 sawa na asilimia 100 ya makadirio ya km 32.25 zilizopangwa kuwekwa lami. Tathmini kwa ajili ya malipo ya fidia imefanyika kwa barabara nne (Mwakaje-Mwachealale-Bumbwisudi, Kidoti, Mfurumatonga-Mlilile skuli-New Road na Dunga zuze). Maombi ya fedha yamewasilishwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya kuwalipa wananchi fidia kwa upande wa Unguja baada kufanyiwa uhakiki. Kwa upande wa Pemba km 89.95 sawa na asilimia 100 ya lengo la kusafisha barabara tayari zimesafishwa kwa kuanza ujenzi , jumla ya km 13.8 sawa na asilimia 100 ya lengo la km 13.8 tayari zimewekwa kifusi tabaka la kwanza katika barabara za Mapofu-Tumbe Kojifa-Bandarini zenye urefu wa 12.7km, 12.6Km zimeshakamilika kwa tabaka la kwanza na Micheweni-Kiuyu –Maziwa Ng'ombe zenye urefu wa 7.5km, 1.2km zimeshakamilika kwa tabaka la kwanza na utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 39.98.

Programu itasaidia kuunganisha mitaa na maeneo 62 ya Unguja na Pemba. Kukamilika kwa programu hii itasaidia kupunguza msongamano katika barabara kuu pamoja na kuongeza haiba ya kupendezesha mitaa na maeneo mengi ya miji na vijiji. Aidha, programu itasaidia kurahisisha usafirishaji wa mizigo na kuimarisha ukuaji wa uchumi, kuongeza kipato cha mwananchi mmoja mmoja pamoja na kuimairika kwa sekta nyengine za kiuchumi zikiwemo sekta ya kilimo na biashara. Vilevile, Barabara hizi zitapunguza ajali za barabarani, misongamano ya magari kwenye barabara kuu, uharibikaji wa vyombo vya usafiri na mituwamo ya maji.

#### *d) Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini*

Programu hii imeanza kutekelezwa mwaka 2022/2023 na imehusisha ujenzi wa kilomita 100.9 za barabara za mjini. Kwa mwaka 2023/2024 programu hii inahusisha uimarishaji wa barabara katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Programu itahusisha ujenzi wa barabara; ujenzi wa njia za wapita kwa miguu; uwekaji wa taa pamoja na ujenzi wa mitaro ya maji katika barabara za mijini. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, programu imepangiwa kutumia kiasi cha TZS 80.1 bilioni kutoka Serikalini na kwa kipindi cha miezi tisa, programu imepangiwa TZS 60.07 bilioni. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya TZS 70.34 bilioni sawa na asilimia 117 zimetumika. Kazi ya matengenezo makutano ya barabara ya Kiembe Samaki na Amani – Mtoni, barabara ya Mkapa km 8.5, uwekaji wa lami km 5.14 kwa baadhi ya maeneo yamekamilika na kufanya utekelezaji wa ujenzi wa barabara hio kufikia asilimia 60.47. Ujenzi wa barabara ya Uwanja wa

ndage ya Abeid Amani Karume – Kiinua Miguu – Mnazimmoja unaendelea kwa ujenzi wa Mitaro ya kupitishia maji kwenye kingo za Barabara pamoja na njia za kupitishia miundombinu ya mawasiliano. Utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Uwanja wa ndage ya Abeid Amani Karume – Kiinua Miguu – Mnazimmoja km 6.5 unaendelea na umefikia asilimia 99 na barabara ya Mwanakwerekwe Gapco – Kwerekwe Skuli – kanisani kwa mchina imefikia asilimia 78. Vilevile, barabara ya Mombasa Planned Area km 6.20 ujenzi unaendelea kwa hatua mbali mbali zikiwemo uwekaji wa lami na zege. Kwa barabara ya Mpendae Planned Area km 7.35 kazi zinazoendelea kwa uwekaji wa lami ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 44.08 na barabara ya Michenzani, Gongoni, Kisiwandui Msikiti Mabati - Hailesalasie ujenzi unaendelea na umefikia asilimia 40. Aidha, ujenzi wa njia mbili za juu km 10.78 kwa upande wa mzunguko 'round about' ya Mwanakwerekwe, barabara ya juu (fly over) inaendelea kwa hatua ya ujenzi wa nguzo na umefikia asilimia 25.60. Kukamilika kwa programu hii kutaongeza haiba na kupendezesha miji yetu na kusaidia kuimarika kwa baadhi ya sekta ikiwemo sekta ya usafirishaji, utalii na biashara na kuondoa misongamano katika maeneo ya Mwanakwerekwe na Amani.

### *e. Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA)*

Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA) unatarajiwa kutekelezwa kwa miaka sita (2022-2027) na unakadiriwa kutumia jumla ya TZS 372.48 bilioni kwa lengo la kuimarisha sekta ya nishati kwa kuimarisha miundombinu ya umeme na kuzijengea uwezo taasisi zinazoshughulikia masuala ya nishati. Mradi unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Benki ya Dunia. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 16.08 bilioni (TZS 7.20 bilioni kutoka Serikalini na TZS 8.88 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa TZS 12.06 bilioni zimepangwa. Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya TZS 1.2 milioni ya fedha zilizopangwa zimepatikana kutoka kwa Benki ya Dunia. Kazi ya kuandaa michoro na kumtafuta mkandarasi wa ujenzi wa laini ya mkondo mkubwa wa umeme yenye uwezo wa kilovolti 132 kutoka Welezo hadi Ubago, Ubago hadi Matemwe na Ubago hadi Makunduchi pamoja na ujenzi wa kituo cha kutawanya umeme katika eneo la Welezo imefanyika na taratibu za zabuni zinaendelea kumpata mkadarasi wa umeme wa jua. Eneo kwa ajili ya uzalishaji wa umeme wa jua limeshapatikana lenye ukubwa wa hekta 18 huko Makunduchi. Ripoti ya tathmini imeshaandaliwa na kuwasilishwa Benki ya Dunia kufanyiwa mapitio na kutoa idhini (no objection) ili kuendelea na hatua nyengine za utekelezaji.

Shehia zitakazoathirika ni 21 na watu 1,024 katika utekelezaji wa mradi huo na malipo ya fidia yameshawasilishwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa hatua ya malipo na tayari Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango imeridhia waathirika wa ujenzi huo kuanza kulipwa fidia zao.

### iii. Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, eneo hili lilipangiwa kutekeleza miradi mitano kwa jumla ya TZS 272.29 bilioni, katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 204.22 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2024, TZS 193.81 sawa na asilimia 95 ya fedha zilizopangwaa zimepatikana na kutekeleza program na miradi ya eneo hili ni kama ifuatavyo:-

#### a. Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo

Lengo la Programu hii ni kuiwezesha Sekta ya Michezo kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo Zanzibar itakayokidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa pamoja na kuibua vipaji vya michezo Zanzibar. Programu hii imeanza mwaka 2021/22 hadi 2025/26. Kwa mwaka 2023/2024 programu imepangiwa kutumia TZS 25.71 bilioni ambapo TZS 24.75 bilioni kutoka Serikalini na TZS. 0.96 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (GERMANY/GIZ). Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 25.71 bilioni na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 31.78 bilioni sawa na asilimia 124 zimeingizwa. Kazi zilizofanyika ni ukarabati wa uwanja wa Amani pamoja na ujenzi wa viwanja vya michezo viwili vilivyo nje ya uwanja huo ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 95. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ukamilishaji wa milango ya maduka; hoteli na migahawa ili kuweza kukabidhiwa kwa Serikali. Aidha, Wizara inakamilisha maandalizi ya ujenzi wa viwanja vya michezo vidogo vidogo (6-in-1 multi-sports Centre) vya Wilaya Unguja na Pemba vyenye hadhi ya kimataifa vitakavyojengwa katika maeneo ya Mkokotoni na SUZA kwa Unguja na Mchangamdogo na Kangani kwa Pemba. Viwanja hivyo vitajumuisha michezo ya basketball, handball, baseball, vollyball, netball na tennis.

Hadi kufikia Machi 2023, kazi zilizofanyika ni upimaji wa Viwanja vya Wilaya pamoja na kuandaa michoro na BoQ, tayari Wizara imefunga mkataba na GIZ. Kwa upande mwengine, viwanja vya Matumbaku Sports Complex vimekamilika na tayari vimeshafunguliwa. Ukarabati wa Uwanja wa Gombani unaendelea umefikia asilimia 97 ya utekelezaji na kazi zinazoendelea ni kufanya marekebisho

katika kasoro ambazo zimejitokeza kabla ya kuukabidhi kwa Wizara ya Vijana, Utamaduni na Michezo kwa matumizi.

Kukamilika kwa viwanja hivyo kutaongeza vipaji vya michezo kwa vijana na kuweza kuvitumia viwanja vyetu kwa mashindano ya Kitaifa na Kimataifa, kuongezeka kwa watalii, kuongeza mapato kwa Serikali pamoja na kuitangaza nchi yetu Kimataifa.

**b. Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya na Mkoa**

Programu ina lengo la kuimarisha makaazi kwa wafanyakazi ili waweze kufanyakazi katika mazingira mazuri yenye utulivu kwa kuongeza ufanisi na kuweza kupatikana muda wote katika mazingira ya kazi hasa wakati wa dharura. Programu hii imeanza mwaka 2022/2023 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2023/2024. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya TZS 20.0 bilioni zimetengwa kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi , 2024 programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 15 bilioni. Programu hii imejumuisha Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Mkoa Lumumba na hospitali za Wilaya – Pangatupu, Mwera Pongwe, Kitogani, Vitongoji na Kinyasini. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya TZS 3.08 bilioni sawa na asilimia 21 zimetolewa. Kazi za ujenzi zinaendelea katika hatua tofauti katika hospitali za Wilaya. – Pangatupu, Ujenzi unaendelea na hadi kufikia machi 2024 msingi (foundation) umekamilika, nguzo zimesimamishwa na matayarisho ya kuweka tofali yanaendelea.Mwera Pongwe,ujenzi unaendelea kwa kukamilisha kujenga msingi ; Kitogani Mkandarasi amekamilisha kujenga msingi na kusimamisha nguzo; Kinyasini Mkandarasi amekamilisha ujenzi wa msingi na tayari ameanza kusimamisha nguzo Vitongoji ipo katika kukamilisha zabuni na kumpata Mkandarasi na kwa upande wa hospitali ya Mkoa –Lumumba, matayarisho ya awali ujenzi ya yameanza.

**c. Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa – Binguni**

Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Binguni ni mradi unaotarajiwa kufadhiliwa na Serikali ya Jamuhuri ya Watu wa Korea, mradi huu umeanza mwaka 2023/24 na kukamilika mwaka 2025/26 ikiwa ni mkopo nafuu kutoka katika Serikali ya Korea.Hadi kufikia Machi 2023, hatua zilizokamilika ni pamoja na upembuzi yakinifu na utiaji wa saini baina ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya watu wa Korea tayari kwa kupata mkopo huo.

**d. Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Elimu;**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuinua ubora wa elimu kwa kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunza. Kwa mwaka 2023/2024 Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 131.23 bilioni (TZS 59.04 bilioni kutoka Serikalini na TZS 72.19 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (ADB/ AUSTRIA/ BADEA/DLI/ WB/ GPE/ KOICA/ SIDA/ UNICEF). Kwa kipindi cha Julai 2023- Machi, 2024, programu ilipangiwa jumla ya TZS 98.42 bilioni. Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya TZS 105.59 bilioni sawa na asilimia 107 zimeingizwa kwa ajili ya ujenzi wa skuli 31 za ghorofa zikiwemo 12 za msingi na 19 za Sekondari. Katika fedha hizo TZS 65.56 ni kutoka Serikalini na TZS 49.09 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Ujenzi unaendelea katika Skuli 22, za msingi 9 na Sekondari 13 katika hatua mbali mbali na kufikia utekelezaji kwa asilimia 70. Aidha, ujenzi wa nyumba 20 za walimu umeanza. Kwa kuanzia nyumba 10 zimejengwa na kufikia asilimia 50 ya utekelezaji. Vile vile, kukamilisha ujenzi wa madarasa 12 mapya ya Msingi katika maeneo ya Kisakasaka (8) na Umbuji (4), ujenzi unaendelea na umefikia asilimia 85 ya utekelezaji wa bajeti. Pamoja na ujenzi wa Dakhalia katika Skuli za Paje Mtule na Chwaka Tumbe umekamilika kwa asilimia 100 na ujenzi wa ofisi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba unaendelea na umefikia asilimia 40. Katika programu hii Wizara imeweza kukarabati Skuli 23 za Maandalizi, Msingi na Sekondari zikiwemo Kidongo Chekundu, Chanjamjawiri, Muyuni Sekondari, Chumbuni Msingi, Faraja Sekondari, Kengeja-Dakhalia Sekondari, Kiuyu Minungwini, Chutama, Mikunguni, Fidel Castro Ukumbi, Dakhalia ya watoto wa Kiume Lumumba, Maungani, Uzini Msingi, Chaani Sekondari, Jang'ombe Maandalizi, Kizimbani Msingi, Mahonda, Ndagoni Msingi, Ole, Maziwa Ng'ombe na Mahonda, kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 35.
Kwa upande mwingine ujenzi wa Majengo sita ya Ofisi za Walimu katika Wilaya ya Kaskazini A, Magharibi B, Kusini Unguja, Mkoani, Micheweni, Chake Chake umefanyika kwa Ofisi za Walimu zenye maktaba , Ofisi ya Mkaguzi wa elimu na Ofisa TEHAMA Unguja na Pemba pamoja na ununuzi wa vifaa, utekelezaji umefanyika kwa asilimia 100. Kwa sasa hatua za kumtafuta Mshauri Elekezi zinaendelea kwa ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Unguja.

**e. Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)**

Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar ina dhamira ya kuimarisha miundombinu, huduma za msingi pamoja na kuimarisha haiba ya Miji ya

Zanzibar. Programu inatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2021- 2026) kwa gharama za jumla ya TZS 346.5 bilioni ikiwa ni mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia. Kwa mwaka 2023/2024, programu imepangiwa kutumia kiasi cha TZS 22.8 bilioni na kwa kipindi cha miezi tisa jumla ya TZS 17.1 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya TZS 16.7 bilioni sawa na asilimia 98 zimeingizwa na kutumika kwa kazi ya ununuzi wa vifaa vya usafi ikiwa ni pamoja na magari ya taka; makontena ya kuwekea taka na gari la kusafishia barabara kwa matumizi ya Mabaraza ya Miji na Manispaa Unguja na Pemba. Kampuni zilizoshinda zabuni zimeshajuilishwa kwa ajili ya kusambaza vifaa hivyo na Mikataba tayari imeshapitishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwezi wa Disemba 2023. Jumla ya loti tatu (3) kati ya 5 zinategemewa kusambaziwa vifaa hivyo, na loti mbili (2) zilizobaki zitatangazwa tena kumpata Mzabuni kutokana na wazabuni wote waliowasilisha kutofikia vigezo vilivyowekwa. Taratibu za manunuzi kwa loti mbili (2) tayari zimeshaanza. Katika programu hii inahusisha upembuzi yakinifu wa uendelezaji wa urithi wa kihistoria Mji Mkongwe (Green Corridor) ambapo makubaliano yamefikiwa na Mzabuni aliyeshinda. Programu inaendelea kufanya tathmini ya zabuni ya mradi wa Maeneo yanayokuwa kwa kasi Zanzibar (Area Upgrading Unguja na Area Upgrading Pemba-AUP-Unguja) kwa ajili ya ujenzi ambao unategemea kuanza ifikapo Aprili 2024. Kampuni ya kujitegemea (Independent RAP Monitor) imepatikana kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia mchakato wa ulipaji wa fidia. Kamati za kushughulikia malalamiko wakati wa ulipaji wa Fidia na wakati wa utekelezaji wa Mradi wa AUP-Unguja zimeandaliwa pamoja na kutoa mafunzo ya njia za kurikodi na kuwasilisha malalamiko kwa kamati zinazoshughulikia malalamiko hayo ikiwa ni sharti la msingi kwa miradi inayopata fedha za Benki ya Dunia.

### *f) Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar*

Programu hii ina lengo la kusimamia na kuhakikisha huduma za usambazaji maji safi na salama zinapatikana katika maeneo yote ya mijini na vijijini ili kuwawezesha wananchi wote kunufaika na huduma hiyo muhimu katika jamii. Kwa mwaka 2023/2024, programu imepangiwa jumla ya TZS 77.54 bilioni (TZS 24.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 53.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (INDIA (EXIM BANK), KFW/ Germany na JICA).Kwa kipindi cha Julai 2023 - Machi 2024, jumla ya TZS 58 bilioni zilipangwa kugharamia programu hii (TZS 18.37 bilioni kutoka Serikalini na TZS 39.75 bilioni kutoka kwa Washirika wa maendeleo (INDIA (EXIM BANK), KFW/ Germany na JICA)). Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 36.34 bilioni (TZS 10.54

billioni kutoka Serikalini na TZS 25.89 bilioni kutoka kwa Washirika) ya fedha zilizopangwa zimepatikana na kutekeleza miradi kama ifuatavyo:-

**i) Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA)**

Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA) una lengo la kuimarisha miundombinu ya usambazaji maji safi na salama katika maeneo ya Wilaya ya Magharibi A, (Mfenesini, Masingini na Kizimbani) Magharibi B (Dimani na Kidutani) na Wilaya ya Kati (Jumbi- Mkorogo) pamoja na ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Mamlaka ya Maji Zanzibar. Lengo la mradi huu ni kuhakikisha kuwa tatizo la maji katika maeneo hayo linaondoka na wananchi kupata huduma ya maji safi na salama. Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya India. Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 29.66 bilioni (TZS 11.16 bilioni kutoka Serikalini na TZS 18.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (India Exim Bank). Kwa kipindi cha miezi tisa jumla ya TZS 22.24 bilioni zilipangwa (TZS 8.36 bilioni kutoka Serikalini na TZS 13.87 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (India Exim Bank) kuhgaramia utekelezaji wa mradi huu . Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya TZS 29 bilioni sawa na asilimia 131 zimepatikana. Kati ya fedha hizo TZS 6.7 bilioni kutoka Serikalini na TZS 22.38 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kazi zilizofanyika ni uchimbaji wa visima 64 katika maeneo ya Dole (8), Kidutani (14), Dimani (5), Mfenesini (10), Maungani (9), Mkorogo (8) na Masingini (10), utekelezaji wake ni asilimia 100. Vile vile, ujenzi wa matangi 15 ya maji kwa LOT 1 (Mfenesini na Dole) umefikia wastani wa asilimia 95 ya utekelezaji. Kwa upande wa LOT 2 (Mkorogo, Maungani, na Dimani) umefikia wastani wa asilimia 98, na LOT 3 (Kidutani na Masingini) ujenzi wa matangi umefikia wastani wa asilimia 99. Kazi ya ukamilishaji wa matangi zinaendelea kwa baadhi ya matangi ambayo hayajakamilika. Kazi ya ulazaji wa mabomba umefikia kilomita 453.7 kati ya kilomita 466.9 sawa na asilimia 97 ya makadirio ambapo kwa LOT 1 (Mfenesini na Dole) zimefikia kilomita 176.57, na kwa LOT 2 (Mkorogo, Maungani, na Dimani) kilomita 151.34 na LOT 3 (Kidutani na Masingini) kilomita 122.9. Tayari majaribio yameanza kwa wananchi ambao wameshaunganishwa, huduma ya maji imeanza kupatikana katika maeneo ya Fumba, Dimani na Masingini na kwa upande wa Dole tayari wameanza kufunga mita kwa wananchi. Kadhalika, ujenzi wa jengo la Ofisi za Makao Makuu ya Mamlaka ya Maji (MAJI HOUSE) umekamilika kwa asilimia 100 na tayari limeanza kutumika kwa kutoa huduma kwa wananchi.

### ii) Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar

Mradi huu una lengo la kuendeleza na kuimarisha huduma ya maji safi na salama Zanzibar kwa maeneo ya Kizimbani No. 2, Jendele- Chwaka, Banda Maji, Donge, Miwani, Ndijani -Muembe Punda, Ubago - Nyakurungwi, Dunga jumba la mawe, Mwera- Pongwe, Chaani -Kikobweni, Mkataleni – Msufini, Mchangani-Mkiwa, Pangeni, Machui kwa Bavuai, Upenja, Kitope- Skuli na Mkokotoni. Kwa mwaka 2023/2024, mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS 10.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023- Machi 2024) jumla ya TZS 7.88 billioni zilipangwa kugharamia mradi huu. Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya TZS 3.43 bilioni sawa na asilimia 44 zimetolewa na Serikali. Kazi zilizofanyika ni uchimbaji wa misingi na ulazaji wa mabomba, jumla ya km 13 sawa na asilimia 50 zimelazwa mabomba ya maji kati ya kilomita 26 zilizopangwa , zabuni kwa ajili ya viungio (Pipe Fittings) imekamilika na tayari mzabuni ameshapatikana (Yumuza na Peritus.). Ujenzi wa vibanda 13 vya mashine za maji unaendelea kwa kuweka miundombinu ya umeme na maji, tarazo na dari pamoja rangi umefikia asilimia 70. Aidha bajeti ya kazi ya kuweka umeme mkubwa katika visima imeshawasilishwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya malipo.

### iv. Kuimarisha Utawala Bora na Uhimili

Kwa mwaka 2023/2024 katika eneo hili lilipangiwa kutekeleza miradi mitatu (3) jumla ya TZS 75.08 bilioni zilipangwa, kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 56.31 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 20.28 bilioni sawa na asilimia 36.01 ya TZS 56.31 bilioni zimepatikana . Utekelezaji wa programu na miradi katika eneo hili ni kama ifuatavyo:-

### a. Mradi wa kuimarisha Ulinzi na Usalama

Mradi una lengo la kuimarisha ulinzi na usalama kwa kufikia viwango vya kimataifa ili kuweka mazingira salama kwa wananchi na wageni katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar ikiwa Zanzibar ni nchi inayopokea Watalii kutoka katika mataifa mengi duniani ambao Watalii hao wanachangia asilimia 32 ya Pato la Taifa. Hivyo, usalama wa Wageni hao wa kuwepo Zanzibar ni muhimu. Mradi huu umeanza mwaka 2023/2024 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26 na utagharimu jumla ya TZS 31.09 bilioni hadi kukamilika kwake. Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa kiasi cha TZS 20.0 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa mradi umepangiwa jumla ya TZS 15.0

bilioni. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya TZS 13.057 bilioni sawa na asilimia 87 zimetolewa kwa kutekeleza shughuli za kuweka miundombinu mipya ya mawasiliano ya ulinzi na usalama; ununuzi wa vitendea kazi vya operesheni vya Idara Maalum za SMZ na kusimamia uendeshaji wa Mradi wa Mji Salama. Kazi zilizotekelezwa ni kuanza kwa usambazaji wa vifaa kutoka kwa wazabuni walioshinda kwa mujibu wa mkataba ulioidhinishwa kutoka katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mradi huu utasaidia kuboresha utawala bora na ubora katika sekta ya Utalii pamoja na kuongeza mapato ya Serikali kutokana na uongezekaji wa Watalii nchini, kuongeza ajira na kipato kwa wananchi.

**b. Ujenzi wa Mji wa Serikali**

Mradi una lengo la kuweka mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi ili waweze kutoa huduma bora na zenye ufanisi. Mradi umepanga kujenga Ofisi mpya katika eneo la Kisakasaka. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa jumla ya TZS 55.08 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 41.3 bilioni zilipangwa kugharamia ujenzi wa Mji wa Serikali. Hadi kufikia Machi 2024, kazi zilizofanyika ni kutayarisha michoro pamoja na usafishaji wa eneo kwa ajili ya kuanza ujenzi.

## SURA YA KUMI NA MOJA

## 11.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024

### 11.1 UTANGULIZI

Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/24 ni mpango wa tatu wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP 2021-2026) pamoja na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050. Mpango huo ulipanga kutekeleza programu 31 na miradi ya maendeleo 58. Jumla ya Programu na Miradi 69 sawa na asilimia 77.5 ya Programu na Miradi yote 89 ilipangiwa fedha za Serikali. Programu na Miradi 19 sawa na asilimia 21 ilipangiwa fedha za Serikali na Washirika wa Maendeleo kwa pamoja. Programu na Miradi 35 sawa na asilimia 39.2 ilipangiwa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo pekee na jumla ya programu na miradi ya maendeleo 50 sawa na asilimia 56 ilipangiwa fedha na Serikali pekee .

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imepanga kutumia jumla ya TZS 1,521.99 bilioni kwa kutekeleza shughuli za maendeleo ambapo TZS 1,514.79 bilioni kwa ajili ya Serikali Kuu na TZS 7.2 bilioni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni ongezeko la TZS 162.60 bilioni sawa na asilimia 12.0 ikilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2022/23 ya TZS 1,352.19 bilioni. Kati ya fedha hizo (TZS 1,514.79 bilioni), Serikali ilielekeza kutumia TZS 886.0 bilioni sawa na asilimia 58.2 ya Bajeti ya Maendeleo kutoka Serikalini na TZS 628.79 bilioni (TZS 101.24 bilioni ni Ruzuku na TZS 527.55 ni Mkopo) sawa na asilimia 41.3 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kati ya fedha za Serikali (TZS 886.0 bilioni), TZS 144.0 bilioni sawa na asilimia 9.5 ni kwa ajili ya Mfuko wa Huduma ya Mikopo kwa Miradi ya Maendeleo – “Debt Service Fund”. Jumla ya TZS 915.87 bilioni sawa na asilimia 60.46 zimepangwa kutumika kwa Programu na Miradi ya Maendeleo ya Kimkakati na TZS 454.92 bilioni sawa na asilimia 30.03 ni kwa Miradi Mengineyo inayojumuisha miradi inayoendelea na ambayo Serikali ina dhima kwa Washirika wa Maendeleo.

Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 – Machi 2024), Serikali imepanga kutumia jumla ya TZS 1,244.09 bilioni ya fedha iliyopangwa kutumika kwa ajili ya Serikali kuu kwa kutekelezwa Programu na Miradi ya Maendeleo ambayo ni ongezeko la asilimia 41.54 ukilinganisha na mpango wa mwaka 2022/2023 . Kati ya fedha hizo, Serikali ilipanga kutumia TZS 772.5 bilioni sawa na asilimia 62.09 ya bajeti ya Maendeleo kutoka fedha za ndani na TZS 471.59 sawa na

asilimia 37.09 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kati ya fedha hizo (TZS 1,244.09 bilioni), TZS 686.90 bilioni zilipangwa kugharamia Programu na Miradi ya Kimkakati na yenye dhima na TZS 469.89 bilioni zilipangwa kutumika kwa Programu na Miradi mengineyo. Aidha, Jumla ya TZS. 5.4 bilioni zilipangwa kutumika kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Programu na Miradi ya Maendeleo na TZS. 108.0 bilioni zilipangwa kwa ajili ya Mfuko wa Huduma ya Mikopo kwa Miradi ya Maendeleo - "Debit Service Fund"

Sura hii inaeleza Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 kwa kila Wizara.

## 11.2 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 KWA KILA WIZARA

Katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo, jumla ya Programu na Miradi 52 sawa na asilimia 58 kati ya programu na miradi 89 iliyopangwa iliingiziwa fedha kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024. Kati ya Programu na Miradi iliyopangiwa fedha za Serikali pekee (50), Programu na Miradi 27 sawa na asilimia 54 iliingiziwa fedha katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 - Machi 2024). Kati ya Programu na Miradi iliyopangiwa fedha na Washirika wa Maendeleo pekee (35), jumla ya Programu na Miradi 9 sawa na asilimia 25.7 iliingiziwa fedha katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 - Machi 2024). Jumla ya Programu na Miradi 14 kati ya 19 sawa na asilimia 74 iliingiziwa fedha kwa pamoja kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo.

Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, matumizi ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo yamefikia jumla ya TZS 1,297.91 bilioni sawa na asilimia 104 ya lengo la TZS 1,244.09 bilioni. Kati ya Fedha hizo TZS 836.56 bilioni sawa na asilimia 108 ya lengo la TZS 772.5 bilioni ni kutoka Serikalini na TZS 461.52 bilioni sawa na asilimia 97.8 ya lengo la TZS 471.59 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Katika matumizi hayo, TZS 2.03 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zimetumika kwa kazi za kawaida ikiwemo kuimarisha takwimu, Sensa, vizazi na vifo kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano pamoja na ushiriki wa vijana katika stadi za maisha. Aidha, jumla ya TZS. 1.58 bilioni ya lengo la TZS 5.4 bilioni sawa na asilimia 29.25 zimeingizwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo na TZS 273.44 bilioni zimepatikana kwa ajili ya Mfuko wa Huduma ya Mikopo kwa Miradi ya Maendeleo - "Debit Service Fund". Fedha hizo zitatumika kwa

ajili ya kulipia madeni ya Programu na Miradi ya Maendeleo muda utakapofikia (Maturity Period). Sehemu hii inaeleza Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 kwa kila Wizara kama ifuatavyo;

### 11.2.1 Ofisi ya Rais Ikulu

Ofisi ya Rais Ikulu ina jukumu la kusimamia majukumu ya kikatiba na kisheria ya Baraza la Mapinduzi ili kuhakikisha jamii inapata uelewa juu ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo na sera zinazotekelezwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024,Ofisi ya Rais Ikulu imetekeleza miradi miwili kama ifuatavyo:-

### a) Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali

Mradi huu umeanza mwaka 2019/20 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024/2025. Mradi una lengo la kuimarisha makaazi ya viongozi wa nchi na kuyaweka makaazi hayo katika mandhari na mazingira mazuri ili kuzipa hadhi na kuimarisha usalama wa nyumba hizo. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.4 bilioni kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 600 millioni sawa na asilimia 33 ya TZS 1.80 billioni ya fedha iliyopangwa kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya matengenezo ya Ikulu ya Mnazi Mmoja. | Asilimia ya matengenezo iliyofanyika | 100 | 100 | 100 | Matengenezo yamefanyika kwa kuziba nyufa katika jengo, kulipaka rangi jengo la Ikulu,kukarabati milango na madirisha, na kubadilisha taa za mapambo katika ukumbi wa kuapishia viongozi wa kitaifa. |
| Kujenga upya ukuta wa Ikulu ya Migombani. | Asilimia ya ujenzi iliyofikia | 100 | 70 | 70 | Kazi zinazoendelea ni kupiga plasta, kutia rangi na kuweka miundombinu ya umeme |

### b) Mradi wa Uimarishaji Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mheshimiwa Rais

Mradi huu una lengo la kuimarisha ulinzi na usalama katika majengo ya Ikulu na makaazi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuhakikisha kunapatikana miundombinu iliyo imara ya mifumo ya ulinzi na usalama katika majengo hayo. Mradi umeanza mwaka 2022/2023 na unatarajiwa kukamilika 2024/2025 ambapo kwa mwaka 2023/2024, umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.0 bilioni kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 248.07 millioni sawa na asilimia 33 ya TZS 750 millioni ya fedha iliyopangwa kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufunga CCTV Camera katika Ikulu ndogo ya Dar es Salaam, Pemba na Dodoma | Idadi ya CCTV kamera zilizofungwa. | 100 | 25 | 25 | Kamera 25 zilizo nunuliwa zimefungwa katika Ikulu ndogo ya Pemba. |

### 11.2.2 Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji

Ofisi ya Rais – Kazi, Uchumi na Uwekezaji inasimamia Idara na Taasisi ambazo zina jukumu la kutekeleza malengo ya Wizara ambayo ni pamoja na kusimamia upatikanaji wa kazi za staha na kuzingatia sheria na viwango vya kazi, kuimariasha hali ya kijamii na kiuchumi ya wananchi wa Zanzibar pamoja na kuimarisha na kukuza uwezeshaji wananchi kiuchumi. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, wizara imetekeleza mradi mmoja kama ifuatavyo:-

**a) Mradi wa Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji**

Mradi huu umeanza mwaka 2021/22 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26 Mradi una lengo la kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika maeneo yote yalioainishwa kwa uwekezaji ambapo miundombinu muhimu ikiwemo barabara, maji na umeme itawekwa kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Mradi huu unatekelezwa na Serikali. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 3.5 bilioni kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2024, Jumla ya TZS 9.69 billioni sawa na asilimia 369 ya TZS 2.62 billioni ya fedha iliyopangwa kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Upelekaji wa miundombinu katika maeneo ya uwekezaji Micheweni | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 98 | 98 | Utekelezaji wa Mradi huu umetumia fedha za mwaka uliopita (2022/2023) na umejumuisha ujenzi wa barabara km 13.5 na umekamilika kwa asilimia 98, kazi zinazoendelea ni kuweka alama na mitaro ya maji machafu na upelekaji wa miundombinu ya maji na umeme imekamilika kwa asilimia 98 |

### 11.2.3 Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango

Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ina majukumu ya kusimamia shughuli zote zinazohusiana na mapato na matumizi ya fedha za Serikali. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imetekeleza Programu tatu na Mradi mmoja wa maendeleo kama ifuatavyo.

#### i) Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar

Programu hii ina lengo la kuweka mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi ili waweze kutoa huduma bora kwa wananchi. Programu imepanga kujenga Ofisi mpya katika maeneo ambayo yamependekezwa na Serikali na kukarabati majengo ambayo yameonekana kuchakaa au kupungua nafasi katika Ofisi hizo. Kwa mwaka 2023/2024, programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 74.12 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023- Machi 2024) jumla ya TZS 55.59 bilioni zimepangwa. Hadi kufikia Machi 2024, Jumla ya TZS 5.64 bilioni sawa na asilimia 40 ya fedha iliyopangwa imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ukamilishaji wa kazi ya utanuzi na ujenzi wa Ofisi za Serikali ikiwemo: Skuli ya Sheria, Ofisi ya Mufti, Nyumba ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Nyumba ya Makamo wa Pili wa Rais, Ofisi ya Shirika la Magazeti, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Wakala wa | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Skuli ya Sheria. | 100 | 5 | 5 | Kiwanja cha ujenzi kimeshapatikana, uandaaji wa michoro umeshafanyika na mchakato wa kumtafuta Mkandarasi umeshaanza. |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya Mufti, | 100 | 90 | 90 | Kazi zinazoendelea ni kuweka fremu ya lift, kujenga vyoo vitatu pamoja na ofisi mpya katika eneo liliokuwa wazi, kupiga rangi ofisi za chini nje na ndani. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati (SMIDA), Tume ya Utangazaji na Tume ya Uchaguzi; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya Shirika la Magazeti | 100 | 20 | 20 | Ujenzi umeanza na upo katika hatua ya awali (Misingi) |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. | 100 | 50 | 50 | Kazi zinazoendelea ni uwezuaji wa paa kwa ajili ya kuweka zege ghorofa ya kwanza ili kuanza ujenzi wa ghorofa ya pili |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati (SMIDA). | 100 | 80 | 80 | Ujenzi upo katika hatua za mwisho kukamilika |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Tume ya Utangazaji | 100 | 5 | 5 | Hati ya kiwanja ya eneo la ujenzi imeshapatikana, usafishaji wa eneo na upimaji wa udongo umefanyika na michoro imeshaandaliwa. |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Tume ya Uchaguzi; | 100 | 30 | 30 | Kazi zinazoendelea ni usimamishaji wa nguzo kwa ajili ya ujenzi wa ghorofa ya chini |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza ujenzi wa Mji wa Serikali katika eneo la Kisakasaka - Unguja | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 5 | 5 | Eneo la ujenzi wa mji huo limeshapatikana katika eneo la Kisakasaka- Unguja na Andiko la Dhana ya ujenzi wa mji huo limeshaandaliwa. |
| Ujenzi wa Ofisi ya Ikulu Pemba | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa ofisi ya Ikulu -Pemba | 100 | 5 | 5 | Shughuli zilizofanywa ni ulipaji wa fidia kwa kuwalipa Fidia Wananchi wa kijiji cha Pagali ambapo utajengwa ukuta wa Ofisi ya Ikulu ya Pemba |
| Ujenzi wa nyumba za Shirika la Nyumba | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa. | 100 | 60 | 60 | Ujenzi unaendelea katika hatua tofauti tofauti, majengo mawili yapo katika hatua ya kumalizia (finishing) na majengo mawili yanaendelea katika hatua ya plasta katika eneo la Kwamchina |

### ii) Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)

Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar inalenga kuimarisha miundombinu na huduma za msingi pamoja na kuimarisha haiba ya Miji ya Zanzibar. Programu hii inatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2021- 2026) kwa gharama za jumla ya TZS 346.5 bilioni. Kwa mwaka 2023/2024, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 22.810 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 17.10 bilioni zilipangwa. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 16.72 bilioni sawa na asilimia 98 ya fedha iliyopangwa imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa vifaa vya usafi (magari ya taka, makontena ya kuwekea taka na gari la kusafishia barabara) kwa Mabaraza ya Miji na Manispaa za Unguja na Pemba | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa. | 100 | 60 | 60 | Mkataba umesainiwa tarehe 07 Februari 2024 na wanunuzi ambao ni (Unit Export Limited kutoka nchini Uengereza, Eristic (T) Investment Limited kutoka Tanzania Bara) na inatarajiwa kupokea vifaa miezi minne baada ya kusainiwa kwa mkataba |
| Kufanya mapitio ya usarifu wa michoro na kuanza matayarisho ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi wa kuendeleza eneo la Michenzani na mradi salama wa watembea kwa miguu Mji Mkongwe; | Asilimia ya kazi ya mapitio ya usarifu wa michoro iliyofikiwa. | 100 | 20 | 20 | Mkataba baina ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango na mshauri elekezi (Da Alhandas) umesainiwa tarehe 06 February 2024 |
| Ununuzi wa vifaa vya uchunguzi vya maabara ya Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS); | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Vifaa vimenunuliwa na vishakabidhiwa kwa ZBS kwa ajili ya matumizi |
| Kuzijengea uwezo Taasisi za Serikali zinazosimamia maendeleo ya Miji pamoja na ununuzi wa vitendea kazi; | Idadi ya maafisa waliojengewa uwezo kutoka taasisi za Serikali zinazosimamia maendeleo ya Miji | 162 | 35 | 22 | Jumla ya Maafisa 35 wamepatiwa mafunzo ya kufanya zabuni kwa wadau mbali mbali ambao wanafanya tathmini (evaluation) ya zabuni mbali mbali za mradi wa BIG Z |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutayarisha Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi Pemba (Pemba Master Plan); | Asilimia ya matayarisho iliyofikiwa | 100 | 7 | 7 | Mshauri Elekezi wa kutayarisha Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi Pemba amepatikana na Rasimu ya Mkataba imeshaandaliwa na imepelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata ithibati. |
| Kuanza kazi za ujenzi wa mitaro na barabara za ndani kwa Unguja na kukamilisha usarifu wa michoro kwa ajili ya ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua na barabara za ndani kwa Pemba. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Mkandarasi (Kampuni ya CRJE kutoka China) amepatikana na ameshasaini mkataba kwa ajili ya kuanza kazi na kazi ya ulipaji fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi inaendelea. Kwa upande wa Pemba Mshauri elekezi (Khatib and Alami) anaendelea na kazi ya usarifu wa michoro kwa ajili ya ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua na barabara za ndani |

## a) Mradi wa Uimarishaji Rasilimali za ndani na Usimamizi wa Maliasili

Lengo la mradi huu ni kuimarisha rasilimali za ndani na usimamizi wa maliasili. Mradi umeanza mwaka 2016/2017 na umekadiriwa kutumia jumla ya TZS 6.20 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2023/2024, Mradi huu umepangiwa kutumia TZS 1.72 bilioni (TZS 34.70 milioni kutoka Serikalini na TZS 1.69 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 1.29 bilioni zimepangwa (TZS 26 milioni kutoka Serikalini na TZS 1.26 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 474.85 milioni zimeingizwa sawa na asilimia 37.68 na kutekelezwa shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoa huduma za uratibu na usimamizi wa mradi | Asilimia ya huduma zilizotolewa | 100 | 100 | 100 | |
| Huduma za ushauri kwa kuandaa Mkakati, Sera, Sheria ya Madini Zanzibar na Kanuni zake; | Asilimia ya maandalizi ya uandaaji wa Mikakati na Sera ya Madini iliyofikiwa | 100 | 85 | 85 | Rasimu ya pili ya Ushauri kwa kuandaa Mkakati na Sera ya madini imewasilishwa kwa Wizara ya Nishati, Maji na Madini |
| | Asilimia ya maandalizi ya uandaaji wa Sheria na Kanuni za Madini iliyofikiwa | 50 | 5 | 10 | Hadidu rejea tayari imeandaliwa kwa ajili ya kuendelea na taratibu za zabuni ili kumpata mshauri elekezi wa kufanya kazi hiyo |
| Huduma za ushauri kwa ajili ya mapitio ya rasimu ya Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta (PRMA) ikiwa ni pamoja na Kanuni za Governemnt Financial Statistics (GFS) za Mafuta na Gesi; | Asilimia ya maadalizi ya uandaaji wa mapitio ya rasimu ya Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta iliyofikiwa | 100 | 85 | 85 | Rasimu ya pili ya Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta (PRMA) imewasilishwa katika Wizara ya Nishati, Maji na Madini |
| Huduma za ushauri kwa maendeleo na Rasimu ya Sheria ya Ushuru wa Mafuta, ikiwa ni pamoja na Ushuru wa Faida ya Ziada; | Asilimia ya maadalizi ya uandaaji wa Rasimu ya Sheria ya Ushuru wa Mafuta iliyofikiwa | 50 | 5 | 10 | Hadidu rejea tayari imeandaliwa kwa ajili ya kuendelea na taratibu za zabuni ili kumpata mshauri elekezi kufanya kazi hiyo |

### 11.2.3.1 Tume ya Mipango Zanzibar

Tume ya Mipango ni chombo cha juu chenye mamlaka ya kuratibu, kuandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Tume imetekeleza Programu moja kama ifuatavyo;

**a) Uratibu wa Programu ya Urasimishaji Ardhi na Biashara Zanzibar**

Programu hii imelenga kukamilisha shughuli za urasimishaji wa ardhi na biashara Zanzibar ili ziweze kutumika katika juhudi za kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Utekelezaji wa Programu hii utawawezesha wananchi wanaomiliki rasilimali na kuendesha biashara nje ya mfumo usio rasmi ili waweze kuzirasimisha, kuzitumia na kupata mitaji kwa ajili ya kushiriki katika uchumi wa kisasa ulio rasmi. Kwa mwaka 2023/2024, Programu imepangiwa kutumia kiasi cha TZS 2.5 bilioni (TZS 2.0 bilioni kutoka Serikalini na 500 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 1.88 bilioni zimepangwa (TZS 1.5 bilioni kutoka Serikalini na TZS 375 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2024, Jumla ya TZS 911.9 milioni sawa na asilimia 49 ya fedha zote zilizopangwa zimeingizwa kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya utambuzi wa ardhi katika maeneo ya Mombasa kwa Mchina, Kidoti, Mahonda, Fuoni na Amani kwa upande wa Unguja, Utaani na Micheweni kwa upande wa Pemba | Idadi ya viwanja vilivyotambuliwa taarifa zake na kusajiliwa | 2000 | 1,575 | 79 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutayarisha na kuchapisha hati za usajili kwa maeneo yaliyotambuliwa | Idadi ya hati zilizotolewa kwa wananchi | 2000 | 570 | 29 | Kazi ya kutayarisha na kuchapisha hati za usajili kwa maeneo yaliyotambuliwa inaendelea |
| Kuimarisha Mfumo wa Usajili wa Hati za Matumizi ya Ardhi; | Asilimia ya uimarishaji Mfumo iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Mfumo wa usaji wa Hati za matumizi ya Ardhi umeimarishwa kwa kuanza na kuweka makabati ya Kielektroniki ya kuhifadhi nyaraka za Ardhi.. |
| Kutoa mafunzo na kuwahakiki wafanyabiashara wadogo 150 kwa kila Wilaya Unguja na Pemba; | Idadi ya wafanyabishara waliopatiwa mafunzo | 1500 | 200 | 13 | Wafanyabiashara 200 wamepatiwa mafunzo Wilaya ya Chake Chake |
| Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za mradi | Idadi ya ziara zilizofanyika | 8 | 2 | 25 | |
| Kufanya mikutano ya Kijamii kuhamasisha umuhimu wa usajili wa Ardhi na Biashara | Idadi ya mikutano iliyofanyika | 20 | 08 | 40 | |
| Kufanya vikao vya uratibu wa Programu | Idadi ya Vikao vilivyofanyaka | 06 | 01 | 16 | |
| Kufanya mafunzo na ziara za kujifunza kwa watendaji wa Programu | Idadi ya ziara za kimafunzo zilizofanyika | 04 | 01 | 25 | |

### 11.2.3.2 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali

**a) Programu ya Uendelezaji Takwimu Zanzibar (ZSDP)**

Mpango wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II) ni Programu ya kuendeleza Takwimu kwa matokeo ambayo yanalenga kuimarisha takwimu za kawaida (Routine data) sambamba na uimarishaji wa mfumo wa Taifa wa Takwimu. Mpango huu umejikita katika maeneo makuu matatu ambayo ni; kuhakikisha ubora na uwasilishaji wa taarifa; utoaji wa Takwimu, Uimarishaji na Uendelezaji wa Taasisi; na kuimarisha mifumo ya taarifa za Kiutawala ili iweze kutoa Takwimu kwa lengo la kupunguza gharama za tafiti kubwa. Programu hii imepangwa kutekelezwa kwa muda wa miaka mitano (2022/23-2026/27). Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii imepangiwa kutumia jumla TZS 4.4 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 3.32 bilioni zimepangwa. Hadi kufikia Machi 2024, Jumla ya TZS 5.98 bilioni sawa na asilimia 180 ya fedha zote zilizopangwa zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya mapitio na kuimarisha Takwimu za Pato la Taifa; | Asilimia ya kazi iliyofikiwa | 100 | 50 | 50 | Ofisi kupitia Sehemu ya Pato la Taifa inaendelea na kazi ya kufanya mapitio na kuimarisha Takwimu za Pato la Taifa |
| Kufanya Sensa ya Viwanda ya Robo Mwaka na Mwaka 2022 ya Uzalishaji Mali Viwandani; | Asilimia ya kazi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Utekelezaji wa Sensa ya Viwanda kwa Mujibu wa Mpango Kabambe wa Uimarishaji Takwimu utafanyika mwaka wa Fedha |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2024/2025, hatua za awali za matayarisho zimeshaanza. |
| Kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii ikiwemo Utafiti wa Mwaka wa Kilimo; Utafiti wa Uajiri na Mapato wa Mwaka 2022; Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa kufanya kazi kwa Mwaka 2023/2024; Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya na Utafiti wa kufuatilia Kaya; | Asilimia ya kazi iliyofikiwa. | 100 | 60 | 60 | Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) zimekamilisha kazi za ukusanyaji wa taarifa kwa tafiti tano, kazi zinazoendelea ni usafishaji pamoja na uchakataji wa taarifa zilizokusanywa kwenye tafiti hizo. |
| Kukusanya takwimu za mfumuko wa bei katika maeneo mengine ya Mjini na Vijijini; | Asilimia ya kazi iliyofikiwa. | 100 | 65 | 65 | Kazi ya ukusanyaji wa taarifa katika maeneo ya masoko na vituo mbalimbali imefanyika kwa ajili ya ukokotoaji wa Fahirisi na mfumko wa bei na kuwasilishwa kwa wadau kupitia vyombo vya habari. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa Mkakati wa Uhamasishaji na Mawasiliano; | Asilimia ya kazi iliyofikiwa. | 100 | 90 | 90 | Takwimu Rasimu ya awali ya Mkakati wa Uhamasishaji na Mawasiliano imeshakamilika na imewasilishwa kwa wadau kwa ajili ya kupata maoni. |
| Kuandaa Mfumo wa Kielektroniki wa Usambazaji Takwimu; | Asilimia ya kazi iliyofikiwa. | 100 | 40 | 40 | |
| Kufanya mapitio ya sheria na kanuni za Takwimu; | Asilimia ya kazi iliyofikiwa. | 100 | 100 | 100 | Takwimu Rasimu ya awali ya Kufanya Mapitio ya Sheria na kanuni za Takwimu imeshakamilika. |
| Kuanza matayarisho ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mtakwimu Pemba. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 85 | 85 | Matayarisho ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mtakwimu Pemba yanaendelea na Uchoraji wa Michoro (Architectural Drawing), Tathmini ya Mazingira (Environmental Assessment), Usanifu wa Udongo (Soil Test) pamoja na Usimamizi wa Ujenzi (Construction Supervision tayari vimekamilika. |

### 11.2.4 Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora

Ofisi ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Wilaya na Shehia zilizomo katika Mikoa, kujenga mazingira mazuri ya ushiriki wa wananchi katika kudumisha amani, usalama, ulinzi wa mali zao na kuimarisha huduma za kijamii. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imetekeleza miradi mitatu ya maendeleo kama ifuatavyo-:

**a) Mradi wa Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki kwa Wanawake katika Kesi za Udhalilishaji (UN-WOMEN)**

Mradi huu una lengo la kupunguza vitendo vya udhalilishaji kwa vijana, wanawake na watoto. Mradi umeanza mwaka 2023/2024 na unatekelezwa kwa kipindi cha miaka minne ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 umepangiwa jumla ya TZS 373 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 280 milioni. Hadi kufikia Machi 2024, Jumla ya TZS 163.4 millioni sawa na asilimia 58 ya fedha iliyopangwa imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha uratibu na taratibu za usimamizi wa kesi katika ngazi ya kitaifa kupitia mikutano kati ya polisi, mahakama na DPP; | Idadi ya mikutano iliyofanyika | 4 | 1 | 25 | |
| Kuandaa Miongozo ya Hukumu ya Kimahakama; | Asilimia ya uandaaji wa miongozo iliyofikiwa | 100 | 50 | 50 | Maoni ya uandaaji wa muongozo yameshakusanywa, Rasimu ya mwanzo imeshaandaliwa na kuwasilishwa kwa uongozi wa Wizara. |
| Kujenga uwezo wa Kitengo cha Ulinzi cha kesi za jinai cha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka | Idadi ya Maafisa waliojengewa uwezo | 50 | 50 | 100 | Maafisa wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo katika masuala ya ukatili na udhahalilishaji wa kijinsia (SGBV) |

### 11.2.4.1 Mahakama Kuu

**a) Mradi wa Ujenzi wa Mahakama za Mikoa**

Mradi huu una lengo la kujenga majengo ya mahakama za Mikoa na Wilaya kwa ajili ya kuimarisha mazingira ya kazi na kuwa na Ofisi za kisasa zitakozoongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kisheria na upatikanaji wa haki. Mradi umeanza mwaka 2022/2023 na umepangwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitano (2022-2027), mradi utagharimu jumla ya TZS 48.6 bilioni hadi kukamilika kwake. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 25 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 18.7 bilioni zimepangwa na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 7.2 bilioni sawa na asilimia 39 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Mjini Magharibi katika eneo la Mazizini Unguja. | Asilimia ya ujenzi ilyofikiwa | 100 | 40 | 40 | Ujenzi unaendelea katika hatua ya kusimamisha nguzo kwa ajili ya ujenzi wa ghorofa ya kwanza |
| Kujenga Mahakama ya wilaya ya Magharibi “B” eneo la Kisakasaka. | Asilimia ya ujenzi ilyofikiwa | 100 | 40 | 40 | Ujenzi unaendelea katika hatua ya kusimamisha nguzo kwa ajili ya ujenzi wa ghorofa ya kwanza |
| Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini katika eneo la Pale; | Asilimia ya ujenzi ilyofikiwa | 100 | 40 | 40 | Ujenzi unaendelea katika hatua ya kusimamisha nguzo kwa ajili ya ujenzi wa ghorofa ya kwanza |
| Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Kusini Unguja katika eneo la Tunguu/ Binguni; | Asilimia ya ujenzi ilyofikiwa | 100 | 40 | 40 | Ujenzi unaendelea katika hatua ya kusimamisha nguzo kwa ajili ya ujenzi wa ghorofa ya kwanza |
| Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Pemba katika eneo la Kinyasini; | Asilimia ya ujenzi ilyofikiwa | 100 | 30 | 30 | Ujenzi upo katika hatua ya ya kuweka jamvi kwa ajili ya kuendelea na ghorofa ya kwanza. |
| Kujenga Mahakama ya Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba katika eneo la Konde | Asilimia ya Ujenzi iliyofikiwa | 100 | 29 | 29 | Ujenzi upo katika hatua ya ya kuweka jamvi kwa ajili ya kuendelea na ghorofa ya kwanza. |
| Kujenga Mahakama ya Wilaya Mkoa wa Kusini Pemba katika eneo la Mkoani | Asilimia ya Ujenzi iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Kazi inayoendelea ni ujenzi wa matufali katika ghorofa ya chini (Ground floor) |
| Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Kusini Pemba katika eneo la MfikiwaChake Chake. | Asilimia ya ujenzi ilyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Maandalizi ya ujenzi yanaendelea ikiwemo matayarisho kwa ajili ya kusaini Mkataba baina ya Mkandarasi na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania |

### 11.2.5 Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais

Ofisi ina dhamana ya kuratibu na kusimamia shughuli za sekta mtambuka zikiwemo mazingira, Ukimwi, Watu Wenye Mahitaji Maalum pamoja na udhibiti wa madawa ya kulevya. Kwa kipindi cha Julai 2023-Machi 2024 Ofisi imetekeleza miradi mitano ya maendeleo kama ifuatavyo:-

**a) Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii ya Pwani**

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kujenga uwezo wa wakulima wadogo, kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa njia za vitendo na ubunifu ambazo zitakua na matokeo yenye tija. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2021/2022 hadi 2023/2024, unagharimu jumla TZS 2.4 bilioni. Mradi unatekelezwa kwa pamoja baina ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo kutoka Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (Adaptation Fund) na kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 774 milioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-March 2024) jumla ya TZS 580.8 milioni zilipangwa. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 290 millioni sawa na asilimia 50 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo na kuandaa vitini vya kufundishia kwa maafisa wilaya | Idadi ya vitini vilivyoandaliwa | 2 | 2 | 100 | |
| Kutoa taarifa za matokeo au faida ya shughuli za mradi kwa kupitia Utaarishaji wa video ya mradi (documentary) | Idadi ya makala ya video zilizo taarishwa | 1 | 1 | 100 | Makala ya matokeo ya utekelezaji wa kazi za mwaka za mradi katika maeneo ya Bumbwini (Makoba, Mafufuni, Kiongwe Kidogo) kwa Unguja na Tovuni kwa upande wa Pemba imetayarishwa |

## b) Mradi wa Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mfumo wa Ikolojia Vijijini

Mradi una lengo la kusaidia uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kwa kurejesha uoto wa asili kwa kutumia mifumo ya ikolojia, kutoa elimu ya kilimo chenye kustahamili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuwajengea uwezo jamii juu ya njia mbadala za kujipatia kipato ambazo hazina athari za kimazingira. Mradi unatekelezwa kwa miaka sita, kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2023/2024, na unagharimu jumla ya TZS 1.10 bilioni. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo kutoka (United Nations Environment Programme - UNEP) na kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 234 milion. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 175.8 milioni zilipangwa . Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 15.4 millioni sawa na asilimia 9 ya fedha iliyopangwa imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| Kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Amali (Kituo cha sabuni na vipodozi, kituo cha ushoni wa vyarahani na upakasaji na kituo cha uendelezaji wa mifugo ) kwa Shehia za Kijini, Mbuyu tende na Jugakuu | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 100 | 100 | |
| | Idadi ya vituo vya Amali vilivyojengwa | 3 | 3 | 100 | |
| Kukamilisha ujenzi wa vitalu nyumba katika eneo la Mradi kwa ajili ya kutolea mafunzo ya kilimo chenye kustahmili ukame (climate smart Agriculture) | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 100 | 100 | |
| | Idadi ya ujenzi vitalu nyumba vilivyojengwa. | 3 | 3 | 100 | |
| Kumalizia kazi za Ujenzi wa visima kwa shehia tatu za Matemwe zinazotekeleza mradi | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 100 | 100 | Jumla ya visima 6 vimekamilika, minara ya kuhifadhia maji pamoja na uwekaji wa *solar power* kwa kila kisima katika Shehia zote tatu umekamilika |
| Ununuzi wa vyerehani na kuandaa mafunzo ya ushoni na upakasaji kwa Shehia za kijini,Mbuyutende na Jugakuu | Idadi ya vyerehani vilivyonunuliwa | 42 | 42 | 100 | |
| | Idadi ya vikundi vilivyopatiwa mafunzo | 3 | 3 | 100 | |
| | Idadi ya washiriki waliopatiwa mafunzo | 45 | 45 | 100 | |
| Kuandaa mafunzo ya ufugaji kuku kwa shehia tatu za Matemwe Kijini Mbuyutende na Jugakuu | Idadi ya Shehia zilizopatiwa mafunzo | 3 | 3 | 100 | |

**c) Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Maji Machafu katika Eneo la Msingini Kichungwani Chake Chake Pemba.**

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kusafisha maji taka katika maeneo ya makaazi kwa kutumia Mfumo wa kiasili (Nature Based System) kama vile nyasi kwa ajili ya kupunguza uchafu wa mazingira hasa katika pwani ya hifadhi ya ukanda wa Pemba (PECCA). Mradi unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo kutoka (United Nations Environment Programme-UNEP). Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 192 milioni na kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 144 milioni zilipangwa. Hadi kufikia Machi 2024 shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa uzio wa kiunganishi cha mnyororo wa kuzunguka mabwawa; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | |
| Kutoa mafunzo ya matumizi ya mimea katika kazi za mikono kwa wenyeji. | Idadi ya wenyeji waliopatiwa mafunzo | 30 | 30 | 100 | |
| Kutoa tope, kuosha kokoto, kupanga mawe katika mabwawa ya kusafishia maji kwa ajili ya kujenga kituo cha kupima kina cha maji ya bahari. | Asilimia ya ujenzi iliofanyika | 100 | 100 | 100 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukarabati mabomba yaliyoharibika na uwekaji milango katika mashimo (Chembers) pamoja na ulazaji wa mabomba mapya katika eneo la mradi | Asilimia ya ukarabati uliofikiwa | 100 | 100 | 100 | |
| Kupanda majani aina nne (typhaspp, vetiver,napier na Cyperus) | Asilimia ya eneo la mraba (square meter) lililopandwa majani. | 100 | 100 | 100 | |
| Kufanya ujenzi wa matuta,ukataji mlima na upandaji majani (vetiver)kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | |

### d) Mradi wa Kuimarisha Jamii kwa Kuzingatia Ikolojia na Shughuli za Kujipatia Kipato kwa Wavuvi Wadogo Wadogo na Usimamizi wa Eneo la Hifadhi la Mkondo wa Pemba (PECCA)

Mradi umeanzishwa kwa mpango endelevu wa matumizi ya maliasili za bahari na shughuli za kujipatia kipato kwa jamii ya eneo la Hifadhi - PECCA. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka 2022/23 hadi 2023/2024. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa jumla ya TZS 249.8 milioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 187.3 milioni zilipangwa na hadi kufikia Machi 2024 shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya mikutano ya kuhamasiha jamii juu ya usimamizi wa Taka bahari kwenye shehia ya Tibirinzi Chakechake Pemba | Idadi ya mikutano iliyofanyika | 6 | 6 | 100 | |
| | Idadi ya watu walioshiriki | 200 | 200 | 100 | |
| Kukabidhi vifaa vya usafi kwa ajili ya usimamizi wa taka kwa shehia ya Tibirinzi | Asilimia ya vifaa vilivotolewa. | 100 | 70 | 70 | |
| Kutoa mafunzo ya usarifu na kuongeza thamani ya Dagaa | Idadi ya watu waliopatiwa mafunzo | 76 | 76 | 100 | |
| Kutoa mafunzo ya ulimaji wa zao la mwani kwenye kina kikubwa cha maji | Idadi ya washiriki waliopatiwa mafunzo | 100 | 100 | 100 | |
| Kutoa mafunzo ya kuogolea kwa kina mama wanaojishughulisha na ulimaji wa zao la mwani | Idadi ya watu waliopatiwa mafunzo | 40 | 45 | 113 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoa vifaa mbalimbali vya ukulima wa mwani katika shehia za fundo na kilindi pamoja na vifaa vya kukaushia madagaa katika shehia za wesha na Ndagoni | Asilimia ya vifaa vilivyotolewa | 100 | 100 | 100 | Vifaa vilivyotolewa ni :-Chanja,Ving'amozi Kamba, Taitai na Maboya. |
| Kutoa vifaa mbalimbali vya ukulima wa mwani katika shehia za fundo na kilindi pamoja na vifaa vya kukaushia madagaa katika shehia za wesha na Ndagoni | Asilimia ya vifaa vilivyotolewa | 100 | 100 | 100 | Vifaa vilivyotolewa ni :-Chanja,Ving'amozi Kamba, Taitai na Maboya. |
| Kuweka vifaa vya kuhifadhi chupa za plastiki katika maeneo mbalimbali ya shehia inayotekelezwa mradi | Asilimia ya vifaa vilivyowekwa | 100 | 100 | 100 | |
| Kufanya mikutano ya kukusanya maoni ya wadau juu ya Rasimu ya miongozo wa uzuiaji wa muda wa shughuli za uvuvi | Idadi ya mikutano iliyofanyika | 2 | 2 | 100 | |
| | Idadi ya watu walioshiriki. | 46 | 46 | 100 | |
| Kufanya mikutano ya mashauriano juu ya ufanyaji wa doria kwa maeneo matatu yaliyo fungiwa kwa ajili ya uvuvi wa pweza (voluntary octopus closure) | Idadi ya mikutano iliofanyika | 3 | 3 | 100 | |
| | Idadi ya watu walioshiriki. | 47 | 47 | 100 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya kikao cha uzinduzi wa mpango wa usimamizi ya matumizi ya bahari kwa ukanda wa eneo la hifadhi ya mkondo wa Pemba Pecca, kilichohakikiwa na mapitio ya jamii juu ya matumizi ya bahari’’Verification of previous participatory resource mapping’’ | Idadi ya watu walioshiriki | 190 | 190 | 100 | |

### 11.2.5.1 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya

**a) Mradi wa Kuimarisha Mamlaka ya Kupambana na Madawa ya Kulevya**

Mradi wa Ujenzi wa Kituo umeanza utekelezaji wake awamu ya pili (II) mwaka 2018/19 hadi 2024/2025. Mradi una lengo la kuimarisha kituo cha matibabu na kurekebisha tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya. Mradi unatekelezwa na Serikali pekee na kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa kiasi cha TZS 1.5 bilioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 1.125 bilioni zilipangwa na hadi kufikia Machi 2024 jumla ya TZS 973 millioni sawa na asilimia 86 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| **Shughuli Iliyopangwa** | **Kiashiria** | **Shabaha** | **Utekelezaji Halisi** | **Asilimia ya Utekelezaji** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa jengo kuu la utawala katika kituo cha Kidimni | Asilimia ya ujenzi uliofikia | 100 | 100 | 100 | |
| Ukarabati wa jengo la Ofisi za Mamlaka iliopo Kilimani; | Asilimia ya ujenzi uliofikia | 100 | 100 | 100 | |
| Kukamilisha jengo la kituo cha tiba na marekebisho ya tabia Kidimni | Asilimia ya ujenzi iliofikia | 100 | 100 | 100 | |
| Kujenga nyumba za wafanyakazi (madaktari) (4in 1) | Asilimia ya ujenzi uiliofikia | 100 | 100 | 100 | |
| | Idadi ya nyumba zilizojengwa | 4 | 4 | 100 | |
| Kujenga viwanja vya michezo | Asilimia ya ujenzi uliofikiya | 100 | 100 | 100 | |
| | Idadi ya viwanja vilivyojengwa | 2 | 2 | 100 | |

### 11.2.6 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi

Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais - Sera Uratibu na Baraza la Wawakilishi ina dhamana ya kusimamia, kuratibu na kufuatilia shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kwa kipindi cha miezi tisa ( Julai 2023- Machi 2024) Wizara imetekeleza Programu moja ya maendeleo kama ifuatavyo:-

**a) Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini Awamu ya Tatu (TASAF III) Kipindi cha Pili**

Programu inatekelezwa baina ya Tanzania Bara na Zanzibar, inagharimu jumla ya TZS 112.2 bilioni. Programu imeanza utekelezaji kwa awamu (III) mwaka 2020/21 na kumalizika ifikapo mwaka 2024/25, ikiwa na lengo la kuziwezesha kaya masikini sana kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu ya kibinadamu hasa chakula, afya na elimu. Programu hii inakusudia kutekeleza miradi iliyoibuliwa na wananchi katika nyanja mbali mbali za elimu, afya na ajira za muda, kwa lengo la kuwawezesha wananchi ili waweze kujikwamua na umasikini. Kwa mwaka 2023/2024 programu hii imepangiwa kiasi cha TZS 17.6 bilioni ambazo TZS 100 milioni kutoka Serikalini na TZS 17.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 13.2 bilioni zilipangwa na hadi kufikia Machi 2024 jumla ya TZS 15.9 billioni sawa na asilimia 121 ya fedha

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza ujenzi wa kituo cha mama na mtoto katika eneo la Upenja Unguja | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 21 | 21 | Ujenzi upo katika hatua ya msingi. |
| Kuanza ujenzi wa ukumbi wa kufanyia mitihani skuli ya Bambi - Unguja; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 98 | 98 | Ujenzi uko katika hatua ya umaliziaji (finishing) |
| Uhaulishaji wa fedha kwa kaya masikini (walengwa wa mradi Unguja na Pemba). | Idadi ya kaya zilizohaulishiwa fedha Unguja. | 24,491 | 24,396 | 99.6 | |
| | Idadi ya kaya zilizohaulishiwa fedha Pemba | 26,220 | 26,125 | 99 | |
| Kuwapatia ruzuku ya uzalishaji walengwa Unguja na Pemba | Idadi ya kaya zilizopatiwa ruzuku Unguja. | 2,918 | 2,918 | 100 | |
| | Idadi ya kaya zilizopatiwa ruzuku Pemba | 926 | 926 | 100 | |
| Ujenzi wa Kituo cha Afya daraja la pili Shehia ya Kinyikani Pemba | Asilimia ya ujenzi wa iliyofikiwa. | 100 | 60 | 60 | Kazi zinazoendelea ni kupiga plasta, kuweka sakafu pamoja na madirisha |
| Ujenzi wa Kituo cha Afya daraja la pili Shehia ya Uzi | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 100 | 100 | |
| Kuwapatia mafunzo na ushauri Kaya za Shehia zilizopata ruzuku ya uzalishaji | Idadi ya Kaya zilizopatiwa mafunzo na ushauri | 29 | 29 | 100 | |

### 11.2.7 Wizara ya Afya

Wizara ya Afya ina jukumu na wajibu wa kusimamia afya za wananchi wote wa Zanzibar ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za ujenzi wa Taifa na kuleta maendeleo endelevu. Kwa kipindi cha Julai 2023-Machi 2024 Wizara imetekeleza programu sita na miradi miwili ya maendeleo.

#### i) Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi

Programu hii imeanza mwaka 2023/2024 na ina lengo la kuimarisha afya ya msingi kwa kuimarisha miundombinu ya vituo vya afya ya msingi ili viweze kutoa huduma za afya ya msingi zenye kiwango na kuimarisha afya ya jamii. Programu hii inatekelezwa na Serikali ambapo kwa mwaka 2023/2024 imepangiwa jumla ya TZS. 20.0 bilioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 - Machi 2024) jumla ya TZS 15.0 bilioni zilipangwa na hadi kufikia Machi 2024 shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuvifanyia ukarabati vituo vya afya; | Idadi ya vituo vya afya vilivyofanyiwa ukarabati | 142 | 11 | 8 | Vituo 11 vimefanyiwa ukarabati wa mindombinu ya maji, na vyoo |
| Kuvijenga tena vituo vya afya 25 ambavyo havijafikia vigezo vinavohitajika | Idadi ya vituo vya Afya vilivyojengwa | 53 | 5 | 9.4 | Zabuni imefanyika na wazabuni wameshapatikana na tayari wapo kwenye hatua za kuanza kwa ujenzi Unguja na Pemba. |

### ii) Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya na Mikoa

Programu ina lengo la kuimarisha makaazi kwa wafanyakazi ili wawe na utulivu wa kufanya kazi na kuongeza ufanisi na kupatikana muda wote itakapotokea dharura. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya TZS 20.0 bilioni zimetengwa kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-March 2024) jumla ya TZS 15.0 bilioni zilipangwa na hadi kufikia Machi 2024 jumla ya TZS 3.08 billioni sawa na asilimia 21 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Mkoa –Lumumba | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 15 | 15 | Ujenzi umeanza kwa hatua za awali |
| Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Wilaya – Pangatupu; | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 17 | 17 | Ujenzi unaendelea katika hatua ya kusimamisha nguzo |
| Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Wilaya - Mwera Pongwe | Asilimia ya ujenzi iliofikiya | 100 | 15 | 15 | Ujenzi upo katika hatua za mwisho za kukamilisha msingi, |
| Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Wilaya – Kitogani; | Asilimia ya ujenzi iliofikiya | 100 | 20 | 20 | Ujenzi unaendelea katika hatua ya kusimamisha nguzo |
| Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Wilaya – Kinyasini. | Asilimia ya ujenzi iliofikiya | 100 | 20 | 20 | Ujenzi unaendelea katika hatua ya kusimamisha nguzo |
| Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Wilaya Vitongoji | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 0 | 0 | Hatua za zabuni zinaendelea ambapo tathmini imekamilika na mkandarasi anasubiria kuitwa kwa ajili ya mapatano ili aweze kusaini mkataba na kuanza ujenzi. |

### iii) Programu ya Kuimarisha Huduma za Mama na Mtoto

Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za mama na mtoto nchini. Programu imeanza mwaka 2022/23 na inatarajiwa kutekelezwa kwa muda wa miaka mitano kwa gharama ya *USD* 25 milioni. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.7 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 1.34 bilioni zilipangwa na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 1.13 bilioni sawa na asilimia 84 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga miundombinu ya usafi wa mazingira (WASH) katika vituo vya Afya vya Miwani, Shungi na Finya; | Idadi ya vituo vilivyojengwa miundombinu ya usafi wa mazingira | 14 | 0 | 0 | Taratibu za manunuzi ya vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya vituo vya afya Imefanyika na makubaliano baina ya wizara na UNICEF kwa ajili ya kufanya manunuzi hayo yamefanyika |
| Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wataalamu wa afya kwa ngazi ya Shahada ya Uzamili | Idadi ya Madaktari bingwa waliopatiwa mafunzo katika ngazi ya shahada ya uzamili | 30 | 30 | 100 | Jumla ya Madaktari bingwa 30 wa ngazi ya shahada ya uzamili. |

### iv) Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar.

Programu hii ina lengo la kutokomeza maradhi ya malaria kwa kuhakikisha kwamba maradhi haya yanamalizika kabisa hapa Zanzibar. Aidha, programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 1.53 bilioni (TZS 550.0 milioni kutoka Serikalini na TZS 977.7 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa ajili ya utekelezi. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 1.15 bilioni (TZS 412.5 milioni kutoka Serikalini na TZS 733.3 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zilipangwa na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS1.94 billioni sawa na asilimia 170 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Uchunguzi na utibabu wa ugonjwa wa malaria; | Idadi ya wagonjwa waliofanyiwa uchunguzi | 260,112 | 442,939 | 170 | Jumla ya washukiwa 442,939 walifanyiwa uchunguzi wa ugonjwa wa maleria (Unguja - 392,042 na Pemba 50,897) |
| Udhibiti wa mbu waenezao malaria. | Idadi ya nyumba zilizopigwa dawa | 11,154 | 11,047 | 99 | Jumla ya nyumba 11,047 zimepigwa dawa (Unguja nyumba 8,025 na Pemba nyumba 3,022) |
| | Idadi ya vyandarua vilivyotolewa kwa wananchi | 81,000 | 93,225 | 115 | Jumla ya vyandarua 93,225 vilitolewa kwa mama wajawazito na watototo chini ya umriwa mwaka mmoja (Unguja 62,265 na Pemba 30,960). Aidha, jumla ya vyandaraua 252,155 viligawiwa kwa jamii katika Shehia 75 kwa ajili ya kujikinga na malaria |
| Ufuatiliaji wa mwenendo wa ugonjwa wa malaria; | Idadi ya wagonjwa wa Malaria waliofatiliwa | 13,895 | 19,074 | 137 | Jumla ya wagonjwa 19,074 waligundulika na ugonjwa wa malaria .Ongezeko la wagonjwa wa malaria imesababishwa na mabadiliko ya Tabianchi na kuchelewa kufika katika vituo vya afya mapema |

### v) Programu Shirikishi ya UKIMWI, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma

Programu hii ina lengo la kupambana na maradhi ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma. Lengo kuu ni kupunguza kasi ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi, kupunguza vifo vitokanavyo na maradhi ya kifua kikuu, homa ya Ini na kupunguza maambukizi ya ukoma. Kwa mwaka 2023/2024 Programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Jumla ya TZS 1.55 bilioni zimetengwa kutekeleza mradi huu (TZS 1.05 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS. 500.0 milioni kutoka Serikalini). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 1.16 bilioni zimepangwa na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS1.64 bilioni sawa na asilimia 142 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha huduma ya utoaji wa kinga ya maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto | Asilimia ya mama wajawazito wanaohudhuria kliniki wanaopatiwa huduma za upimaji wa VVU | 100 | 95 | 95 | Jumla ya kina mama wajawazito walihudhuria katika klinik kwa mara ya kwanza ni 51,480 waliohudhuria Kliniki wakati wa ujauzito kati ya hao 46,430 walipimwa VVU katika vituo vya Afya. Jumla ya wajawazito 58 waligundulika kua na maambukizi ya VVU. |
| | Idadi ya watu waliopewa ushauri nasaha na waliopimwa VVU | 69,656 | 65,643 | 94 | Jumla ya watu 65,643 (wanaume 29,990 na wanawake 35,653) walipatiwa huduma ya ushauri nasaha na uchunguzi wa VVU kati ya hao 572 (0.9%), (Unguja 519 na Pemba 53) waligundulika kua na maambukizo ya VVU |
| Kuimarisha utoaji wa huduma za kinga na tiba ya Homa ya Ini | Idadi ya watu waliogundulika na virusi vya homa ya ini B | 33,521 | 18,922 | 56 | Jumla ya wateja 1,302 (710 wanaume na 592wanawake) kwa Unguja na Pemba waligundulika na maambukizi ya vurus ya homa ya Ini B, kati ya wagonjwa hao jumla ya wateja 473 wamesajiliwa katika kliniki za homa ya Ini kwa Unguja na Pemba. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha utoaji wa huduma za UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma | Idadi ya wagonjwa wa kifua kikuu waliogunduliwa | 840 | 752 | 89 | Jumla ya wagonjwa 752 wa kifua kikuu waligundulika (Unguja 553 na Pemba ni 199). Aidha jumla ya wagonjwa wapya 50 (44 Unguja na Pemba 6) waligundulika na maradhi ya Ukoma wagonjwa wote hao waliogundulikana magonjwa hayo wameanzishiwa matibabu. |
| Kuimarisha utoaji wa huduma za matibabu kwa wagonjwa wanoishi na virusi vya UKIMWI; | Idadi ya watu wanaoishi na VVU waliopatiwa ARVs | 9,942 | 8,561 | 86 | Malengo hayakuweza kufikiwa kutokana upungufu wa vitendanishi ambavyo vingeweza kuibua watu waliogundulika na VVU na kupelekwa kwenye kliniki za huduma na tiba kwa kuanzishiwa dawa za kupunguza mazaliano ya VVU ARVs |

### vi) Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto (IRCH)

Programu hii ina lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi pamoja na vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Jumla ya TZS 5.8 bilioni zimetengwa kwa programu hii (TZS 1.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 4.8 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa mwaka 2023/2024. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 4.35 bilioni (TZS 750 milioni kutoka Serikalini na TZS 3.6 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zilipangwa. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS1.91 bilioni sawa na asilimia 44 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha huduma za afya ya uzazi na kupunguza vifo vya mama na mtoto; | Idadi ya akina mama waliojifunguwa | 60,951 | 41,129 | 67 | Jumla ya akina mama 41,129 (Unguja 28,307 na Pemba 12,822) walijiguwa katika vituo vya afya na hospitali |
| | Idadi ya vifo vya watoto wachanga vilivyohakikiwa | 1,418 | 1,418 | 100 | Matokeo ya uhakiki yamebainisha miongoni mwa sababu za vifo hivyo ni watoto kukosa hewa wakati wa kuzaliwa, uzito pungufu na matatizo yatokanayo na mtoto njiti. |
| | Idadi ya vifo vya mama vitokanavyo na uzazi vilivyohakikiwa | 60 | 60 | 100 | Sababu za vifo ni upungufu wa damu; kifafa cha mimba, kutokwa na damu nyingi wakati wa ujauzito na kisukari |
| | Idadi ya akina mama wanaopata huduma ya afya ndani ya masaa 48 baada ya kujifungua | 45,713 | 34,237 | 75 | Takwimu zinaonesha ongezeko la kina mama wanaofika kituoni na hospitali hupatiwa huduma za matibabu ndani ya siku mbili baada ya kujifungua. Ila bado kuna kina mama ambao wanaojifungulia majumbani |
| | Idadi ya wateja wapya wanaotumia njia za kisasa za uzazi wa mpango | 382,393 | 26,790 | 7.0 | Jumla ya wasichana 26,790 (Unguja 20,016 na Pemba 6,774) walijiunga na njia za kisasa za uzazi wa mpango kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 – Machi 2024). |
| Kuimarisha huduma za mama na watoto chini ya miaka 5 na watoto wachanga; | Idadi ya watoto walioripotiwa kuwa na ulemavu wa ghafla | 2 /100,000 | 12/100,000 | 600 | Jumla ya visa 12 (Unguja7 na Pemba 5) vya washukiwa wa ulemavu wa ghafla vimeripotiwa kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 |
| Kuimarisha upatikanaji wa taarifa za mama na mtoto; | Idadi ya mama wajawazito waliohudhuria kliniki angalau mara moja | 60,951 | 46,209 | 75 | Jumla ya kina mama 46,209 walihudhuria kliniki angalau mara moja katika vituo na Hospitali kwa Unguja na Pemba. Kati ya hao kina mama 9,538 sawa na asilimia 21 walihudhuria kliniki mapema chini ya wiki 12. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya vituo vya afya vya Serikali vinavyotoa huduma za dharura wakati wa kujifungua | 181 | 47 | 26 | Vituo vinavyotoa huduma za dharura wakati wakujifungua ni 47 kwa lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na mama na watoto wachanga. |
| Kuimarisha huduma za damu salama | Idadi ya wagojwa waliopatiwa damu | 15,000 | 11,811 | 79 | Jumla ya *unit* 12,954 sawa na asilimia 33 kati ya maombi ya *unit* 38,595 ya damu zilizosambazwa kupitia hospitali za umma na hospitali binafsi kwa matumizi mbali mbali ikiwemo mama wajawzito na watoto |
| Kuimarisha utoaji wa huduma za chanjo za mama na watoto. | Idadi ya mama waliopatiwa chanjo | 45,713 | 44,207 | 97 | Jumla ya kinamama 32,743 wamepatiwa chanjo ya Pepopunda (TT) kwa Unguja na kwa upande wa Pemba ni 14,464 |
| | Idadi ya watoto waliochanjwa PENTA 3 kwa watoto chini ya mwaka mmoja | 55,779 | 49,347 | 88.5 | Jumla ya watoto walipatiwa dozi ya tatu ya chanjo ya PENTA kwa Unguja ni 32,334 na Pemba ni 17,013. |
| | Idadi ya wasichana waliopatiwa chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi | 18,707 | 4,109 | 22 | Wasichana wenye umri kati ya miaka 9 mpaka miaka 14 wamepatiwa chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi ndani ya kipindi cha miezi tisa Julai 2023 – Machi 2024. |

### a) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya-Kizimkazi

Mradi huu umeanza mwaka 2023/2024 na unalengo la kuimarisha miundombinu ya afya kwa kujenga kituo cha afya ambacho kitatoa huduma bora kwa wananchi wa eneo hilo na maeneo jirani. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo jumla ya TZS. 4.0 bilioni zimetengwa kwa mwaka 2023/2024. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 3.0 bilioni zimeingizwa. Hadi kufikia Machi 2024 shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Kituo cha Afya; | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 75 | 75 | Kazi zinazoendelea ni kuezeka na kupiga plasta. Aidha vifaa tiba vitaingizwa baada ya kukamilika kwa ujenzi. |

## b) Mradi wa Kuipandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mradi huu unalengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Mradi huu unatekelezwa na Serikali na kwa mwaka wa fedha 2023/2024, umetengewa TZS 1.1 bilioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 843.9 milioni zilipangwa na hadi kufikia Machi 2024 jumla ya TZS 1.045 bilioni sawa na asilimia 124 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa machine na vifaa tiba; | Asilimia ya vifaa vilivyonunuliwa | 100 | 10 | 10 | Maombi ya ununuzi ya vifaa yamefanyika, hata hivyo ununuzi haujafinyika kutokana na zabuni hizo kusitishwa kwa kupisha ujenzi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja |
| Ununuzi wa mtambo wa kuchomea taka tiba (incinerator); | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa. | 100 | 20 | 20 | Zabuni imeshakamilika na wazabuni watatu wamejitokeza kwenye zabuni hiyo, hata hivyo ununuzi haujafinyika kutokana na zabuni hizo kusitishwa kwa kupisha ujenzi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja |
| Ununuzi wa samani. | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa. | 100 | 20 | 20 | |

### c) Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma katika hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa. Kupitia mradi huu Serikali imepanga kufanya ukarabati mkubwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuiwezesha kutoa huduma nzuri na zenye kukidhi mahitaji. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 10.0 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 7.5 bilioni zilipangwa na hadi kufikia machi 2024, jumla ya TZS 281.6 milioni sawa na asilimia 4 ya fedha iliyopangwa imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kumlipa Mshauri Elekezi; | Asilimia ya fedha zilizolipwa | 100 | 76.3 | 76.3 | Kwa kipindi cha Miezi tisa Mshauri elekezi amelipwa TZS 970,905,000 ya lengo la TZS 1,273,025,959.75 kwa ajili ya malipo ya mshahara na ushauri elekezi |
| Uratibu na usimamizi wa mradi. | Asilimia ya uratibu iliyofanyika | 100 | 10 | 10 | Mkataba wa ununuzi wa gari kwa ajili ya uratibu wa mradi umewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kupata ithibati |

### 11.2.8 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ina jukumu la kukuza na kuendeleza sekta ya biashara na viwanda kwa lengo la kuleta maendeleo nchini. Kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi 2024, Wizara imetekeleza miradi miwili ya maendeleo kama ifuatavyo:-

### a) Mradi wa Kuimarisha Maeneo Tengefu ya Viwanda (Industrial Park)

Mradi huu umeanza mwaka 2019/20 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26, Mradi una lengo la kuvutia uwekezaji, kutengeneza ajira na kuongeza mauzo ya nje kwa kukabiliana na vikwazo vinavyozuia michakato ya ukuaji wa viwanda Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 26.0 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 19.5 bilioni zilipangwa na hadi kufikia Machi 2024 jumla ya TZS 8.4 bilioni sawa na asilimia 43 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga ukuta wa uzio, mabanda matatu ya viwanda, miundombinu ya barabara za ndani pamoja na miundombinu ya umeme na TEHAMA katika eneo la uwekezaji Dunga | Asilimia ya ujenzi wa miundombinu iliyofikiwa. | 100 | 50 | 50 | Hatua ya ujenzi wa barabara ya mzunguuko katika eneo la mradi imekamilika kwa kiwango cha kifusi na kazi zakuweka miundombinu ya umeme na TEHAMA bado haujaanza katika eneo la uwekezaji Dunga |
| Kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi (Master Plan) katika eneo la Viwanda la Dunga na Chamanangwe. | Asilimia ya kazi iliyofikiwa katika eneo la viwanda la Dunga | 100 | 100 | 100 | |
| | Asilimia ya kazi iliyofikiwa katika eneo la viwanda la Chamanangwe | 100 | 80 | 80 | Kwa upande wa Chamanangwe mpango umekamilika umeshawasilishwa katika uongozi wa Wizara |
| Kujenga mnara na tangi la maji la lita 1,000,000 katika eneo la uwekezaji Dunga. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 46 | 46 | Kazi ya ujenzi ipo katika hatua ya kuweka jamvi kwa ajili ya kuweka tangi la maji. |

**b) Mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho Zanzibar**

Mradi huu ulianza mwaka 2017/18 na kutarajia kukamilika mwaka 2024/25 ambapo lengo kuu ni kuweka mazingira mazuri ya kibiashara kwa kuweka miundombinu ya huduma bora za kibiashara na kutoa msaada kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.4 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 1.8 bilioni zilipangwa, hadi kufikia Machi 2024 jumla ya TZS 5.4 bilioni sawa na asilimia 299 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukamilisha uwekaji wa miundombinu ya umeme na maji; | Asilimia ya uwekaji wa miundombinu ya umeme iliyofikiwa. | 100 | 100 | 100 | Miundombinu ya umeme imekamilika katika kituo cha Biashara Nyamanzi |
| | Asilimia ya uwekaji wa miundombinu ya maji iliyofikiwa. | 100 | 100 | 100 | Miundombinu ya maji imekamilika katika kituo cha Biashara Nyamanzi |
| Kuweka sawa (Leveling) eneo la maonesho na kujenga ukuta; | Asilimia ya uwekaji sawa eneo (leveling) iliyofikiwa. | 100 | 100 | 100 | |
| | Asilimia ya ujenzi wa ukuta iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | |
| Ununuzi wa vifaa vya maonesho mashamiana na zana zake; | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Vifaa vyote vimenunuliwa na vimeanza kutumika |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa vibaraza vya kuwekea mashamiana, vyoo, maegesho ya vyombo vya moto pamoja na ufungaji wa vifaa vya ulinzi katika Uwanja wa Maonesho | Asilimia ya ujenzi wa vibaraza iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | |
| | Asilimia ya ujenzi wa vyoo iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | |
| | Asilimia ya ujenzi wa maegesho ya vyombo vya moto iliyofikiwa | 100 | 80 | 80 | |
| Ujenzi wa jengo la utawala. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 30 | 30 | Hatua ya msingi imekamilika. |

### 11.2.9 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Wizara inajukumu la kuweka misingi imara ya elimu inayoenda sambamba na mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia , kuboresha miundombinu ya elimu kwa lengo la kuwa na mazingira bora ya utoaji elimu. Kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi 2024 Wizara imetekeleza programu moja na miradi miwili ya maendeleo kama ifuatavyo:-

**i) Programu ya Uimarishaji Miundombinu ya Elimu**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuinua ubora wa elimu kwa kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunza. Kwa mwaka 2023/2024 Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 131.23 bilioni (TZS 59.04 bilioni kutoka Serikalini na TZS 72.19 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 98.42 bilioni zimepangwa (TZS 44.27 bilioni kutoka Serikalini na TZS 54.15 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 105.59 bilioni sawa na asilimia 107 ya fedha iliyopangwa imeingizwa (TZS 66.49 bilioni sawa na asilimia 150 kutoka Serikalini na TZS 39.10 bilioni sawa na asilimia 72 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa vituo vitano vya Mafunzo ya Amali, Chuo cha Ubaharia na jengo la mafunzo ya mafuta na gesi na kituo cha kuwaendeleza wajasiriamali | Asilimia ya Ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Maeneo ya ujenzi yameshatambuliwa na waathirika katika maeneo ya mradi wameshalipwa fidia,hatua iliyopo sasa ni kutafutwa Mshauri elekezi wa Mradi |
| Ujenzi wa nyumba 20 za walimu; | Asilimia ya Ujenzi iliyofikiwa | 100 | 50 | 50 | Jumla ya nyumba 10 kati ya 20 zilizopangwa zimejengwa katika maeneo ya visiwa vidogo vidogo Unguja na Pemba |
| Kujenga skuli 31 za ghorofa zikiwemo 12 za msingi na 19 za Sekondari; | Asilimia ya Ujenzi iliyofikiwa | 100 | 64 | 64 | Ujenzi unaendelea katika skuli 22,za msingi (8) na sekondari 13,skuli zenyewe ni,Kidichi ( 65%) Mwera (75%),Chumbuni(75%) Donge(90%) Mwambe(75%) Michakaini(30%) Kojani (65%) Fuoni (95%),Muungano(55%),Regeza mwendo(55%),Maungani(55%), Chukwani (55%),Tumbatu(35%),Mkokoton i(75%) Bumbwini Makoba(75%) Bumbwini misufini(55%),Kiwani(95%) Ole (65%), Makunduchi (55%), kifundi (55%), Gamba (55%) na Mfenesini (55%) |
| Ujenzi wa dakhalia katika Skuli za Paje Mtule na Chwaka Tumbe | Asilimia ya Ujenzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Ujenzi umekamilika kwa dakhalia zote na tayari kuanza kutumika |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Majengo sita (6) ya Ofisi katika Wilaya (Kaskazini A, Magharibi B, Kusini, Micheweni na Chake Chake) na kukamilisha Ofisi ya Wilaya ya Elimu ya Mkoani zenye | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Ofisi zote zimeshakamilika ujenzi wake na kufunguliwa katika sherehe za miaka 60 ya Mapinduzi. |
| maktaba, Ofisi za ukaguzi wa elimu na chumba cha TEHAMA Unguja na Pemba pamoja na kuzipatia vifaa; | | | | | |
| Ukarabati wa Skuli 23 za Maandalizi, Msingi na Sekondari zikiwemo Kidongochekundu, Chanjamjawiri, Muyuni Sekondari, Chumbuni Msingi, Faraja Sekondari, Kengeja-Dakhalia Sekondari, Kiuyu Minungwini, Chutama, Mikunguni, Fidel Castro Ukumbi, Dakhalia ya watoto wa Kiume Lumumba, Maungani, Uzini Msingi, Chaani Sekondari, Jang'ombe Maandalizi, Kizimbani Msingi, Mahonda, Ndagoni Msingi, Ole, Maziwa Ng'ombe na Mahonda; | Idadi ya skuli zilizofanyiwa ukarabati | 23 | 8 | 35 | Ukarabati unaendelea katika skuli mbalimbali na nyengine hazijaanza |
| Kujenga jengo la Ofisi la Wizara Unguja na Pemba; | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa | 100 | 40 | 40 | Kazi imeanza kufanyika kwa upande wa jengo la Pemba tayari limeshawekwa jamvi kwa ajili ya kuendelea na kujenga ghorofa ya kwanza na kwa upande wa Unguja hatua za kumpata mshauri elekezi zinaendelea |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa skuli ya ghorofa ya Mtambile iliyoanzishwa na wananchi. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 7 | 7 | |

## a) Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuhakikisha watoto wote waliofikia umri wa kuanza skuli kwa ngazi ya maandalizi na msingi wana mazingira mazuri ya kupata elimu bora. Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 6.12 bilioni (TZS 4.62 ni Ruzuku na TZS 1.50 ni mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023- Machi 2024) jumla ya TZS 4.6 bilioni zilipangwa na hadi kufikia Machi 2024, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuzipatia skuli vikalio zikiwemo skuli mbili za elimu mjumuisho Unguja na Pemba (makabati 40 (4 in 1), vitanda 160 na magodoro 160); | Asilimia ya vifaa vilivyonunuliwa | 100 | 10 | 10 | Hatua za manunuzi zinaendelea kwa kumtafuta mzabuni ambaye atanunua vifaa hivyo |
| Kuimarisha elimu ya msingi katika kusoma, kuandika na kuhesabu kwa darasa la kwanza hadi la nne; | Asilimia ya uimarishwaji iliyofikiwa | 100 | 25 | 25 | Wizara inaendelea katika hatua ya kupanga mikakati ya namna ya kuinua viwango vya wanafunzi katika KKK. |
| Kuimarisha vituo vya Habari na Mawasiliano ya Elimu; | Asilimia ya uimarishwaji iliyofikiwa. | 100 | 100 | 100 | Katika kuimarisha vituo vya Habari, Vifaa vimenunuliwa ambavyo ni Kamera 1, Komputa ya mezani 2, Komputa mpakato 2, Kamera ya kurikodi 1 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuzipatia skuli vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya Mitaala Mipya; na | Asilimia ya vifaa vilivyonunuliwa | 100 | 40 | 40 | Vifaa vinaendelea kununuliwa na kusambazwa katika skuli mbali mbali nchini, vifaa hivyo ni vitabu vya Maandalizi 1,Darasa la kwanza 1,Darasa la 4 na Darasa la 7, kwa upande wa mkoa wa Kusini na Kaskazini Unguja vifaa vyote vimekamilika, zoezi linaendelea kwa mikoa iliyobakia. |
| Kutoa mafunzo kwa walimu wa maandalizi na msingi kupitia mtaala mpya. | Idadi ya walimu waliopatiwa mafunzo | 4,722 | 6,657 | 141 | Mafunzo yametolewa zaidi kutokana na kuongezeka walimu wa skuli za binafsi ambao awali hawakujumuishwa katika mpango huo. |

### b) Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuongeza Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya juu kwa kuwapatia mikopo na kuimarisha miundombinu ya Vyuo Vikuu. Kwa mwaka 2023/2024 mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 21.60 bilioni (TZS 20.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 1.60 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 – Machi 2024) jumla ya TZS 16.2 bilioni zilipangwa (TZS 15.0 bilioni kutota Serikalini na TZS 1.2 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 23.6 bilioni sawa na asilimia 146 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa (TZS 13.1 bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 87 na TZS 10.5 bilioni sawa na asilimia 875 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuwapatia mikopo wanafunzi wanaojiunga na masomo katika vyuo vya elimu ya juu | Idadi ya wanafunzi waliopatiwa mikopo | 6,060 | 6,060 | 100 | Wanafunzi wote waliomba mikopo wameingiziwa fedha kwa muhula wa kwanza |

### 11.2.10 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Wizara ina jukumu la kuhakikisha habari zinatolewa na kupokelewa kwa usahihi na kwa wakati, kuwawezesha vijana na kuwatafutia fursa mbali mbali za ajira, kudumisha utamaduni na kuimarisha michezo kwa lengo la kuimarisha afya za wananchi na kuongeza ajira. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imetekeleza programu moja ya maendeleo kama ifuatavyo:-

#### i) Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo

Lengo la programu hii ni kuiwezesha sekta ya michezo kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo Zanzibar itakayokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa. Programu hii imeanza mwaka 2021/22 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26. Kwa mwaka 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 34.28 bilioni kutoka Serikalini na Washirika wa Maendeleo (TZS 33.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 1.28 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 25.7 bilioni zilipangwa (TZS 24.8 bilioni kutoka Serikalini na TZS 958.5 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 37.8 bilioni sawa na asilimia 123 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ukarabati wa uwanja wa Amani na Mao Ze Dong; | Asilimia ya ukarabati wa uwanja wa Amani iliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | Ukarabati wa uwanja wa Amani pamoja na viwanja vya nje vya Michezo umekamilika. Kazi zinazoendelea ni ukamilishaji wa milango ya maduka, hoteli na mikahawa ili kukabidhiwa kwa Serikali kwa ajili ya matumizi rasmi. Aidha, uwanja wa Gombani pia umekarabatiwa na umekamilika na utakabidhiwa kwa wizara mara baada ya kukamilisha kasoro zilizoonekana. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa viwanja vya michezo vya Wilaya vinne (6 in 1). | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 5 | 5 | Upimaji wa Viwanja pamoja na kuandaa michoro na BOQ umekamilika na Wizara imeshafunga mkataba na kampuni ya GIZ kutoka Ujerumani |
| Ujenzi wa Viwanja vya Wilaya Unguja na Pemba | Idadi ya viwanja vilivyojengwa | 16 | 0 | 0 | Hatua za upimaji wa maeneo ya ujenzi wa viwanja, uchoraji wa ramani na BOQ zimekamilika na hatua inayoendelea ni kufanya maandalizi ya mkataba baina ya Wizara na Kampuni ya reform Sports ya nchini Uturuki |

### 11.2.11 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo

Wizara ina jukumu la kusaidia upatikanaji wa mbegu na utoaji wa mafunzo kwa wakulima na wafugaji. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imepanga kutekeleza programu tatu na miradi mitatu ya maendeleo kama ifuatavyo:-

**i) Programu ya Umwagiliaji (Awamu ya II)**

Lengo la programu hii ni kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga, kuwawezesha wakulima kwa kuwajengea uwezo wa uzalishaji kwa kutumia pembejeo za kilimo. Programu hii itagharimu jumla ya kiasi cha TZS 40.0 bilioni hadi kukamilika kwake na kwa mwaka 2023/2024, programu imepangiwa jumla ya TZS 31.70 bilioni (TZS 500 milioni kutoka Serikalini na TZS 31.20 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 23.8 bilioni (TZS 37 milioni kutoka Serikalini na TZS 24 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zilipangwa kutekeleza programu hii. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 17.8 bilioni sawa na asilimia 75 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa kutokakwa Washirika wa Maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya malipo ya fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji | Idadi ya wakulima waliolipwa fidia | 20 | 0 | 0 | Wizara kwa kushirikiana na Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali inamalizia ripoti 2 za Tathmini ya mali za wananchi zilizoathirika na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika bonde la Kilombero kwa Unguja na Mlemele kwa Pemba kwa ajili ya kuwasilisha kwa Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa malipo. |
| Ujengaji wa misingi ya ndani (tertial canals) kwa kiwango cha saruji yenye urefu wa kilomita 47.74 katika bonde la Cheju A, Kinyasini, Kilombero, Kibokwa, Chaani na Mlemele; | Idadi ya kilomita zilizojengwa | 43 | 30 | 70 | Kazi ya ujenzi imekamilika kwa bonde la Kibokwa, Chaani na Mlemele na kazi inaendelea katika bonde la Cheju A, Kinyasini na Kilombero. |
| Uungaji wa umeme mkubwa kwenye visima vya umwagiliaji maji kwenye bonde la Cheju B; | Idadi ya visima vilivyoungwa umeme | 4 | 0 | 0 | Uungaji wa umeme ni kazi ya mwisho baada ya kumalizika kazi zote za visima. Hata hivyo tayari ZECO washakabidhi ripoti ya Tathmini ya Uungaji umeme kwa ajili ya kuombea fedha kwa Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa Malipo. |
| Kujenga na kusimamia miundombinu ya umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 301 katika bonde la Cheju B; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Kazi za ujenzi wa miundombinu katika bonde la Cheju B zinaendelea katika hatua za mwisho. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kusimamia maeneo yaliyokwisha kujengwa miundombinu mipya ya umwagiliaji maji yenye ukubwa wa hekta 1,053 ikiwemo kuwapa mafunzo ya taaluma juu ya kilimo cha umwagiliaji maji kwa kamati na wakulima viongozi; | Idadi ya Wakulima waliopata mafunzo | 300 | 250 | 83.33 | Kazi ya utoaji wa mafunzo kwa kamati na wakulima na viongozi katika mabonde 5 ya mradi imeshafanyika, maandalizi ya mafunzo kwa bonde la Chaani yapo katika hatua ya mwisho kufanyika. |
| Ukamilishaji na utatuaji wa changamoto ya uvujaji maji katika Bwawa la Chaani; | Asilimia ya kazi iliofanyika | 100 | 100 | 100 | Kazi ya utatuaji wa uvujaji maji wa Bwawa la Chaani umeshakamilika. |
| Ukamilishaji wa uungaji wa bomba za maji kwenye visima katika bonde la Kilombero | Idadi ya visima vilivyoungwa mabomba | 5 | 5 | 100 | Kazi ya uungaji wa bomba umeshakamilika katika bonde la Kilombero na tayari visima hivyo vinatumika. |
| Kujenga misingi ya kutolea maji ya ziada katika bonde la Cheju B | Idadi ya kilomita za msingi iliyojengwa | 35 | 28 | 80 | Kazi zinaendelea za uchimbaji wa misingi ya kutoa maji (drainage canals) katika bonde la Cheju B. |
| Kujenga na uchimbaji wa Visima vinne katika bonde la Cheju B | Idadi ya Visima vilivyochimbwa | 4 | 2 | 50 | Kazi ya uchimbaji visima inaendelea katika bonde la Cheju B |
| Kujenga uzio (fence) kwenye bwawa la Kinyasini (400m) na Chaani (1000) | Idadi ya mita zilizojengwa uzio | 1400 | 1400 | 100 | Kazi za ujenzi wa uzio katika bwawa la Kinyasini na Chaani zimekamilika |

### ii) Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Mifugo

Programu ina lengo la kuimarisha na kuinua sekta ya kilimo na mifugo kwa wakulima na wafugaji wadogo wadogo nchini. Programu hii inajumuisha miradi miwili inayogharimu jumla ya TZS 4.3 bilioni ambapo (TZS 2.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 2.3 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

#### a) Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo

Mradi huu una lengo la kuimarisha miundombinu ya mifugo ili kuongeza kasi ya uzalishaji na usalama wa mifugo inapoingia nchini pamoja na mazingira bora ya uchinjaji wa mifugo. Mradi umeanza mwaka 2021/22 hadi 2023/2024 unagharimu jumla ya TZS 11.2 bilioni hadi kukamilika kwake. Kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa jumla ya TZS 2.0 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 1.5 bilioni zilipangwa na hadi kufikia Machi 2024 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa mtambo wa kuzalisha gesi ya naitrojeni (liquid nitrogen) kwa ajili ya kuhifadhia mbegu za kupandisha ng'ombe kwa sindano; | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Hatua za manunuzi zinaendelea kwa ununuzi wa mtambo mpya wa kuzalisha gesi. Aidha, mtambo mkongwe umefanyiwa matengenezo na kwa sasa unazalisha kwa asilimia 85. |
| Ujenzi wa miundombinu ya karantini ya mifugo katika eneo la Gando Nziwengi; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 0 | 0 | Barua ya kuomba uandaaji wa michoro na BOQ tayari imeshapelekwa kwa Wakala wa Ujenzi (ZBA) kwaajili ya ujenzi wa miundombinu ya karantini. |

### b) Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC)

Mradi huu unatekelezwa kisiwani Pemba, kwa lengo la kuimarisha mchango wa sekta ya ufugaji nyuki katika ukuaji wa uchumi shirikishi nchini Tanzania pamoja na kuzalisha asali bora kwa njia endelevu ya mazingira ya kuingia katika masoko. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2023/2024 umepangiwa jumla ya TZS 514 milioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 385 milioni na hadi kufikia Machi 2024 shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoa mafunzo kwa wafugaji nyuki juu ya mbinu mpya za ufugaji nyuki na uzalishaji bora, kutambua aina za nyuki pamoja na mazao mengine ambayo yanapatikana kutokana na nyuki nchini Tanzania; | Idadi ya vikundi vilivyopatiwa mafunzo | 100 | 96 | 96 | Jumla ya wafugaji nyuki 724 kutoka vikundi 96 wamejengewa uwezo wa Ufugaji Bora wa Nyuki. Mada walizofundishwa ni Ufugaji Nyuki wa Kibiashara, Mazao ya Nyuki, Aina za Nyuki, Uanzishwaji na Huduma za Manzuki, Kalenda ya Ufugaji Nyuki na Udhibiti wa Wadudu Waharibifu katika Mizinga ya Nyuki. Mafunzo haya ni ya muendelezo kwa wafugaji nyuki katika maeneo yao. |
| Kununua pikipiki za Maafisa Misitu wa Wilaya | Idadi ya Pikipiki zilizonunuliwa | 5 | 5 | 100 | Pikipiki 5 aina ya Honda zilinunuliwa na kukabidhiwa kwa WKUMM. Pikipiki 4 kwa ajili ya Maafisa wa Misitu wa Wilaya za Micheweni, Wete, Chake Chake na Mkoani na 1 kwa Mkuu wa Idara ya Misitu Pemba. |
| Kukusanya sampuli za asali kulingana na uoto wa Pemba | Idadi ya sampuli zilizokusanywa | 12 | 12 | 100 | |
| Kutoa mafunzo ya uchongaji wa mizinga kwa Mafundi Seremala. | Idadi ya mafundi Seremala waliopatiwa mafunzo. | 20 | 20 | 100 | Fundi Seremala 20 (10 Kaskazini Pemba and 10 Kusini Pemba) wamepata mafunzo ya uchongaji wa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | mizinga bora ya ufugaji nyuki kutoka kwa wakufunzi wa Chuo cha Nyuki Tabora. |
| Kushiriki Maonesho ya Siku ya Chakula katika viwanja vya maonesho Chamanangwe Pemba | Idadi ya watu walioshiriki katika maonesho ya Siku ya Chakula | 285 | 285 | 100 | Jumla ya wafugaji nyuki 285 (wanaume 194 na wanawake 91) walitembelea banda la maonesho la BEVAC na kupata mafunzo ya ufugaji bora wa nyuki. |
| Kuanzisha manzuki (apiary) kama shamba darasa kwa ufugaji nyuki | Idadi ya manzuki yaliyoanzishwa kama mashamba darasa ya ufugaji nyuki. | 5 | 3 | 60 | Manzuki (apiaries) 3 zimeanzishwa kama ni mashamba darasa kwa kutoa elimu kwa wafugaji nyuki. Manzuki hizo zipo Taifu (Wete), Chamanangwe (Wete) na Stahabu (Mkoani) |
| Kutoa mafunzo ya Uvunaji wa Asali kwa Wafugaji Nyuki. | Idadi ya Vikundi vya wafugaji nyuki vilivyopata mafunzo. | 50 | 48 | 96 | Kwa kushirikiana na PEBA, mafunzo ya uvunaji wa asali yamefanyika kwa wawakilishi wa vikundi 23 kwa Mkoa wa Kusini Pemba na 25 kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba. |

### iii) Programu ya Kudhibiti Maradhi na Upotevu wa Mazao

Programu hii ina lengo la kupunguza upotevu wa mazao ya kilimo ili kuongeza upatikanaji wa chakula kwa wakulima na wananchi nchini. Kwa mwaka 2023/2024, programu imepangiwa jumla ya TZS 32.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Programu hii itajumuisha miradi 5.

#### a) Mradi wa Kupambana na Sumu Kuvu Tanzania (TANIPAC)

Mradi huu una lengo la kupuguza athari zinazotokana na sumukuvu katika mahindi na njugu nyasa kwa kutoa taaluma na kuimarisha miundombinu na teknolojia kabla na baada ya mavuno. Mradi unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Mradi huu ni wa miaka mitano kuanzia mwaka 2019/2020 hadi 2023/2024. Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 485 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 364 milioni zilipangwa. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 1.9 bilioni sawa na asilimia 532 ya fedha iliyopangwa izmeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoa mafunzo ya udhibiti wa sumukuvu kwa wadau wa mnyororo wa thamani kwa wakulima wa mazao ya mahindi na njugu nyasa; | Idadi ya watu waliopatiwa mafunzo | 175 | 175 | 100 | Mafunzo yalifanyika kwa wadau wa Mikoa yote ya Zanzibar. Mkoa wa Mjini Magharibi 35, Mkoa wa Kaskazini Unguja 35, Mkoa wa Kusini Unguja 35, Mkoa wa Kaskazini Pemba 35 na Mkoa wa Kusini Pemba 35 |
| Kutoa mafunzo ya utengenezaji wa vizimba vya chuma kwa vijana 40 Unguja na Pemba na utoaji wa teknolojia ya darasa za kukaushia. | Idadi ya watu waliopatiwa mafunzo | 100 | 100 | 100 | |
| Kuendelea na ujenzi wa maghala ya kuhifadhia nafaka. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 90 | 90 | Jumla ya maghala 2 yamejengwa, 1 limejengwa Kizimbani Unguja na 1 limejengwa Ole Dodeani Pemba. Ujenzi unaendelea katika hatua za ukamilishaji |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kushiriki maonesho ya Kitaifa mfano Siku ya Chakula Duniani, Nanenane na Maonesho ya Biashara. | Idadi ya maonesho yaliyofanyika | 3 | 3 | 100 | Maonesho yaliyofanyika ni Nanenane ambayo yaliyofanyika Kizimbani Unguja, Siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika Chamanangwe Pemba na Maonesho ya Biashara yaliyofanyika Nyamanzi Unguja |
| Kufanya mikutano ya uelimishaji kwa viongozi | Idadi ya mikutano iliyofanyika | 2 | 2 | 100 | Mikutano hii ilifanywa kwa ajili ya kuwasilisha ripoti ya tathmini ya hali ya Sumukuvu Zanzibar. |
| Kutoa mafunzo ya uwelewa wa kanuni za kudhibiti sumukuvu | Idadi ya washiriki waliopatiwa mafunzo | 100 | 100 | 100 | Mafunzo yalifanyika kwa Wafanya biashara 30 Unguja na 20 Pemba na wakaguzi 30 Unguja na 20 Pemba |
| Kutoa mafunzo kwa watendaji wa mradi | Idadi ya watendaji waliopatiwa mafunzo | 3 | 3 | 100 | Watendaji watatu wa Mradi wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi kwa muda wa wiki 2 kila mmoja |
| Kuendelea na udhamini wa wanafunzi wa shahada ya uzamili na uzamivu | Idadi ya wanafunzi waliodhaminiwa | 3 | 3 | 100 | |
| Usimamizi na uendeshaji wa mradi | Kuandaa ripoti za utekelezaji | 2 | 2 | 100 | |

### 11.2.12 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za jamii, wazee na watoto ili kuwa na hali bora za kimaisha. Aidha, Sekta hii imeundwa kwa lengo la kushughulikia maendeleo ya kijamii na kuleta usawa wa kijinsia. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imetekeleza jumla ya miradi minne ya maendeleo kama ifuatavyo:-

#### a) Mradi wa Hifadhi ya Wazee

Mradi una lengo la kuimarisha hali za wazee kwa kuimarisha makaazi yao, usalama na upatikanaji wa huduma za msingi kikamilifu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.1 bilioni (TZS 1.5 bilioni kutoka Serikalini na TZS 636 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 – Machi 2024) jumla ya TZS 1.1 bilioni zilipangwa. Hadi kufikia Machi 2024, shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya ukarabati katika makaazi ya wazee yaliopo Limbani - Pemba na Sebleni - Unguja; | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa katika makaazi ya wazee Limbani-Pemba | 100 | 5 | 5 | Zabuni zimeshawasilishwa kwa Washauri Elekezi kwa ajili ya kumpata Mkadarasi wa ukarabati wa makaazi ya wazee Pemba. |
| | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa katika makaazi ya wazee Sebleni- Unguja. | 100 | 5 | 5 | Wizara imewasilisha ramani ya eneo (site plan) kwa Mfadhili kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kwa ajili ya kufadhili ujenzi wa kisasa wa makaazi ya Wazee Sebleni. |
| Ununuzi wa vifaa na samani. | Asilimia ya manunuzi iliyofanyika. | 100 | 10 | 10 | Zabuni imeshapitishwa na mkataba umeshatayarishwa unasubiri kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu. Vifaa vinavyotarajiwa kununuliwa ni vitanda, magodoro, meza na vyombo vya ndani. |

### b) Mradi wa Hifadhi ya Mtoto

Mradi una lengo la kuimarisha Hifadhi ya Mtoto na Mifumo ya Maendeleo kwa Mtoto. Mradi huu ulianza mwaka 2000 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2028. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, mradi umepangiwa jumla ya TZS 150.0 milioni Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 113.0 milioni zilipangwa na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 50.4 sawa na asilimia 45 ya fedha iliyopangwa imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa warsha ya siku moja ya wataalam wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wanawake na Watoto na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya kuandaa mpango kazi wa Skuli Salama Zanzibar (Safe school Program ) | Idadi ya washiriki wa warsha. | 22 | 22 | 100 | |
| Kujenga uwezo kwa kuandaa warsha ya siku mbili kwa WMJJWW, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora na Ofisi ya Mufti kwa ajili ya kujenga uwezo wa kuandaa mipango kazi na uandaaji wa ripoti za utekelezaji kwa kuzingatia Mfumo elekezi wa UNICEF. | Idadi ya wafanyakazi waliojengewa uwezo. | 29 | 29 | 100 | |
| Kuandaa warsha ya siku 5 ya Wawezeshaji wa Mafunzo (TOT) ya Malezi ya watoto kwa watendaji wanaosimamia masuala ya Watoto. | Idadi ya wawezeshaji waliojengewa uwezo | 25 | 25 | 100 | |

### c) Mradi wa Hifadhi ya Mtoto na Ufuatiliaji wa Kesi za Watoto.

Mradi una lengo la kuimarisha Hifadhi ya Mtoto na Ufuatiliaji wa Kesi za Watoto. Mradi huu ulianza mwaka 2000 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2028. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, mradi umepangiwa jumla ya TZS 200 milioni kutoka kwa Washirika wa maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 – Machi 2024) jumla ya TZS 150.0 milioni zilipangwa. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 14.5 sawa na asilimia 10 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoa huduma za Hifadhi ya Mtoto katika kufanya ufuatiliaji wa kesi katika ngazi ya shehia | Asilimia ya huduma iliyotolewa | 100 | 42 | 42 | |
| | Idadi ya kesi zilizofuatiliwa | 60 | 25 | 42 | |
| Kuwarejesha watoto makwao wanaohifadhiwa Nyumba Salama | Idadi ya Watoto waliorejeshwa makwao | 50 | 7 | 14 | |
| Kutoa mafunzo ya msaada wa kisaikolojia kwa wahudumu na walezi wa vituo vya kulelea watoto. | Idadi ya Wahudumu waliopatiwa mafunzo. | 60 | 20 | 33 | |
| | Idadi ya Walezi waliopatiwa mafunzo. | 27 | 27 | 100 | |
| Kutayarisha Ripoti ya mwaka ya Zanzibar kuhusu Hifadhi ya Mtoto | Asilimia ya matayarisho iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Ripoti 1 ya hifadhi ya mtoto Zanzibar imeandaliwa |
| Kufanya Mkutano wa siku tatu wa mashauriano ya wadau kuhusu Usafirishaji Haramu wa Watoto | Idadi ya mikutano iliyofanyika | 2 | 1 | 50 | |

### d) Mradi wa Kujikinga na Kupambana na Vitendo vya Udhalilishaji.

Mradi una lengo la kupingana na Vitendo vya Udhalilishaji. Mradi huu ulianza mwaka 2002 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2028. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, mradi umepangiwa jumla ya TZS 279.3 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 209.5 milioni zilipangwa. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 160.8 sawa na asilimia 77 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kupata maoni juu ya uandaaji wa Mpango kazi mpya wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa kijinsia 2023-2028 | Idadi ya Mikutano iliyofanyika | 4 | 1 | 25 | |
| Kufanya mkutano wa Robo mwaka wa kupambana na vitendo vya Ukatili na udhalilishaji ujulikanao kama Chaguo langu haki yangu | Idadi ya Mikutano iliyofanyika | 4 | 1 | 25 | |
| Kufanya Mkutano unaohusisha watu wenye ulemavu kwaajili ya kuipitia taarifa ya awali ya uandaaji wa Mpango kazi wa Kitaifa wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinisia 2023-2028. | Idadi ya Mikutano iliyofanyika | 1 | 1 | 100 | |
| Kufanya Ufuatiliaji wa kazi za Mradi katika Wilaya za Unguja na Pemba. | Idadi ya Wilaya zilizofikiwa. | 11 | 2 | 18 | Wilaya zilizofikiwa ni Wilaya ya Mjini Unguja na Mkoani Pemba |
| Kufanya Tathmini ya ufanyaji kazi wa huduma ya kituo cha mkono kwa mkono Zanzibar. | Asilimia ya Tathmini iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Hatua za kumpata Mshauri Elekezi wa kufanya tathmini zimeshaanza na tangazo la Zabuni limeshatoka. |

### 11.2.13 Wizara ya Maji, Nishati na Madini

Wizara ya Maji, Nishati na Madini inajukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zote zilizo chini ya sekta hiyo ili kuweza kuhakikisha wakaazi wa Zanzibar wanafaidika na huduma za maji safi na salama, Kwa kipini cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imetekeleza jumla ya programu mbili na miradi mitano ya maendeleo kama ifuatavyo-:

#### i) Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar

Programu hii ina lengo la kusimamia na kuhakikisha huduma za usambazaji maji safi na salama zinapatikana katika maeneo yote ya mijini na vijijini ili kuwawezesha wananchi wote kunufaika na huduma hiyo muhimu katika jamii. Kwa mwaka 2023/2024, program hii imepangiwa jumla ya TZS 77.51 bilioni (TZS 24.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 53.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa kutekeleza shughuli zake kupitia miradi mitatu ya maendeleo kama ifuatavyo:-

#### a) Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA)

Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA) unalenga kuimarisha miundombinu ya usambazaji maji safi na salama katika maeneo ya Wilaya ya Magharibi A, (Mfenesini, Masingini na Kizimbani) Magharibi B (Dimani na Kidutani) na Wilaya ya Kati (Jumbi- Mkorogo) pamoja na ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Mamlaka ya Maji Zanzibar. Lengo la mradi huu ni kuhakikisha kuwa tatizo la maji katika maeneo yaliyokusudiwa linaondoka kabisa na wananchi wanaweza kupata maji safi na salama muda wote. Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya India. Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 29.66 bilioni (TZS 11.16 bilioni kutoka Serikalini na TZS 18.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 22.2 bilioni zilipangwa (TZS 8.3 bilioni kutoka Serikalini na TZS 13.8 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 29.0 bilioni zimeingizwa sawa na asilimia 131 ya fedha zilizopangwa (TZS 6.7 bilioni sawa na asilimia 80 kutoka Serikalini na TZS 22.4 bilioni sawa na asilimia 161 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyo pangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuchimba visima | Idadi ya visima vilivyo chimbwa | 64 | 64 | 100 | Mradi umefanikiwa kuchimba visima vyote 64 katika lot 3 za mradi. |
| Ujenzi wa matangi | Idadi ya matangi yaliyo jengwa | 15 | 15 | 98 | Mradi umefanikiwa kujenga matangi yote 15 ambayo yapo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji. Kazi za ujenzi zinazoendelea ni kuunga umeme na mfumo wa tehama kwa baadhi ya matangi na Kuweka 'land scaping' |
| Ulazaji wa bomba | Idadi ya kilomita za bomba zilizolazwa | 466.9 km | 453.7 km | 97 | Kazi zinazoendelea ni kufanya majaribio ya mabomba kwa maeneo ya Mfenisini na Mkorogo |
| Ujenzi wa Ofisi | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 100 | 100 | |
| Ulipaji wa fidia za vipando na majengo katika maeneo ya Mkorogo, Dimani, Maungani, Mfenesini, Dole, Kidutani na Masingini; | Idadi ya Wananchi waliolipwa fidia | 1,282 | 99 | 7.7 | |

### b) Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi (JICA)

Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi una lengo la kuongeza uzalishaji wa maji katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi ili kutosheleza mahitaji kwa wananchi. Mradi huu umeanza mwaka 2023/2024 na kwa mwaka 2023/2024, jumla ya TZS 9.96 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zimepangwa kutumika. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 7.5 bilioni zilipangwa, hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 3.5 bilioni zimeingizwa sawa na asilimia 51 ya fedha zilizopangwa kati ya fedha hizo TZS 306 milioni kutoka Serikalini na TZS 3.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 47 na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya mapitio ya taarifa zilizopo na makadirio ya mahitaji ya maji; | Asilimia ya kazi ya mapitio ya taarifa makadirio ya mahitaji ya maji iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Utafiti unaonesha Lita 89.5 Milioni kwa siku zinahitajika kwa maeneo |
| Kufanya utafiti wa maeneo ya uchimbaji wa Visima, Ujenzi wa Matangi na ulazaji wa mabomba | Asilimia ya utafiti iliyofikiwa | 100 | 30 | 30 | Kazi ya utafiti (Topographic Survey, Geophysical Survey and Geotechnical Survey) kwa maeneo ya uchimbaji ya visima, matangi na ulazaji wa mabomba inaendelea |

### c) Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar

Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar una lengo la kuendeleza na kuimarisha huduma ya maji safi na salama Zanzibar kwa maeneo ya Kizimbani No. 2, Jendele- Chwaka, Banda Maji, Donge, Miwani, Ndijani -Muembe Punda, Ubago - Nyakurungwi, Dunga jumba la mawe, Mwera- Pongwe, Chaani -Kikobweni, Mkataleni – Msufini, Mchangani-Mkiwa, Pangeni, Machui kwa Bavuai, Upenja, Kitope- Skuli na Mkokotoni. Kwa mwaka 2023/2024, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 10.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 7.9 bilioni zilipangwa na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 3.4 bilioni zimeingizwa sawa na asilimia 44 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| **Shughuli Iliyopangwa** | **Kiashiria** | **Shabaha** | **Utekelezaji Halisi** | **Asilimia ya Utekelezaji** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|---|
| Uchimbaji msingi na ulazaji bomba; | Idadi ya Kilomita za ulazaji mabomba zilizolazwa | 50 | 13 | 26 | Kazi haijakamilika kutokana na baadhi ya mabomba kutumika kwenye maeneo ya ujenzi wa barabara |
| Ununuzi wa mabomba na viungio (Pipe Fittings); | Asilimia ya manunuzi yaliofanyika | 100 | 40 | 40 | Zabuni kwa ajili ya viungio (Pipe Fittings) imekamilika na tayari mzabuni keshapatikana Yumuza na Peritus. Aidha, ununuzi wa mabomba upo katika hatua ya kusaini mkataba na Mzabuni |
| Ujenzi wa vibanda, uzio na uwekaji umeme; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 70 | 70 | Kazi inayoendelea kwa ukamilishaji vibanda 13 ni kuweka miundombinu ya umeme, maji, tarazo, dari na rangi na kwa upande wa ujenzi wa uzio kazi haijaanza. |
| | Asilimia ya miundombinu ya umeme iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Bajeti ya kazi ya kuweka umeme mkubwa katika visima imeshawasilishwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya malipo |
| Ununuzi wa mita za maji (Smart meter) | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa | 100 | 30 | 30 | Malipo ya awali kwa ajili ya kufanya manunuzi ya mita 6,000 yameshakamilika. |

### ii) Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar

Programu hii ina lengo la kuimarisha huduma za usambazaji wa umeme katika maeneo ya mijini na vijijini ili kuwawezesha wananchi kupata huduma hiyo kwa uhakika zaidi. Kwa mwaka 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 33.14 bilioni (TZS 24.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 8.94 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na kutekeleza shughuli zake kupitia miradi miwili ya maendeleo kama ifuatavyo:-

#### a) Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Umeme

Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Umeme umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha huduma za umeme katika vijiji 305 (180 Unguja na 125 Pemba) ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma salama na ya uhakika. Mradi huu ni wa miaka minne (2021-2025) na unatarajiwa kugharimu jumla ya TZS 162.75 bilioni. Kwa mwaka 2023/2024, Serikali imepanga kutumia jumla ya TZS 17.0 bilioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023 hadi Machi 2024) jumla ya TZS 12.8 bilioni zilipangwa na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 11.7 bilioni sawa na asilimia 91 zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Usambazaji wa umeme katika vijiji vya Unguja na Pemba; | Idadi ya vijiji vilivyosambazi wa umeme Unguja | 27 | 28 | 103 | Vijiji vilivyozambaziwa umeme ni Upenja Chokwe, Matemwe Muyuni, Kilombero Maskan, Kazole M/Hemari, Mkwajuni Kiongele, Makunduchi Ukweta, Bungi Miembe mingi, Mchangani Michongomani, Kilombero juu, Matemwe Dodoma, Matemwe Kijini, Kitope Mbaleni, Upenja Choke, Kilombero Maendeleo, Kazole Mgombewa, Pete Kichangani, Pete Kiungani, Bwejuu Wananchi Kwenye Kisima cha Maji, Marumbi Wananchi Kwenye Kisima cha Maji, Uroa Nyanje Wananchi na Wakulima, Kandwi Kinduni, Upenja Uwandani, Muyuni C, Mungoni, Marumbi na Kandwi |
| | Idadi ya vijiji vilivyosambazi wa umeme Pemba | 18 | 17 | 94 | Vijiji vilivyosambaziwa umeme ni Mapape B, Tumbe Muembe Jivuli, Kipangani, Migombani, Utaani, Mtekofi, Mtemani, Kwa Delo Wambaa, Bahani Wambaa, Mpakani Kichunjuu, Jipinde Konde, Misufini Makangale, Mapungwi Kengeja, Mchanga mdogo |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya nguzo zilizonunuliwa | 39,658 | 39,658 | 100 | |
| Ununuzi wa nguzo na vifaa vya umeme; | Asilimia ya vifaa vilivyonunuliwa | 100 | 35.56 | 35.56 | Nguzo, Mopemounten cutout, Bimetalic lug, waya, Transfoma, Lightning arrestor,Drop out fuse, Cross arm, |
| Uvutaji wa njia mpya za umeme | Idadi ya njia mpya za umeme zilizowekwa | 116 | 82.57 | 71 | |

### b) Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA)

Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA) unatarajiwa kutekelezwa kwa miaka sita (2022-2027) na unakadiriwa kutumia jumla ya TZS 372.48 bilioni kwa lengo la kuimarisha utekelezaji katika sekta ya nishati kwa kuimarisha miundombinu ya umeme na kuzijengea uwezo taasisi zinazoshughulikia masuala ya nishati. Mradi unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 16.08 bilioni (TZS 7.20 bilioni kutoka Serikalini na TZS 8.88 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 12.0 bilioni zimepangwa. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 1.21 milioni  zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ulipaji wa fidia katika maeneo yatakayoathirika na mradi. | Idadi ya wananchi waliolipwa fidia | 1520 | 0 | 0 | Malipo ya Fidia kwa waathirika wa mradi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa takriban kilomita 100 taratibu za malipo zinaendelea baada ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kujiridhisha. |
| Ujenzi wa laini kubwa ya umeme wenye uwezo wa kilovoti 132 pamoja na kufanya malipo kwa Mshauri Elekezi; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 30 | 30 | Mshauri Elekezi amesaini mkataba mwezi Mei 2023, Zabuni ya ujenzi wa miundombinu ilitangazwa mwezi Septemba 2023. Kazi ya uthamini ilikamilika na ripoti iliwasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kibali (No Objection) na wakandarasi wawili wanategemewa kupatikana katika zabuni hiyo, mmoja kwa ajili ya njia ya umeme na mwengine kwa ajili ya vituo vya usambazaji umeme. |
| Kufanya tafiti za popo na ndege katika njia kuu ya umeme (132KV) | Idadi ya tafiti zilizofanyika | 2 | 2 | 100 | Hadi kufikia Machi 2024, Tafiti hizi zimekamilika na ripoti ya mwisho (Final Report) imewasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kibali (No Objection). |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Uwekeaji wa mfumo wa kidigitali wa usimamizi na undelezaji wa miundombinu ya umeme (SCADA); | Asilimia ya uwekaji wa mfumo wa kidigitali iliyofikiwa | 100 | 30 | 30 | Kazi hii inaendelea na Msahuri Elekezi amesaini mkataba mwezi Mei 2023. Hadi kufikia Machi 2024 amekamilisha ripoti ya usanifu (Design report) na imeshapata no objection ya Benki ya Dunia na rasimu ya zabuni (Draft Bidding Documents) kwa ajili ya kupitiwa na ZECO na Benki ya Dunia ili kutoa kibali (No Objection) kabla ya kutangaza zabuni hiyo imekamilika na zabuni ya ujenzi inategemewa kutangazwa mwishoni mwa mwezi Mei 2024. |
| Kuanza ujenzi wa miundombinu ya umeme wa jua. (Solar PV Plant) na kihifadhio (Battery Energy Storge System - BESS). | Asilimia ya Ujenzi iliyofikiwa | 100 | 30 | 30 | Mshauri Elekezi amesaini mkataba Julai 2023, Rasimu ya upembuzi yakinifu (Draft Feasibility Studies of Solar PV and BESS) imekamilika, zabuni kwa ajili ya kzi za awali (Preparatory Works) kwa ajili ya kituo cha umeme wa jua Makunduchi imekamilika. Zabuni ya upimaji wa kijiofisikia na Topografiki (Geotechnical and Topographical surveys), Uwekaji wa uzio wenye urefu wa kilomita 3.2 katika eneo la kituo cha kufua umeme wa jua cha Makunduchi na ujenzi wa barabara ndani ya eneo la mradi (Access Roads) itatangazwa baada kurejeshewa kutoka Benki ya Dunia. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Uboreshaji wa njia za usambazaji umeme katika Mji Mkongwe (Stone town), uendelezaji wa njia mpya (extension) za misongo ya kilovoti 33 na 11 katika visiwa vya Unguja na Pemba | Asilimia ya uboreshwaji wa umeme Mji Mkongwe uliofikiwa | 100 | 20 | 20 | Msahuri Elekezi alisaini mkataba mwezi Novemba 2023 na amewasilisha ripoti ya awali ya upembuzi yakinifu (Draft Feasibility Study). Ripoti hii inapitiwa na ZECO kabla ya kuwasilishwa Benki ya Dunia kwa jili ya kupitiwa na kupata kibali (No Objection), rasimu ya zabuni (Drfat Bidding Document) iemwasilishwa kwa ajili ya kupitiwa na ZECO na Benki ya Dunia ili itangazwe kwa ajili ya kumpata Mkandarasi. |
| Uunganishaji wa mifumo ya utayarishaji wa bili za malipo kwa ZECO (SAP ERP and Hexing AMR Billing System Integration and Customer Data Migration). | Asilimia ya utayarishaji wa mfumo iliofikiwa | 100 | 10 | 10 | Zabuni ilitangazwa na Kampuni 2 ziliwasilisha zabuni zao, Tathmini (Combined Technical and Financial Proposals) imekamilika.Kazi ya kutayarisha Mkataba inaendelea. Mkataba huu unategemewa kusainiwa tarehe 30 Aprili 2024. Shughuli za ushauri wa kazi za zabuni hii zitatekelezwa kwa muda wa miezi 6 baada ya kusaini Mkataba |

### 11.2.14 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

Lengo kuu la Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni kukuza uchumi wa Zanzibar kwa kuimarisha matumizi endelevu ya bahari pamoja na kuwawezesha wajasiriamali ili kukuza ubunifu, Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imetekeleza jumla ya programu mbili na miradi miwili ya maendeleo kama ifuatvyo:-

### i) Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi

Programu hii ina lengo la kuongeza tija endelevu, uthabiti, faida na biashara ya mbegu za mazao, uvuvi na ufugaji wa samaki kwa kutilia mkazo uwezeshaji wa wanawake na ushiriki wa vijana. Programu imeanza mwaka 2021/22 na inatarajiwa kumaliza mwaka 2025/2026 programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa kutumia fedha za Washirika wa Maendeleo pekee. Kwa mwaka 2023/2024, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 11.92 bilioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 8.9 bilioni zimepangwa na hadi kufikia Machi 2024, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| **Shughuli Iliyopangwa** | **Kiashiria** | **Shabaha** | **Utekelezaji Halisi** | **Asilimia ya Utekelezaji** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanzisha uvuvi wa ubia na sekta binafsi kwa kununua meli 2 za uvuvi, kutayarisha mfumo wa uvuvi wa kibiashara na mfumo wa ubia | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Hatua iliyopo ni kufanya Upembuzi yakinifu (Feasibilty Study) ili kuendelea na mchakato wa manunuzi. |
| Ununuzi wa lori la jokofu la tani 10 kwa ajili ya matumizi ya kampuni ya ZAFICO; | Asilimia ya mnunuzi iliyofikiwa | 100 | 25 | 25 | Hatua iliyopo ni kusubiri ridhaa kutoka IFAD |
| Ujenzi wa maabara moja ya uzalishaji wa mbegu bora za mwani pamoja na vitalu 41 vya uzalishaji wa mbegu bora za mwani pamoja na kuwajengea uwezo wakulima; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 30 | 30 | Kinacho subiriwa ni kupata ridhaa kutoka IFAD ili kuanza ujenzi huo. |
| Kufanya utafiti wa uzalishaji na ukuzaji wa aina tatu za samaki ambao ni majongoo bahari, kaa na "milk fish"; | Asilimia ya kazi ya utafiti iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Hatua iliyopo ni kukusanya taarifa kwa ajili ya kuanza utafiti. |

### ii) Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia

Programu hii ina lengp la ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia ya juu na chini (Upstream and Downstream) kwa kuimarisha mnyororo wa thamani ya mafuta na gesi asilia kwa kutengeneza miundombinu inayotakikana. Programu hii ni ya miaka mitano imeanza mwaka 2022/23 na inatarajiwa kumalizika mwaka 2026/27 programu itagharimu jumla ya TZS 173.36 bilioni hadi kukamilika kwake. Programu hii itatekelezwa kupitia miradi miwili kwa mwaka 2023/2024, imepangiwa jumla ya TZS 11.0 bilioni kutoka Serikali.

**a) Mradi wa Kuanzisha Kituo cha Taifa cha Uhifadhi wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (NDR)**
Mradi huu una lengo la kujenga kituo cha uhifadhi wa taarifa za mafuta na gesi asilia. Mradi huu ni wa miaka mitano umeanza mwaka 2022/2023 mpaka mwaka 2026/2027 mradi unatarajiwa kugharimu jumla ya TZS 43.36 bilioni. Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 4.0 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 3.0 bilioni zilipangwa na hadi kufikia Machi 2024 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukamilisha ununuzi wa vifaa na vitendea kazi pamoja na kufanya marekebisho ya chumba kinachotumika kwa ajili ya kituo cha muda cha uhifadhi wa Taarifa; | Asilimia ya manunuzi yaliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Kazi ya ununuzi na ufungaji wa vifaa imekamilika,na vifaa vifuatavyo vimenunuliwa (*workstation 1 ,Data safe Cases 6, Tape Reader 3, Tape Cartridges 245, Tape Reader Cleaner 1 na Rack Cabinet).* |

### b) Mradi wa Utafiti wa Usalama wa Chakula na Maisha Endelevu kwa Jamii

Mradi huu una lengo la kujenga uelewa kupitia kutoa ufadhili wa elimu ya juu kwa mashirikiano ya tafiti juu ya kudumisha uchumi, usalama wa chakula na maisha endelevu. Mradi huu ni wa miaka mitatu umeanza mwaka 2023/24 mpaka mwaka 2025/26. Mradi unatarajiwa kutumia gharama ya *USD* 86,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo mpaka kukamilika kwake. Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 198 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 148.9 milioni zilipangwa. Hadi kufikia Machi 2024 shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoa udhamini wa kufanya tafiti katika sekta ya kuimarisha uvuvi hasa kwa wavuvi wadogo wadogo; | Asilimia ya utafiti uliyofanyika | 100 | 25 | 25 | Utafiti wa dagaa kavu kwa Zanzibar umefanyika ili kuangalia virutubisho vya kiafya na ubora. |

### 11.2.15 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi

Wizara hii inajukumu la kusimamia ubora wa miundombinu wa usafirishaji kwa abiria na mizigo kutoka sehem mmoja kwenda sehemu nyengine, Kwa kipini cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imetekeleza jumla ya programu tatu na mradi mmoja wa maendeleo kama ifuatavyo:-

#### i) Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu

Programu hii ina lengo la kujenga kwa kiwango cha lami, ujenzi wa mitaro pamoja na uwekaji wa taa na alama za barabarani kwa barabara kuu za Unguja na Pemba. Programu itasaidia kwa kiasi kikubwa kuunganisha miji mikubwa ya Zanzibar sambamba na kuhuisha uchumi na uwekezaji kwa vile barabara hizi ni kiunganishi cha miji na maeneo ya usafirishaji ikiwemo viwanja vya ndege na bandari pamoja na maeneo mengine ya kiuchumi. Programu imeanza mwaka 2022/23 na itahusisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 407.6. Kwa mwaka 2023/2024 programu inahusisha ujenzi wa barabara kuu ikiwemo barabara mpya na zinazoendelea na inatarajiwa kutekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo.

Kwa mwaka 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 249.38 bilioni (TZS 75.39 bilioni kutoka Serikalini na TZS 174.0 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai-Machi 2024) jumla ya TZS 187.0 bilioni zilipangwa (TZS 56.5 bilioni kutoka Serikalini na TZS 130.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 245.8 bilioni sawa na asilimia 131 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa (TZS 64.7 bilioni sawa na asilimia 114 kutoka Serikalini na TZS 181 bilioni sawa na asilimia 139 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Wete – Chake Chake km 22.1; | Idadi ya kilomita zilizojengwa | 10 | 2.7 | 27 | Kazi zilizofanyika ni kusafisha, kutia fusi tabaka la mwanzo na la pili pamoja na ujenzi wa makalvati, madaraja na miundombinu ya mabomba ya kupitishia maji. |
| Ujenzi wa barabara za Kisauni-Fumba, Tunguu-Makunduchi na Chake Chake-Mkoani | Asilimia ya Ujenzi iliofikiwa | 100 | 5 | 5 | Mkandarasi wa barabara hizo tayari ameshalipwa malipo ya awali kwa ajili ya kuanza kazi na tayari ameshawasili nchini kwa kuanza kazi ya ujenzi |

## ii) Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani

Programu hii ina lengo la kuunganisha mitaa na maneneo mbalimbali na barabara kuu. Hivyo, kukamilika kwa programu hii kutasaidia kupunguza msongamano katika barabara kuu pamoja na kuongeza haiba ya kupendezesha maeneo ya miji na vijiji. Vile vile itasaidia kurahisisha usafirishaji wa mizigo na kuchochea ukuaji wa uchumi na kumairika kwa sekta nyengine za kiuchumi ikiwemo sekta ya kilimo na biashara. Programu imeanza mwaka 2022/23 na itahusisha ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 katika maeneo ya mijini na vijijini kwa Unguja na Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 44.0 billioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 33.0 bilioni zimepangwa. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 16.5 bilioni sawa na asilimia 50 ya fedha iliyopangwa imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya tathmini pamoja na ulipaji wa fidia za nyumba na vipando vitakavoathirika na ujenzi; | Idadi ya barabara zilizofanyiwa tathmini | 4 | 4 | 100 | Barabara zilifanyiwa tathmini kwa ajili ya kulipwa walioathirika na ujenzi ni barabara za Mwakaje-Mwachealale-Bumbwisudi, Kidoti, Mfurumatonga-Milele skuli-New Road na Dunga Zuze. Maombi ya fedha yameshawasilishwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya kuidhinisha malipo. |
| Usafishaji wa maeneo pamoja na kuanza uwekaji wa fusi na lami kwa baadhi ya barabara; | Idadi ya kilomita zilizosafishwa | 89.95 | 89.95 | 100 | **Kwa upande wa Pemba Barabara zilizosafishwa ni**<br>i. Pembeni-Pandani (3.3Km)<br>ii. Mzambarautakao-Mchangamdogo (6.0Km)<br>iii. Mapofu-Tumbe Kojifa-Bandarini (12.7Km)<br>iv. Finya-Kicha (8.6Km)<br>v. Micheweni-Shumba Mjini-Bandarini (2.5Km)<br>vi. Micheweni-Kiuyu –Maziwa Ng'ombe (7.5Km)<br>vii. Konde-Msuka (4.1Km)<br>viii. Kiungoni-Tovuni (1.5Km)<br>ix. Penjewani-Mjini Kiuyu (2.2Km)<br>x. Mkarafuu Mmoja-Jumapili (5.15Km)<br>xi. Gando-Chokaani (2.1Km)<br>xii. Gando-Chaoni (1.5Km) xiii. Bwagamoyo-Kele (6.5Km)<br>xiv. Ukutini-Mtangani-Bandarini (4.0Km)<br>xv. Uondwe-Nyali (1.5Km)<br>Idadi ya kilomita zilizokamilika xvi. Barawa-Mleteni (2.0Km)<br>xvii. Mgagadu-Kwautao (5.6Km)<br>xviii. Makongeni-Kinazini (3.2Km)<br>xix. Wesha-Mkumbuu (10Km) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya km zilizowekwa kifusi | 13.8 | 13.8 | 100 | **Barabara zilizokamilika katika hatua ya uwekaji wa Kifusi Pemba**<br>i. Mapofu-Tumbe Kojifa-Bandarini (12.7 km) ambapo 12.6 km zimeshakamilika kwa tabaka la kwanza<br>ii. Micheweni-Kiuyu –Maziwa Ng'ombe (7.5Km) ambapo 1.2Km zimeshakamilika kwa tabaka la kwanza ,jumla ni 13.8Km |
| | Idadi ya Kilomita zinazoendelea kwa kifusi | 29.11 | 18.67 | 64.1 | Barabara zinazoendelea hatua ya kifusi kwa Unguja<br>Donge-Kijumoto-Usi Kombo (1.6Km) ambapo 1.44Km zimeshakamilika kwa tabaka la tatu<br>Bwekunduni – Soko la Samaki (2.66Km) ambapo 1.73Km zimeshakamilika kwa tabaka la tatu<br>Fukuchani-Kidagoni Skuli-Kidoti (6.0Km) ambapo 5.2Km zimeshakamilika kwa tabaka la kwanza<br>Kajengwa-Koba-Kinandi-Mnarani (5.0Km) ambapo 3.8Km zimeshakamilika kwa tabaka la tatu.<br>Mto wa Pwani-Fungurefu (2.0Km) ambapo 0.6Km zimeshakamilika kwa tabaka la kwanza.<br>Pwani Duta (Kidiko Uwanga)-Shashamine (Majoka) (2.5Km) ambapo 2.0Km zimeshakamilika kwa tabaka la kwanza.<br>Kajengwa-Uwandani-Kibwegele (6.75Km) ambapo 1.8Km zimeshakamilika kwa tabaka la kwanza.<br>Ndijani Skuli-Binguni (2.6Km) ambapo 2.1Km zimeshakamilika kwa tabaka la kwanza.<br>Jumla ya zilizokamilika ni 18.67Km |
| | Idadi ya km zilizowekwa kifusi | 31 | 31 | 100 | Barabara zilizokamilika hatua ya kifusi: Unguja<br>Upenja-Kibumbwi (1.9Km)<br>Mfurumatonga-Mbuyupopo (3.3Km) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Mfurumatonga-Mlilile Skuli (2.4Km)<br>Kitaruni-Kichaka Mabundi-Mkarafuu Pakacha (1.8Km)<br>Donge Mbiji-Chechele (1.73Km)<br>Bumbwini Skuli-Kiongwe (4.0Km)<br>Mtandao-Chiabonde (1.37Km)<br>Jambiani Kibigija-Jambiani Mfumbwi (5.0Km)<br>Bwejuu-Viamboni kwa Lila (1.9Km)<br>Kajengwa-Koba-Kinandi-Mnarani(5.0Km)<br>Muungoni Skuli-Pwani Duta (2.6Km) |
| Ujenzi wa mitaro pamoja na uwekaji wa lami kwa baadhi ya barabara zilizoanza kujengwa; | Idadi ya Km zilizowekwa lami | 32.25 | 32.25 | 100 | Barabara zilizowekwa lami, mitaro na alama za barabarani Unguja<br>i. Mgenihaji-Kwambani (2.4Km)<br>ii. Mchangani-Dongongwe (4.30Km)<br>iii. Bumbwisudi-Kizimbani (3.30Km)<br>iv. Jumbi – Ipa – Tunguu (4.9km)<br>v. Dungazuze (1.85km)<br>vi. Jumbi Sokoni – Kibondeni skuli-Hospital (4.40)<br>vii. Cheju – Kibele (3.8km)<br>viii. Tunguu- Ndijani Mseweni Mkwajungoma (7.80km)<br>ix. Kombeni – Nyamanzi (1.0km)<br>x. Dimani Market – Dimani Beach (1.8km) |
| | Idadi ya barabara zilizojengwa mitaro | 16 | 10.0 | 62.5 | |

### iii) Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini

Programu hii ina lengo la kuimarisha barabara kadhaa katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi na itahusisha matengenezo ya barabara, ujenzi wa njia za wapita kwa miguu, uwekaji wa taa pamoja na ujenzi wa mitaro ya maji katika barabara za mijini. Hivyo, Kukamilika kwa programu hii kutaongeza haiba na kupendezesha miji. Vile vile kusaidia kuimarika kwa baadhi ya sekta ikiwemo sekta ya usafirishaji, utalii na biashara. Programu inahusisha ujenzi wa kilomita 100.9 za barabara za mjini na imeanza mwaka 2022/2023. Kwa mwaka 2023/2024, programu imepangiwa jumla ya TZS 80.1 kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 60.0 bilioni zilipangwa. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 70.3 bilioni sawa na asilimia 117 ya fedha iliyopangwa imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara kuu za njia mbili (Two lanes dual) ikiwemo barabara ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume –Kiinua Miguu (6.5 km) | Idadi ya kilomita zilizokamilika kwa kiwango cha lami | 6.5 | 6 | 92 | Ujenzi wa mitaro ya kupitishia maji kwenye kingo za Barabara unaendelea kwa barabara pamoja njia za kupitishia miundombinu ya mawasiliano na maji na njia za watembea kwa miguu |
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara kuu za njia mbili (Two lanes dual) Kiembesamaki-Amani-Mtoni (Mkapa road) km 8.8; | Idadi ya kilomita zilizokamilika | 8.5 | 5.14 | 60.5 | Kazi ya uwekaji wa lami umekamilika kwa baadhi ya maeneo ya barabara. Kazi ya ujenzi inaendelea kwa maeneo ambayo hayajakamilika. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara ya Msumbiji-kinyangunya - Mwanakwerekwe na barabara zilizounganishwa km 2.83; | Idadi ya kilomita zilizokamilika | 2.83 | 2.24 | 79.15 | Kazi ya uwekaji wa mitaro kwenye kingo za barabara unaendelea |
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara ya Jangombe-matarumbeta km 0.6 | Idadi ya kilomita zilizokamilika | 0.6 | 0.45 | 75 | Kazi ya usafishaji na uchimbuaji wa barabara kwa ajili ya ujenzi unaendelea |
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara ya Saateni Kwaalimsha JKU km 1.28 | Idadi ya kilomita zilizokamilika | 1.28 | 0.74 | 57.81 | |
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara ya Gulioni – GAPCO- Makadara-Kwaabasi hussein km 0.58 | Idadi ya kilomita zilizokamilika | 0.58 | 0.33 | 56.89 | |
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara ya Mpendae Planned Area km 7.35 | Idadi ya kilomita zilizokamilika | 7.35 | 3.3 | 44.89 | Ujenzi unaendelea kwa hatua mbali mbali za uwekaji wa lami |
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara ya Michenzani, Gongoni, Kisiwandui Msikiti Mabati - Hailesalas km 1.3 | Idadi ya kilomita zilizokamilika | 1.3 | 0.52 | 40 | Ujenzi umekamilika kwa kiwango cha lami kutoka Michenzani Jumba nambari 10 hadi Msikiti Mabati |
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara ya Mombasa Panned Area km 6.20 | Idadi ya kilomita zilizokamilika | 6.20 | 3 | 48.38 | Ujenzi naendelea kwa hatua mbali mbali ikiwemo uwekaji wa lami na zege |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara ya Mazizini Vitambulisho - Zanzibar beach resort - Fish Market na Associated Roads km 1.830 | Idadi ya kilomita zilizokamilika | 1.830 | 1.46 | 79.78 | Ujenzi unaendelea katika hatua tofauti tofauti (kuna baadhi ya sehemu zishawekwa lami) |
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara ya Mbweni - Afya - Madina Mbweni Matrekta km 2.32 | Idadi ya kilomita zilizokamilika | 2.32 | 0.62 | 26.7 | |
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara ya Mbweni estate (TOT ) - Mbweni ruins plus Mbweni - BOT quarter - Kiembesamaki Uwanja wa ndege na barabara zinazounganishwa km 3.814 | Idadi ya kilomita zilizokamilika | 3.81 | 2.9 | 76 | |
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara ya Miembeni roundabout - Bomani - K/Chekundu mental hospital km 1.2 | Idadi ya kilomita zilizokamilika | 1.2 | 0.8 | 66.66 | |
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara ya Mtoni deport - ZECCO Power station - Mtoni Kidatu km 0.67 | Idadi ya kilomita zilizokamilika | 0.67 | 0.38 | 56.7 | |
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara ya Miembeni Roundabout - Michenzani Block number 1 na 9 km 0.52 | Idadi ya kilomita zilizokamilika | 0.52 | 0.3 | 57.69 | |
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwa barabara za juu (fly over). Round about ya Mwanakwerekwe | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 25.60 | 25.60 | Kazi ya ujenzi wa barabara za juu Mwanakwerekwe inaendelea kwa uwekaji wa nguzo kwa ajili ya barabara hizo |

### iv) Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani

Mradi huu una lengo la kujenga bandari kubwa na ya kisasa ambayo itahusisha gati tano ikiwemo gati ya mizigo, eneo la ushushaji na upakiaji wa mafuta, bandari ya uvuvi, pamoja na chelezo cha kukarabati meli. Hivyo kuamilika kwa bandari hii kutasaidia kuimarika shughuli za usafirishaji hivyo kupunguza msongamano uliopo katika bandari ya Malindi vile vile kutasaidia kuimarika kwa sekta nyengine za kiuchumi ikiwemo ya sekta uvuvi, biashara na viwanda. Mradi huu umeanza mwaka 2022/23 na unatarajiwa kutekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali na Wawekezaji kutoka katika sekta binafsi. Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 20.0 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 15.0 bilioni zilipangwa. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 29.1 bilioni sawa na asilimia 194 ya fedha iliyopangwa izmeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Upelekaji wa miundombinu ya maji, umeme na barabara katika eneo la ujenzi wa Bandari; | Idadi ya km zilizokamilika | 5.6 | 4.25 | 75.8 | Kazi ya ujenzi inaendelea kwa upande wa Barabara ya magharib yenye kilomita 4.6, kiasi cha kilomita 4.35 zimeanza kuwekwa lami ya mwanzo (Primary) yenye upana wa mita 12 na kwa upande wa njia ya kaskazini yenye kilomita 1.2 kazi ya ujazaji kifusi kwa tabaka la tatu Inaendelea |
| | Asilimia ya Miundombinu ya maji na umeme iliyofikiwa | 100 | 80 | 80 | Kazi ya upelekaji wa huduma za maji na umeme zinaendelea katika hatua za mwisho kukamilika |
| Kufanya tathmini pamoja na ulipaji wa fidia kwa maeneo yaliokuwa hayajakamilishwa malipo yake; | Asilimia ya tathmini iliyofanyika | 100 | 60 | 60 | Kazi ya tathmini ya fidia ya Barabara ya Mashariki na Kaskazini imekamilika na watu wameshalipwa na kwa upande wa barabara ya Kusini na Magharibi tathmini imefanyika na uhakiki wa tathmini ya fidia umefanyika na ripoti |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | imewasilishwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya kuidhinisha malipo. |
| | Idadi ya wananchi waliolipwa fidia. | 804 | 201 | 25 | Fidia imelipwa kwa waathirika katika njia ya maharibi na kaskazini |
| Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini; | Asilimia ya kazi iliyofanyika | 100 | 80 | 80 | Kazi ya Uratibu na na ufuatiliaji wa ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na umeme kwa eneo la ujenzi la Bandari ya Mangapwani inaendelea kufanyika |

### v) Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege

Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya anga ili iweze kuwa katika viwango vya kimataifa. Kwa mwaka 2023/2024 programu itahusisha ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba na hatua za awali za ujenzi. Programu itahusisha ujenzi wa maegesho, njia za kupitia ndege pamoja na sehemu za kukaa abiria. Aidha programu hii inatarajiwa kutekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 160.0 (TZS 10.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 150.0 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) programu ilipangiwa jumla ya TZS 120 bilioni (TZS 7.5 bilioni kutoka Serikalini na TZS 112.5 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya TZS 146.57 bilioni sawa na asilimia 122 ya fedha zilizopangwa zimeingizwa (TZS 12.69 bilioni sawa na asilimia 169 kutoka Serikalini na TZS 133.87 sawa na asilimia 119 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukamilisha tathmini pamoja na kulipa fidia kwa maeneo yatakayoathirika na ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba; | Asilimia ya tathmini iliofanyika | 100 | 100 | 100 | Kazi ya tathmini imekamilika. |
| | Idadi ya wananchi waliolipwa fidia | 719 | 649 | 90.2 | Malipo yamefanyika kwa baadhi ya wananchi na uhakiki unaendelea kufanyika kwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili kujiridhisha na kuwalipa waliokua hawajalipwa |
| Kuanza kwa hatua za awali za ujenzi wa uwanja wa ndege Pemba. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Mkandarasi wa barabara hizo tayari ameshalipwa malipo ya awali kwa ajili ya kuanza kazi na tayari ameshawasili nchini kwa kuanza kazi ya ujenzi |

### 11.2.16 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale

Wizara ina jukumu la kusimamia utalii na mambo ya kale kwa kuibua na kuongeza vivutio vipya sambamba na kuitangaza Zanzibar kiutalii. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imetekeleza programu moja ya maendeleo kama ifuatavyo:-

**Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria**

Programu hii ina lengo la kuimarisha maeneo ya kihistoria ili yawe ni kivutio kikubwa cha Utalii na Watalii ndani na nje ya Zanzibar. Sekta ya Utalii ni sekta ya huduma inayokua kwa kasi hapa Zanzibar ambapo hutoa fursa nyingi za ajira na kuongeza pato la Taifa. Programu hii imeanza mwaka 2017/18 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2024/25. Kwa mwaka 2023/24, programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 7.0 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) jumla ya TZS 5.3 bilioni zilipangwa. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya TZS 976.6 milioni sawa na asilimia 19 ya fedha iliyopangwa zimeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha eneo la Ras – Mkumbuu Pemba; | Asilimia ya uimarishaji iliyofikiwa | 100 | 45 | 45 | Katika uimarishaji wa eneo la Ras- Mkumbuu Pemba, ujenzi umefanyika na upo katika hatua ya kuezeka katika majengo yote, kisima kimekamilika na tayari kinatoa maji, Matenki ya kuhifadhia maji (Underground Storage Water Tank and Water Tower Tank) yamefikia 75%, Ukarabati wa majengo ya kihistoria (Restoration work) umefikia hatua ya uchimbaji "Excavation" kwaajili ya utafiti wa Akiolojia sawa na 50%. |
| Kuimarisha maeneo ya kihistoria ya Mangapwani (Pango la watumwa, Mahandaki ya vita na Kisima cha chini kwa chini) | Asilimia ya uimarishaji iliyofikiwa | 100 | 85 | 85 | Katika uimarishaji wa maeneo ya kihistoria Mangapwani kisima cha chini kwa chini kimeshakamilika. Jengo la kutolea huduma lipo katika hatua ya kupaka plasta ya mawe nje, mnara wa kuwekea tangi la maji umeshajengwa na madirisha yameshawekwa.<br>Vile vile, eneo la Mnara na Banka plasta na rangi tayari imeshawekwa pamoja na kuweka sawa njia za kufikia katika banka hizo. Majengo ya kutolea huduma yapo katika hatua ya kuweka tarazo. Kwa upande wa Chemba ya watumwa ujenzi umeshakamilika. Jengo jipya la kutolea huduma limeshawekwa plasta kwa ndani na kwa nje kazi inaendelea. |

**UPATIKANAJI WA FEDHA KWA PROGRAMU NA MIRADI YA KIMKAKATI KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 - MACHI 2024 KWA MUJIBU WA WIZARA/TAASISI (TZ MILIONI)**

| Wizara/Taasisi | Kilichopangwa | | | Kilichotoka | | | Asilimia | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAMU/MIRADI** | **SMZ** | **WM** | **Jumla** | **SMZ** | **WM** | **Jumla** | **SMZ** | **WM** | **Jumla** |
| **OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO** | | | | | | | | | |
| **i)Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar** | | | | | | | | | |
| i) Ujenzi wa Mji wa Serikali | 41,308,500 | 0 | 41,308,500 | 0 | 0 | 0 | 0 | | 0 |
| **ii) Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)** | 0 | 17,107,500 | 17,107,500 | 0 | 16,729,114 | 16,729,114 | 0 | 98 | 98 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **41,308,500** | **17,107,500** | **58,416,000** | **0** | **16,729,114** | **16,729,114** | **0** | **98** | **29** |
| **AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama | 15,000,000 | 0 | 15,000,000 | 13,057,764 | 0 | 13,057,764 | 87 | 0 | 87 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **15,000,000** | **0** | **15,000,000** | **13,057,764** | **0** | **13,057,764** | **87** | **0** | **87** |
| **WIZARA YA AFYA** | | | | | | | | | |
| **i) Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya na Mkoa** | 15,000,000 | 0 | 15,000,000 | 3,088,679 | 0 | 3,088,679 | 21 | 0 | 21 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **15,000,000** | **0** | **15,000,000** | **3,088,679** | **0** | **3,088,679** | **21** | | **21** |
| **WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI** | | | | | | | | | |
| i) Programu ya Uimarishaji Miundombinu ya Elimu | 44,278,610 | 54,146,900 | 98,425,510 | 66,486,667 | 39,103,256 | 105,589,923 | 150 | 72 | 107 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **44,278,610** | **54,146,900** | **98,425,510** | **66,486,667** | **39,103,256** | **105,589,923** | **150** | **72** | **107** |
| **WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** | | | | | | | | | |
| **i) Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo** | 24,750,000 | 958,541 | 25,708,541 | 31,776,064 | 0 | 31,776,064 | 128 | 0 | 124 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **24,750,000** | **958,541** | **25,708,541** | **31,776,064** | **0** | **31,776,064** | **128** | **0** | **124** |
| **WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI** | | | | | | | | | |
| **i) Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar** | | | | | | | | | |
| i) Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA) | 8,366,223 | 13,877,777 | 22,244,000 | 6,708,794 | 22,381,914 | 29,090,708 | 80 | 161 | 131 |
| ii) Uimarishaji Huduma Endelevu za maji Safi Zanzibar | 2,137,500 | 8,538,750 | 10,676,250 | 0 | 0 | - | 0 | 0 | 0 |
| iii) Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar | 7,875,000 | 0 | 7,875,000 | 3,439,963 | 0 | 3,439,963 | 44 | 0 | 44 |
| ii) Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar | | | | | | | | | |
| ii) Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZEST) | 5,400,000 | 6,658,759 | 12,058,759 | 0 | 1,201 | 1,201 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **23,778,723** | **29,075,285** | **52,854,008** | **10,148,757** | **22,383,115** | **32,531,872** | **43** | **77** | **62** |
| **WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI** | | | | | | | | | |
| iii) Ujenzi wa Bandari za Kisasa za Uvuvi | 7,875,000 | 0 | 7,875,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| v) Ujenzi wa Diko na Soko la Kisasa | 9,750,000 | 0 | 9,750,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **17,625,000** | **0** | **17,625,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI** | | | | | | | | | |
| **i) Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu** | 56,540,250 | 130,500,000 | 187,040,250 | 64,667,236 | 181,148,166 | 245,815,402 | 114 | 139 | 131 |
| **ii) Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani** | 33,045,000 | 0 | 33,045,000 | 16,458,652 | 0 | 16,458,652 | 50 | 0 | 50 |
| **iii) Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mijini** | 60,075,000 | 0 | 60,075,000 | 70,339,339 | 0 | 70,339,339 | 117 | 0 | 117 |
| Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege | | | | | | | | | |
| i) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba | 7,500,000 | 112,500,000 | 120,000,000 | 12,693,129 | 133,879,004 | 146,572,133 | 169 | 119 | 122 |
| Miradi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| ii) Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi - Mangapwani | 15,000,000 | 0 | 15,000,000 | 29,116,910 | 0 | 29,116,910 | 194 | 0 | 194 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **172,160,250** | **243,000,000** | **415,160,250** | **193,275,266** | **315,027,170** | **508,302,436** | **112** | **130** | **122** |
| **JUMLA YA KUBWA** | **348,257,683** | **338,644,826** | **686,902,509** | **317,833,198** | **393,242,655** | **711,075,853** | **91** | **116** | **104** |

**UPATIKANAJI WA FEDHA KWA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 - MACHI 2024 KWA MUJIBU WA WIZARA/TAASISI (TZ MILIONI)**

| Wizara/Taasisi | Kilichopangwa | | | Kilichotoka | | | Asilimia | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAMU/MIRADI** | **SMZ** | **WM** | **Jumla** | **SMZ** | **WM** | **Jumla** | **SMZ** | **WM** | **Jumla** |
| **OFISI YA RAIS - IKULU** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali | 1,800,000 | **0** | 1,800,000 | 600,000 | **0** | 600,000 | 33 | **0** | 33 |
| ii) Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika majengo ya Ikulu na Makazi ya Mheshimiwa Rais | 750,000 | **0** | 750,000 | 248,071 | **0** | 248,071 | 33 | **0** | 33 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,550,000** | 0 | **2,550,000** | 848,071 | 0 | 848,071 | 33 | 0 | **33** |
| **TAASISI YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Uimarishaji wa Shughuli za Taasisi za Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar | 3,375,000 | **0** | 3,375,000 | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **3,375,000** | 0 | **3,375,000** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **OFISI YA RAIS - KAZI NA UWEZESHAJI** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo, Wakati na Wakubwa | 3,375,000 | 1,882,500 | 5,257,500 | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **3,375,000** | **1,882,500** | **5,257,500** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **OFISI YA RAIS - UCHUMI NA UWEKEZAJI** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji Zanzibar** | 2,625,000 | **0** | 2,625,000 | 9,695,364 | 0 | 9,695,364 | 369 | | 369 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,625,000** | **0** | **2,625,000** | **9,695,364** | | **9,695,364** | **369** | | **369** |
| **OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar** | | | | | | | | | |
| i) Ukamilishaji wa Ofisi za Serikali | 14,283,000 | 0 | 14,283,000 | 5,643,891 | 0 | 5,643,891 | 40 | | 40 |
| ii) Ujenzi wa Mji wa Serikali | 41,308,500 | **0** | 41,308,500 | 0 | 0 | 0 | 0 | | 0 |
| **ii) Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)** | 0 | 17,107,500 | 17,107,500 | 0 | 16,729,114 | 16,729,114 | 0 | 98 | 98 |
| **iii) Programu ya Mageuzi Katika Usimamizi wa Fedha (PFMRPV)** | 96,300 | 2,826,660 | 2,922,960 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Miradi** | 0 | 0 | 0 | | | | 0 | 0 | 0 |
| i) Kuongeza Uwezo wa Kiutendaji | 0 | 262,500 | 262500 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ii) Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili | 26,025 | 1,268,455 | 1,294,480 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mfuko wa Huduma ya Mikopo kwa Miradi ya Maendeleo – "Debt Service Fund" | 108,000,000 | 0 | 108,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **163,713,825** | **21,465,115** | **185,178,940** | **5,643,891** | **16,729,114** | **22,373,005** | **3** | **78** | **12** |
| **TUME YA MIPANGO** | | | | | | | | | |
| Uratibu wa Programu ya Urasimishaji Ardhi na Biashara Zanzibar | 1,500,000 | 375,000 | 1,875,000 | 911,912 | 0 | 911,912 | 61 | 0 | 49 |
| Mradi wa Kuimarisha Ufanisi katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa | 1,500,000 | 0 | 1,500,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| iii) Mradi wa Usimamizi wa Upembuzi Yakinifu wa Programu na Miradi | 1,125,000 | **0** | 1,125,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **4,125,000** | **375,000** | **4,500,000** | **911,912** | **0** | **911,912** | **22** | **0** | **20** |
| **OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Uendelezaji wa Takwimu Zanzibar (ZSDP) | | 3,320,550 | 3,320,550 | 0 | 5,989,198 | 5,989,198 | 0 | 180 | 180 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **0** | **3,320,550** | **3,320,550** | **0** | **5,989,198** | **5,989,198** | **0** | **180** | **180** |
| **OFISI YA RAIS - KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** | | | | | | | | | |
| Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma (Phase II) | 562,500 | 0 | 562,500 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Programu ya Mageuzi Sekta ya Sheria | 187,500 | 727,224 | 914,724 | 0 | 300,595 | 300,595 | 0 | 41 | 33 |
| Mradi wa Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki kwa Wanawake Katika Kesi za Udhalilishaji (UN-WOMEN) | 0 | 280,200 | 280,200 | 0 | 163,407 | 163,407 | 0 | 58 | 58 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **750,000** | **1,007,424** | **1,757,424** | **0** | **464,002** | **464,002** | **0** | **46** | **26** |
| **MAHAKAMA KUU** | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| i) Mradi wa Uimarishaji Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Kesi (ECMIS) | 1,500,000 | 0 | 1,500,000 | **344,000** | **0** | **344,000** | **23** | **0** | **22.9333** |
| ii) Mradi wa Ujenzi wa Mahakama za Wilaya na Mikoa | 18,750,000 | **0** | 18,750,000 | **7,220,336** | **0** | **7,220,336** | **39** | **0** | 39 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **20,250,000** | **0** | **20,250,000** | **7,564,336** | **0** | **7,564,336** | **37** | **0** | **37** |
| **AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama | 15,000,000 | 0 | 15,000,000 | 13,057,764 | 0 | 13,057,764 | 87 | 0 | 87 |
| ii) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Masheha Zanzibar | 2,250,000 | 0 | 2,250,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **iv) Ujenzi wa Masoko Matatu (Mwanakwereke, Jumbi na Chuini)** | 0 | 0 | 0 | 50,716,390 | 0 | 50,716,390 | 0 | 0 | |
| iii) Mradi wa Ujenzi wa Viwanda vya Idara Maalum za SMZ | 3,750,000 | 0 | 3,750,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **21,000,000** | **0** | **21,000,000** | **63,774,154** | **0** | **63,774,154** | **304** | **0** | **304** |
| **WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili | 712,500 | 0 | 712,500 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **712,500** | **0** | **712,500** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM | 1,875,000 | 0 | 1,875,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,875,000** | **0** | **1,875,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **KIKOSI CHA VALANTIA** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Maaskari | 1,125,000 | 0 | 1,125,000 | 396,108 | 0 | 396,108 | 35 | 0 | 35 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,125,000** | **0** | **1,125,000** | **396,108** | **0** | **396,108** | **35** | **0** | **35** |
| **CHUO CHA MAFUNZO** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga | 1,125,000 | 0 | 1,125,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,125,000** | **0** | **1,125,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **JESHI LA KUJENGA UCHUMI** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Kambi za JKU | 2,250,000 | 0 | 2,250,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,250,000** | **0** | **2,250,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari | 1,125,000 | 0 | 1,125,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ii) Mradi wa Ununuzi wa Magari ya Zimamoto | 1,500,000 | 0 | 1,500,000 | 622,029 | 0 | 622,029 | 41 | 0 | 41 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,625,000** | **0** | **2,625,000** | **622,029** | **0** | **622,029** | **24** | **0** | **24** |
| **OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa mazingira | 1,500,000 | 0 | 1,500,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ii) Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Jamii ya Pwani. | 0 | 580,891 | 580,891 | 0 | 290,137 | 290,137 | 0 | 50 | 50 |
| iii) Uhimili wa Mabadiliko wa Tabianchi kwa kutumia Mfumo Ikolojia Vijijini | 0 | 175,813 | 175,813 | 0 | 15,463 | 15,463 | 0 | 9 | 9 |
| iv) Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Maji Machafu katika Eneo la MsinginiKichungwani Chake Chake Pemba. | 0 | 144,184 | 144,184 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| v) Mradi wa Kuimarisha Jamii kwa Kuzingatia Ikolojia na Shughuli za Kujipatia Kipato kwa Wavuvi Wadogo Wadogo na Usimamizi wa Eneo la Hifadhi la Mkondo wa Pemba (PECCA) | 0 | 187,372 | 187,372 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| vi) Mpango wa Kuirithisha Zanzibar Kijani | 1,125,000 | 0 | 1,125,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,625,000** | **1,088,259** | **3,713,259** | **0** | **305,600** | **305,600** | **0** | **28** | **8** |
| **TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Kuimarisha Mamlaka ya Kupambana na Madawa ya Kulevya | 1,125,000 | 0 | 1,125,000 | 973,072 | 0 | 973,072 | 86 | 0 | 86 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,125,000** | **0** | **1,125,000** | **973,072** | **0** | **973,072** | **86** | **0** | **86** |
| **OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI** | | | | | | | | | |
| **Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III) Kipindi cha pili** | 75,000 | 13,159,843 | 13,234,843 | 25,000 | 15,930,485 | 15,955,485 | 33 | 121 | 121 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **75,000** | **13,159,843** | **13,234,843** | **25,000** | **15,930,485** | **15,955,485** | **33** | **121** | **121** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar** | 412,500 | 733,296 | 1,145,796 | 0 | 1,942,301 | 1,942,301 | 0 | 265 | 170 |
| **Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi** | 15,000,000 | 0 | 15,000,000 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Programu ya Kuimarisha Huduma za Mama na Mtoto** | 0 | 1,342,253 | 1,342,253 | 0 | 1,131,600 | 1,131,600 | 0 | 84 | 84 |
| **Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya na Mkoa** | 15,000,000 | 0 | 15,000,000 | 3,088,679 | 0 | 3,088,679 | 21 | 0 | 21 |
| **Programu ya Kudhibiti Maradhi ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma** | 375,000 | 787,655 | 1,162,655 | 0 | 1,649,004 | 1,649,004 | 0 | 209 | 141.831 |
| **Programu ya kuimarisha Miundombnu ya Afya** | 750,000 | 0 | 750,000 | 1,405,505 | 0 | 1,405,505 | 187 | 0 | 187 |
| Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Afya-Kizimkazi | 0 | 3,000,000 | 3,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Afya | 7,500,000 | 0 | 7,500,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto (IRCH) | 750,000 | 3,606,259 | 4,356,259 | 0 | 1,909,853 | 1,909,853 | 0 | 53 | 44 |
| Matumizi kwa Miradi ya UVIKO - 19 na Madeni | 0 | 0 | 0 | 17,150,359 | 0 | 17,150,359 | | | |
| **JUMLA YA FUNGU** | **39,787,500** | **9,469,463** | **49,256,963** | **21,644,543** | **6,632,758** | **28,277,301** | **54** | **70** | **57** |
| **HOSPITAL YA MNAZI MMOJA** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Kuipandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja | 843,900 | 0 | 843,900 | 1,045,951 | 0 | 1,045,951 | 124 | 0 | 124 |
| ii) Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja | 0 | 7,500,000 | 7,500,000 | 0 | 281,649 | 281,649 | 0 | 4 | 4 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **843,900** | **7,500,000** | **8,343,900** | **1,045,951** | **281,649** | **1,327,600** | **124** | **4** | **16** |
| **WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI** | | | | | | | | | |
| **KAMISHENI YA ARDHI** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Utayarishaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi | 3,412,500 | 0 | 3,412,500 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **3,412,500** | **0** | **3,412,500** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA** | | | | | | | | | |
| i) Kuimarisha na kuendeleza maeneo maalum ya viwanda (Industrial Parks) | 19,509,000 | 0 | 19,509,000 | 8,362,721 | 0 | 8,362,721 | 43 | 0 | 43 |
| ii) Mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho ya Kimataifa Zanzibar | 1,803,750 | 0 | 1,803,750 | 5,396,029 | 0 | 5,396,029 | 299 | 0 | 299 |
| ii) Uimarishaji wa Miundombinu ya Kiwanda cha Kusindikia Mazao ya Kilimo Zanzibar | 0 | 22,955 | 22,955 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **21,312,750** | **22,955** | **21,335,705** | **13,758,750** | **0** | **13,758,750** | **65** | **0** | **64** |
| **WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI** | | | | | | | | | |
| Programu ya Uimarishaji Miundombinu ya Elimu | 44,278,610 | 54,146,900 | 98,425,510 | 66,486,667 | 39,103,256 | 105,589,923 | 150 | 72 | 107 |
| i) Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi | 0 | 4,593,300 | 4,593,300 | 0 | 0 | - | 0 | 0 | 0 |
| ii) Uimarishaji wa Elimu ya Lazima | 11,379,443 | 1,635,000 | 13,014,443 | 0 | 2,937,868 | 2,937,868 | 0 | 180 | 23 |
| iii) Kuimarisha Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali | 3,570,000 | 0 | 3,570,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| iv) Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu | 15,000,000 | 1,200,000 | 16,200,000 | 13,106,858 | 10,499,800 | 23,606,658 | 87 | 875 | 146 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **74,228,052** | **61,575,200** | **135,803,252** | **79,593,525** | **52,540,924** | **132,134,449** | **107** | **85** | **97** |
| **WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo** | 24,750,000 | 958,541 | 25,708,541 | 31,776,064 | 0 | 31,776,064 | 128 | 0 | 124 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **24,750,000** | **958,541** | **25,708,541** | **31,776,064** | **0** | **31,776,064** | **128** | **0** | **124** |
| **WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Umwagiliaji** | 375,000 | 23,400,445 | 23,775,445 | 0 | 17,764,530 | 17,764,530 | 0 | 76 | 75 |
| **Programu ya kuendeleza Sekta ya kilimo na Mifugo** | | | | | | 0 | | | |
| i) Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo | 1,500,000 | 0 | 1,500,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ii) Mradi wa Kilimo Tija | 0 | 1,755,000 | 1,755,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Programu ya Kudhibiti Maradhi na Upotevu wa Mazao** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| i) Mradi wa Kudhibiti Upotevu wa Mazao | 0 | 316,182 | 316,182 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ii) Mradi wa Kuwaunganisha Wakulima wa Mboga na Matunda (AGRICONNECT) | 0 | 6,422,010 | 6,422,010 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| iii) Kupambana na Sumukuvu Tanzania (TANIPAC) | 0 | 364,169 | 364,169 | 0 | 1,936,403 | 1,936,403 | 0 | 532 | 532 |
| iv) Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC) | 0 | 385,500 | 385,500 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| v) Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula | 16,875,000 | 0 | 16,875,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **JUMLA YA FUNGU** | **18,750,000** | **32,643,305** | **51,393,305** | **0** | **19,700,933** | **19,700,933** | **0** | **60** | **38** |
| **WIZARA YA MAENDELEO YA VIJANA, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Hifadhi ya wazee | 1,125,000 | **0** | 1,125,000 | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | 0 |
| ii) Mradi wa Kutokomeza Udhalilishaji na Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana | 0 | 477,241 | 477,241 | 422,122 | **0** | **422,122** | **0** | **0** | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,125,000** | **477,241** | **1,602,241** | **422,122** | **0** | **422,122** | **38** | **0** | **26** |
| **WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar** | | | | | | | | | |
| i) Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA) | 8,366,223 | 13,877,777 | 22,244,000 | 6,708,794 | 22,381,914 | 29,090,708 | 80 | 161 | 131 |
| ii) Uimarishaji Huduma Endelevu za maji Safi Zanzibar | 2,137,500 | 8,538,750 | 10,676,250 | 0 | 0 | - | 0 | 0 | 0 |
| iii) Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar | 7,875,000 | 0 | 7,875,000 | 3,439,963 | 0 | 3,439,963 | 44 | 0 | 44 |
| iv) Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi | 0 | 7,471,238 | 7,471,238 | 306,239 | 3,511,138 | 3,817,377 | 0 | 47 | 51 |
| v) Mradi wa kufanya upembuzi Yakinifu wa Rasilimali Maji | 0 | 7,863,345 | 7,863,345 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| vi)Mradi wa Ununuzi wa Chlorine, Usimamizi na Uangalizi bora wa Maji | 0 | 56,250 | 56,250 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| vii) Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Maji Zanzibar | 0 | 1,950,000 | 1,950,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| i) Mradi wa kuimarisha Miundombinu ya Umeme | 12,750,000 | 0 | 12,750,000 | 11,651,735 | 0 | 11,651,735 | 91 | 0 | 91 |
| ii) Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZEST) | 5400000 | 6,658,759 | 12,058,759 | 0 | 1,201 | 1,201 | 0 | 0 | 0 |
| iii) Mradi wa Nishati Jumuishi Zanzibar (Zanzibar Energy Consolidation) | 0 | 50,721 | 50,721 | 0 | 0 | - | 0 | 0 | 0 |
| **iv) Matumizi kwa miradi ya UVIKO - 19** | 0 | 0 | 0 | 169,534 | | 169,534 | | | |
| **JUMLA YA FUNGU** | **36,528,723** | **46,466,839** | **82,995,562** | **22,276,265** | **25,894,253** | **48,000,984** | **61** | **56** | **58** |
| **WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi** | 0 | 8,940,775 | 8,940,775 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| i)Mradi wa Kuanzisha Kituo cha Taifa cha Uhifadhi wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (NDR) | 3,000,000 | 0 | 3,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ii) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Gesi Asilia na Miundombinu ya Usambazaji wa Gesi (LPG) | 750,000 | 0 | 750,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **iii) Ujenzi wa kituo cha kuhifadhia bidhaa za petroli iliyosafishwa na usambazaji** | 2,250,000 | 0 | 2,250,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| i. Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maabara ya Uthamini wa Ubora wa Bidhaa za Baharini | 3,000,000 | 0 | 3,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ii) Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini | 0 | 2,550,000 | 2,550,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| iii) Ujenzi wa Bandari za Kisasa za Uvuvi | 7,875,000 | 0 | 7,875,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| iv) Mradi wa Maendeleo ya Uchumi wa Buluu | 0 | 2,625,000 | 2,625,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| v) Ujenzi wa Diko na Soko la Kisasa | 9,750,000 | 0 | 9,750,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| vi)Mradi wa Bahari Maisha | 0 | 4,500,000 | 4,500,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| vii) Mradi wa Mashirikiano wa Usimamizi wa Bahari na Uvuvi kwa Nchi za Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi (SWIOFC) | 0 | 259,159 | 259,159 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| viii)Mradi wa Utafiti wa Usalama wa Chakula na Maisha Endelevu kwa Jamii | 0 | 148,866 | 148,866 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ix) Mradi wa Kuongeza Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Usimamizi Jumuishi wa Rasilimali za Bahari na Uchumi wa Buluu Endelevu (ZAN BLUE) | 0 | 173,100 | 173,100 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| x) Mradi wa Kuweka Mitambo ya Kuhifadhia Baridi | 0 | 402,560 | 402,560 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| xi) Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Ukusanyaji wa Tozo katika Maeneo ya Hifadhi | 0 | 86,550 | 86,550 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| xii) Mradi wa Maendeleo Endelevu wa Mazao ya Baharini(TASFAMP) | 0 | 4,875,000 | 4,875,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| xiii) Mradi Jumuishi wa Kuhifadhi Ikolojia na Kuendeleza Uchumi wa Bahari Tanzania | 0 | 2,625,000 | 2,625,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **xiv) Matumizi kwa miradi ya UVIKO - 19** | 0 | 0 | 0 | 2,184,044 | 0 | 2,184,044 | 0 | 0 | 0 |
| JUMLA YA FUNGU | **26,625,000** | **27,186,009** | **53,811,009** | **2,184,044** | **0** | **2,184,044** | **0** | **0** | **0** |
| **WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Ujenzi wa Barabara** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu** | 56,540,250 | 130,500,000 | 187,040,250 | 64,667,236 | 181,148,166 | 245,815,402 | 114 | 139 | 131 |
| **Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani** | 33,045,000 | 0 | 33,045,000 | 16,458,652 | 0 | 16,458,652 | 50 | 0 | 50 |
| **Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mijini** | 60,075,000 | 0 | 60,075,000 | 70,339,339 | 0 | 70,339,339 | 117 | 0 | 117 |
| Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| i) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba | 7,500,000 | 112,500,000 | 120,000,000 | 12,693,129 | 133,879,004 | 146,572,133 | 169 | 119 | 122 |
| Miradi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| i) Mradi wa Uboreshaji wa Mfumo wa Mawasiliano | 4,425,000 | 0 | 4,425,000 | 1,420,409 | 0 | 1,420,409 | 32 | 0 | 32 |
| ii) Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi - Mangapwani | 15,000,000 | 0 | 15,000,000 | 29,116,910 | 0 | 29,116,910 | 194 | 0 | 194 |
| **iii) Mkopo Ujenzi wa Jengo la Abiria Terminal 2** | 0 | 0 | 0 | 17,850,000 | 0 | 17,850,000 | | | |
| JUMLA YA FUNGU | **176,585,250** | **243,000,000** | **419,585,250** | **212,545,675** | **315,027,170** | **527,572,845** | **120** | **130** | **126** |
| **WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE** | | | | | | | | | |
| Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria | 5,250,000 | 0 | 5,250,000 | 976,627 | 0 | 976,627 | 19 | 0 | 19 |
| JUMLA YA FUNGU | **5,250,000** | **0** | **5,250,000** | **976,627** | **0** | **976,627** | **19** | **0** | **19** |
| **Mfuko wa Huduma ya Mikopo kwa Miradi ya Maendeleo – "Debt Service Fund".** | **108,000,000** | **0** | **108,000,000** | **273,442,700** | **0** | **273,442,700** | 253 | | 253 |
| **Mfuko wa Miundombinu** | | | | **86,441,418** | **0** | **86,441,418** | **0** | | **-** |
| **JUMLA YA KUBWA** | **772,500,000** | **471,598,242** | **1,244,098,242** | **836,561,622** | **459,496,086** | **1,295,888,174** | **108** | **97** | **104** |